2 FEBRUARI, 2023

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI

**Kikao cha Tatu – Tarehe 2 Februari, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa. Kwa niaba yake Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Dennis Londo.

**MHE. DENNIS L. LONDO - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022.

**SPIKA:** Tunaendelea, Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha sote kuendelea na Kikao cha Tatu cha Mkutano huu wa Kumi wa Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Kanuni ya 44(3), inaeleza kuhusu uwepo wa kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu siku ya Alhamisi. Hata hivyo, Ibara ya (4)

inaeleza kuwa, Waziri Mkuu anaweza kutumia kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu kutoa taarifa au ufafanuzi kuwa kuhusu suala lolote linalohusiana na Shughuli za Serikali na lenye maslahi kwa umma.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni hiyo na kutokana na baadhi ya matukio yanayotokea hivi sasa ikiwemo la taarifa na malalamiko kwenye jamii yanayohusu masuala ya malezi na maadili, nimeona ni vema nitumie kipindi hiki kutoa ufafanuzi na mwelekeo wa Serikali kwenye baadhi ya masuala husika. Jambo ambalo ningependa kulitolea ufafanuzi ni changamoto ya nidhamu na malezi ya wanafunzi na adhabu zinazotolewa shuleni.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nyote mtakubaliana nami kwamba shule zetu zimekuwa kioo cha malezi ya watoto wetu hususani katika kusimamia na kujenga nidhamu katika jamii. Siku zote jukumu hili limekuwa likitekelezwa kwa ushirikiano wa karibu kati ya walimu na wazazi, kwa lengo la kuwajenga watoto wetu na pale ambapo mtoto anakwenda kinyume na nidhamu iliyotarajiwa viboko hutumika kama moja ya adhabu ya kumrejesha mtoto katika mstari.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha adhabu hiyo inaleta tija na kufikia malengo yaliyokusudiwa Serikali iliweka utaratibu maalum wa namna ya kusimamia adhabu hiyo bila kuathiri afya na saikolojia ya mtoto. Licha ya malengo tajwa ya adhabu ya viboko, hivi karibuni kupitia redio, *television*, magazeti na mitandao ya kijamii tumeshuhudia kusambaa kwa taarifa zenye kuonesha matukio mengi dhidi ya watoto katika jamii na baadhi ya shule zetu. Vitendo hivyo vimesababisha madhara mengi ikiwemo kuleta taharuki kwa jamii, athari ya kimwili na

kiakili au msongo wa mawazo kwa wahanga wa matukio hayo wakimemo wazazi na walezi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza afua mbalimbali katika kuhakikisha ulinzi na usalama wa mtoto awapo kwenye mazingira yote (Watoto waliopo shuleni na wasiokuwapo shuleni). Kwa mfano, Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 iliyotungwa na Bunge letu Tukufu kwa madhumuni ya kuhakikisha mtoto analindwa na hatimae aweze kukua na kuwa raia mwema wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, licha ya kuwepo kwa mifumo hiyo bado wapo baadhi ya wenzetu au watu ambao wamekuwa wakifanya ukiukwaji wa sheria na taratibu hizo kwa makusudi na hivyo kusababisha madhara makubwa kwa jamii yetu. Mathalani hivi karibuni tumeshuhudia kupitia vyombo vya habari, vitendo vya adhabu kali dhidi ya wanafunzi kwa baadhi ya shule zetu. Adhabu hizo zimefanywa na baadhi ya Walimu walio na mafunzo ya kutosha ya malezi, mahali pengine Mwalimu Mkuu mwenye dhamana ya kuongoza ambaye pia anafahamu utaratibu wa utoaji wa adhabu shuleni.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kueleza kwamba Serikali haitofumbia macho na wala kukubaliana na aina hiyo ya adhabu kali. Tayari Serikali imechukua hatua za kinidhamu kwa wahusika na nitumie fursa hii adhimu kukumbusha mamlaka za elimu nchini kuhakikisha kuwa utoaji wa adhabu shuleni unazingatia Waraka Namba 24 wa Mwaka 2002 kwa Wizara ya Elimu na Utamaduni ambao umeainisha utaratibu wa utoaji wa adhabu kama ifuatavyo:-

(i) Adhabu itazingatia ukubwa wa kosa, jinsia na afya ya mtoto na isizidi viboko vinne kwa wakati mmoja;

(ii) Mwanafunzi wa kike atapewa adhabu ya viboko mkononi na Mwalimu wa Kike, isipokuwa kama shule hiyo haina mwalimu wa kike;

(iii) Adhabu ya viboko itapotolewa iorodheshwe katika kitabu kilichotengwa kwa kusudi hili, ikiwa ni pamoja na jina la mwanafunzi aliyepewa adhabu, kosa alilotenda, idadi ya viboko na jina la Mwalimu aliyetoa adhabu hiyo;

(iv) Mwalimu Mkuu ni lazima atie saini katika vitabu kila mahala baada ya adhabu hiyo inapotolewa; na

(v) Mwanafunzi akikataa adhabu ya viboko atasimamishwa shule.

Mheshimiwa Spika, waraka wetu huo umeweka bayana kuwa hatua za kinidhamu zitachukuliwa kwa Mwalimu yoyote ambaye atakiuka utaratibu wa adhabu ya viboko. Hapa nisisitize tu kuwa, hatua kali zitachukuliwa hata kwa Walimu Wakuu au Walimu wa Shule wanaokiuka utaratibu uliowekwa. Kwa upande wa wanafunzi na wazazi wenzangu, hatuna budi kuhakikisha kuwa tunatimiza wajibu wetu ipasavyo wa kuhakikisha tunashirikiana na Walimu wetu katika kujenga nidhamu na masomo kwa watoto wetu ili hatimaye waweze kutimiza malengo yao katika maisha.

Mheshimiwa Spika, licha ya changamoto zilizojitokeza na hatua za awali zilizochukuliwa, naomba

kusisitiza kuwa bado shule zetu ni mahali salama kwa malezi ya watoto wetu, walimu wetu wameendelea kufanya kazi nzuri kwa bidii na kwa kujituma katika mazingira waliyopo. Changamoto ya nidhamu mbaya ya wanafunzi siyo jukumu la Mwalimu pekee kulisimamia, hivyo wazazi na jamii kwa ujumla wanapaswa kushirikiana kwa karibu na Walimu wetu katika kuhakikisha kuwa wanatekeleza majukumu yao ya kuwafundisha, kuwalea, kuwaongoza na kuwaendeleza wanafunzi kimwili, kiakili na kiroho kwa uadilifu na kwa kuzingatia sheria, mila, desturi na tamaduni zetu. Nitoe wito kwa wazazi kuhakikisha katika majukumu yao ya kila siku wanatenga muda wa kufuatilia mwenendo na maendeleo ya mtoto kuzungumza na kuwasikiliza watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, Walimu wamekuwa wakifanyakazi kubwa sana nchini, kuliko mapungufu machache tunayoyaona hasa katika kupitia mitandao ya kijamii. Walimu wamekuwa wakifundisha, wakilea vijana wetu katika mazingira tofauti pamoja na kutoa huduma mbalimbali ambazo nyingine zilitakiwa kutolewa na wazazi au walezi majumbani mwao. Bahati mbaya kwa jamii zetu ni kuwa jambo baya husambaa kwa haraka zaidi kuliko jema, hata hivyo licha ya mapungufu kutoka kwa baadhi ya walimu kama nilivyoainisha awali, Walimu wetu wanafanya mambo mengi na makubwa ya kimalezi kwa watoto wetu ambayo pengine hayasambazwi na kuonekana.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa msingi wa maelezo yangu hapa juu, nitoe wito kwa jamii kutobeza juhudi zinazofanywa na Walimu kote nchini badala yake tuwatie moyo, hasa wale wanaozingatia miiko ya taaluma zao na misingi ya malezi. Pia nitoe wito kwa jamii hasa wale wanaochukua au kupata matukio haya na kuyarusha

kwenye mitandao kutofanya hivyo kwani yanajenga chuki kwa walimu na taswira hasi, kwa walimu wote badala ya wahusika wachache. Pale matukio kama haya yanapojitokeza utaratibu umewekwa taarifa zake zitumwe kwa mamlaka husika ili hatua stahiki zichukuliwe hukohuko badala ya kuleta taharuki kwa jamii nzima.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nieleweke hapa kuwa lengo siyo kuficha taarifa bali ni kuzuia taharuki, chuki na uhasama ndani ya jamii zetu. Si kwa waalimu tu bali kwenye nyanja nyingine za utumishi kama Afya, Vyombo vya Ulinzi na Usalama na maeneo mengine yanayofanana kama haya.

Mheshimiwa Spika, ninatambua siyo kusudio la Walimu kuwadhuru wanafunzi lakini tukubaliane kuwa kuna udhaifu katika utaratibu wa utoaji wa na usimamizi wa adhabu ya viboko shuleni, hivyo nitoe wito kwa Maafisa Elimu wa Mikoa na Maafisa Elimu wa Wilaya, kuwakumbusha Walimu wetu nchini kuzingatia muongozo wa utoaji wa adhabu shuleni, chini ya Kifungu namba 61 cha Sheria ya Elimu, Sura ya 353 ya Sheria zetu pamoja na kanuni zake. Muongozo umesisitiza kuwa adhabu ya viboko itatolewa iwapo tu patatokea utovu wa nidhamu au kosa kubwa litakalofanywa ndani au nje ya shule ambalo litaishushia shule heshima, na kuwa adhabu hii itatolewa kwa kuzingatia umri, jinsia na afya ya mwanafunzi kama nilivyotangulia kueleza hapo awali. Aidha nitoe wito kwa Walimu Wakuu na Wakuu wa Shule kutumia walimu wa malezi, ushauri, unasihi pamoja na Viongozi wa Dini walioko majirani katika kurekebisha watoto wetu na kuwajenge kimaadili ili kuepukana na matumizi ya adhabu ya viboko pale ambapo sio lazima kutumia viboko.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali itaendelea kiusimamia weledi, kanuni na uadilifu utumishi katika nyanja zote, pia katika kila sekta ya utumishi wa umma. Aidha pale patakapojitokeza uvunjifu wa maadili na miiko iliyowekwa hatua stahiki za kinidhamu zitachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maelezo hayo. Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni yetu hiyo 44 maswali yanaruhusiwa isipokuwa ni maswali yanayohusiana na taarifa ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameisoma, na sioni Mbunge yoyote akiwa amesimama …ooh! Mheshimiwa Ally Kassinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kutokana na taarifa iliyowasilishwa. Kwa mujibu wa waraka ambao unaelekeza adhabu za viboko kwa wanafunzi wenye utovu wa nidhamu, viboko visizidi vinne na ameidhinishwa Mwalimu Mkuu au Mkuu wa Shule au atakayeidhinishwa na wakuu hao kutoa adhabu hiyo. Kutokana na usimamizi au udhibiti ambao hauko sawa, imebainika taharuki kama ambavyo imejiri hivi karibuni.

Je, kwanini Serikali isirekebishe waraka huu na kuongeza kwamba wakati aliyeidhinishwa kama ni Mkuu wa Shule au mwingine aliyeidhinishwa anatoa adhabu kukawa na Kamati maalum ya usimamizi na kubariki adhabu hiyo ili kuondokana na taharuki kama hizi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli waraka wetu wa elimu umetoa maelezo thabiti ya namna ya utoaji wa adhabu shuleni, kama nilivyosema kwenye maelezo yangu, adhabu ya viboko ni moja kati ya adhabu zinazotumika katika kumjenga mtoto na kumfanya aweze kutii sheria za shuleni na viboko visizidi vinne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa uundwaji wa Kamati Shule zote za Msingi zina Kamati ya Shule, na Shule zote za Sekondari zina Bodi ya Shule. Pale ambako mwanafunzi hufanya kosa kubwa kuliko haya makosa madogo madogo basi mtoto huyo, kwanza hatua inayochukuliwa mzazi kuitwa kujulishwa tabia na mwenendo wa mtoto huyo ili sasa kumshirikisha mzazi katika kumjenga mtoto kinidhamu. Mbili, pale ambako adhabu hiyo inahitaji kumfukuza shule unashirikisha sasa Kamati ya Shule. Kwa hiyo, utaratibu wa utoaji adhabu umewekwa vizuri kabisa na ndiyo ambao unafuatwa mashuleni. Hili ambalo limejitokeza hivi karibuni ni tatizo la mmoja kati ya watumishi wengi kutenda bila kufuata utaratibu lakini siyo utaratibu ambao umewekwa na siyo ambao unatumika kwenye maeneo mengi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa matukio haya hayatokei tu kule shuleni, hata huku majumbani tumeshuhudia watoto wakipewa adhabu kali kinyume na kufuata utaratibu.

Je, nini maelekezo au ushauri wa Serikali kwa wazazi wanapotoa adhabu kwa watoto wao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe hilo haliko kwenye mwongozo ambao ameusema Mheshimiwa Waziri Mkuu na kuutolea taarifa, lakini wazo lako japokuwa ni zuri, kwamba na nyumbani kuwekewe utaratibu wa namna ya kutoa adhabu kwa watoto, lakini mwongozo aliousema Mheshimiwa Waziri Mkuu unahusu adhabu mashuleni, sasa kama tunalo wazo la kwamba kuwe na utaratibu wa namna wazazi wanavyoadhibu watoto wao, hilo litakuwa kidogo nje ya kile alichokisema Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimuwa Waziri Mkuu kwa kuwa changamoto hii ya Walimu kuchapa watoto bila utaratibu na tena kikatili, nini sasa Serikali haioni kama kuna haja ya kuwaelimisha Walimu hawa somo la maadili la namna ya malezi ya watoto na makuzi katika shule zetu za Msingi na hata Sekondari?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lemburis, Mbunge wa Arumeru kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, taasisi zote za elimu zina taratibu zake, na uendeshaji wa elimu nchini una sheria na kanuni zake ambazo zimewekwa, na ndizo zinazosaidia kuongoza wakuu wa taasisi na wale watumishi wa taasisi husika katika kuzingatia sheria na kanuni zilizowekwa; na ndiyo sababu unaona mambo yanaenda vizuri. Hiyo ni kuanzia elimu ya awali, ya msingi, sekondari mpaka elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo uainishaji wa sheria hizi na kanuni ndio unaoongoza watumishi walio kwenye sekta hiyo au taasisi hiyo kufuata. Ndiyo maana tunaona sasa utulivu upo na kazi zinaenda kwa sababu kila mmoja anazingatia sheria na kanuni zilizopo. Kwa hiyo hatuwezi kusema tutachukua hatua kali kwa sababu miongozo ipo pale ambapo mtumishi anakiuka taratibu na sheria, sheria ile imeelekeza na adhabu ambazo zinatolewa kwa mhusika. Kwa hiyo utaratibu huo unatumika kama ni adhabu ndogo kwa aliyekiuka utaratibu umeainishwa, kama ni adhabu kubwa imeainishwa lakini pia hata akitakiwa kwenda mahakamani imeainishwa.

Mheshimiwa Spika, lakini tuzingatie tu kwamba taaluma ya ualimu ina misingi yake na imewekea utaratibu pia chini ya Wizara ya Elimu na kwa hiyo zipo kamati za maadili mioongoni mwa walimu. Wakati mwingine vyama vya wafanyakazi kama vile CWT yenyewe inachukua nafasi pia kukaa na walimu kuwafanyia *counselling* pia kuwaelimisha ili kufanya mambo yanavyokwenda kama utulivu ambao sasa upo na utaratibu huo ndio ambao tunautumia kwa sasa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza swali la nyongeza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri Mkuu anatoa maelezo yake amesema sasa ni marufuku watu kutoa taarifa ya matokeo haya katika *social media.* Matendo haya yamekuwa yakifanyika na yanafichwa na wakati mwingine viongozi wahusika wanalinda waliyoyatenda. Je, Waziri Mkuu haoni kuwa kitendo cha kuwazuia watu kutotoa taarifa ambayo ilikuwa inasaidia viongozi wahusika kuchukua hatua haraka, huoni kwamba matendo hayo yataendelea kufanyika na yataendelea kufichwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rwamlaza, Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeeleza kwenye taarifa yangu, kwamba malengo ya kutahadharisha kuleta mkanganyiko, taharuki kwenye jamii hayalengi kulinda maovu yanatotokea bali yanalenga katika kuifanya jamii iendelee kuwa tulivu. Kwa sababu gani; taratibu zibainishwe pale ambapo mtu anakiuka utaratibu basi hatua kali zinachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, tunatambua tukio ambalo limejitokeza pale Kyelwa aliyechukua video ni mwalimu ambaye alishindwa kumwelekeza mwalimu mwenzake kwamba jambo hilo lisifanyike kwa sababu ni kiongozi wa juu kwa cheo. Lakini bado alikuwa ana uwezo wa kutoa taarifa kwa maafisa elimu wao wa kata, pia tuna afisa elimu wa wilaya na adhabu zikachukuliwa. Kwa hiyo

video ile aliyochukua badala ya kuirusha kwenye mtandao angeweza kuipeleka pia kwa afisa elimu kama ushahidi wa tukio lililotokea mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo bado hatusisitizi sana hilo kwa sababu limesaidia pia kutoa taarifa. Hata hivyo, katika kuzuia taharuki na kutoa picha ambayo kwa jamii juu ya matendo yanayotendeka kwenye maeneo haya tulilazimika pia kushauri kwamba ni vizuri taratibu zikaenda kwenye mamlaka husika, kwa sababu mamlaka zipo na zimeainishwa kisheria pia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Olelekaita swali la kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwa kuwa viboko hivi vinaleta taharuki kubwa sana kwa nini msilete mwongozo tu aidha tukafuta kabisa ama walau kutoka nne iwe moja? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Olelekaita, Mbunge wa Kiteto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Olelekaita ametoa ushauri; na kwa kuwa hii ilikuwa ni kanuni zilizokuwa zimewekwa na zikatolewa na waraka kutoka Wizara ya Elimu na Utamaduni, basi kwa ushairi huo tunauzingatia tutaona kama inawezekana, wadau watahusishwa, wataangalia mwenendo wa nidhamu, matatizo ya nidhamu yaliyopo nchini na pia wakati tulionao, ambao ndio unaowezesha. Hata sisi Wabunge kubadilisha sheria

moja na kuifanyia maboresho inatokana na wakati. Kwa hiyo nalo pia tutaliangalia kama wakati unaruhusu kuondoa viboko vinne mpaka kimoja au kuondoa kabisa basi wadau watatushauri, na Serikali tupo tayari kutekeleza pale ambako inaonekana wadau watakubaliana na hilo, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa kuna nchi kadhaa ambazo zimeshafuta adhabu hii ya viboko, na kwa kuwa tafiti za elimu zinaonyesha kwamba unaweza kuwa na adhabu mbadala na wanafunzi wakaelewa bila kutumia viboko, na kwa kuwa nchi yetu sasa hivi tunafanya mapitio na maboresho makubwa kuhusu sera, mtaala, sheria na kanuni za elimu. Mheshimiwa Waziri Mkuu huoni ni muda muafaka sasa kuleta muswada wa kufuta kabisa adhabu ya viboko katika shule zetu na kutumia adhabu mbadala?

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota nahisi swali lako linafanana na la Mheshimiwa Olelekaita. Kwa hiyo nafikiri tutasubiri kile alichosema Mheshimia Waziri Mkuu kwamba jambo hilo wanalichukua wakalifanyie kazi kama Serikali halafu waone kama yanaweza kubalika mabadiliko. Mheshimiwa Bahati Ndingo swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Kwenye huo waraka nimeona tumetoa tu adhabu ya viboko, lakini tunatambua watoto wetu wengi ambao wanaonekana ni wakaidi shuleni inatokana kwa sababu wameathirika aidha na makuzi au malezi ya

nyumbani. Kwa nini tusiweke pia nafasi ya watoto hawa kupewa ushauri kabla ya kutanguliza viboko; kwamba, kuwepo na ushauri kabla ya kuadhibiwa kwa viboko kwenye huo waraka? Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ndingo Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwenye maelezo pia niliyoyatoa hapa nimetoa wito kwa walimu wetu wa shule za msingi, sekondari, lakini hii inaenda hata pia kwenye vyuo vya kati na vyuo vya juu; kwamba tuangalie ukubwa wa makosa, umri, mahali na wakati wa makosa yalipofanyika. Nataka tu nitoe taarifa kwamba kwenye taasisi zetu za elimu tuna walezi wa watoto wa kiume na wa watoto wa kike na tumeweka hii walezi kwa lengo la kutoa ushauri pale ambapo tunaona kuna umuhimu wa ushauri. Kazi hii inaendelea shule ya msingi, sekondari na tunatumia zaidi majina ya kingereza *matron* na *patron* ndio ambao wanatumika kutoa ushauri nasaha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo pale ambako mwanafunzi anatenda kosa ambalo linahitaji kushauriwa wanafanya; na ndio hii ndiyo inasaidia kupunguza pia hata mkanganyiko kwenye jamii kutokana na nidhamu za watoto hawa. Hata hivyo bado kwenye taarifa yangu nimeeleza walimu wana kazi nyingi sana wanazozifanya shuleni. Wanatumia muda wao katika kuwafanya watoto kuwajenga katika maadili, pia katika kuwafanya wadumishe mila, desturi na utamaduni tulionao huku pia wakiwapa taaluma mbalimbali. Nimetoa wito pia kwa walezi ambao ndio wana nafasi kubwa ya malezi yam toto huyu kuanzia nyumbani pia hata mwenendo wake

na baadaye nimetoa ushauri kwamba ni vyema wazazi na walezi wakawa wafuatiliaji wa karibu wa mtoto huyu badala ya kuwaachia majukumu hayo waalimu pekee ili wasaidie watoto hawa kubadilisha mwenendo. Mzazi akishiriki tunaamini mtoto huyu atabadilika sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tutaendelea kutumia hizo taaisisi na idara hizo za ushauri ambazo ziko katika kutusaidia pia kurekebisha mwenendo wa mtoto awapo shuleni, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa kumuuliza maswali Mheshimiwa Waziri Mkuu umekwisha, kwa sababu inabidi aulizwe maswali ndani ya nusu saa, na ameshamaliza muda wake. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na ratiba, kwa sababu leo Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa taarifa hiyo kwa mujibu wa hiyo kanuni yetu ya 44; Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu matukio kama haya isingekuwa rahisi sana kuyafahamu kama asingekuwepo mtu ambaye amechukua hayo matukio. Sasa kwa utaratibu ule ule na kwa sababu taarifa huwa tunataka tuzipate za matukio mazuri lakini na mabaya ili tuchukue hatua; kwa muktadha huo yule mtoa taarifa ikiwa hajakosea zile sheria zetu namna ya kuitumia ile taarifa basi alindwe ili tuendelee kuzipata hizo taarifa. Kwa sababu asipolindwa tutakuwa hatupati hizo taarifa.

Ninasema hivyo kwa sababu matukio tunayatazama na huko duniani kwa sababu ukatili huu hauko kwetu tu uko sehemu nyingi na zisipokuwepo taarifa watu husema vitu tofauti. Hivyo tunatamani yule mtoa taarifa kwa

vyovyote vile afuate utaratibu wa kupeleka taarifa zinapotakiwa lakini alindwe. Kwa sababu mtoa taarifa akichukuliwa hatua maana yake watu wataacha kuchukua hayo matukio halafu watoto wataathirika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nafikiri hata watoa taarifa tuwatie moyo ni muhimu isipokuwa wafuate utaratibu wa kuzipeleka taarifa. Wewe chukua ile taarifa halafu zipeleke taarifa pale panapotakiwa ili hatua zichukuliwe kwa wote wanaofanya vitendo vya ukatili katika jamii yetu ikiwa ni pamoja na hayo maeneo ya shule.

Kwa hiyo nimeona nilisisitize hilo kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tunashukuru sana kwa taarifa hiyo muhimu ambayo inapeleka ujumbe kwa jamii, kwamba ni muhimu sana watoto walindwe shuleni na pia nyumbani. Huu mfano unaotolewa wa shuleni ni kwa sababu shuleni wale ni walezi na pia nyumbani wako walezi.

Waheshimiwa Wajumbe, ameuliza hapa Mheshimiwa Mbunge Mheshimiwa Saashisha Mafue, kwamba kuhusu kule nyumbani inakuwaje. Nadhani Serikali ndiyo maana imetengeneza Wizara hasa kwa ajili ya kushughulika na mambo kama hayo.

Kwa hiyo tujitahidi kutoa taarifa hata zile za nyumbani kunakotokea ukatili ili Serikali iweze kuchukua hatua. Kila mmoja awe mlinzi wa mtoto ili ukatili usiwepo dhidi ya watoto wetu. Baada ya kusema hayo tutaendelea.

Katibu!

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali ya kawaida tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu Mbunge wa Singida Mashiriki sasa aulize swali lake.

Na. 37

### Hitaji la Stendi ya Kisasa – Ikungi

**MHE. MIRAJI J. MTATURU** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga stendi ya kisasa Ikungi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ina uhitaji wa stendi ya mabasi yenye ubora itakayowezesha huduma bora za usafiri.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri imekwishalipa fidia ya eneo la ukubwa wa hekari tano kiasi cha shilingi milioni 36 lililopo katika Kijiji

cha Muungano Kata ya Unyahati ili kupisha ujenzi wa stendi hiyo.

Mheshimiwa Spika; katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023, Halmashauri imetenga kiasi cha shilingi milioni 110 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa stendi hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Miraji Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Serikali kwa sababu imekuwa ni kilio cha muda mrefu kupata stendi ya kisasa katika Mji wetu Ikungi. Sasa. ili kujiridhisha, ni hatua gani sasa zimeanza kuchukuliwa katika kuanza ujenzi huu mapema?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa fedha zilizotengwa, kwa maana milioni 110, ni fedha kidogo. Nini mkakati wa kuongeza fedha za kujenga stendi yenye hadhi ili tuweze kuwa na stendi kubwa kwa sababu ni *main road* na inapokea magari mengi yanayoelekea Dar es Salaam na Mwanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna uhitaji wa stendi katika eneo hilo la Ikungi, na tayari shughuli za awali za ujenzi ikiwemo kusafisha eneo lakini pia kufanya

upembuzi imeshaanza kwa ajili ya kuanza ujenzi huo; na tunaamini shilingi milioni 110 itaanza kazi katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, lakini tathmini iliyofanyika inahitaji shilingi milioni 700 ili kukamilisha stendi hii ya Ikungi. Tumeshakubaliana kama Serikali kupitia mapato ya ndani ya halmashauri kila mwaka watatenga shilingi milioni 150 na katika mwaka ujao wa fedha 2023/2024 halmashauri imakwishatenga fedha hiyo kwa ajili ya kuendelea na ujenzi ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simon Songe swali la nyongeza.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais mwaka jana alipotembelea Mji wa Lamadi aliahidi ujenzi wa stendi. Je, ni lini ujenzi huu sasa utaanza ili kuokoa maisha ya watu kwa sababu ya msongamano mkubwa ulioko pale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Simon Songe Lusongekile, Mbunge wa Jimbo la Busega kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Rais Daktari Samia Suluhu Hassan alielekeza mamlaka za Halmashauri ya Busega kuanza mpango wa kujenga stendi katika eneo la Lamadi. Ofisi ya Rais TAMISEMI tumekwishamwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Busega kufanya tathmini na kuandaa makadirio ya gharama kwa ajili ya kuanza ujenzi huo. Kazi hiyo

inaendelea watawasilisha Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa ajili ya hatua zaidi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mwandabila swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongea.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu Mkoa wa Songwe ni Mkoa Mchanga na una uhitaji wa stendi kuu ya mkoa. Serikali imefikia hatua gani katika kuhakikisha ujenzi wa stendi hii unakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikwishatoa maelekezo na utaratibu wa mikoa yote na halmashauri zote ambazo zina uhitaji wa miundombinu ya stendi kuandaa maandiko pamoja na kufanya tathmini ili kuziwasilisha Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa ajili ya kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango ili kuona kama inakidhi vigezo vya kuwa miradi ya kimkakati yatafutiwe fedha lakini kama hayakidhi basi kupitia vyanzo vingine vituo hivyo viweze kujengwa. Kwa hiyo naomba nimwakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inalifanyia kazi suala la stendi ya Mkoa wa Songwe na utekelezaji utafanyika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, swali la nyongeza.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ile stendi ya Musoma Mjini Manispaa kipindi kama hiki cha mvua huwa inabadilika badala kuwa stendi inakuwa sawasawa na zizi, kwa maana tope zinajaa. Kwa kuwa Serikali ilishaahidi kuijenga tangu mwaka 2020 ni lini hiyo stendi itajengwa ili na sisi watu wa Musoma tuweze kuwa na stendi nzuri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mbunge wa Jimbo la Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba stendi ya Manispaa ya Musoma ni mbovu na Serikali imeshachukua hatua kwanza kwa kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Musoma kuandaa tathmini ya mahitaji ya gharama za ujenzi, lakini pia kuanza kutenga fdha kwenye mapato ya ndani kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwakumbusha Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini kwamba kunapohitajika miundombinu muhimu kama hii lazima wafanye tathmini, waanze kutenga fedha za mapato ya ndani asilimia 40 au 60 kwa ajili ya kuanza

ujenzi wa miradi kama hii ili kuondoa changamoto kwa wananchi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato David Chumi, swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mradi wa Miji 45 utakaoboresha miji 45 maarufu kwa jina la *TACTIC,* sehemu mojawapo ni pamoja na ujenzi wa barabara, lakini pia pamoja na ujenzi wa stendi ambazo zitakuwa chanzo cha mapato cha Halmashauri zetu likiwemo pia Jiji la Mbeya. Je, ni lini mradi huo utaanza ili kuwezesha Halmashauri na Miji hiyo kuwa na stendi za uhakika ambazo zitakuwa pia chanzo cha mapato?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Jimbo la Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Miradi ya *TACTIC* imegawanywa katika *phases* tatu. *Tier one, two and three,* lakini *tier one* hatua zinaendelea, *tier two* na *three* pia hatua zinaendelea ili kuhakikisha katika kipindi hicho miradi yote hii inatekelezwa kwa kuboresha barabara, masoko lakini pia na stendi katika miji hiyo 45. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Mafinga pia itatekelezewa mradi huo kama ilivyopangwa kwenye mpango wa *TACTIC*, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru…

**SPIKA:** Samahani Mheshimiwa nitakupa fursa.

Waheshimiwa Wabunge maswali mafupi, nenda moja kwa moja kwenye swali ili uwape na wenzako fursa ya kuuliza swali, usitoe historia kwenye swali. Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Stendi iliyopo katika Wilaya ya Karatu haikidhi vigezo na hasa wakati wa masika inakuwa na changamoto kubwa. Je ni lini Serikali itajenga stendi ya kisasa tukizingatia karatu ni mji mdogo wa kitalii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecilia Paresso Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uhitaji wa stendi katika Halmashauri ya Karatu ni muhimu na ni kweli kwamba kuna uhitaji huo, lakini tumekwishamwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu kufanya tathmini ya gharama, lakini kama gharama ni kubwa juu ya uwezo wa halmashauri, walete kama mradi wa kimkakati, lakini

tunasisitiza halamashauri kutenga fedha za mapato ya ndani kuanza kukarabati stendi hii ya karatu, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo Mbunge wa Nkenge sasa aulize swali lake.

Kabla ya Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Mbunge.

Na. 38

**Barabara ya Kibaoni, Kakunyu hadi Bugango**

**MHE. FLORENT L. KYOMBO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakasimu kwa *TANROADS* Barabara ya Kibaoni, Kakunyu hadi Bugango wakati taratibu za kupandisha hadhi zikiendelea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu, Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Jimbo la Nkenge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kibaoni, Kakunyu hadi Bugango ina sehemu mbili ambazo zinahudumiwa na Wakala mbili za barabara ambazo ni *TANROADS* na *TARURA*. Sehemu ya kwanza ya barabara hiyo inaanzia

Kibaoni hadi Kakunyu yenye urefu wa kilomita 76 ambayo inahudumiwa na *TANROADS* na sehemu ya pili inaanzia Kakunyu hadi Bugango yenye urefu wa kilomita 12.4 ambayo inahudumiwa na *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa mwaka 2022/2023 kupitia *TARURA* imetenga fedha kiasi cha shilingi milioni 200 kwa ajili ya matengezo ya barabara kutoka Kakunyu hadi Bugango yenye urefu wa kilomita 12.4 kwa kiwango cha changarawe.

Aidha, Serikali itaendelea kuhudumia barabara hiyo na kuhakikisha inapitika wakati wote hadi hapo taratibu za kupandishwa hadhi zitakapokamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Florent Kyombo, swali la nyongeza.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini pia niendelee kuipongeza Serikali kwa fedha walizotuletea tulizipokea na barabara inaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeshasema kwamba itaendelea kuihudumia barabara hiyo mpaka itakapopandishwa hadhi, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, ni hatua gani imefikiwa ya barabara hiyo kupandishwa hadhi kutoka *TARURA* kwenda *TANROADS* kwa sababu ina vigezo vyote vinavyostahili?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; je, ni nini mkakati wa Serikali kwa barabara za namna hiyo ambazo zina vigezo na zinaunganisha Nchi ya Tanzania na nchi za jirani ili ziweze kuwekwa katika mkakati wa

kuzipandisha hadhi kutoka *TARURA* kwenda *TANROADS*? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Jimbo la Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara zikishatoka katika ngazi ya *TARURA* ili zipandishwe hadhi zinakwenda Wizara ya Ujenzi ambao ndio wasimamizi wa *TANROADS*. Kwa hiyo, hatua ya sasa zipo huko ambapo wanafanya uchambuzi wa mwisho, wakishamaliza nafikiri watatangaza kwenye Gazeti la Serikali kwa taratibu ambazo zimewekwa.

Mheshimiwa Spika, la pili, mkakati wa Serikali ni kuhakiksha barabara hizo kwanza kwa sasa zinapitika wakati wote na kulingana na mahitaji ya wakati uliopo na wakati ujao, maana yake tutaendelea kuzingatia ili kama zinahitaji kupandishwa hadhi zitafanyika hivyo, kama haitahitajika basi tutaendelea kuzihudumia ili zipitike wakati wote, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Ni lini Serikali itahamisha barabara ya Bashnet – Bassodesh – Hirbadaw - Singida kutoka *TARURA* kwenda *TANROADS* kwa kuwa upande wa kutoka Bassodesh - Hirbadaw ipo *TANROADS* na

Singida ipo *TANROADS* matengenezo yake huwa yako tofauti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Xaday Hhayuma, Mbunge wa Jimbo la Hanang, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nizielekeze tu halmashauri zenye mahitaji hayo zifuate taratibu na utaratibu unaeleweka unaanzia ngazi za halmashauri baadaye zinaenda katika Bodi ya Barabara Mkoa halafu zinapelekwa Wizara ya Ujenzi kwa ajili ya uthibitisho. Kwa hiyo sisi tunapokea tu kama ombi ili hizo taratibu ziweze kufuatwa, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Segerea, sasa aulize swali lake.

Na. 39

**Kuwawekea mazingira mazuri ya kazi walimu katika Jimbo la Segerea**

**MHE. BONNAH L. KAMOLI** aliuliza:-

Je, ni lini adha ya Walimu kukaa chini kwa kukosa Ofisi Shule za Msingi za Maendeleo, Bonyokwa na Kinyerezi *JICA* itatatuliwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Jimbo la Segerea, kama ifuatavyo; -

Mheshimiwa Spika, mwongozo wa kuanzishwa kwa shule yoyote ni pamoja na kuwepo kwa jengo la utawala ambalo litawawezesha Walimu kuwa na chumba maalum cha kufanyia maandalizi kabla ya kufundisha *(staff room)*.

Mheshimiwa Spika, Shule za Msingi Maendeleo, Bonyokwa, Kinyerezi *JICA* na Shule ya Sekondari Kimanga hazina majengo ya utawala ambayo ndio huwa na ofisi ya walimu (*staff room*) hivyo, baadhi ya madarasa ya ziada yamekuwa yakitumika kama ofisi wakati Serikali ikifanya utaratibu wa kujenga ofisi.

Mhesmiwa Spika, ili kutatua changamoto ya Ofisi za Walimu katika Jiji la Dar es Salaam, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumeielekeza Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya utawala katika shule hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bonnah Kamoli, swali la nyongeza.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, kuna pesa ambazo zinakuja sasa hivi kwa ajili ya ujenzi wa madarasa. Swali la kwanza; je, ni kwa nini Serikali wakati inaleta hizo pesa ilete pamoja na hizo pesa za kujenga Ofisi za Walimu kwa

sababu kumekuwa kuna tofauti kubwa kati ya madarasa ambayo yanakuja kujengwa lakini Walimu wanakuwaqa hawana ofisi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je ni lini Serikali itanunua *furniture* za ofisi ambazo zimejengwa na manispaa zipo tu na hazina *furniture* za walimu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Jimbo la Segerea kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkakati wa sasa wa Serikali ni kujenga na kuongeza madarasa katika maeneo ambayo yana uhitaji na ndio maana katika miradi mikubwa ambayo tunayo sasa kwa maana Mradi wa *SEQUIP* pamoja na *BOOST* yote miwili kwa pamoja ina thamani karibU trilioni 2.35.

Mheshimiwa Spika, katika yale madarasa maeneo mengine wanajiongeza, ukipeleka madarasa mawili wanajenga na ofisi katikati ambalo ni jambo jema. Tumekuwa tukipeleka fedha kwa ajili ya majengo ya utawala. Kwa hiyo sisi tutaendelea tu kuziagiza halmashauri kutenga fedha kujenga maeneo ya utawala, lakini ofisi nyingine waendelee kujiongeza kwa kuweka ofisi katikati ya madarasa ambayo tumekuwa tukiyapeleka huko. Kuhusu fanicha nafikiri ni maelekezo yetu pia kwa halmashauri zote nchini kuwapatia *furniture* kwenye *staff rooms* zote za shule katika maeneo yao, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kuishukuru Serikali kwamba katika Mkoa wa Simiyu tuna madarasa mengi sana, lakini kuna upungufu wa Ofisi za Walimu. Walimu wetu hawafanyi kazi kwa furaha kwa sababu hawana ofisi wengi wanakaa kwenye miti. Je, ni nini kauli ya Serikali kuhusu ujenzi wa Ofisi za Walimu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Minza Mjika, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Mkoa wa Simiyu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumeziagiza halmashauri kujenga ofisi kwa kila halmashauri kutenga mapato yao ya ndani kwa sababu moja ya jukumu letu sasa ni kujenga madarasa, mabweni, mabwalo ya chakula ambayo ndio kazi kubwa tunayoifanya sasa ikiwemo na majengo ya utawala kwa baadhi ya shule. Kwa hiyo kwa kadri tutakavyokuwa tunatafuta fedha tutakuwa tunapeleka, lakini tumeziagiza halmashauri kutumia mapato yao ya ndani kufanya hivyo. Kwa hiyo tunafanya hivyo kwa Mkoa wa Simiyu na mikoa yote nchini, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Walimu wengi wanakosa viti na meza nzuri

za kukaa na kuweza kufanya kazi zao vizuri. je, Serikali inalijua hilo na ina mkakati gani wa kulitatua? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza umeuliza maswali mawili. Mheshimiwa Naibu Waziri unaweza kujibu moja. Je Serikali mnalifahamu hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mtwara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunatambua changamoto hizo katika baadhi ya shule na tunazifanyia kazi,, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay Mbunge wa Mbulu Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 40

**Utekelezaji wa Miradi ya *TACTIC***

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza:-

Je ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Soko, Stendi, Dampo na Machinjio na barabara kilomita 12 za lami kupitia *TACTIC* katika Mji wa Mbulu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay Mbunge wa Jimbo la Mbulu Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mji wa Mbulu ipo kwenye kundi la tatu lenye miji 18 ambayo utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa stendi kuu ya mabasi, soko jipya na barabara kwa kiwango cha lami unatarajiwa kuanza mwaka huu wa fedha 2022/2023 kwa kuandaa mipango kabambe *(master plans)*.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeanza kupokea taarifa za hatua mbalimbali za utambuzi wa mipaka ya kila mji pamoja na taarifa nyingine kwa ajili ya kuandaa hadidu za rejea ili kuwapata Washauri waliobobea katika kuandaa mipango kabambe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha maandalizi ya mipango kabambe, kazi ya usanifu kwa halmashauri za kundi hili utaanza mwaka ujao wa fedha 2023/2024 na kazi za ujenzi zinategemea kuanza katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, Halmashauri ya Mji wa Mbulu iliko soko na stendi ni mahali pamoja kwenye kiwanja kimoja hali inayohatarisha watumiaji wa huduma na wapokea huduma katika eneo hilo.

Swali la kwanza; je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu mkubwa wa Halmashauri ya Mji wa Mbulu kusogezwa kwenye kundi la pili?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa tatizo hili ni kubwa na tumesubiri mradi huu kwa muda mrefu, Mheshimiwa Waziri ana kauli gani ya kuweza kufika Mbulu na wataalam wa TAMISEMI ili waone tatizo lenyewe kwa undani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini , kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kikubwa ni kwamba makundi yote matatu yatapatiwa hizo fedha za *TACTIC* na miradi yote iliyoainishwa itajengwa. Jukumu kubwa tunalolifanya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa sasa ni kuhakikisha miradi hii inatekelezeka kama ambavyo imepangwa katika mkakati tulionao. Niwahakikishie tu hata wale wa *tier one* kwa maana ya kundi la kwanza, miradi yao inaanza kutekelezeka katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi kuchelewa, niko tayari kwenda Mbulu pamoja na wataalam kwenda kujionea haya ambayo Mheshimiwa Mbunge anayazungumza, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sebastian Kapufi, swali la nyongeza.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Je, ni lini Serikali itakamilisha kwa maana ya Mradi huu wa *TACTIC* kilometa 15 Mji wa Mpanda, Soko la Kazima na kilomita 29 kutoka Mwankulu mpaka Mpanda?

**SPIKA:** Mheshimiwa ni swali moja la nyongeza, kwa hiyo hilo la pili halipo. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Sebastian Kapufi Mbunge wa Jimbo la Mpanda Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Manispaa ya Mpanda ipo katika kundi la pili ambalo kwa sasa mwezi wa Pili huu tulioanza zabuni za kutafuta wataalam washauri zinaanza na utekelezaji wa miradi hiyo kwa wenzetu watu wa Mpanda utaanza mwakani mwezi Aprili, 2024. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Swali la nyongeza.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mradi wa *TACTIC* pia upo kwenye Jimbo la Arusha Mjini na mnategemea kujenga stendi ya kisasa *Bondeni City* na lami maeneo ya Engosheraton na Olasiti na kwa kuwa mradi huu ulitegemea kuanza toka Julai, 2022. Je, ni nini changamoto inayochelewesha mradi huu kuanza kwa wakati maana miezi saba imeshapita mpaka sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mrisho Gambo, Mbunge wa Jimbo la Arusha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tulichelewa kidogo kwa sababu ya zile taratibu ambazo tulipaswa kuzifuata, lakini mpaka sasa tuko katika hatua nzuri. Kwa mfano, Jiji la Arusha lipo katika kundi la kwanza ambalo mwezi Februari, mwezi huu ambao tuko sasa, Serikali inatangaza kuwapata Wakandarasi watakaoanza kutekeleza na tunatarajia mchakato huu utakamilika mwezi Aprili na wakandarasi watakuwa *site* kujenga. Kwa hiyo, nimhakikishie Mbunge kwamba utekelezaji katika kundi la kwanza unaanza mwaka huu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pia namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa sababu ameshajibu swali nililokusudia kuliuliza kuhusu lini *TACTIC* itaanza kutangazwa na kuleta ujenzi wa makusudio. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Jerry William Slaa, swali la nyongeza.

**MHE. JERRY W. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Barabara ya Banana – Kitunda – Kivule - Msongola inayoenda hospitali ya wilaya kilometa 11.7 ina hali mbaya sana.

Je, Waziri na nimemwona Waziri mwenye dhamana yupo atakuwa tayari baada ya Bunge hili kuambatana na mimi kwenda kutoa majibu ya Serikali, lini barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Slaa aliyesimama hapa ni Naibu Waziri na mimi sijamwona Waziri. Sawa, Waziri naye amesimama. Haya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jerry Slaa kuhusiana na barabara ya kilometa 11 ya kutoka Banana kwenda Msongola na nimhakikishie kwamba mwezi huu wa Februari tutakapomaliza Bunge atakapokuwa tayari tutaongozana naye kwenda kuangalia barabara hiyo na kuitekeleza, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 41

**Kuwanusuru wananchi wa Mtwara dhidi ya vumbi la Makaa ya Mawe**

**MH. ANASTAZIA J. WAMBURA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwanusuru wananchi wa Manispaa ya Mtwara dhidi ya vumbi la makaa ya mawe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamza Hamza, majibu

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imeshachukua jitihada za kuweka miundombinu ya kupunguza vumbi la makaa ya mawe ili kuwanusuru wananchi. Tayari Mamlaka ya Bandari Tanzania imefunga mfumo maalum wa *dust suppression system* unaotumia maji kupunguza vumbi. Pia, limetengwa eneo maalum kwa ajili ya kujenga *conveyor belt* itakayotumika kupakia makaa ya mawe katika meli. Aidha limetengwa eneo maalum nje ya mji takribani kilometa 34 katika Kijiji cha Kisiwa Mgwao kutoka Mtwara Mjini kwa ajili ya kuhifadhi mizigo ya namna hiyo. Hatua hii itasaidia kupunguza, kusambaa kwa vumbi katika mazingira.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia *NEMC*, kwa kushirikiana na Manispaa ya Mtwara na Mamlaka ya Bandari Tanzania *(TPA)*, kwa pamoja tunaendelea kufuatilia na kusimamia usafirishaji wa makaa ya mawe ili waweze kuzingatia taratibu za

uhifadhi wa mazingira katika maeneo hayo, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Anastazia Wambura, swali la nyongeza.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hii *dust suppression system* inapunguza vumbi kwa kiasu kidogo sana, lakini pia ukienda bandarini pale utakuta maji yameshakuwa meusi kutokana na hili vumbi. Swali langu la kwanza: Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inatunza au inalinda vyanzo vya maji ili kusudi visiweze kuathirika kutokana na yale maji ya mvua yanayotiririka ambayo tayari yameshakuwa na vumbi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili: Je, Serikali itakuwa tayari kupokea ushauri kwamba haya makaa ya mawe kutoka kwenye migodi yawe yakisafirishwa yakiwa yamefungwa kwenye vifungashio, kwa mfano, labda viroba au maboksi ili kusudi kuzuia lile vumbi lisitimke wakati wa usafirishaji, wakati wa kushusha mzigo na vile vile wakati wa kupakia mzigo katika meli? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba swali la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Mkoa wa Mtwara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usimamizi na Utunzaji wa Vyanzo vya Maji imewaelekeza watu wote, makampuni, taasisi zote zinazofanya shughuli zote ambazo zitakuwa zinagusia sehemu zenye maji au vyanzo vya maji; tumeshawaelekeza pamoja na hawa wa Mtwara wanaofanya biashara hiyo. Kwanza tumewaelekeza kwa kuwapa taaluma, lengo na madhumuni, watunze vyanzo vya maji. Pia tumekuwa tunasimamia sheria kwa kushirikiana na wenzetu wa *NEMC,* watu wa Halmashauri na wengine. Lengo na madhumuni ni watu watunze vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, pia tumeshakaa nao kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunachukua hatua mbalimbali, na tayari zipo hatua ambazo *NEMC* wamezichukua kwa baadhi ya watu hawa. Hapa nataka nitoe wito kwa Watanzania wote wanaofanya shughuli za kibinadamu karibu na vyanzo vya maji, wahakikishe kwamba wanatunza vyanzo vya maji. Kinyume na hapo, sheria na taratibu zitakuwa zinachukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili, tupo tayari, tumepokea huo ushauri. Ingawa makaa ya mawe haya yanakuwa ni mawe makubwa, lakini tutajua namna ya kuwashauri wafanyabiashara wawe wanaweka katika *package* maalum ili yaweze kupunguza hilo vumbi ambalo linaweza kuathiri afya za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE**: Mheshimiwa Spika, ahsante. Suala la makaa ya mawe kutoka Ngaka kupita Songea –

Tunduru mpaka Mtwara kuna baadhi ya madereva wamekuwa na tabia ya kusambaza yale makaa ya mawe barabarani, aidha kwa magari kuanguka au kwa kutokufunika. Hii imekuwa ni hatari sana kwa wananchi wanaokaa karibu na barabara hizi. Je, Serikali iatoa kauli gani kwa hawa madereva wanaofanya tabia hii ya kusambaza makaa ya mawe barabarani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Daimu Mpakate, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hii ni changamoto, tumeiona na mara kadhaa tumekuwa tukikaa na wafanyabiashara hawa pamoja na vyombo vingine au taasisi nyingine zinazohusika ili kuwaeleza hawa wafanyabiashara kwamba wasiyatawanye ama wasiyaweke makaa ya mawe haya katika maeneo tofauti, bali wawe na vituo maalum vya kuweka ili kuepusha athari zinazojitokeza zikiwemo hizo za uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kutoa taaluma na kuwaambia wananchi wasiyasambaze haya mwisho wa siku yakawa yanaleta athari. Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Felista Njau, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Katika Kata ya Wazo, Mkoa wa Dar es Salaam, kuna kiwanda cha Twiga *cement* ambacho kinatiririsha

vumbi jingi kuelekea kwa makazi ya wananchi: Nini mkakati wa Serikali kuwanusuru wananchi hawa kuhakikisha hawapati athari za kiafya? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la moja la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Felista Njau, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hili jambo tumekuwa tunalipigia kelele sana na hasa hivi viwanda ambavyo vipo karibu na makazi ya wananchi. Tumekuwa tunalisemea sana na tumeshachukua hatua nyingi za kinidhamu lakini pamoja na hayo. tumeshakuwa tunakaa na wamaliki wa viwanda hivi na pia tumekuwa tunawapa taaluma.

Mheshimiwa Spika, nimwambie tu Mheshimiwa kwamba jambo hili tunaendelea kulifanyia kazi ili tuhakikishe kwamba wananchi wanaendelea kuwa salama kutokana na hizi adha na changamoto za viwanda ambazo zinaweza zikawaathiri wananchi kwa njia moja ama nyingine, nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Suleiman Haroub Suleiman, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 42

**Taasisi za Zanzibar na Muungano kushirikiana**

**MHE. SULEIMAN HAROUB SULEIMAN** aliuliza:-

Je, ni kwa kiasi gani Taasisi za Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zinashirikiana katika shughuli za kiuchumi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Haroub Suleiman, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Taasisi za *SMT* na *SMZ* zina ushirikiano wa kuridhisha katika shughuli za kiuchumi ambapo kupitia miradi na *program* mbalimbali, taasisi zetu za *SMT* na *SMZ* zimekuwa zikishirikiana katika shughuli za kiuchumi hasa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Mzunguko wa Pili, mradi wa kuongeza tija na uzalishaji wa zao la mpunga; mradi wa udhibiti uvuvi na maendeleo shirikishi Kusini Magharibi ya Bahari ya Hindi; mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabia nchi kwa kutumia mifumo ikolojia vijijini; Mkakati wa Kudhibiti Sumu Kuvu Tanzania; na Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Suleiman Suleiman, swali la nyongeza.

**MHE. SULEIMAN HAROUB SULEIMAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, pamoja na majawabu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni lini miradi ambayo inahusiana na mabadiliko ya tabia nchi iliyopo Zanzibar *SMT* wataimaliza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, Zanzibar inashirikishwa vipi kwenye mikutano ya Kimataifa hasa inayohusu masuala ya tabia ya nchi? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman, Mbunge Mwakilishi kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ipo miradi mingi ambayo inatekelezwa ama inasimamaiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na inatekelezwa Zanzibar. Kuna miradi ile ambayo inasimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais lakini kuna miradi inayosimiamiwa na *NEMC*. Kwa mfano, kuna Mradi wa *Adaptation Fund* ambayo ipo Zanzibar na imetekelezwa maeneo tofauti. Hii tayari imeshakamilika na wananchi wameshaanza kunufaika na miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia kuna miradi ya *EBA* ambayo hivi karibuni kama mnakumbuka tuliwahi kukabidhi boti za uvuvi Tumbatu na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, lengo na madhumuni Serikali ya Jamhuri ya Tanzania inaunga mkono juhudi za Uchumi wa Bluu kwa upande wa Zanzibar na suala nzima la uhifadhi na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna miradi ya *LSDF*. Hii ni miradi ambayo imekuja kwa ajili ya kukuza kilimo, kuboresha ardhi iliyoathirika na athari za mabadiliko ya

tabia nchi. Pia kuna miradi ambayo haijakamilika; hii tumeshatoa maelekezo kwamba ndani ya mwezi huu ianze. Ni mradi wa uchimbaji wa bwawa la maji uliopo Bumbwini Makoba. Tumesema ndani ya mwezi huu uanze na utaanza kwa ajili ya kunufaisha wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili…

**SPIKA:** Kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, Zanzibar inapata ushirikiano mkubwa kushirikishwa kutoka Serikali ya Jamhuri katika vikao vinavyohusina na mazingira katika mambo ya Kimataifa. Hivi karibuni tulikuwa tuna kikao cha *COP27* Mkutano wa Kimataifa ambapo Zanzibar tulishiriki. Tanzania tulishiriki lakini Zanzibar walileta *delegation* yao, tulikuwa na Mkurugenzi wa Mazingira na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha kuonesha kwamba tunao ushirikiano wa karibu baina ya Serikali mbili hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 43

**Mkakati wa kupunguza gharama za gesi nchini**

**MHE. NORAH W. MZERU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza gharama ya gesi ili kuepuka matumizi ya mkaa na kuni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa January Makamba majibu.

**WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania hatuzalishi gesi iliyosindikwa kiwandani *(LPG)* ambayo pia hutumika kama nishati ya kupikia. Gesi ya *LPG* huagizwa kutoka nchi za nje. Kama ilivyo kwa bidhaa nyingine zinazotokana na mafuta ya petroli, gharama za *LPG* pia hutegemea bei katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuhamasisha na kushirikiana na sekta binafsi kuwekeza katika miundombinu ya kupokea na kuhifadhi *LPG* ili kuwa na uwezo mkubwa zaidi ya tani 16,000 za sasa. Hii itatuwezesha kuanza kuagiza *LPG* kwa mfumo wa uagizaji wa pamoja na hivyo kupungua kwa gharama za uagizaji na kupata nafuu katika gharama ya gesi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali kupitia *TPDC* imetenga fedha Shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kusambaza gesi asilia ambayo ipo hapa nchini na kuwaunganisha wateja kwa maeneo yaliyopitiwa na mradi wa Bomba la Gesi Asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo kupikia. Gesi hiyo

inayotumika kwa kupikia ni nafuu kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na vyanzo vingine vyanzo vingine vya nishati ya kupikia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Norah Mzeru, swali la nyongeza.

**MHE. NORAH W. MZERU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina swali langu la nyongeza, Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Watanzania wa hali ya chini wanapata elimu ya madhara ya kutumia nishati chafu ya kupikia na kuona umuhimu wa kutumia nishati safi ya kupikia? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Wizara ya Nishati ya Mwaka huu wa Fedha, tulieleza moja ya kipaumbele kikubwa ni kuhakiksha kwamba nishati safi na salama ya kupikia inawafikia Watanzania walio wengi. Katika jitihada hizo, elimu kwa Watanzania kuhusu madhara ya nishati chafu ni jambo la muhimu. Itakumbukwa kwamba tarehe 01 Novemba mwaka uliopita Mheshimiwa Rais alizindua mjadala wa Kitaifa wa nishati safi ya kupikia na alitoa maelekezo mahusus ikiwemo ya mjadala ule kuendelea katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyozungumza, Serikali inaandaa dira ya kuelekea katika nishati safi ya kupikia, dira ambayo itajumuisha elimu kwa umma, elimu ambayo itawafikia Watanzania wote kila mahali walipo. Kwa hiyo, tutazindua dira hiyo mwezi Juni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa gharama kubwa huongezeka kutokana kwamba waagizaji wa gesi hufanya binafsi binafsi, kwa maana hakuna *bulk procurement:* Je, ni mpango gani wa muda mfupi kuhakikisha *bulk procurement* inaanza kufanya kazi ili kupunguza na kudhibiti gharama ya gesi inayopanda holela? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyozungumza kwenye jibu la msingi, uagizaji mkubwa na uwezo mkubwa wa kuhifadhi na miundombinu ya kupakua na kuhifadhi gesi kwa wingi inasaidia kushusha gharama. Ndiyo maana Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imeingia makubaliano ya kuongeza uwezo wa Bandari ya Dar es Salaam kushusha, kupokea na kuhifadhi gesi kwa wingi. Kwa hiyo, Serikali iko mbioni kutekeleza mpango huo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Kwa kuwa kwa kupunguza bei na matumizi ya mkaa mpango mmojawapo ni kutumia gesi asilia: Je, mna mkakati gani

wa kuwaingizia majumbani gesi asilia wananchi wa Mkoa wa Morogoro? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, gesi asilia inatoka Mtwara mpaka Dar es Salaam kwa bomba na uwekezaji ule ni wa gharama kubwa kutona na gharama kubwa za ujenzi wa miundombinu ya bomba. Tunaamini kwamba kwa wakati huu mfupi wa sasa, miundombinu ya kujenga bomba la gesi asilia kutoka Dar es Salaam - Morogoro mpaka Dodoma ni mpango wa muda mrefu. Imani yetu ni kwamba tutashirikiana na sekta binafsi kujenga vituo vidogo, vinaitwa 'vituo dada' ambavyo vitachukua gesi iliyogandamizwa kutoka Dar es Salaam na kuisambaza katika vituo mbali mbali nchini na baada ya hapo itasambazwa kutokea katika vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, tumeshapokea mpango wa uwekezaji wa jambo hilo na tutautangaza pale tutakapokuwa tumefikia makubaliano na sekta binafsi ya kupeleka gesi hii katika maeneo ambayo ni mbali na Dar es Salaam ambapo bomba halijafika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji; Mheshimiwa Abdala Jafari Chaurembo, Mbunge wa Mbagala, sasa aulize swali lake.

Na. 44

**Usambazaji Maji katika Jimbo la Mbagala**

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO** aliuliza:-

Je, lini maji yatasambazwa Toangoma, Chamazi, Mianzini, Kilungule, Kiburugwa, Kijichi, Mbagala, Charambe, Kibondemaji na Mbagala Kuu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Mbagala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata za Toangoma, Chamazi Mianzini, Kilungule, Kiburugwa, Kijichi, Mbagala, Charambe, Kibondemaji na Mbagala Kuu zinapata huduma ya majisafi na salama kupitia vyanzo vya maji ya visima virefu na vifupi. Changamoto iliyopo katika kata hizo ni kuwa baadhi ya maeneo hayajafikiwa na mtandao wa maji.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kutumia vyanzo vya visima vya Kimbiji kwa ajili ya kumaliza tatizo la maji katika kata hizo. Kwa sasa, taratibu za kumpata mkandarasi zinaendelea na ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2023/2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Wizara inafahamu kwamba baadhi ya maeneo mtandao wa maji haujafika; je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapatia maji wananchi hawa kwa dharaura?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, Naibu Waziri yupo tayari kuongozana nami kwenda kuona adha kubwa wananchi wa kata hizi wanazopata katika kukosa maji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali yake mawili, Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkakati wa dharura, mara zote *DAWASA* imekuwa ikijitahidi kuona inafanya kila linalowezekana wananchi wasikose maji kabisa, lakini nawaomba uvumilivu kwa sababu visima tisa ambavyo tunatarajia kuja kuvichimba katika maeneo yale ya Kimbiji; na tutajenga tenki kubwa maeneo ya Lugwadu la Shilingi milioni 15. Haya matatizo yatakoma kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi jitihada ndogo ndogo zinazoendelea kufanywa na *DAWASA,* naomba tuendelee kuwavumilia. Kuongozana nawe ni sehemu ya majukumu yangu, hakuna neno, tutakwenda kufanya kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Furaha Matondo, swali la nyongeza.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Jiji la Mwanza hususan Manispaa ya Ilemela inakabiliwa na tatizo la maji. Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua visima virefu vya maji ambavyo havifanyi kazi kwa muda mrefu; mfano, Nsumba Kata ya Kiseke, Mtongo Kata ya Kayenze, Lugeye Kata ya Sangabuye na Kisami Kata ya Bugogwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Furaha Matondo, Mbunge Viti Maalum Mwanza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli maeneo haya aliyoyataja hususani eneo hili la Jimbo la Ilemela kwa Mheshimiwa dada yangu Angelina Mabula tayari tumeanza kazi ya ufufuaji wa visima. Tayari visima viwili vimeweza kufufuliwa na kazi zinaendelea kuhakikisha visima vyote ambavyo bado vina maji ya kutosha tunakwenda kuvifufua.

**SPIKA:** Niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge, tena maswali mafupi, Mheshimiwa Zaituni Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii, katika mradi mkubwa wa maji wa shilingi bilioni 520 wa Mkoa wa Arusha kuna baadhi ya kata ya wilaya ambazo mradi huu unapita lakini maji hayajasambazwa katika Wilaya ya Arumeru na Arusha Mjini.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kusambaza maji kwenye maeneo haya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zaytun Swai, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi huu ni mkubwa na umetumia fedha nyingi na tunatarajia tija iwe ni kubwa maeneo yote ambayo mradi unapita lazima maji yatawafikia. Naomba niwe nimelipokea na kuhakikisha nalifuatilia kwa karibu maji yaweze kuwafikia kwa haraka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, siko mbali sana na swali alilouliza mtu wa Mbagala kwa sababu kata ulizozitaja ndiyo mtandao huo huo wa Kata ya Buza, Makangarawe, Sandali na Vituka. Tunaomba na sisi maji haya yaweze kusambazwa kule kwetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba niseme nimepopkea, maji yatafika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masache Kasaka swali la nyongeza.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona. Mradi wa maji wa Matwiga

*phase one* ni wa muda mrefu na unakwenda kwa kusuasua. Je, ni lini Serikali sasa itaukamilisha mradi huu ili wananchi wa Kipembawe waweze kunufaika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Masache Kasaka, Mbunge wa Lupa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi huu unafanyiwa kazi kwa jitihada kubwa sana, Mheshimiwa Mbunge naomba uendelee kuwa na subira kidogo, mambo mazuri yanafika pale.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, Wilaya ya Makete mlitupatia shilingi bilioni 1.7 za mradi wa maji kutoka Lumage kwenda Madihani na kutoka Usalimwani kwenda Mfumbi, mkandarasi hajafika hadi leo.

Ni ipi kauli ya Serikali dhidi ya mkandarasi huyu ambaye anaigharimu Serikali hadi sasa kwenye suala la maji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Festo Sanga, Mbunge wa Makete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara tulishatoa tamko kwa wakandarasi wote ambao watataka kuturudisha

nyuma watarudi wao. Mheshimiwa Mbunge nafuatilia mkandarasi huyu sababu zilizompelekea kutofika, mimi na wewe naomba tukutane baada ya Bunge hili tuweze kufanyia kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia Mtamba swali la nyongeza.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Katika maeneo yenye changamoto kubwa sana ya maji ikiwemo ni Jimbo la Mtwara Vijijini, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inaondoa kero hii ya maji katika Jimbo la Mtwara Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Shamsia, Mbunge wa Mtwara Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge naamini unafahamu jitihada ambazo zinafanywa na Wizara katika eneo lako na tumeshaongea mara nyingi, Mheshimiwa Mbunge naomba tuendelee kuwasiliana kama unavyofanya tutakuja kuhakikisha maji yanafika maeneo yote ambayo tayari miradi inaendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, kuna utekelezaji wa maji katika miji 28, ningependa kufahamu ni jambo gani linakwamisha uwezeshaji wa utekelezaji wa mradi huu hadi hivi sasa haujaanza katika miji 28?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Yahya Mhata kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa miji 28 kimacho unaweza ukaona haujaanza lakini tayari wakandarasi walifika maeneo yote na tayari wanaendelea kufanya kazi ambazo siyo za *site* lakini kuanzia Februari hii tunatarajia wakandarasi wengi kuja kuanza kuwaona huko kwenye *site* na kufanya kazi zile zinazoonekana kwa macho moja kwa moja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Jimbo la Kigoma Kusini vipo vijiji vilivyopakana kabisa na Ziwa Tanganyika lakini vijiji hivyo havijapatiwa maji. Ni mpango upi wa Serikali kuvipatia vijiji hivyo vinavyopakana na Ziwa Tanganyika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo haya anayoyatamka Mheshimiwa Mbunge tayari jitihada zinafanyika na sisi kama Wizara tunatamani kuona tunatumia vyanzo vya uhakika kwa miradi yetu kwa hiyo vijiji hivi ambavyo viko pembezoni mwa Ziwa Tanganyika navyo ni sehemu ya

maeneo ambayo tunaendelea kuyawekea mkakati wa kupata maji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Katani Katani, swali la nyongeza.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, Vijiji vya Kata ya Mkundi, Nanyanga pamoja na Mchichira, Wizara ilileta mitambo ya kuchimba maji na maji yakapatikana lakini mpaka leo wananchi wale hawajaanza kuyatumia maji yale. Je, ni upi mpango wa Serikali kuhakikisha inaleta vitu ili wananchi waweze kutumia maji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Katani Katani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuchimba kisima ni hatua moja, baada ya hapo tunakuja sasa kwenye usambazaji. Hivi punde tutajitahidi kuhakikisha visima hivi vilivyochimbwa siyo tu kwenye eneo lako hata pale Mtwara mjini tuna visima tulishachimba na sasa tunaelekea sasa kwenye utekelezaji wa usambazaji Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na jitihada kubwa ambayo Serikali imefanya ya kutupa mkandarasi Palemon kwa ajili ya maji katika Kijiji cha Puulu, Songambele na Ngee. Mkandarasi huyu ana zaidi ya miezi mitano toka alipoonyeshwa mradi hajaonekana kabisa, wananchi

wanalalamika, nini kauli ya Serikali kuhusu mkandarasi huyu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mbunge wa Nyasa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia Bunge lako Tukufu kusema wakandarasi wote ambao hawajafika kwenye maeneo ya kazi wafike mara moja kadiri ya mikataba yao inavyowataka. Nje ya hapo sisi kama Wizara tutachukua nafasi yetu na wasije wakatulaumu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Kinondoni sasa aulize swali lake.

Na. 45

**Kusimama kwa ujenzi wa baadhi ya majengo Dar es Salaam**

**MHE. TARIMBA G. ABBAS** aliuliza:-

Je, nini kauli ya Serikali kuhusu majengo yaliyopo maeneo ya Mkoa wa Dar es Salaam ambayo ujenzi wake umesimama kwa muda mrefu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali namba 45 lililoulizwa na Mheshimiwa Tarimba Abbas Mbunge wa Kinondoni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya Serikali ni kwamba majengo yote yaliyosimama yaendelezwe kwa kikamilifu kama ilivyoainishwa kwenye milki zao na vibali vya ujenzi ili majengo hayo yasitumike kwa matumizi yasiyofaa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, swali la nyongeza.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nimepokea majibu ya Serikali lakini sheria ilivyo sasa inaelekeza kwamba ujenzi au uendelezaji uanze ndani ya miaka mitatu lakini sheria hiyo haitoi ukomo ni lini majengo hayo yamalizike kujengwa. Je, Serikali haioni sasa ni wakati wa kuleta sheria ambayo itaweka ukomo katika uendelezaji wa majengo na wale ambao watakaidi waweze kupata adhabu kwa kuchelewesha ujenzi?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pil, ni nini kauli ya Serikali hasa katika uendelezaji wa majengo ya miradi ya taasisi za umma kama vile *NSSF, PSSSF* na *National Housing* ikiwemo suala la majengo yale ambayo yametelekezwa kama vile *Hotel Embassy, Motel Ajib* kule Dar es Salaam na mengineyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tarimba Abbas kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na sheria inazungumza vipi juu ya yale majengo ambayo hayajaendelezwa; kwanza nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ndani ya sheria ya Ardhi inayohusu uendelezaji, inamtaka muendelezaji au mtu anayepewa milki aendeleze ndani ya miaka mitatu, ni kweli lakini wako baadhi ya watu wamekuwa wanafanya kazi ya kuanzisha ujenzi ndani ya miaka mitatu na kwa sababu sheria hiyo imetoa ombwe katika lini anatakiwa amalize.

Mheshimiwa Spika, ushauri wako ulioutoa tunauchukua Mheshimiwa Mbunge na ndani ya Wizara tumeendelea kufanyia kazi na itakapofika punde tutakuja kuwasilisha mbele ya Bunge lako ili Waheshimiwa Wabunge, wapate kujua sasa ni kipande gani au mwaka gani mtu anatakiwa kumaliza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, juu ya Serikali inaendelezaje majengo yaliyosimama, maelekezo ya Serikali ni kwamba majengo yote ambayo hayajaendelezwa yaendelezwe ili yaweze kukamilika yasije yakatumika kwa matumizi yasiyofaa. Juu ya Shirika la *National Housing,* hasa *in particular,* Serikali imekwishaelekeza juu ya shirika hilo liweze kukopa na mwanzo lilikopa shilingi bilioni 44.7 kwa ajili ya uendelezaji na sasa tupo katika mazungumzo na wenzetu wa Hazina ili tuweze kukopa katika kipande kilichobakia ili tuweze kumalizia sehemu iliyobakia katika majengo mengine.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk, Mbunge wa Tumbe sasa aulize swali lake.

Na. 46

**Kuboresha Jengo la Kituo cha Polisi Konde**

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaboresha jengo la Kituo cha Polisi Konde, Wilaya ya Micheweni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk Mbunge wa Tumbe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uchakavu wa jengo la Kituo cha Polisi cha Konde kilichopo Wilaya ya Micheweni. Tathmini ya uchakavu ili kufanya ukarabati imefanyika mwezi Novemba, 2022 na kiasi cha fedha shilingi 92,000,000 zinahitajika kwa ajili ya ukarabati huo. Fedha hizo zitatengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk, swali la nyongeza.

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nina swali moja la nyongeza; kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, yupo tayari baada ya Bunge hili kwenda kukitembelea kituo hicho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kwamba niko tayari ratiba itakavyoruhusu tutatembelea eneo hilo ili kuona kiwango cha uchakavu hicho kilichofikiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ussi Pondeza, swali la nyongeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza. Ningependa nimuulize Mheshimiwa Waziri, nimekuwa nikisimama mara nyingi kuhusu matatizo ya vituo vyangu vya Chumbuni. Je, sasa nataka kauli yake, yuko tayari kuongozana na mimi mpaka kwenye jimbo langu kutokana na uhalifu umekuwa ukiongezeka na zaidi ya mara sita nimekuwa nikiuliza bila kupata majibu sahihi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Pondeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishasema, tutakapokuwa tunakwenda kwa Mheshimiwa Amour kwa sababu kote ni Zanzibar niko tayari pia kupita kwenye jimbo lake ili kuona kiwango cha uhalifu anachozungumza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janeth Mahawanga, swali la nyongeza.

**MHE. JANET E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kufuatia changamoto ya Mkoa wa Dar es Salaam maeneo mengi kukosa vituo vidogo vya polisi hususan kata ya Makongo ambayo Serikali ilishaahidi kukamilisha ujenzi huo. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Janet kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali kwa nyakati tofauti ilishasema iko tayari kushirikiana na mamlaka za Serikali za Mitaa na Waheshimiwa Wabunge kukamilisha vituo vya polisi vilivyojengwa kwa nguvu za wananchi. Sasa kupitia Bunge lako tukufu nimuombe Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, labda niseme *IGP,* kubaini vituo vyote vya Dar es Salaam ambavyo viko njiani havijakamilika kufanya tathmini ya kiwango cha ukamilifu unaohitajika ili viweze kutengewa fedha za kukamilisha vituo hivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sylvia Sigula, swali la nyongeza.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza, Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kibondo hakina hadhi ya kituo cha wilaya maana ni kidogo sana lakini pia ni chakavu mno. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kituo hicho ili kiwe na hadhi ya wilaya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunafahamu kituo cha Kibondo ni kidogo kwa *size* lakini pia ni chakavu kinahitaji kufanyiwa ukarabati. Nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kupitia Jeshi la Polisi mpango wa kukarabati kituo hicho kimewekwa katika Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2023/2024 kwa hiyo ukae kwa subira kwamba mwaka ujao tukipitisha bajeti hapa kituo hicho pia kitakuwa kimezingatiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi Kengeja ambacho kipo Mkoani Pemba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maryam Mwinyi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kituo hiki cha Kengeja kipo isipokuwa ni chakavu sana. Nimekitembelea katika ziara yangu ya mwezi uliopita nikajiridhisha kwamba ni kituo chakavu na Wizara kupitia Jeshi la Polisi imekiweka kwenye mpango wa ukarabati katika bajeti ya mwaka 2023/2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Jengo la Polisi Mkoa wa Manyara kwa kuwa takribani ni miaka 10 sasa lipo katika hatua ya msingi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asia Halamga, Mbunge wa Viti Maalum Manyara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli nasi tumebaini kwamba jengo hilo limekaa muda mrefu na lilikuwa halijapangiwa bajeti lakini nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika bajeti ya mwaka 2023/2024, Jeshi la Polisi limeweka kituo hicho katika mpango wake wa ujenzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Godwin Kunambi, swali la nyongeza.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Kituo cha Polisi cha Mlimba ni kituo ambacho kinatumia majengo ya Shirika la Reli *(TAZARA)* na

majengo yenyewe ni chakavu. Nini sasa mpango wa Wizara kujenga kituo cha polisi pale Mlimba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kunambi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri swali hili tumelijibu jana lilikuwa limeulizwa na Mbunge mwingine anayetoka Ifakara. Tunatambua uchakavu wa kituo hicho, ahadi ya Serikali ni kwamba kadiri tutakavyopata fedha katika bajeti ya mwaka 2024/2025, vituo hivi tena viwili, Ifakara na Mlimba vitawekwa kwenye mpango wa ujenzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 47

**Kupunguza bei ya mbolea**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafanya kilimo kuwa kipaumbele cha kwanza cha Taifa kwa kupunguza bei ya mbolea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ya kupanda kwa bei ya mbolea katika msimu wa mwaka 2020/2021. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, msimu wa mwaka 2022/2023 Serikali inatekeleza mpango wa utoaji wa mbolea za ruzuku kwa wakulima ili kuwaongezea uwezo wa kununua na kutumia mbolea. Hadi kufikia tarehe 31 Januari, 2023 jumla ya tani 246,714 za mbolea zimenunuliwa na wakulima kwa bei ya ruzuku ikilinganishwa na tani 173,957 za mbolea ambazo zilinunuliwa katika kipindi cha mwezi Julai hadi Januari, 2021.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali iliahidi Bilioni 150 katika kutoa fedha kwenye ruzuku na imetoa Bilioni 50 tu, sasa haioni sababu ya kuongeza hiyo Bilioni 100 iliyobaki ili mbolea iweze kupatikana kwa wingi zaidi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tunaomba Serikali iongeze *speed* kusajili mawakala ambao watasaidia mbolea ipatikane kwa wingi, kwa maana mawakala waliopo ni wachache na inakuwa na uzito mkubwa sana wa kupeleka mbolea mpaka kule vijijini. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza kuhusiana na fedha za ruzuku, kama ambavyo yalitolewa majibu na Mheshimiwa Waziri hapa, fedha zinaendelea kuletwa kwa ajili ya kushughulikia suala la ruzuku ya mbolea na nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba yale yote ambayo tuliyaahidi tutayasimamia ili wakulima wetu waweze kupata mbolea na Wizara ya Fedha wameendelea kushirikiana nasi kwa ukaribu sana.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu *speed* ya usajili wa mawakala, tumetoa maelekezo hivi sasa ya kuwataka Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa katika maeneo amabako mbolea hazifiki kwa wakati na wakulima wako mbali, kuanza kusajili vituo vingine vipya ili kuwarahisishia huduma wakulima na mbolea hizo ziweze kuwafikia kwa uharaka. Nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba zoezi hilo linaendelea na usajili umeendelea kusajili vituo vingine vipya.

**SPIKA:** Wabunge mlio katika mapito ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ana dharua muacheni aende. Wabunge mliopo katika mapito ya Mheshimiwa Waziri Mkuu muacheni aende ana dharura. Nawasubiri. Haya ahsante sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Ezra Chiwelesa swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Serikali kwa mbolea ya ruzuku lakini kwa kuwa mbolea hii tangu tumepitisha bajeti hapa, maeneo kama ya Kagera ambao tunakuwa na msimu wa kilimo umeshapita na mbolea haikupatikana kwa wakati kwa sababu mawakala hawapo kabisa.

Je, ni nini kauli ya Serikali kwa wananchi hususan wa Wilaya ya Bihalamuro ambao wamekosa kabisa mbolea hii ya ruzuku ili kipindi cha msimu unaofuata waweze kuwa na matumaini ya kupata mbolea hii kwa wakati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ezra Chiwelesa, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tulipata changamoto ya mfumo wa usambazaji, ambao hivi sasa tumeendela kuurekebisha na hivi sasa tumeruhusu pia usajili wa vyama vya ushirika, kuwa kama sehemu ya wasambazaji wa mbolea vilevile na vyama vya wakulima vilivyosajiliwa na pia tutatumia baadhi ya maghala yaliyokuwa katika mradi wa *MIVARF* kama sehemu ya usambazaji wa mbolea hizi. Kwa hiyo, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika kipindi kinachokuja changamoto hii haitajirudia tena, tutahakikisha kwamba mbolea inawafikia wakulima kwa wakati lakini katika maeneo yao walipo pia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Msheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumekuwa na malalamiko na changamoto kadhaa kwa upatikanaji wa mbolea na bei kuwa juu. Je, Serikali ina mpango gani wa kushajihisha kilimo hai ambacho kinatumia mbolea asilia na kina gharama nafuu ambazo pia hakitumiii kemikali na vilevile ina uwezo wa kuhuisha afya ya udongo na afya zetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asha Juma, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara tumekuwa tukifanya jitihada mbalimbali za kuwakaribisha wadau mbalimbali wanaozalisha mbolea ambao ni *organic* na habari njema tu ni kwamba nilipata nafasi ya kwenda katika maonesho ya kilimo hai Ujerumani na tukakutana na wawekezaji wengi ambao wameonesha nia ya kuja uwekeza hasa katika Mkoa wa Lindi na Mtwara. Hivyo, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba ni sehemu ya mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba mbolea hii pia inazalishwa ili kupunguza gharama hii kwa wakulima.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Cherehani.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Zao la pamba ni kati ya mazao ya kimkakati hapa nchini lakini wakulima wake bado wanazalisha kilo 300 mpaka 400 kwa heka moja.

Je, ni nini mkakati wa Serikali sasa kwa wakulima hawa waweze kuzalisha kilo 500 mpaka 1,000 kwa heka moja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, anachokizungumzia Mbunge hapa ni tija na sisi tumejipanga katika Wizara kuhakikisha wakulima wetu wanalima kwa tija. Kwanza, kabisa kuwasaidia kupata viuatilifu sahihi; pili, kuwasaidia kupata teknolojia za kisasa za kilimo cha pamba; na tatu, ni kuhakikisha kwamba wanajifunza kanuni bora za kilimo kama ambavyo hivi sasa tumeona kule kupitia *TARI* na Balozi wa Pamba juu ya mfumo mpya wa *spacing* ambao umesaidia sana kuongeza uzalishaji katika zao la pamba.

Kwa hiyo, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba, tunatambua changamoto hizo na tumejipanga kuhakikisha kwamba mkulima wa pamba anazalisha kwa tija.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi

chetu cha maswali kutoka kwenu na Serikali kutoa majibu, sasa nilete tangazo nililonalo hapa mbele.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo la wageni walioko hapa Bungeni, kwanza ni wageni waliokaa Jukwaa la Spika.

Wapo wageni wangu wanne kutoka Dar es Salaam *Stock Exchange (DSE)* na hawa ni Ndugu Mary Mniwasa ambae ni Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu; yupo pia Ndugu Ibrahimu Msindo ambae ni Mkurugenzi wa Maendeleo ya Soko; Ndugu Emmanuel Nyalali ni Meneja Miradi; Ndugu Benitho Kyando ambae ni Mkurugenzi Mkuu wa kampuni tanzu ya *DSE* ambayo ni *CSDR*, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wangu wawili ambao ni Mabalozi wa *Silent Ocean* kutoka Dar es Salaam na hawa ni Ndugu Mwemba Burton ambae kwa jina maarufu anajulikana kama Mwijaku; pia yupo Ndugu Clayton Chipando, maarufu kama Baba Levo, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 18 wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambao ni vijana wa kike wa Kitanzania walioshiriki katika mashindano ya kwanza ya *Global Robotics Challenges* ama ni *challenge,* lakini hapa imeandikwa *challenges* iliyohusu masuala ya teknolojia ya habari na mawasiliano yaliyofanyika tarehe 12 - 16 Oktoba, 2022 nchini na kuibuka washindi wa pili na kupata medani ya fedha, hawa wameambatana na wawezeshaji wao kutoka Kampuni ya Simu ya *TiGO*.

Wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu karibuni sana na hongereni sana kwa ushindi ambao mmeupata,

ushindi wa pili si haba. Waheshimiwa wabunge wapigieni makofi mengi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ushindi wa pili si haba, ukitaka kujua ushindi wa pili si haba unaweza ukamuuliza Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* kwamba tukisema timu ya Bunge ya mpira wa miguu ilikuwa ya tano kwenye michezo ya Afrika Mashariki ndiyo utaelewa namba mbili ni namba ya muhimu sana. *(Makofi)*

Karibuni sana Bungeni na tunawapongeza sana. Siku nyingine tunaamini mtajitahidi zaidi, lakini mmefika mbali na tunawapongeza. Hongereni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wenu ambao tutaanza na wageni 55 wa Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, ambao ni viongozi wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake Tanzania - CCM kutoka Jijini Arusha, karibuni sana, hawa wote wanaongozwa na Mwenyekiti wa Umoja Jumuiya ya Wanawake Tanzania Wilaya ya Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Anastazia Wambura, ambao ni ndugu zake kutoka Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima ambao ni marafiki zake, pamoja na mtoto wake Ndugu Victor Champoa Mavare, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo ambao ni viongozi wa Kanisa la Usa River, Arumeru Mashariki, Jijini Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa hili tangazo Arumeru Mashariki halafu Jijini Arusha sijaelewa vizuri, haya ni Arumeru Mashariki, Mkoani Arusha, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Ni nani huyo anawatoa wageni wakati nimesimama?

Wageni kaeni nikiwa nimekaa ndio mnaruhusiwa kutoka, hamna mtu anaruhusiwa kusimama nikiwa nimesimama, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; kwanza; wanafunzi 100 kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa - Hombolo cha Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni tisa kutoka *Tanzania Youth Empowerment and Development Organization (TAYEDO)*. *(Makofi)*

Tunao pia watumishi wanne wa *Stanbic Bank* ambao wapo viwanja vya Bunge, kutoa elimu kwa Waheshimiwa Wabunge kuhusu huduma wanazozitoa. Wageni kutoka *Stanbic Bank,* karibuni sana Waheshimiwa Wabunge mpate fursa ya kwenda huko kutembelea banda lao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa sababu leo imebidi kutoa na tangazo la wageni kwamba nikiwa nimesimama watu wote inabidi wawe wamekaa, inabidi watumishi wetu wa Bunge wa humu ndani mnaozunguka na ninyi inabidi muwe mmetulia ili Mbunge asikilize tangazo. Nadhani hilo litakuwa limeeleweka, kwa sababu nikisimama hatakiwi mtu kuzungumza, ninyi mkizunguka

kwa maana yake yule anayeandika amekuita na wewe inabidi utembee. Kwa hiyo, na wewe tulizana mpaka nitakapokuwa nimekaa. Huo ndiyo utaratibu wa Kanuni zetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na ratiba sasa.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022**

**na**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. Mheshimiwa Stanslaus Nyongo.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya shughuli za Kamati kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu taarifa ya mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, kuhusu utekelezaji wa majukumu na shughuli za Kamati kwa kipindi cha mwaka kuanzia Februari, 2022 hadi Januari, 2023.

Mheshimiwa Spika, muundo wa Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020, taarifa hii imegawanyika katika maeneo makuu matatu. Sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla, sehemu ya pili ni kuhusu shughuli zilizotekelezwa na sehemu ya tatu ni kuhusu maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, njia iliyotumika katika kutekeleza majukumu ya Kamati kama ilivyo takwa la Kanuni la 142(a), Kamati ilitumia njia kuu tatu ambazo ni kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo, kusoma na kuchambua taarifa za utekelezaji, kuandaa na kutoa maoni kuhusu yatokanayo na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya taarifa. Kama inavyoelekezwa katika Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 madhumuni ya taarifa hii ni kubaishisha mambo yanayohusu uendeshaji wa shughuli za Wizara na Taasisi inazozisimamia kwa kipindi cha Februari 2022 – Januari 2023, lengo ni kuonesha mambo yanayohitaji kuboreshwa ili Bunge liyajadili kwa kuzingatia majukumu yake kwa mujibu wa Ibara ya 63, Fasili ya Pili ya Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili katika kipindi cha mwaka 2022/2023, Kamati ilipata wasaa wa kutekeleza

majukumu yake mbalimbali ambayo imepewa kwa mujibu wa Kanuni ya 137 na Nyongeza ya Nane Kanuni ya 7(a), sehemu (a) mpaka (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, shughuli za Kamati zilizotekelezwa ni pamoja na: -

(i) Kufanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha ya mwaka 2021/2022;

(ii) Kupokea na kuchambua kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2021/2022;

(iii) Mwelekeo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, vilevile tulipokea, kuchambua na kujadili taarifa za utendaji wa Wizara na Taasisi zinazosimamia, kupokea na kuchambua na kujadili taarifa na utendaji wa utekelezaji wa bajeti ya Wizara na Taasisi kwa kipindi cha nusu ya mwaka Julai hadi Disemba, 2022. Pia kushiriki semina na mafunzo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nilipokea taarifa ya utekelezaji wa maazimio, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Wizara inazozisimamia kuhusu utekelezaji wa maazimio ya Bunge yanayotokana na taarifa ya Kamati ya mwaka 2021/2022. Maazimio hayo yalitolewa kwa msingi wa matarajio ya watu kuhusu shughuli za umma na ustawi wa nchi, vilevile kushughulikia suala la Bajeti.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, mara baada ya ukaguzi wa

miradi ya maendeleo, Kamati ilipata wasaa wa kupokea, kuchambua, kuhoji, kujadili taarifa za utekelezaji wa maoni ya Kamati na bajeti kwa mwaka 2021/2022, pamoja na kuchambua, kuhoji kujadili na hatimae kutoa maoni, ushauri na mapendekezo kuhusu makadirio na mapato na matumizi ya Wizara zinazoisimamia kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya kina ya uchambuzi wa bajeti za Wizara Nne zinazosimamiwa na Kamati pamoja na maoni na ushauri wa Kamati ziliwasilishwa katika Mkutano wa Saba wa Bajeti uliomalizika mwezi Juni, 2022. Aidha, Kamati itaendelea kuyasisitiza baadhi ya maoni hayo katika taarifa hii ninayokwenda kuisoma.

Mheshimiwa Spika, mara kwa mara Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kuanzisha mfumo wa bima ya afya kwa watu wote ili kila mwananchi aweze kuwa na uhakika wa kupata matibabu pale anapougua na hivyo kupunguza vifo hatimaye kuwa na jamii yenye afya bora. Kamati imeipongeza Serikali kwani Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote *(Universal Health Insurance Bill)* ulisomwa kwa mara ya kwanza katika Mkutanao wa Nane wa Bunge la 12, Tarehe 23 Septemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya hatua hiyo uliupeleka katika Kamati kwa ajili ya hatua za uchambuzi wa kina ikiwa ni pamoja na kupokea maoni ya wadau. Baada ya hatua ya uchambuzi kukamilika Serikali iliondoa Muswada huu kabla ya kuuwasilisha Bungeni. Hata hivyo, Kamati imefarijika kuona Muswada huu umerejeshwa na unatarajiwa kukamilishwa hatua zake Bungeni katika Mkutano wa Kumi wa Bunge - Tarehe 09 Februari, 2023.

Mheshimiwa Spika, kufuatia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117(1) na Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni 2022, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ilipata wasaa wa kupokea na kujadili taarifa mabalimbali ya miradi ya maendeleo, inayotekelezwa na Wizara na Taasisi inazozisimamia. Aidha Kamati ilifanikiwa kufanya ziara katika Mikoa Sita ambayo ni Arusha, Dodoma, Iringa, Mbeya, Dar es Salaam, Mwanza, ambako ilikagua jumla ya miradi 20.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati, kwa kipindi cha nusu mwaka kuanzia Julai hadi Disemba 2022 napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa hali ya utolewaji wa fedha kwa Wizara zote zinazosimamiwa na Kamati hii ni ya kuridhisha. Mchanganuo ufuatao unaonesha hali ya upatikanaji wa fedha kwa Wizara zote nne zinazosimamiwa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Afya, Wizara ilitengewa kiasi cha shilingi trillion 1.1 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia Disemba 2022, jumla ya kiasi cha shilingi billion 490 kilikuwa kimepokelewa, sawa na asilimia 44 ya fedha zilizoidhinishwa tukienda katika Jedwali namba moja la taarifa ya Kamati inaonesha.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitengewa kiasi cha shilingi trilioni 1.49 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia Disemba kiasi cha shilingi bilioni 775 kilikuwa kimetolewa, sawa na asilimia 51.9 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 43.4 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia Disemba 2022, kiasi cha shilingi billion 19.1kilikuwa kimetolewa, ambapo ni sawa na asilimia 44.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utekelezaji wa bajeti Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo Wizara ilitengewa kiasi cha shilingi billion 35.4 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia Disemba, 2022, kiasi cha shilingi billion16.16 kilikuwa kimetolewa, sawa na asilimia 46 ya fedha zote zilizokuwa zimeidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hali ya utolewaji fedha kwa Wizara hizi zote nne ni ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, taarifa za utendaji za Wizara na taasisi inazozisimamia. Katika vikao vya Kamati vilivyofanyika mwezi Agosti 2022 na Oktoba 2022, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa za utendaji wa Wizara inazozisimamia pamoja na taasisi zake. Taarifa zilizowasilishwa na kuchambuliwa na Kamati ni kama zilivyoonyeshwa kwenye taarifa ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizofikiwa katika Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Huduma ya Maendeleo ya Jamii kwa kipindi cha Januari 2021 hadi Februari 2022

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa kipindi cha Februari 2021 hadi muda huo nilioutaja ilitoa mapendekezo mbalimbali ambayo yaliazimiwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara ya Afya jumla ya maazimio manne (4) yalitolewa. Katika vikao vya Kamati vilivyofanyika mwezi Januari 2023, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa na utekelezaji wa maazimio haya na kubaini kuwa kati ya maazimio manne yaliyotolewa maazimiomatatu utekelezaji wake yanaridhisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa ya utekelezaji wa maazimio na kubaini kuwa kati ya maazimio saba yaliyotolewa, maazimio mawili utekelezaji wake unaridhisha. Aidha, maazimio matano utekelezaji wake bado ni endelevu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Wanawake, Makundi Maalum, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa ya utekelezaji wa maazimio na kubaini kuwa kati ya maazimio matatu yaliyotolewa maazimio mawili utekelezaji wake bado hauridhishi.

Mheshimiwa Spika, mambo yaliyobainika wakati wa ufuatiliaji wa sekta zinazosimamiwa na Kamati ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa yapande wa Wizara ya Afya Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa mbili kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza ni Taarifa ya Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba. Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba ina jukumu la kulinda afya ya jamii kwa kuhakiki ubora, usalama,ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini masuala mbalimbali kama ifuatavyo: -

(a) *TMDA* imerahisisha utoaji huduma kwa wateja, ambapo kwa sasa wateja wanaweza kutuma maombi yao kwa mtandao kwa kupitia mifumo maalum ya TEHAMA ijulikanayo kama *Regulatory Information Management System* na *Laboratory Information Management System* ili kupata vibali mbalimbali. Kutokana na kuwa na mifumo ya TEHAMA na ya uendeshaji na udhibiti imeifanya *TMDA* kuwa taasisi ya mfano barani Afrika katika udhibiti wa bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi; hivyo kuvutia Mamlaka za udhibiti kutoka nchi mbalimbali kuja kujifunza. Baadhi ya nchi hizo ni Nigeria, Zimbabwe, Rwanda, Sudan Kusini, Kenya, Uganda, Ethiopia, Msumbiji, Mauritius, Ghana, Cameroon, Burundi, Botswana, Lesotho na Bangladesh.

Mheshimiwa Spika Mamlaka imeweka mifumo mbalimbali ya udhibiti kabla na baada ya bidhaa kuingia katika soko. Hii imewezesha Mamlaka kuwahakikishia Watanzania kuhakikisha ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi; aidha, kusimikwa kwa vifaa vya kisasa katika maabara za *TMDA*

Mheshimiwa Spika, kwa Bohari ya Dawa *(MSD)*. Kamati ilipokea Taarifa ya Utendaji ya Bohari ya Dawa iliyoishia mwezi Juni, 2022. Kutokana na taarifa hiyo, Kamati imebaini masuala mbalimbali kama ifuatavyo: -

(i) Hali ya Upatikanaji wa bidhaa za afya muhimu 290 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ulikuwa ni wa wastani kwa asilimia 49.

(ii) Kwa kipindi cha kuanzia Januari 2022 hadi Agosti 2022, *MSD* kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imetekeleza afua kadhaa ikiwa ni pamoja na kuwasilisha ajenda ya Mpango wa Ununuzi wa pamoja wa bidhaa za afya kwa nchi wanachama wa *SADC* kwenye Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa *SADC* uliofanyika Lilongwe, Malawi Machi 2022.

(iii) Kuandaa mikataba ya muda mrefu 146 yenye jumla ya bidhaa za afya 1,618 itakayohakikisha upatikanaji endelevu wa bidhaa za afya.

(iv) Ufungaji wa mashine mpya za vifaa vya maabara na vitendanishi vyake katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini na kushusha gharama kwa zaidi ya asilimia 50.

(v) Kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma ya kusafisha damu kwa wagonjwa wa figo kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, *MSD* inakabiliwa na changamoto mbalimbali, changamoto hizo ni pamoja na;

(i) Deni kubwa ambalo *MSD* inadai wadau wake mbalimbali ambapo hadi kufikia mwezi Julai 2022, *MSD* ilikuwa inadai jumla ya Shilingi billion 277.24 kutoka deni la shilingi billion 269.35 mwaka 2021,

(ii) Kushindwa kuhudumia wateja kulingana na maombi ya mahitaji waliyowasilisha.

(iii) Ukosefu wa mtaji utakaoiwezesha *MSD* kuwa na fedha endelevu za kununua bidhaa za afya kulingana na mahitaji.

(iv) Maoteo yasiyokuwa na uhalisia ya bidhaa za afya kutoka vituo vya kutolea huduma za afya ambayo husababisha malalamiko ya wateja, kwisha muda wa matumizi kwa bidhaa za afya yakiwa ghalani na kuzuia mzunguko wa fedha za mtaji. Vilevile, kwa Wizara hii Kamati ilipitia Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu *(NIMR).*

Mheshimiwa Spika, tuliweza pia kupitia Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia. Kupitia Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa tatu zifuatazo;

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu Tume ya Nguvu za *Atomic (Tanzania Atomic Energy Commission)*. Lengo kuu la kuanzishwa kwa Tume ya Nguvu za Atomic Tanzania ni kusimamia, kudhibiti na kusimamia matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia nchini *(TAEC)*. *TAEC* imepewa majukumu mbalimbali ambayo kwa ufupi yapo kwenye mafungu makuu mawili: -

(i) Kudhibiti na kusimamia matumizi ya teknolojia ya nyuklia pamoja na vyanzo vyote vya mionzi ili kulinda afya za wafanyakazi, wagonjwa na wananchi kwa ujumla dhidi ya madhara yanayoweza kusababishwa na vyanzo hivyo; na

(ii) Kuendeleza *(promote)* na kuhamasisha matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TAEC* imeendelea na jitihada za kusogeza huduma karibu na wananchi ili kurahisisha upatikanaji wa huduma zake sawa na Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Nyuklia (2003); Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa 2021na Mpango Mkakati wa *TAEC* pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, Katika kuhakikisha huduma zinasogezwa karibu kwa wananchi *TAEC* imefungua ofisi ya Kanda katika Jijini la Dodoma tarehe 25 Februari, 2021 kwa ajili ya kuhudumia mikoa ya Dodoma, Singida, Iringa na Tabora.

Mheshimiwa Spika, Sehemu (b) Kuhusiana na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kilianzishwa kwa sheria ya Bunge Namba 6 ya Mwaka 2005. Chuo kina kampasi mbili-Kivukoni (Dar es Salaam) na Kampasi ya Karume-Zanzibar na kina Tawi Pemba katika Wilaya ya Chakechake. Aidha, Chuo kinakusudia kufungua matawi mengine Kanda ya Magharibi katika Wilaya ya Tanganyika, Mkoa wa Katavi na Kanda ya Kati katika jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 Chuo kiliidhinishiwa jumla ya shilingi billion 25.49 Katika mwaka huo chuo kilikadiria kukusanya shilingi billion 114 kutokana na vyanzo mbalimbali ikiwepo malipo ya ada, ushauri elekezi, kazi za utafiti, utoaji wa huduma mbalimbali. Hadi mwezi Septemba, 2022 chuo kilikuwa kimekusanya shilingi bilioni 11.5 sawa na asilimia 80 ya lengo lililokuwa limepangwa. Kamati pia ilibaini kuwa chuo kilitumia kiasi cha shilingi billion 3.7 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa fedha za maduhuli.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo chuo kinakabiliwa na changamoto ya upungufu wa watumishi kulingana na mahitaji; vilevile changamoto nyingine kutokutosheleza kwa fedha za ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ya chuo kulingana na mahitaji.

Mheshimiwa Spika, vilevile tuliangalia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano ya Uviko-19. Vilevile katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum utekelezaji wa miradi unaendelea kwa Wizara unaofanyika kupitia Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, mradi wa kukarabati na ujenzi katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Rungemba tayari Taasisi imekamilisha ujenzi wa kumbi pacha za mihadhara *(lecture theatre two in one)* zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 568, zilizogharamiwa kwa kiasi cha shilingi million 993.08 pia Taasisi inaendelea kukamilisha ujenzi wa bweni la wasichana la ghorofa nne 4 utakaogharimu shilingi bilioni 1.7

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati tuliendelea kuchambua na kubaini changamoto mbalimbali zinazokabili Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii;

(i) Upungufu wa Rasilimali watu ngazi ya Jamii hususani maofisa Ustawi wa Jamii,

(ii) Ukosefu wa taarifa na takwimu za Wafanyabiashara ndogo hali inayosababisha Serikali kushindwa kuwatambua na kuwaunganisha na fursa mbalimbali za maendeleo,

(iii) Kuendelea kuwepo kwa mila na desturi zenye madhara katika baadhi ya jamii kunakosababisha kuendelea kwa vitendo vya ukatili vingi ya wanawake, watoto na wazee,

(iv) Udhaifu wa mifumo ya utoaji wa baadhi ya huduma za msaada kwa wahanga wa ukatili wa kijinsia na ukatili jinsi ya watoto hali inayosababisha waathirika wa vitendo vya ukatili kutopata huduma stahiki kwa wakati,

(v) Baadhi ya mashirika yasiyo ya kiserikali kushindwa kuwa endelevu hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria za nchi,

(vi) Uwepo wa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi wakiwemo watoto waliopoteza wazazi au mzazi wa watoto walio telekezwa, watoto walio katika mkinzano na Sheria pamoja na wanaoishi na kufanya kazi mitaani,

(vii) Uchakavu na upungufu wa miundombinu ya kujifunzia na kujifunzia katika vyuo nane vya Maendeleo ya Jamii, Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, na

(viii) Uchakavu wa miundombinu ya kutolea huduma katika vituo vya ustawi wa jamii ikiwemo makazi 14 ya wazee, maabusu 5 za watoto, makao ya taifa ya watoto Kurasini na Shule ya Maandalisho ya Irambo.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo tumepitia katika Taarifa tumeona taarifa ya Baraza la Michezo yaani BMT. Katika uchambuzi wa taarifa wa Baraza hili la Michezo

iliyowasilishwa mbele ya Kamati Mwezi Agusti 2022 Kamati ilibaini kuwa *BMT* imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa kuridhisha. Vilevile tuliweza kuona taarifa ya Baraza la Sanaa la Taifa. Kwa upande wa Baraza la Sanaa la Taifa pamoja na mambo mengine imefanikiwa kurejesha tuzo za mziki kutengeneza mfumo wa kieletroniki wa usajili na usimamizi wa taarifa za wasajiliwa

Aidha mafanikio mengine ni pamoja na kushiriki katika maonyesho ya Kimataifa ya Biashara Sabasaba ya Mwaka 2021 na 2022, kuratibu chaguzi za mashirikisho ya Sanaa na vyama vyake, kutoa vibali kwa Wasanii kuingia na kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kuendesha shughuli za Sanaa na kuhimarisha Mifumo rafiki ya utoaji huduma pamoja na uchambuzi wa wasanii na wadau wa sekta ya sanaa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa kuwa pamoja na mafanikio yaliyopatikana, BASATA inakabiliwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na ufinyu wa rasilimali fedha na upungufu wa watumishi kwa asilimia 50.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna Taasisi ya Haki Miliki Tanzania *(COSOTA)*. Pamoja na mambo mengine Taasisi ya Haki Miliki hii ya *COSOTA* inatekeleza majukumu kwa kukuza na kulinda maslahi ya watunzi, waandishi, wasanii, wafasili, watayarishaji wa kurekodi sauti, watangazaji, wachapishaji na hususani kukusanya na kugawa mirabaha yeyote au ujira unaotolewa kulingana na haki zao zilizoelezwa katika Sheria ya Haki Miliki. Aidha, jukumu lilingine kufuta, kubainisha, kutangaza haki za wamiliki na kutoa uthibitisho wa umiliki wa haki pale itakapotokea ubishani au ukiukwaji wa haki.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kupitia *COSOTA* kwani katika kipindi cha Mwaka 2022/2023 imefanikiwa kukusanya Mirabaha itokanayo na leseni kiasi cha shilingi million 285.3 na kufanikiwa kufanya mgao wa mirabaha ya ujumla ya shilingi million 312.29 kwa wasanii na wabunifu wa haki miliki 1123. Pia *COSOTA* imefanya maboresho katika Mfumo wa Utoaji wa Leseni za Usajili wa Wanachama Ki-digitally; aidha, pia kusimika mifumo ya TEHAMA na kuanza kutumia kutumia mfumo wa ulipaji Serikalini (MUSE).

Mheshimiwa Spika, naomba niende sasa kwenye maoni na mapendekezo ya Kamati yetu, Baada ya maelezo ya kina nianze na maoni ya Jumla.

Mheshimiwa Spika, kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Kamati kama uchambuzi wake naomba kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati ambayo Bunge lako Tukufu itayaazimia kwa ajili ya utekelezaji Serikalini;

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya ukatili wa kijinsia nchini

Kwa kuwa kumekuwepo na ongezeko kubwa la ukatili wa kijinsia nchini hasa kwa vitendo vya ubakaji na ulawiti

Na kwa kuwa, kuwepo kwa changamoto hii kumeongeza uwepo wa walemavu wakudumu maambukizi ya virusi vya uklimwi na wakati mwingine kusababisha vifo na hofu kubwa katika jamii

Kwa hiyo basi Kamati inasisitiza ushauri wakw kwamba Bunge liishauri Serikali;

i) Kufanya Utafiti wa kina, kujua nini chanzo cha ongezeko la ukatili wa kijinsia nchini hususani kwa Wanawake na Watoto,

ii) Kuzifanyia Marekebisho Sheria zote zinazousu adhabu za makosa haya ili zitolewe adhabu kali kwa wale wote watakaohusika na ufanyaji wa vitendo vya ukatili hususani watoto na wanawake,

iii) Kuwekwe mkakati wa ukusanyaji wa Takwimu halisi za matukio yote ya ukatili wa kijinsia nchini ili kujua ukubwa halisi wa tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kuhusu ukatili wa watoto shuleni. Nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maagizo aliyoyatoa. Hata hivyo, sisi kama Kamati tunasema kwamba,

Kwa kuwa kumekuwepo na ongezeko kubwa la matendo ya ukatili wa watoto wa wapo shuleni ama wakiwa njiani kuelekea shuleni

Na kwa kuwa kuwepo kwa ukatili huu kwa Watoto shuleni kunaweza kusababisha matokeo ya wasioridhisha, kuongezeka kwa utoro, magonjwa, ulemavu changamoto ya afya akili pamoja na hofu kwa wazazi,

Kwa hiyo basi, Bunge linashauri Serikali kuweka mikakati thabiti na kuhakikisha vitendo hivi vinatokomezwa kwa kudhibiti vyanzo vyake ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kunawekwa madawati ya Jinsia katika Taasisi zote zinazotoa elimu nchini kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu na katika ofisi zote za Serikali.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhusu upungufu wa watumishi:-

Kwa kuwa katika Wizara zote zinazosimamiwa na Kamati hii kumebainika kuwa na changamoto ya upungufu mkubwa wa watumishi hasa wauguzi, madaktari, walimu, wahadhiri na kadhalika.

Na kwa kuwa upungufu huu wa watumishi umekuwa ukileta athari katika utoaji wa huduma mbalimbali hata wakati mwingine kuchelewesha baadhi ya kuanza katika muda uliopangwa.

Kwa hiyo basi Bunge linaishauri Serikali kutoa kipaumbele cha ajira katika Sekta hizi muhimu ili kuzinusuru.

Mheshimiwa Spika, kwa Wizara ya Elimu; kuhusiana na Upungufu wa Walimu Nchini:-

Kwa kuwa Sekta ya Elimu imekuwa na upungufu mkubwa sana wa watumishi na hasa Walimu;

Na kwa kuwa upungufu wa watumishi katika sekta ya elimu umekuwa ukileta athari katika utoaji wa huduma mbalimbali za elimu nchini ikiwemo matokeo yasiyoridhisha;

Kwa hiyo basi Bunge linaishauri Serikali kutoa kipaumbele kwa ajira kwenye Sekta ya Elimu kwa ajili ya kuajiri Walimu wa kutosha ili kuondoa ombwe la ukosefu wa Walimu nchini.

Mheshimiwa Spika, pili, Utengwaji na Utolewaji wa Fedha:

Kwa kuwa kumekuwa na utengwaji finyu na usioridhisha wa bajeti kwa ajili ya Sekta ya Elimu;

Na kwa kuwa hali hii imekuwa ikiathiri utekelezaji bora wa majukumu ya Wizara, ikiwemo utoaji huduma;

Kwa hiyo basi Bunge linaishauri Serikali kuendelea kuongeza tengeo la bajeti kwa ajili ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Ubora wa Elimu Nchini:

Kwa kuwa imeonekana kuwa hali ya elimu nchini imeendelea kutoridhisha, hali inayofanya wanafunzi kushindwa kuwa na ufaulu mzuri na pia kushindwa kuajirika mara baada ya kumaliza masomo;

Na kwa kuwa Serikali imeamua kupitia upya mtaala wa elimu kwa ngazi zote; ya msingi, sekondari na ngazi za juu ikiwemo ualimu;

Kwa hiyo basi Bunge linaishauri Serikali, kuendelea na mchakato wa kukamilisha utungwaji wa mitaala na Wizara ione namna ya kuharakisha jambo hili bila kuathiri ubora wa elimu.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu:

Kwa kuwa kiwango cha fedha kinachotolewa na Serikali kwa ajili ya kugharamia mikopo ya elimu bado hakitoshelezi mahitaji;

Na kwa kuwa kukosekana kwa mikopo hiyo kunasababisha wanafunzi wengi kushindwa kuendelea na masomo yao ya juu;

Kwa hiyo basi Bunge linaishauri Serikali kuongeza bajeti ya Bodi ya Mikopo ili wanafunzi wengi wa elimu ya juu waweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ualimu cha Mtwara:-

Kwa kuwa muda mrefu sasa takribani miaka 19, Serikali haijatimiza azma yake ya kukibadili Chuo cha Ualimu Mtwara kuwa Chuo Kikuu;

Na kwa kuwa kutokubadilishwa Chuo hiki kuwa Chuo Kikuu kumeleta athari ya kukosekana kwa Walimu na hasa Walimu wa ngazi ya shahada na hivyo kuchelewesha malengo na utekelezaji wa mpango wa Serikali kuhusu kukuza elimu nchini;

Kwa hiyo basi Bunge linaishauri Serikali, kuendeleza mchakato wa kubadili Chuo cha Ualimu Mtwara kuwa Chuo Kikuu Kishiriki ili kutimiza azma yake. Pili, pamoja na malengo yaliyopangwa, Serikali iangalie namna ya kuweka kozi kulingana na mahitaji ya wakati huu.

Mheshimiwa Spika, nikiendelea hivyohivyo na suala la mikopo kwa Vyuo vya Kati:

Kwa kuwa Vyuo vya Kati vimekuwa vikidahili idadi ndogo ya wanafunzi kutokana na wanafunzi wengi wengi kushindwa kugharamia ada za masomo katika vyuo hivyo.

Na kwa kuwa kutokana na uzalishaji mdogo wa wanafunzi wa vyuo vya kati kumekuwa na ombwe kubwa la kuwapata wataalam ambao ndio injini ya uzalishaji wa bidhaa muhimu na mafundi *(technical skills expertise)* kwa ajili ya uzalishaji wa viwandani.

Kwa hiyo basi Bunge linaishauri Serikali kuanza kutoa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vya kati ili kuweza kuzalisha wataalam wa kutosha wa kufanya kazi kwenye viwanda na kutoa huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere – Kivukoni, Dar es Salaam:

Kwa kuwa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kinatoa kozi chache na ni zile zinazohusu sayansi ya jamii *(social sciences)* tu;

Na kwa kuwa uwepo wa kozi chache zitolewazo na Chuo hiki kunapunguza wigo wa utolewaji wa elimu stahiki inayohitajika kwa mazingira ya sasa;

Kwa hiyo basi Bunge linaishauri Serikali kukielekeza Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kuangalia uwezekano wa kuongeza kozi nyingine kama vile kozi za TEHAMA na nyingine ili kuongeza wigo wa utoaji elimu stahiki kwa mazingira na wakati wa sasa wenye ushindani wa kiteknolojia lakini pia kutanua wigo wa udahili.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Nyerere – Butiama:

Kwa kuwa Chuo hiki cha cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Nyerere – Butiama kimekaa takribani miaka 14 bila kudahili wanafunzi licha ya kuwepo kwa wakufunzi na watumishi;

Na kwa kuwa hali hii imesababisha Chuo kutotimiza malengo yake na hivyo kutoleta thamani ya matumizi ya fedha za umma *(value for money);*

Kwa hiyo basi Bunge linaishauri Serikali:-

(1) Kupitia upya namna, utaratibu na sababu za kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Nyerere – Butiama;

(2) Kuweka Mkakati wa kutekeleza haraka malengo ya kuanzishwa kwa chuo hiki;

(3) Ichunguze kama vipo vyuo vingine vyenye changamoto kama hii ili kuepusha upotevu wa rasilimali fedha na rasilimali watu; na

(4) Aidha, rasilimali watu iliyopo katika Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Nyerere – Butiama ipelekwe kwenye vyuo vingine vyenye uhitaji ili kuipa nafasi Serikali kukiweka chuo hicho katika mazingira stahiki na kuanza kudahili wanafunzi na baadaye kuwarejesha mara baada ya chuo kuwa tayari.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Nguvu za Atomiki:

Kwa kuwa majengo ya Ofisi ya Makao Makuu ya Tume ya Nguvu za Atomiki Jijini Dodoma yamejengwa nje ya mji na mbali na makazi ya watu;

Na kwa kuwa kutokana na Ofisi za Tume hii zilizojengwa Makao Makuu Dodoma kuwa mbali na makazi ya watu kunasababisha changamoto ya usafiri kwa watumishi;

Kwa hiyo basi Bunge linaishauri Serikali kuipa fedha Tume ya Nguvu za Atomiki ili iweze kujenga nyumba za makazi kwa ajili ya watumishi na Serikali iendelee kuharakisha mchakato wa uhamiaji Makao Makuu

Dodoma ili wananchi wa Dodoma na Taifa kwa ujumla, wapate huduma zinazotolewa na Tume hii kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni Ujenzi wa Miradi ya Miundombinu ya Elimu Nchini:

Kwa kuwa miradi mingi ya elimu inachelewa kuanza kutokana na changamoto zinazotokana na kutokamilika kwa huduma ambata kama vile majengo ya nyumba za Walimu na udahili wa wanafunzi;

Na kwa kuwa kuchelewa kwa miradi hii kumekuwa kikiathiri thamani halisi ya fedha *(value for money)*, pamoja na kusababisha wanafunzi wanaohitaji kujiunga na shule hizi kushindwa kujiunga na hivyo baadhi yao kuishia mitaani;

Kwa hiyo basi Bunge linaishauri Serikali, mchakato wa uanzaji wa miradi hii uende sambamba na mkakati wa miradi ambata kama vile majengo ya nyumba za Walimu, ajira za Walimu, vyoo na udahili wa wanafunzi ili mara tu mradi unapokamilika na huduma zianze hapo hapo. Aidha, kwa maeneo yote ambayo shule tayari zimejengwa, Serikali iharakishe ujenzi wa miradi ambata.

Mheshimiwa Spika, Ukosefu wa Majengo na Mabweni; tumetoa maazimio ikiwa ni pamoja na Bunge linaishauri Serikali kuweka mkakati wa kujenga mabweni katika shule zote za kata ili kuwawezesha wanafunzi wa kike kusoma katika mazingira rafiki na huru hatimaye Taifa liweze kuwa na ustawi ulio imara.

Mheshimiwa Spika, Hali Duni ya Utoaji wa Chakula Shuleni:

Kwa kuwa wanafunzi wengi katika shule za Serikali hawapati chakula shuleni;

Na kwa kuwa kukosekana kwa chakula shuleni ni sababu mojawapo ya utoro;

Kwa hiyo basi Bunge linaishauri Serikali; kuzingatia suala la chakula katika shule zote na kufanya mapitio na usimamizi wa mwongozo wa lishe shuleni ili kuhakikisha kunakuwepo na chakula jambo linalofanya wanafunzi kuwa na utulivu katika mazingira ya shule.

Mheshimiwa Spika, kwa Wizara ya Afya:-

(1) Utengwaji na Utolewaji wa Fedha:

Kwa kuwa Kumekuwa na utengwaji finyu na utolewaji wa fedha usio wa wakati;

Na kwa kuwa bajeti finyu na utolewaji wa fedha usio wa wakati umekuwa ukiathiri utekelezaji ubora wa majukumu ya Wizara, ikiwemo utoaji wa huduma kwa wananchi;

Kwa hiyo basi Bunge linaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha, lakini pia kuhakikisha fedha hizo zilizoidhinishwa na Bunge zinatolewa zote na kwa wakati ili kuleta ustawi bora wa huduma kwa wananchi.

(2) Uingizwaji Nchini wa Bidhaa Bandia za Chakula, Dawa na Vipodozi:

Kwa kuwa pamoja na Serikali kujitahidi kudhibiti bidhaa bandia za chakula na dawa bado bidhaa hizo

bandia zimekuwa zikionekana kwa wingi katika maduka mbalimbali hapa nchini;

Na kwa kuwa uwepo wa bidhaa bandia umekuwa ukiathiri afya za watu na kusababisha magonjwa hivyo kupoteza nguvu kazi na kurudisha nyuma maendeleo ya nchi;

Kwa hiyo basi Serikali inashauriwa:-

(i) Kuhakikisha inadhibiti mipaka ya kuingia nchini au kulinda usalama na afya za Watanzania;

(ii) Serikali kuwajumuisha wafamasia kwenye kanzidata, hasa wale ambao wako kwenye taasisi binafsi ili kuweza kudhibiti kwa urahisi utoaji wao wa huduma;

(iii) Kuiwezesha *TMDA* kuwa na wataalam wake yenyewe wa mambo ya dawa; na

(iv) Udhibiti wa mambo ya chakula yaondolewe kutoka *TBS* Kamati inashauri yarejeshwe katika taasisi ya *TMDA*.

(3) Bohari Kuu ya Dawa *(MSD):*

Kwa kuwa *MSD* inadai madeni makubwa ambayo bado yanaongezeka lakini ulipwaji wake ni wa kusuasua sana;

Na kwa kuwa kutokulipwa kwa madeni hayo na kuongezeka kwa madeni hayo kunasababisha *MSD* kutotekeleza majukumu yake ipasavyo na hivyo kusababisha kilio kwa wananchi juu ya kutopatikana kwa dawa hospitalini na katika hospitali;

Kwa hiyo basi Bunge linaishauri Serikali kwamba, Bohari kuu ya Dawa iandae mikakati ya ziada ili kuhakikisha madeni yaliyopo na yanayoongezeka yanapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, Uwekezaji wa Viwanda vya Dawa na Vifaa Tiba kufanywa na Bohari Kuu ya Dawa:

Kwa kuwa kumekuwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa dawa muhimu na za msingi za binadamu, hasa ikitokea majanga mbalimbali kidunia, kama vile wakati wa janga la UVIKO – 19;

Na kwa kuwa kutokana na kutopatikana huko kwa dawa kumekuwa kukisababisha kuzorota kwa huduma katika sekta ya afya na kusababisha madhara makubwa kwa wananchi;

Kwa hiyo basi Bunge linaishauri Serikali:-

(1) Kuweka mikakati thabiti ya kushirikisha sekta binafsi *(PPP)* pamoja na kuwekeza na kurahisisha uwekezaji wa viwanda wa vifaa tiba pamoja dawa nchini ili kukidhi soko la ndani na nje na pia kupunguza gharama ya uingizaji wa dawa kutoka nje ya nchi; na

(2) *MSD* ifanye mchakato wa haraka wa uzalishaji wa bidhaa zinazotokana na pamba ili kupunguza uagizwaji wa bidhaa hizo kutoka nje ya nchi kwa kuwa malighafi ya pamba tunayo hapa nchini, ambapo inapatikana.

Mheshimiwa Spika, Kuhusiana na Dawa Asili:

Kwa kuwa kumekuwa na dawa za aina nyingi za asili zinazouzwa katika maeneo mbalimbali nchini;

Na kwa kuwa uwepo wa dawa hizi ambazo zinauzwa kiholela na wananchi kuzitumia bila kujua kama zina ubora, madhara na faida yake, kwani baadhi yake zinakuwa hazijafanyiwa utafiti;

Kwa hiyo basi Bunge linaishauri Serikali:-

(1) Kupitia Taasisi ya Utafiti wa Dawa nchini *(NIMR)* kufanya utatifi wa ubora wa athari na matumizi salama ya dawa hizo;

(2) Kupitia *NIMR* iweke mfumo wa kuhifadhi tafiti zote zinazofanyika nchini ili kujua kutumia tafiti zote zinazofanyika kwa maslahi ya Taifa;

(3) Kuweka mpango mkakati wa kutenga fedha kutoka vyanzo vya ndani kwa ajili ya kufanya tafiti mbalimbali kutegemea fedha zinazotokana na wafadhili wa nje ili kufanya tafiti nyingi zaidi; na

(4) *NIMR* iwekeze kwenye tafiti zaidi katika magonjwa yasiyoambukiza kwa kuwa magonjwa haya kwa sasa yanachangia asilimia kubwa zaidi ya vifo kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa Wizara ya Utamaduni. Uibuaji wa vipaji; Bunge linaishauri Serikali…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kengele imegonga na taarifa yako itaingia kwenye *Hansard,* malizia hapo mwisho, dakika moja.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nimalizie kwa kusema kwamba, kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, yaani kwa Watoto wa Mitaani:

Kwa kuwa tatizo la watoto wa mitaani limeendelea kuwepo;

Na kwa kuwa kuendelea kuwepo kwa watoto mitaani kumesababisha kuongeza kwa vitendo vya uhalifu na kufanyika kwa ukatili wa Watoto;

Kwa hiyo basi Bunge linaishauri Serikali, kuweka mikakati ya kutoa elimu kwa jamii kuhusu changamoto hii na namna jamii inavyoweza kukabiliana nalo ikiwa ni pamoja kusambaza Mwongozo wa Uwezeshwaji hasa kwa akinamama ili kuweza kujiepusha na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, niendelee kusema kwamba, kwa mara nyingine naomba kuchukua fursa hii tena kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu na napongeza sana kwa kazi kubwa unayofanya ya kuliongoza Bunge lako vizuri na nawashukuru pia, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nakushukuru sana, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa

sababu, tunasimamia zaidi ya Wizara nne. Kwa hiyo, kwa kweli, tunafanya kazi kubwa, natoa pongezi kubwa sana kwa wajumbe wa Kamati hii kwa kazi kubwa wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nenda mwisho wa hiyo taarifa yako, soma hiyo sehemu ya mwisho.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII KWA KIPINDI CHA KUANZIA FEBRUARI, 2022 HADI JANUARI, 2023 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SURA YA KWANZA**

1.0 **UTANGULIZI**
1.1 **Maelezo ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Mwaka ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji

wa Majukumu na shughuli za Kamati kwa kipindi cha Mwaka kuanzia mwezi Februari 2022 hadi Januari 2023.

1.2 **Muundo wa Taarifa**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Taarifa hii imegawanyika katika maeneo makuu yafuatayo: -

i) Sehemu ya Kwanza, inatoa maelezo ya jumla ikiwemo msingi wa shughuli za Kamati, mbinu na njia zilizotumika pamoja na orodha ya shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja;

ii) Sehemu ya Pili, ambayo inafafanua shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi wa yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto zilizojitokeza;

iii) Sehemu ya Tatu, inatoa maoni ya jumla na mapendekezo ili kuliwezesha Bunge kufanya maamuzi, na

iv) Hitimisho na kutoa hoja kwa ajili ya Bunge kuweza kujadili na kufanya maamuzi.

1.3 **Njia iliyotumika kuteleleza Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake, kama ilivyo takwa la Kanuni ya 142 (a), Kamati ilitumia njia kuu tatu kama ifuatavyo: -

(i) Kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara pamoja na Taasisi inazozisimamia;

(ii) Kusoma na kuchambua taarifa za utekelezaji wa majukumu zilizowasilishwa na Wizara na Taasisi zake;

(iii) Kuandaa na kutoa maoni na ushauri kuhusu yatokanayo na taarifa za Wizara na taasisi inazozisimamia.

1.4 **Madhumuni ya Taarifa**

**Mheshimiwa Spika,** kama inavyoelekezwa katika Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Madhumuni ya Taarifa hii ni kubainisha mambo yanayohusu uendeshaji wa shughuli za Wizara na Taasisi inazozisimamia kwa kipindi cha Februari, 2022 hadi Januari, 2023. Lengo ni kuonesha mambo yanayohitaji kuboreshwa ili Bunge liyajadili kwa kuzingatia majukumu yake kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba.

1.5 **Msingi wa Shughuli za Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge kwa niaba ya wananchi, lina jukumu kubwa la kuisimamia na kuishauri Serikali. Aidha, Ibara ya 96(1) ya Katiba inaweka utaratibu na msingi wa uwepo wa Kamati za Bunge na utekelezaji wa majukumu ya Kamati ili kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Kanuni ya 137 kwa pamoja na Nyongeza ya Nane zinaweka msingi wa utekelezaji wa shughuli za Kamati za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane 5 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Wizara zifuatazo: -

(i) Wizara ya Afya;

(ii) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia;

(iii) Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; na

(iv) Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Aidha, Nyongeza ya Nane, 7 (1) (a-d) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, imeainisha majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge ikiwemo Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuwa ni pamoja na: -

(i) Kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia;

(ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

(iii) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila mwaka za Wizara hizo pamoja Taasisi zilizo chini yake; na

(iv) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

## SURA YA PILI

## 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA UCHAMBUZI WA YALIYOBAINIKA

### 2.1 Maelezo ya Jumla

(i) **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2022/2023 Kamati ilitekeleza shughuli zake kama ifuatavyo: -

(ii) Kupokea na kujadili Taarifa za utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati yaliyotokana na taarifa mbalimbali za Kamati zilizowasilishwa Bungeni;

(iii) Kushughulikia bajeti za Wizara na taasisi inazozisimamia; na

(iv) Kupokea, kujadili na kukagua miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Wizara na Taasisi inazozisimamia; na

(v) Kupokea na kujadili Muswada wa Bima ya Afya kwa wote.

**Mheshimiwa Spika,** katika Kipindi cha Mwaka 2022/2023, Kamati ilipata wasaa wa kutekeleza majukumu yake mbalimbali ambayo imepewa kwa mujibu wa Kanuni ya 137 na Nyongeza ya Nane, Kanuni ya 7 (1) (a-d) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020. Shughuli ambazo Kamati imezitekeleza ni pamoja na: -

(i) Kufanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

(ii) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na mwelekeo wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

(iii) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za utendaji wa Wizara na Taasisi inazozisimamia;

(iv) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za utendaji na utekelezaji wa bajeti za Wizara na Taasisi kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba 2022); na

(v) Kushiriki Semina za mafunzo.

2.2 **Kupokea Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili taarifa za Wizara inazozisimamia kuhusu Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Kamati ya Mwaka 2021/2022. Maazimio hayo yalitolewa kwa msingi wa matarajio ya watu kuhusu shughuli za umma na ustawi nchini. Kilichofanyika ni kuonesha matarajio na kuacha uhuru kwa utekelezaji ndani ya kipindi cha Februari, 2022 – Januari, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, Ufuatiliaji umefanyika kwa lengo la kuona kama kuna jambo la jumla la kujifunza na kurekebisha au kuona hali inayoendelea kwenye kutatua changamoto. Kwa ufupi mambo matatu yamehusianishwa ambayo ni matarajio (maazimio), matokeo yaliyofikiwa yaani mafanikio na changamoto. (*Utaratibu huu unatokana na kawaida ya uzingatiaji wa*

*dhamana ya Bunge katika usimamizi wa shughulli za umma*)

### 2.3 **Kushughulikia Bajeti**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, mara baada ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilipata wasaa wa kupokea, kuchambua, kuhoji na kujadili taarifa za utekelezaji wa maoni ya Kamati na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na kuchambua, kuhoji, kujadili na hatimaye kutoa maoni, ushauri na mapendekezo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara inazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya kina ya Uchambuzi wa Bajeti za Wizara nne zinazosimamiwa na Kamati pamoja na maoni na ushauri wa Kamati viliwasilishwa katika Mkutano wa Saba wa Bajeti uliomalizika Mwezi Juni, 2022. Aidha, Kamati itaendelea kuyasisitiza baadhi ya maoni hayo katika Taarifa hii.

### 2.4 **Kushughulikia Miswada na Maazimio**

**Mheshimiwa Spika,** mara kwa mara Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kuanzisha mfumo wa bima ya afya kwa watu wote ili kila mwananchi aweze kuwa na uhakika wa kupata matibabu pale atakapougua na hivyo kupunguza vifo hatimae kuwa na jamii yenye afya bora. Kamati inaipongeza Serikali kwani Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote *(The Universal Health Insurance Bill)* ulisomwa kwa mara ya kwanza katika wa Mkutano wa Nane wa Bunge la 12, tarehe 23 Septemba, 2022.

**Mheshimiwa Spika**, mara baada ya hatua hiyo, uliupeleka katika Kamati kwa ajili ya hatua za uchambuzi wa kina ikiwa ni pamoja na kupokea maoni ya wadau. Baada ya hatua ya uchambuzi kukamilika, Serikali iliuondoa Muswada huu kabla ya kuwasilishwa Bungeni. Hata hivyo, Kamati imefarijika kuona Muswada huu umerejeshwa na unatarajiwa kukamilisha hatua zake Bungeni katika Mkutano wa Kumi wa Bunge, tarehe tarehe 9 Februari, 2023.

2.5 **Kufuatilia Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020. Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ilipata wasaa wa kupokea na kujadili taarifa mbalimbali za miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara na Taasisi inazozisimamia. Aidha, Kamati ilifanikiwa kufanya ziara katika Mikoa sita ambayo ni Arusha, Dodoma, Iringa, Mbeya, Dar es Salaam na Mwanza ambako Kamati ilikagua jumla ya Miradi 20.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ukaguzi wa mradi mmoja mkoani Dodoma, mradi mmoja mkoani Mwanza, miradi mitatu mkoani Mbeya, miradi mitatu Mkoani Iringa, miradi minne Mkoani Dar es Salaam na miradi minane Mkoani Arusha na kupokea taarifa za maendeleo ya miradi hiyo. Mchanganuo wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo: -

(i) Mradi wa upanuzi wa majengo ya Tume ya Mionzi Tanzania (TAEC) Arusha (Machi, 2022);

(ii) Mradi wa ujenzi wa madarasa, kumbi na mabweni katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii – Tengeru, Arusha (Machi, 2022);

(iii) Mradi wa ujenzi wa majengo ya madarasa na maabara katika Chuo cha Ufundi, Arusha (Machi, 2022);

(iv) Mradi wa ujenzi wa jengo la Mikutano na mambo mchanganyiko *(Thearter Hall)* katika Chuo cha Sayansi cha Afrika cha Nelson Mandela Arusha (Machi, 2022);

(v) Mradi wa ujenzi wa madarasa, maabara, ofisi na kumbi za mikutano katika Chuo Kikuu cha Ualimu cha Mkwawa Iringa (Machi, 2022);

(vi) Mradi wa majengo kwa ajili ya mikutano, madarasa na ofisi katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba, (Machi, 2022);

(vii) Mradi wa upanuzi wa Chuo Kikuu cha Ufundi Mbeya (Uyole – Mbeya);

(viii) Mradi wa upanuzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya;

(ix) Mradi wa Upanuzi wa Maabara ya Taifa – Dar es Salaam (Septemba, 2022);

(x) Mradi wa Upanuzi cha Hospitali ya Taifa ya Muhimbili – Dar es Salaam (Septemba, 2022);

(xi) Mradi wa Jengo la Makao Makuu ya Tume ya Mionzi (Kikombo – Dodoma);

(xii) Mradi wa ujenzi wa madarasa na ukumbi wa mikutano katika Chuo cha Ualimu cha Arusha (Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia - Julai, 2022);

(xiii) Mradi wa ujenzi wa kumbi pacha na madarasa katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Monduli, Arusha (Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum – Julai, 2022);

(xiv) Mradi wa Majengo ya Ofisi za Mamlaka ya Chakula na Dawa Arusha (Wizara ya Afya – Septemba, 2022);

(xv) Mradi wa Ununuzi na Usimikaji wa Mifumo ya Ukaguzi wa bidhaa za vyakula na dawa katika Mpaka wa Namanga (Wizara ya Afya - Septemba, 2022);

(xvi) Mradi wa Jengo la Ofisi la Mamlaka ya Chakula na Dawa (Buzuruga – Mwanza);

(xvii) Mradi wa Usimikaji wa Mfumo wa Usahihishaji wa Mitihani ya Taifa kwa Njia ya Mtandao kwa Baraza la Mitihani la Taifa (Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia - Dar es Salaam; Oktoba, 2022);

(xviii) Mradi wa Ukumbi wa Mikutano Chuo cha Maendeleo ya Elimu Bagamoyo - ADEN (Bagamoyo Pwani – Oktoba, 2022);

(xix) Mradi wa ujenzi wa mabweni na kumbi za mikutano katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ruaha, Iringa (Wizara ya Maendeleo ya Jamii,

Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum – Novemba, 2022); na

(xx) Mradi wa Ujenzi wa hosteli za wasichana katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole, Mbeya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum – Novemba, 2022).

**Mheshimiwa Spika,** miradi iliyotajwa baadhi yake ilitolewa taarifa wakati wa vikao vya Bunge la Bajeti. Aidha, miradi iliyosalia ilitembelewa na kukaguliwa wakati vikao vingine vya Kamati vilivyofanyika baada ya Bunge la Bajeti.

2.6 **Utekelezaji wa Bajeti za Wizara Zinazosimamiwa na Kamati kwa Kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba, 2022)**

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai-Disemba 2022), napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa hali ya utolewaji wa fedha kwa Wizara zote zinazosimamiwa na Kamati hii ni ya kuridhisha. Mchanganuo ufuatao unaonesha hali ya upatikanaji wa fedha kwa Wizara zote nne (4) zinazosimamiwa na Kamati.


2.6.1 **Wizara ya Afya**

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Afya, Wizara ilitengewa kiasi cha **Shilingi 1,109,421,722,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia Disemba 2022, jumla ya kiasi cha **Shilingi 490,063,524,610.79** kilikuwa kimepokelewa, sawa na **asilimia 44** ya fedha

zilizoidhinishwa kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 1.

***Kielelezo Na. 1.***

**Ulinganisho wa Fedha zilizotengwa na Fedha zilizopokelewa kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai-Disemba 2022) Wizara ya Afya**




*Chanzo; Taarifa ya Wizara ya Afya kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya kwa kipindi cha      Mwaka (Julai-Disemba, 2022)*

### 2.6.2 **Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitengewa kiasi cha **Shilingi 1,493,004,355,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi ya Maendeleo. Hadi kufikia Disemba 2022, kiasi cha **Shilingi 775,214,163,861** kilikuwa kimetolewa, sawa na **asilimia 51.9** ya fedha zilizoidhinishwa; kama inavyoonekana katika kielelezo namba 2.

*Kielelezo Na. 2*
**Ulinganisho wa Fedha zilizotengwa na Fedha zilizopokelewa kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai-Disemba 2022) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**





*Chanzo; Taarifa ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai-Disemba, 2022)*

2.6.3 **Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsi, Wanawake, Watoto na Makundi Maalum**

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa utekelezaji wa bajeti ya Wizara, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ilitengewa kiasi cha **Shilingi 43,403,061,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi ya Maendeleo. Hadi kufikia Disemba 2022, kiasi cha **Shilingi 19,143,301,666** kilikuwa kimetolewa, sawa na **asilimia 44** ya fedha zilizoidhinishwa; kama inavyoonekana katika kielelezo namba 3.

*Kielelezo Na. 3*

**Ulinganisho wa Fedha zilizotengwa na Fedha zilizopokelewa kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai-Disemba 2022) Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsi, Wanawake, Watoto na Makundi Maalum**





*Chanzo; Taarifa ya Wizara Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawakena Makundi Maalum kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai-Disemba, 2022)*

2.6.4 **Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ilitengewa kiasi cha **Shilingi 35,425,991,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi ya Maendeleo. Hadi kufikia Disemba, 2022, kiasi cha **Shilingi 16,161,529,148** kilikuwa kimetolewa, sawa na **asilimia 46** ya fedha zote zilizoidhinishwa.

*Kielelezo Na. 4.*

**Ulinganisho wa Fedha zilizotengwa na Fedha zilizotolewa kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba, 2022) Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**




*Chanzo; Taarifa ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai-Disemba, 2022*)

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla hali ya utolewaji fedha kwa Wizara hizi ni ya kuridhisha kwani Kamati imebaini fedha zilizotolewa kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni asilimia 51.9, Wizara ya Afya asilimia 44, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum asilimia 44, na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo asilimia 46.

### 2.7 Taarifa za Utendaji za Wizara na Taasisi inazozisimamia

**Mheshimiwa Spika,** Katika vikao vya Kamati vilivyofanyika mwezi Agosti 2022 na Oktoba 2022, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili Taarifa za Utendaji wa Wizara inazozisimamia pamoja na Taasisi zake. Taarifa zilizowasilishwa na kuchambuliwa Kamati ni kama ifuatavyo:

#### 2.7.1 Wizara ya Afya

Kamati ilipokea, kijadili na kuchambua taarifa zifuatazo: -

(i) Taarifa ya Wizara ya Afya kuhusu Utendaji wa Bohari Kuu ya Dawa *(MSD);*

(ii) Taarifa ya Wizara ya Afya kuhusu utendaji wa Taasisi ya Utafiti Dawa za Binadamu *(National Institute for Medical Research – NIMR);* na

(iii) Taarifa ya Wizara ya Afya kuhusu Taasisi ya Dawa na Vifaa vya Kiuchunguzi Tanzania *(Tanzania Medicines and Medical Devices Authority – (TMDA)*.

2.7.2 **Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

**Mheshimiwa Spika,** taarifa za Wizara na Taasisi zake zilizopokelewa na kuchambuliwa ni pamoja na: -

(i) Taarifa ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Utekelezaji wa fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19;

(ii) Taarifa ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere - Kigamboni kwa mwaka wa fedha 2021/22;

(iii) Taarifa ya Utekelezaji wa Mradi wa Jengo la Maabara la Tume ya Nguvu za Atomic Tanzania *(TAEC) – Dodoma;* na

(iv) Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Baraza la Mitihani la Taifa kwa mwaka 2021/2022.

2.7.3 **Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua taarifa ya Wizara kwa taasisi zifuatazo: -

(i) Taarifa ya Wizara ya Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hiyo; na

(ii) Taarifa ya kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole.

2.7.4 **Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua taarifa ya Wizara kwa taasisi zifuatazo: -

(i) Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA);

(ii) Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA);

(iii) Baraza la Michezo la Taifa (BMT); na

(iv) Chuo cha Michezo cha Malya.

2.8 **Hatua zilizofikiwa katika Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa kipindi cha Januari 2021 hadi Februari 2022**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa kipindi cha Februari 2021 hadi Januari 2022 ilitoa mapendekezo mbalimbali ambayo yaliazimiwa na Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Wizara ya Afya jumla ya Maazimio manne (4) yalitolewa. Katika vikao vya Kamati vilivyofanyika mwezi Januari 2023, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa ya utekelezaji wa maazimio hayo na kubaini kuwa kati ya maazimio 4 yaliyotolewa maazimio (3) utekelezaji wake unaridhisha ambayo ni kuhusu Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, mkakati wa kuwalinda na kuwahakikishia Watoto njiti wanapata Bima ya afya, TMDA kufanya ukaguzi wa bidhaa za viwandani na mipaka pamoja na kusimamia Sheria taratibu, kanuni na miongozo ya udhibiti, usambazaji na uuzaji wa dawa nchini utekelezaji wake nao unaridhisha na ni endelevu.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa ya utekelezaji wa maazimio na kubaini kuwa kati ya maazimio saba (7) yaliyotolewa, maazimio mawili (2) utekelezaji wake unaridhisha ambayo ni kukamilisha kwa wakati ujenzi wa Vyuo vya Elimu ya Ufundi Stadi (VETA) na mchakato wa kupitia maoni ya wadau kuhusu mitaala mipya ya elimu ili iweze kupatikana kwa wakati na kuanza kutumika na hivyo kusaidia kuboresha elimu nchini. Maazimio matano (5) utekelezaji wake unaridhisha na ni endelevu. Kamati imejulishwa kuwa Serikali imetoa kibali cha kuajiri Walimu 514 watakopelekwa katika vyuo vya VETA ambavyo ni vipya vinavyojengwa pamoja na vya zamani. Taratibu za kuajiri walimu hao zimeshaanza ambapo hadi mwezi Januari 2023 walimu 151 wameshapatikana na kuripoti katika vituo vya kazi.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa ya utekelezaji wa

maazimio na kubaini kuwa kati ya maazimio matatu (3) yaliyotolewa maazimio mawili (2) utekelezaji wake bado hauridhishi. Changamoto ya bajeti finyu na utolewaji wa fedha usioridhisha umekuwa ukiathiri utekelezaji bora wa majukumu ikiwemo utoaji wa huduma kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na kubaini kuwa maazimio yote (3) yaliyotolewa, utekelezaji wake unaridhisha na unaendelea.

2.9 **Yaliyobainika Wakati wa Ufuatiliaji wa Sekta Zinazosimamiwa na Kamati**

2.9.1 **Wizara ya Afya**

**Mheshimiwa Spika,** kupitia Wizara hii, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa mbili zifuatazo: -

a) **Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA)**

**Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ina jukumu la kulinda afya ya jamii kwa kuhakiki ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi. Kuundwa kwa TMDA ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa Serikali wa kuondoa muingiliano wa majukumu miongoni mwa taasisi za Serikali. Aidha, TMDA imeundwa ili kuongeza tija na ufanisi katika udhibiti wa bidhaa tiba.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini masuala mbalimbali kama ifuatavyo: -

(i) TMDA imerahisisha utoaji huduma kwa wateja, ambapo kwa sasa wateja wanaweza kutuma maombi

yao kwa mtandao kwa kupitia mifumo maalum ya TEHAMA ijulikanayo kama *Regulatory Information Management System* (RIMS) na *Laboratory Information Management System* (LIMS)kupata vibali mbalimbali hususan vya uingizaji bidhaa nchini na usajili wa majengo bila kufika ofisi za TMDA. Kutokana na kuwa na mifumo ya TEHAMA na ya uendeshaji na udhibiti imeifanya TMDA kuwa taasisi ya mfano barani Afrika katika udhibiti wa bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi hivyo kuvutia Mamlaka za udhibiti kutoka nchi mbalimbali kuja kujifunza. Baadhi ya nchi hizo ni Nigeria, Zimbabwe, Rwanda, Sudan Kusini, Kenya, Uganda, Ethiopia, Msumbiji, Mauritius, Ghana, Cameroon, Burundi, Botswana, Lesotho na Bangladesh;

(ii) Mamlaka imeweka mifumo mbalimbali ya udhibiti kabla na baada ya bidhaa kuingia katika soko. Mifumo hiyo ni pamoja na mifumo ya kutathmini na kusajili bidhaa baada ya kukidhi vigezo vya ubora, ufanisi na usalama; mifumo ya kufanya ukaguzi wa viwanda na maeneo yanayojihusisha na biashara za bidhaa zinazodhibitiwa na kudhibiti uingizaji nchini na usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi pamoja na mifumo ya kufanya uchunguzi wa kimaabara na kufuatilia madhara yatokanayo na matumizi ya bidhaa zinazodhibitiwa. Mifumo hii imewezesha Mamlaka kuwahakikishia Watanzania Kuhakikisha ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi;

(iii) Kusimikwa kwa vifaa vya kisasa katika Maabara ya TMDA ambavyo hufanyiwa ugezi *(calibration)* kwa muda unaotakiwa kumewezesha maabara hiyo kufanya kazi kwa ufanisi wa hali ya juu na kuwezesha uchunguzi wa sampuli kufanyika kwa usahihi.

Maabara hiyo ya uchunguzi sasa imekidhi vigezo vya kimataifa na kutambuliwa rasmi na Shirika la Afya Duniani *(WHO Prequalification*). Hii inafanya majibu ya uchunguzi yanayotolewa na Maabara ya TMDA kuaminika na hivyo kutambulika kitaifa na kimataifa. Aidha, kutambuliwa huko kumeiwezesha maabara kupewa zabuni za uchunguzi wa dawa kutoka nchi mbalimbali, mfano Rwanda, Liberia, Kenya na Lesotho;

(iv) Mamlaka imeweza kukusanya **Shilingi bilion 40.07** sawa na **asilimia 106** ya lengo la kukusanya **Shilingi 37.79** kwa mwaka 2021/2022 na hivyo kuiwezesha mamlaka kuchangia **Shilingi bilioni 5.008** kama **asilimia 15** ya mapato ghafi kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali, ambapo **Shilingi milioni 500** zilikuwa ziada ya Mtaji uliozidi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

(v) TMDA imeajiri watumishi 28 wa ajira ya mkataba, na kufanya kuwa na jumla ya watumishi 46 wa Mkataba. Hadi mwezi Septemba, 2022 Mamlaka inajumla ya watumishi 293;

(vi) Mamlaka imepata cheti cha umahiri cha kiwango cha ISO 9001: 2015 katika mifumo ya utendaji ya udhibiti wa bidhaa na kuendelea kushikilia cheti hicho mwaka hadi mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo yaliyofikiwa na TMDA, kumekuwepo na changamoto ambazo kwa namna moja ama nyingine zinaathiri utendaji bora wa TMDA. Changamoto hizo ni: -

(i) Upungufu wa watumishi hususan wakaguzi katika vituo vya forodha ambapo Mamlaka imeajiri

wakaguzi wa mkataba katika maeneo haya ili kukabiliana na changamoto;

(ii) Kuchelewa kupata vibali vya kuajiri vya ajira mpya;

(iii) Udhibiti wa mipaka na uingizaji nchini wa bidhaa duni, bandia na ambazo hazijasajiliwa;

(iv) Uchepushaji wa dawa za Serikali kwenye maduka binafsi ya dawa; na

(v) Kuongezeka kwa maduka mengi ambayo hayajasajiliwa na Baraza la Famasi na hivyo kuleta changamoto kubwa kwenye ukaguzi wa dawa zilizohifadhiwa na kuuzwa.

b) **Bohari ya Dawa (MSD)**

**Mheshikmiwa Spika,** Sheria ya Bohari ya Dawa inaipa mamlaka Bohari kutekeleza jukumu la uzalishaji wa bidhaa za afya na hivyo kufanya jumla ya majukumu makuu ya MSD kuwa manne ambayo ni Uzalishaji, Ununuzi, Utunzaji na Usambazaji. Bohari ya Dawa (MSD) inahudumia vituo vya kutolea huduma za afya vya Serikali 7,158 kupitia kanda zake 10 za Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza, Mtwara, Tanga, Tabora, Dodoma, Iringa, Mbeya na Kagera zinazohudumia nchi nzima, kuanzi ngazi ya Zahanati, vituo vya afya na hospitali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea taarifa ya utendaji ya Bohari ya Dawa iliyoishia mwezi Juni, 2022. Kutokana na taarifa hiyo, Kamati imebaini masuala mbalimbali kama ifuatavyo: -

(i) Hali ya Upatikanaji wa bidhaa za afya muhimu 290 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ulikuwa ni wa wastani kwa asilimia 49. Hii ikiwa ni athari ya janga la UVIKO 19 na uwezo mdogo wa wazalishaji wa ndani;

(ii) Kwa Kipindi cha kuanzia Januari 2022 hadi Agosti 2022, MSD kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imetekeleza afua kadhaa ikiwa ni pamoja na: -Kuwasilisha ajenda ya Mpango wa Ununuzi wa pamoja wa bidhaa za afya kwa Nchi wanachama wa SADC kwenye Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa SADC uliofanyika Lilongwe, Malawi Machi 2022. Katika mkutano huo MSD na Sekretarieti ya SADC zilielekezwa kuandaa Mpango kazi wa kuharakisha utekelezaji wa ununuzi wa pamoja wa bidhaa za afya kwa ajili ya Nchi wanachama wa SADC. Mpango kazi huo uliwasilishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa SADC uliofanyika Agosti 2022, Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Tayari MSD imefanya mazungumzo na Nchi tatu za SADC ambazo ni; Eswatini, Zimbabwe na Lesotho,

(iii) Kuandaa mikataba ya muda mrefu 146 yenye jumla ya bidhaa za afya 1,618 itakayohakikisha upatikanaji endelevu wa bidhaa za afya. Katika mikataba hii ipo inayohusisha bidhaa muhimu 214 kati ya 290 zinazopimwa na Wizara ya Afya;

(iv) Ufungaji wa mashine mpya za vifaa vya maabara na vitendanishi vyake katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini na kushusha gharama kwa zaidi ya asilimia 50. Mashine 1,187 zimefungwa na kuanza kutumika katika vituo vya afya nchini. Mashine 1,119 zinatarajiwa kufungwa kuanzia robo ya kwanza

ya mwaka wa fedha 2022/2023 ili kukamilisha awamu ya kwanza;

(v) Kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma ya kusafisha damu kwa wagonjwa wa figo kwa gharama nafuu. Kwa sasa mashine za kusafisha Damu zimefungwa katika hospitali za Amana RRH, Sekouture RRH na UDOM. Aidha mashine hizo zinatarajiwa kusimikwa katika hospitali za Temeke, Mwananyamala, Tumbi, Mawenzi, Chato ZRR na Mbeya RRH baada ya miundombinu kukamilika.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo, MSD inakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

(i) Hadi kufika mwezi Julai 2022, MSD ilikuwa inadai jumla ya **Shilingi bilioni 277.24** kutoka deni la **Shilingi bilioni 269.35** mwaka 2021. Deni hili linatokana na gharama za ugomboaji, utunzaji na usambazaji wa bidhaa za Afya za Miradi Msonge *(Vertical Program)* zinazohusiana na Malaria, Ukimwi na Kifua kikuu;

(ii) Kushindwa kuhudumia wateja kulingana na maombi ya mahitaji waliyowasilisha, ikiwa ni pamoja na kupeleka bidhaa pungufu au kuzifikisha kwa kuchelewa katika vituo vya kutolea huduma vya afya;

(iii) Ukosefu wa mtaji utakaoiwezesha MSD kuwa na fedha endelevu za kununua bidhaa za afya kulingana na mahitaji;

(iv) Maoteo yasiyokuwa na uhalisia ya bidhaa za afya kutoka vituo vya kutolea huduma za afya ambayo husababisha malalamiko ya wateja, kuisha muda wa

matumizi kwa bidhaa za afya zikiwa ghalani na kuzuia mzunguko wa fedha ya mtaji;

(v) Athari za mnyororo wa ugavi unaotokana na Janga la UVIKO – 19 ambazo zimesababisha wazalishaji wengi kuchelewa kuleta bidhaa za afya kwa wakati;

(vi) Kupanda kwa bei ya mafuta kunatokana na migogoro ya kivita hivyo kuongeza gharama za usambazaji na kuathiri bajeti ya taasisi;

(vii) Kupokea misaada ya bidhaa za afya za mradi msonge ambazo MSD tayari inazalisha; na

(viii) Ukosefu wa fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa viwanda.

c) **Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu NIMR**

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu utekelezaji wa miradi ya tafiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, NIMR imetekeleza miradi ya utafiti mkubwa, wa kati na midogo ipatayo 126 kwa kipindi cha mwaka 2021/2022. Miradi hii imetekelezwa na vituo vyote vya NIMR kwa kuzingatia vipaumbele vya magonjwa yanayoisumbua jamii yetu hapa nchini na kwingineko duniani. Kati ya miradi 126, zaidi ya asilimia 60 ya miradi yote ilitafiti juu ya maradhi ya kuambukiza yakiongozwa na; Malaria (miradi 19), Ukimwi (19), Kifua kikuu (17), na magonjwa ya kitropikia yaliyokuwa hayapewi kipaumbele (15). Asilimia saba (7%) tu ya miradi yote ilitafiti juu ya maradhi yasiyoambukiza.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu utekelezaji wa tafiti za afya na maadili ya ufanyaji tafiti za afya nchini. Taasisi ya Taifa ya

Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya utafiti na maendeleo katika sekta ya afya kwa mujibu wa sheria, hii ikiwa ni pamoja na udhibiti na uratibu wa utekelezaji wa tafiti za afya nchini, kuhamasisha matumizi ya matokeo ya tafiti, kufanya na kukuza utafiti wa tiba asilia na tiba mbadala Ili kuweza kufikia Dira na kutimiza Dhima na Malengo ya Taaasisi na Taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa miradi ya ujenzi NIMR imekamilisha ujenzi wa jengo jipya la uzalishaji wa dawa zinazotokana na mimea asilia ambalo limegharibu takribani **Shilingi milioni 736.2** kupitia bajeti ya mapato ya ndani, msaada wa fedha toka COSTECH na bakaa za fedha za maendeleo za miaka ya nyuma. Ujenzi wa jengo jipya la dawa zitokanazo na mimea ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama tawala (CCM) 2020 – 2025, Ibaraya 84(d) kuhusu kuanzisha kituo kikubwa cha utafiti wa mimea dawa na kuanzisha kiwanda cha kimkakati cha kuzalisha dawa zitokanazo na mimea ya asili.

Aidha, kwa upande wa usimikaji wa mitambo, jumla ya mashine/mitambo mitano (5) tayari imeshanunuliwa kupitia Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kwa gharama ya **Shilingi 535,565,000/** na mchakato wa usimikwaji unaendelea.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo NIMR inakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo za kibajeti kama ifuatavyo: -

(i) Wadau wa utafiti kuchelewa kutoa fedha au kutoa fedha pungufu tofauti na makubaliano ya awali;

(ii) Kuchakaa kwa miundombinu mbalimbali ya utafiti na ofisi kama vile mashine za maabara, magari na majengo;

(iii) Kuendelea kulipa kodi ya pango kwa vituo visivyo na majengo yake ya Ofisi ikiwemo kituo cha NIMR Muhimbili;

(iv) Upungufu wa rasilimali watu kwa baadhi ya kada zikiwemo kada za udaktari, ufamasia, wataalam wa mimea na mitidawa, wataalam wa bioteknolojia za afya, wataalam wa mitambo ya uzalishaji, wataalam wa maabara za afya, mipango, tehama na Sheria; na

(v) Kuchelewa kwa usimikaji wa Mitambo katika kiwanda cha Uzalishaji wa Tiba Asili.

**Mheshimiwa Spika,** NIMR inakabiliwa na changamoto kadhaa katika utendaji wake kama ifuatavyo: -

(i) Wadau wa utafiti kuchelewa kuleta fedha au kuleta fedha pungufu tofauti na makubaliano ya awali na wakati mwingine fedha hiyo inatekeleza vipaumbele tofauti na vya wakati huo;

(ii) Kuchakaa kwa miundombinu mbalimbali ya utafiti na ofisi kama vile mashine za maabara, magari na majengo - hasa kwa kituo cha utafiti Amani Hill, kwa upande wa majengo;

(iii) Kuendelea kulipa kodi ya pango kwa vituo visivyo na majengo yake ya Ofisi ikiwemo kituo cha NIMR Muhimbili;

(iv) Upungufu wa rasilimali watu kwa baadhi ya kada zikiwemo kada za udaktari, ufamasia, wataalam wa mimea na mitidawa, wataalam wa bioteknolojia za afya, wataalam wa mitambo ya uzalishaji, wataalam wa maabara za afya, mipango, tehama na Sheria. Hata hivyo tunaishukuru Serikali kwa kutupa kibali cha kuajiri watumishi wapya 11 wakiwemo - Wanasayansi 10 na Tehama 1; na

(v) Kuchelewa kwa Usimikaji wa Mitambo katika kiwanda cha Uzalishaji wa Tiba Asili. kutokana na Wataalam wa Kichina Kushindwa kusafiri kuja nchini kusimika Mitambo husika kutokana na kuwepo kwa sheria kali za udhibiti wa mlipuko wa UVIKO-19, nchini China, hivyo kuwanyima fursa ya kusafiri kuja Tanzania.

2.9.2**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

**Mheshimiwa Spika**, kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa tatu zifuatazo: -

a) **Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania *(Tanzania Atomic Energy Commission - TAEC)***

**Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la kuanzishwa kwa Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania (TAEC) ni kusimamia, kudhibiti na kuhamasisha matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia nchini. TAEC imepewa majukumu mbalimbali ambayo kwa ufupi yapo kwenye mafungu makuu mawili ambayo ni: -

(i) Kudhibiti na kusimamia matumizi ya teknolojia ya nyuklia pamoja na vyanzo vyote vya mionzi ili kulinda afya za wafanyakazi, wagonjwa na

wananchi kwa ujumla dhidi ya madhara yanayoweza kusababishwa na vyanzo hivyo; na

(ii) Kuendeleza *(promote)* na kuhamasisha matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TAEC imeendelea na jitihada za kusogeza huduma karibu na wananchi ili kurahisisha upatikanaji wa huduma zake sawa na Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Nyuklia (2003); Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa (2021/22 – 2025/26) na Mpango Mkakati wa TAEC (2018/2019 - 2022/2023) pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020/2025 Ibara ya 101(h) vinavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha huduma zinasogezwa karibu na wananchi, TAEC imefungua Ofisi ya Kanda ya Kati Jijini Dodoma tarehe 25 Februari, 2021 kwa ajili ya kuhudumia mikoa ya Dodoma, Singida, Iringa na Tabora. Aidha, ili Tume iweze kutoa huduma bora kwa wananchi, Serikali imetenga kiasi cha **Shilingi bilioni 3.8** kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo hilo litakalokuwa na ofisi 27, chumba cha mikutano chenye uwezo wa kuchukua watu 115, kantini itakayochukua watu 44 na maabara tano ambazo zitatumika kwa madhumuni yafuatayo: -

(i). Maabara ya kupima sampuli za vyakula na mazingira;

(ii). Maabara ya kupima na kutathmini ya viwango vya mionzi kwa wafanyakazi;

(iii). Maabara ya matengenezo ya vifaa vya nyuklia;

(iv). Maabara ya maandalizi ya sampuli; na

(v). Kituo cha usalama wa kinyuklia.

**Mheshimiwa Spika,** kukamilika kwa ujenzi wa jengo hili, kutafanikisha azma ya kuhamishia Makao Makuu ya TAEC Jijini Dodoma, ambapo pamoja na manufaa ya kusogezea huduma karibu na jamii na kupunguza gharama za utawala ikiwemo gharama za vikao ambavyo kila wakati inalazimu manejimenti na wajumbe wa bodi kusafiri kwa ajili ya kushughulikia mambo mbalimbali. Vilevile, manufaa mengine ya kukamilika kwa jengo la Makao Makuu Dodoma ni:-

(i). Kuimarika kwa usalama wa kinga ya mionzi kwa watu na mazingira hivyo kuchangia ipasavyo maendeleo ya kijamii na kiuchumi;

(ii). Kuchangia nchi kufaidika kutokana na teknolojia za nyuklia katika nyanja za afya, kilimo, mifugo, ujenzi wa barabara, maji na viwanda;

(iii). Kusogeza huduma ya upimaji wa sampuli za vyakula na mazingira na kuongeza ufanisi zaidi;

(iv). Huduma ya upimaji wa viwango vya mionzi kwa wafanyakazi wa hospitali na viwanda zitaimarika;

(v). Uhifadhi wa sampuli utaimarika zaidi; na

(vi). Utengenezaji wa vifaa vya mionzi utafanyika kwa ufanisi.

b) **Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere**

**Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kilianzishwa kwa sheria ya Bunge namba 6 ya mwaka 2005. Chuo kina kampasi mbili-Kivukoni (Dar es Salaam) na Kampasi ya Karume-Zanzibar na kina Tawi Pemba katika Wilaya ya Chakechake. Aidha, Chuo kinakusudia kufungua matawi mengine kanda ya magharibi katika Wilaya ya Tanganyika, Mkoa wa Katavi na Kanda ya kati katika jiji la Dodoma ambapo tayari chuo kimepata maeneo ya kujenga. Lengo la Chuo ni kusogeza huduma karibu na wahitaji.

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 Chuo kiliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 25,492,597,859.00.** Katika mwaka huo huo Chuo kilikadiria kukusanya **Shilingi 14,338,981,220.00** kutokana na vyanzo mbalimbali ikiwepo malipo ya ada, ushauri elekezi, kazi za utafiti na utoaji wa huduma mbalimbali. Hadi mwezi Septemba,2022 Chuo kilikuwa kimekusanya S**hilingi bilioni 11.5** sawa na asilimia 80 ya lengo.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile miradi mbalimbali ya maendeleo imekuwa ikitekelezwa. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa mabweni mawili ya wanafunzi yenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 1,536 katika Kampasi ya Karume ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022 kulitengwa jumla ya **shilingi 1,000,000,000.00** fedha za maendeleo kutoka Serikali Kuu. Hadi kufika tarehe 30 Juni 2022.Chuo kilikuwa kimepokea jumla ya **shilingi 1,315,624,580.12** sawa na **asilimia 132**. Aidha, majengo yote yanayotarajiwa kujengwa katika Chuo hicho yatagharimu jumla ya Shilingi **15,530,812,531.84.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilibaini kuwa Chuo kilitumia kiasi cha **Shilingi 3,786,859,005.24** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Fedha za Maduhuli. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Chuo kilitengewa kiasi cha **shilingi 4,800,000,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa fedha za ndani. Hadi wakati wa kuwasilisha taarifa hii Chuo kilikuwa kimepokea **asilimia 79** ya fedha hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafaniko hayo, Chuo kinakabiliwa na changamoto ya upungufu wa watumishi kulingana na mahitaji, mfano kampasi ya Pemba pekee ina upungufu wa watumishi waendeshaji na wanataaluma 59. Vilevile, changamoto nyingine ni kutokutosheleza kwa fedha za ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ya chuo kulingana na mahitaji.

c) **Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya Uviko-19**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19 (TCRP) ilitengewa kiasi cha **Shilingi bilioni 64.902** kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya ujenzi na ukarabati wa madarasa, mabweni, kumbi za mihadhara katika Vyuo vya Ualimu na Vyuo vinavyotoa Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini. Hadi Septemba, 2022 Kamati Wizara ilitoa taarifa kuwa ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi bilioni 63.46** sawa na **asilimia 97.7** ya fedha hizo. Sehemu ya fedha hizo ilielekezwa katika ununuzi wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu wenye mahitaji maalumu. Vilevile, sehemu ya fedha hizo iliwezesha uchapaji wa

vitabu kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu (wasioona na wale wenye uoni hafifu) katika ngazi ya Elimu ya Sekondari.

**Mheshimiwa Spika,** fedha hizo zililenga kutumika kwa ajili ya kukamilisha ujenzi Vyuo vinne (4) vya VETA ngazi ya Mkoa (RVTSC), ujenzi wa jengo la maabara la Arusha Technical Collage- ATC na mabweni mawili ya Chuo cha Waalimu wa VETA MVTTC Morogoro. Vilevile zililenga kutumika kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Vyuo 25 vya VETA vya Wilaya pamoja na uwekaji wa samani mbalimbali katika vyuo 25 vya Wilaya na kwa ajili ya umaliziaji wa ujenzi wa vyuo 25 vya Wilaya.

**Mheshimiwa Spika,** fedha hizo pia zimetengwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika Vyuo 34 vya Maendeleo ya Wananchi, ununuzi wa vifaa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu wa Elimu ya Juu, uchapaji wa vitabu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu, pamoja na ujenzi miundombinu katika vyuo vya Ualimu

**Mheshimiwa Spika,** katika taarifa yake kwa Kamati Wizara ilitaarifu kuwa fedha hizo zimewezesha umaliziaji wa ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Rukwa, ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Njombe, umaliziaji wa ujenzi wa Chuo cha Ufundi stadi na Huduma cha Mkoa wa Geita, ujenzi wa Chuo cha Ufundi stadi na Huduma cha Mkoa wa Simiyu. Umaliziaji wa Jengo la Madarasa, Maabara na Ofisi katika Chuo cha ufundi Arusha, umaliziaji na ujenzi wa mabweni mawili katika Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi Mkoa wa Morogoro, umaliziaji wa ujenzi wa vyuo 25 vya VETA Wilaya.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa mafanikio haya kwani Kamati imebaini kuwa maeneo yote fedha ilikopelekwa utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa ulifikia asilimia zaidi ya themanini (80%).

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo, kumekuwepo na changamoto mbalimbali za utekelezaji wa miradi hii; mfano, mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Rukwa ambapo changamoto kubwa ilikuwa ni kushindwa kupatikana kwa vifaa vya ujenzi kwa wakati kutoka viwandani kutokana na uhitaji mkubwa wa vifaa hivyo katika miradi mbalimbali ya ujenzi. Aidha, miradi iliathirika kwa ongezeko la bei za vifaa vya ujenzi ukilinganisha na gharama zilizoainishwa awali *(Schedule of Materials)* wakati wa kuwasilisha maombi ya fedha za kukamilisha mradi.

**Mheshimiwa Spika**, baadhi ya miradi utekelezaji wake uliathiriwa na mvua kubwa iliyonyesha katika kipindi cha mwezi Januari hadi Aprili 2022 ambayo ilisababisha uharibifu wa miundombinu na shughuli za ujenzi kushindwa kutekelezwa kwa wakati. Hali hii iliathiri umaliziaji wa ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Geita na ujenzi wa Chuo cha Ufundi stadi na Huduma cha Mkoa wa Njombe, ujenzi wa Chuo cha Ufundi stadi na Huduma cha Mkoa wa Simiyu.

Aidha, kuchelewa kwa unganishwaji wa umeme kwenye maeneo ya mradi, hali iliyosababisha kuchelewa kwa kazi zilizohitaji kutekelezwa kwa kutumia nishati ya umem. Hali kadhalika kuchelewa kuunganishwa/kupatikana maji kwenye maeneo ya mradi, hali iliyosababisha kuchelewa kwa kazi na kuongeza gharama za ujenzi kwa mfano, Ikungi, Monduli, Kwimba, Pangani na Ulanga.

### 2.9.3 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Wizara hii unafanyika kwa kupitia Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, mradi wa ukarabati na ujenzi katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Rungemba. Tayari Taasisi imekamilisha ujenzi wa kumbi pacha za mihadhara *(lecture theatre two in one)* zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 568, zilizogharimu kiasi cha **Shilingi 993,087,150.63**, pia Taasisi inaendelea kukamilisha ujenzi wa bweni la wasichana la ghorofa nne 4 utakaogharimu **Shilingi 1,712,252,281.31** mpaka mradi utakapokamilika katika Taasisi ya Maendeleoya Jamii Tengeru.

**Mheshimiwa Spika,** miradi mingine inayosimamiwa na Wizara hii ni pamoja na; Ujenzi wa Hosteli ya wanafunzi kampasi ya Kisangara yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 100 utakaogharimu **Shilingi 400,000,000,** ujenzi wa Maktaba ya kisasa unaotekelezwa na SUMA JKT utakaogharimu **shilingi 464,000,000** yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 800, na uboreshaji wa miundombinu katika Vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Jamii Buhare, Mlale, Misungwi, Mabughai, Monduli, Rungemba, Ruaha na Uyole.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mapato Wizara katika mwaka 2022/2023, inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 8,500,000,000** kutokana na ada za wanafunzi katika Vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Jamii vya Buhare, Uyole, Rungemba, Mlale, Misungwi, Ruaha, Mabughai na Monduli; na ada za mwaka na faini kutoka Mashirika yasiyo ya Kiserikali kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 pamoja na

marekebisho yake. Aidha Wizara inatarajia kutumia **Shilingi 43,403,061,000**. Wizara pia imetengewa kiasi cha **Shilingi 45,000,000,000** maalum kwa ajili ya wafanyabiashara ndogondogo (Machinga) kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa miundombinu katika masoko na kuwawezesha kupata mitaji ya kuendeleza biashara zao ili kuanzisha miradi ya kiuchumi katika sekta za mifugo, kilimo, uvuvi, madini na nyinginezo. Fedha hizi zimewekwa kwenye Fungu 21 la Wizara ya Fedha na Mipango. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa hatua hii muhimu kwa wafanyabiashara za uchuuzi nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine Wizara ilitekeleza jukumu lake la kuhamasisha na kuelimisha kuhusu ulinzi wa mtoto. Ni ukweli usiopingika kuwa watoto ni sehemu muhimu ya jamii na ndiyo tegemeo la Taifa lolote, hivyo wanahitaji kukua, kufikia utimilifu wao na hatimaye kuwa raia wema. Kwasababu hiyo wanatakiwa kupewa malezi stahiki na mahitaji yao ya msingi ikiwa ni pamoja na kuwezeshwa kuishi, kulindwa, kuendelezwa, kushirikishwa na kutobaguliwa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwepo kwa haki hizo za msingi za watoto, Kamati imebaini kuwa bado vitendo vya ukatili dhidi ya watoto vimeendelea kuongezeka hapa nchini. Kwa mujibu wa taarifa ya Jeshi la Polisi mwaka 2021 jumla ya matukio 11,429 ya ukatili kwa watoto yalitolewa taarifa kupitia vituo mbalimbali vya Polisi. Baadhi ya matukio makubwa ni ubakaji (5,899), mimba kwa wanafunzi (1,677), ulawiti (1,114), kuzorotesha mwanafunzi masomo (790) na mashambulio ya kimwili (350).

**Mheshimiwa Spika**, katika kutatua changamoto hii, Serikali imeandaa na kutekeleza Mwongozo wa Taifa wa

Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto ambao unaotumika kuanzisha na kusimamia madawati uendeshwaji wa madawati katika shule za msingi na sekondari hapa nchini. Hatua nyingine zilizochukuliwa ni pamoja na:-

(i) Kuratibu utekelezaji wa Kampeni ya Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii (SMAUJATA) katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara kwa lengo la kuhamasisha jamii kutokomeza ukatili dhidi ya watoto;

(ii) Kuratibu huduma ya simu bila malipo kwa watoto wanaofanyiwa vitendo vya ukatili na unyanyasaji *(Child Helpline)* Na.116 ili kuwezesha watoto na jamii kutoa taarifa ya vitendo vya ukatili kwa haraka; na

(iii) Kushirikiana na Wadau wa Maendeleo kuandaa rasimu ya vitini vya elimu ya athari za ukatili dhidi ya watoto kupitia mtandao vinavyolenga kujenga uelewa wa wazazi, walimu na wanafunzi kuhusu umuhimu wa matumizi sahihi ya TEHAMA ikiwemo vifaa vya kieletroniki kama vile simu na kompyuta.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu kutekeleza Programu Jumuishi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau kutambulisha Programu hiyo kwenye Mikoa 7 kati ya 10 ya kipaumbele. Mikoa hiyo ni Tabora, Lindi, Morogoro, Arusha, Manyara, Mbeya na Rukwa. Katika mikutano hiyo ya utambulisho, kila Mkoa na Halmashauri zake imeandaa Mpango wa Utekelezaji wa Programu kulingana na mazingira ya Mkoa husika.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mambo mengine Wizara pia Wizara imeendelea kutekeleza Programu mbalimbali za kuleta usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake ili kuongeza fursa za kiuchumi na kuwajengea uwezo wa kibiashara, mbinu za kupata mitaji, masoko na mikopo, kuboresha huduma za ustawi wa jamii kwa kuimarisha utoaji huduma kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi wakiwemo, kusimamia utoaji huduma za ustawi katika mahabusu tano (5) za watoto za Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha na Dar es Salaam, kutoa huduma za malezi ya kambo na kuasili kwa watoto walio katika mazingira hatarishi kwa kuhakikisha kuwa watoto wanalelewa katika ngazi ya familia kulingana na Sheria ya Mtoto Sura ya 13 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019, pamoja na kuendelea kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma za msingi kwenye makao ya watoto ikiwemo malazi, chakula, malezi, matunzo, ulinzi, afya na elimu kwa watoto walio katika mazingira hatarishi nchini.

Vilevile Wizara pia imeendelea kutoa huduma za msingi za chakula, malazi, mavazi na matibabu kwa wazee wasiojiweza wanaoishi katika makazi 14 ya wazee yanayomilikiwa na Serikali na kusimamia na kuratibu kutolewa kwa huduma za msingi kwa wazee kwenye makazi 20 ya wazee ya Taasisi binafsi katika Mikoa 11 ya Kagera, Lindi, Njombe, Dar es Salaam, Tabora, Morogoro, Dodoma, Tanga, Pwani, Shinyanga na Mara.

Aidha, Wizara, imeendelea kuratibu huduma ya afya ya akili, msaada wa kisaikolojia na kijamii, kuendelea kuratibu huduma za usuluhishi wa ndoa na migogoro

ya familia kupitia Baraza la Usuluhishi wa Ndoa la Kamishna Makao ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wa Kamati umebaini changamoto mbalimbali zinazoikabili Wizara hii kama zifuatazo: -

(i) Upungufu wa rasilimali watu ngazi ya jamii hususani Maafisa Ustawi wa Jamii (21,204) na Maafisa Maendeleo ya Jamii (2,322);

(ii) Ukosefu wa taarifa na takwimu za wafanyabiashara ndogondogo hali inayosababisha Serikali kushindwa kuwatambua na kuwaunganisha na fursa mbalimbali za maendeleo;

(iii) Kuendelea kuwepo kwa mila na desturi zenye madhara katika baadhi ya jamii kunakosababisha kuendelea kwa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake, watoto na wazee;

(iv) Udhaifu wa mifumo ya utoaji wa baadhi ya huduma za msaada kwa wahanga wa ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto hali inayosababisha waathirika wa vitendo vya ukatili kutopata huduma stahiki kwa wakati;

(v) Baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kushindwa kuwa endelevu hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Sheria za nchi;

(vi) Uwepo wa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi wakiwemo watoto waliopoteza mzazi au wazazi; watoto waliotelekezwa; watoto walio katika mkinzano na sheria pamoja na wanaoishi na kufanya kazi mitaani;

(vii) Uchakavu na upungufu wa miundombinu ya kujifunzia na kufundishia katika Vyuo nane vya Maendeleo ya Jamii, Taasisi ya Ustawi wa Jamii na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii - Tengeru; na

(viii) Uchakavu wa miundombinu ya kutolea huduma katika vituo vya ustawi wa jamii ikiwemo makazi 14 ya wazee, mahabusu 5 za watoto, Makao ya Taifa ya Watoto Kurasini na Shule ya Maadilisho Irambo;

2.9.4 **Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Wizara hii, Kamati ilipokea, ilichambua na kujadili taarifa ya Wizara pamoja na Taasisi zilizo chini ya usimamizi wake kama ifuatavyo: -

a) **Baraza la Michezo la Taifa (BMT)**

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wa taarifa ya Baraza la Michezo Tanzania (BMT) iliyowasilishwa mbele ya Kamati mwezi Agosti, 2022, Kamati ilibaini kuwa BMT imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa kuridhisha. Miongoni mwa mafanikio yaliyofikiwa ni pamoja na:-

(i) Ongezeko la makusanyo ya mapato ambapo BMT ilikadiria kukusanya **Shilingi 300,000,000** kwa mwaka 2021/2022. Hadi kufika mwezi Juni, 2022, BMT ilikuwa imekusanya **Shilingi 488,658,310** sawa na **asilimia 163** ya lengo lililowekwa. Kamati imejulishwa kuwa ongezeko la makusanyo hayo limetokana na kuongezeka kwa mbinu na jitihada mbalimbali za makusanyo;

(ii) Kuwezesha timu za Taifa zinaposhiriki mashindano mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa, ambapo jumla ya timu 14 zimewezeshwa. Timu hizo ni pamoja na netiboli, riadha, kikapu, wavu, judo, ngumi, karate, kuogelea n.k;

(iii) Kusajili vyama na vilabu vya michezo ambapo Katika kipindi cha mwaka 2021/22, BMT imefanikiwa kusajili jumla ya vilabu 207, vyama vya michezo 20, vituo vya michezo 15, akademia 12, taasisi 12 na mawakala na wakuzaji 38;

(iv) Kutoa Mafunzo ya Michezo kwa Walimu wa Michezo. Katika jitihada za kuimarisha michezo katika jamii na kupunguza tatizo la uhaba wa wataalamu wa michezo, BMT kwa kushirikiana na vyama/ Mashirikisho ya michezo lilitoa mafunzo kwa walimu na makocha wa michezo 64 katika mkoa wa Mara kuanzia tarehe 22 Februari hadi 04 Machi, 2022;

(v) Kusimamia Chaguzi za Vyama/Mashirikisho ya Michezo. Moja ya jukumu la BMT ni kuhakikisha vyama/mashirikisho ya michezo yanaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora ikiwemo viongozi kuchaguliwa kwa njia ya kidemokrasia. Katika kufanikisha hilo, Baraza limesimamia chaguzi kwa

vyama na mashirikisho saba (7) yakiwemo: - Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI); Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA); Shirikisho la Mpira wa Kikapu; Chama cha Mpira wa Mikono Tanzania; Chama cha Mpira wa Wavu Tanzania, Shirikisho la Michezo la Mashirika ya Umma na Taasis-SHIMMUTA na Chama cha Kusimamia Ngumi za Kulipwa Tanzania ambapo usimamizi wa uchaguzi umefanywa kwa mujibu wa Katiba zao; na

(vi) Kuidhinisha/kutoa vibali vya kufanya shughuli za michezo kwa vyama/vilabu vya michezo, kuratibu Mfuko wa Maendeleo ya Michezo pamoja na kufanya kikao kazi cha mwaka cha maafisa michezo wa Mikoa na Wilaya nchini.

**Mheshimiwa Spika,** BMT inakabiliwa na changamoto ya rasilimali watu ambapo kwa mujibu wa ikama BMT inatakiwa kuwa na jumla ya watumishi hamsini na saba (57). Hadi kufika mwezi Septemba 2022, BMT ilikuwa na watumishi ishirini nan ne (24) na hivyo kupungukiwa watumishi thelathini na 33 sawa na asilimia hamsini na nane (58).

b) **Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Sheria Na.23 ya mwaka 1984, Baraza la Sanaa la Taifa linawajibika kutekeleza majukumu yafuatayo: -
Kubeba dhamana ya kufufua na kukuza sanaa nchini, kufanya tafiti za masuala mbalimbali yahusuyo Sanaa, kutoa ushauri na misaada ya kiufundi kwa wasanii na wadau wa Sanaa, kuandaa na kuratibu matukio ya sanaa nchini, kutengeneza Kanuni za kusimamia ubora wa kazi za sanaa, kuishauri Serikali juu ya mambo

yahusuyo maendeleo ya sanaa nchini na kutoa mafunzo kwa wasanii na Wadau wa Sanaa nchini kwa lengo la kuwajengea uwezo.

**Mheshimiwa Spika**, Baraza la Sanaa la Taifa pamoja na limefanikiwa katika masuala mbalimbali ikiwemo, kurejesha tuzo za muziki, kutengeneza mfumo wa kielektroniki wa Usajili na Usimamizi wa Taarifa za wasajiliwa. Aidha, mafanikio mengine ni pamoja na

(i) Kushiriki katika Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara Sabasaba mwaka 2021 na 2022, ambapo jumla ya wasanii 14 wa Sanaa za Ufundi walionesha bidhaa zao kupitia banda lililoandaliwa na BASATA. Aidha, Baraza lilihamasisha wasanii wa vyama vingine 34 kushiriki maonesho haya;

(ii) Kuratibu chaguzi za mashirikisho ya Sanaa na vyama vyake ambapo Baraza limesajili mashirikisho ya sanaa manne (4);

(iii) Kutoa vibali kwa Wasanii kuingia na kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kuendesha shughuli za Sanaa ambapo Baraza limetoa jumla ya vibali 111 vya wasanii wa ndani 287 kwenda nje ya nchi kufanya shughuli za Sanaa. Pia Baraza limetoa vibali 34 kwa wasanii 194 waliongia nchini kutoka nje ya nchi;

(iv) Kuimarisha mifumo rafiki ya utoaji huduma pamoja na utambuzi wa wasanii na wadau wa sekta ya sanaa nchini, Baraza kwa kushirikiana na Serikali Mtandao (eGA) limeunda mfumo wa kielektroniki wa usajili na utoaji wa vibali mtandaoni ambapo muda wa msanii kupata huduma za usajili na vibali umepungua kutoka siku 3 hadi nusu saa tu endapo nyaraka zote

zinazohitajika zitapakiwa kwa wakati katika mfumo huu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa pamoja na mafanikio yaliyopatikana, BASATA inakabiliwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na: -

(i) Ufinyu wa Rasilimali Fedha, BASATA inakabiliwa na uhaba wa rasilimali fedha jambo linalosababisha kushindwa kutekeleza baadhi ya shughuli zinazopangwa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vituo vya sanaa *(Art Centers)* na vituo vidogo vya sanaa *(Community centers)* katika ngazi za Mikoa na Wilaya; na

(ii) kwa upande wa watumishi, kwa mujibu wa ikama, Baraza linatakiwa kuwa na watumishi themanini (80). Hadi mwezi Agosti, 2022 Baraza lilikuwa na watumishi (40), na hivyo kuifanya BASATA kuwa na upungufu wa watumishi 40 ikiwa ni sawa na asilimia 50.

c) **Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA)**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa sheriaTaasisi ya Hakimili Tanzania (COSOTA) inatekeleza majukumu yake kama ifuatavyo: -

Kukuza na kulinda maslahi ya watunzi, waandishi, wasanii, wafasiri, watayarishaji wa kurekodi sauti, watangazaji, wachapishaji, na hususani kukusanya na kugawa mirabaha yoyote au ujira unaotolewa kulingana na haki zao zilizoelezwa katika sheria ya Hakimiliki. Aidha, jukumu lingine ni kutunza rejesta za kazi, usanii na vyama vya watunzi, wasanii, wafasiri, watayarishaji wa sauti

zilizorekodiwa, watangazaji na wachapishaji. Kufuta, kubainisha, na kutangaza haki za wamiliki na kutoa uthibitisho wa umiliki wa haki pale inapotokea ubishani au ukiukwaji wa haki. Vilevile, kuchapa, kuchapisha, kutoa au kueneza habari, taarifa, jarida, vitabu, vitini, vipeperushi vyovyote au maandiko mengine yoyote yanayohusiana na hakimiliki na haki za wasanii, watayarishaji na vihifadhia sauti na watangazaji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kupitia COSOTA kwani katika kipindi cha mwaka 2022/2023 imefanikiwa kukusanya mirabaha itokanayo na leseni kiasi cha **Shilingi 285,320,000** na kufanikiwa kufanya mgao wa mirabaha ya jumla ya **Shilingi 312,290,259** kwa wasanii na wabunifu wa Hakimiliki 1,123. Aidha, kupitia usajili wa wasanii na wadau wengine, COSOTA imekusanya ada za usajili wa kazi za wanachama kiasi cha **Shilingi 61,889,000**.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile COSOTA ilifanya maboresho katika Sheria ya Hakimiliki ya Mwaka 2022. Marekebisho hayo yamefanya mabadiliko ya Muundo wa COSOTA ili kuruhusu uwepo wa Ofisi ya Hakimiliki na Vyama vya wadau. Vyama vya wadau vitaanzishwa na wadau wenyewe ili kukusanya na kugawa mirabaha ambapo Ofisi ya Hakimiliki itasimamia masuala ya hakimiliki ikiwepo kusimamia vyama hivyo. Sambamba na mafanikio hayo, COSOTA pia imefanikiwa kufanya mapitio ya Kanuni za Utumishi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/22 na Kanuni za Ukusanyaji na ugawaji mirabaha kama ilivyopangwa.

**Mheshimiwa Spika**, pia COSOTA imefanya maboresho katika mfumo wa utoaji wa leseni na usajili wa wanachama kidijitali. Aidha, kusimika mifumo ya TEHAMA

na kuanza kutumia mfumo wa ulipaji Serikalini (MUSE). Pia, COSOTA imefunga LAN na kutoa mafunzo kwa watumishi juu ya matumizi ya mifumo hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, katika kipindi cha mwaka 2022 COSOTA ilikabiliana na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Kukosekana kwa mifumo ya utambuzi ambapo COSOTA haina mifumo thabiti ya kiteknolojia ya kufuatilia matumizi na mapato ya watumiaji wa kazi za sanaa na ubunifu zinazosimamiwa na Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Namba 7 ya mwaka 1999 kama ilivyorekebishwa mwaka 2019. Kutokana na kasi ya ukuaji wa teknolojia, kuna uhitaji mkubwa wa uwekezaji katika mifumo inayoendana na kasi hiyo katika usajili, utambuzi, ukusanyaji (utoaji wa leseni) na ugawaji mirabaha unaoendana na maelekezo ya Serikali ya kuhakikisha kuwa hakimiliki inasimamiwa zaidi ili kuhakikisha kuwa wasanii na wadau ambao ni wamiliki wa kazi zinazolindwa na Sheria ya Hakimiliki wananufaika kutokana na ubunifu wa kazi zao;

(ii) Kukosekana Muundo wa Kitaasisi kulingana na COSOTA ilifanya maboresho yaliyofanyika katika Sheria ya Hakimiliki ya Mwaka 2022;

(iii) Uhaba wa Watumishi, pamoja na kuwa katika kipindi cha mwaka 2022 watumishi wameongezeka kutoka 15 hadi 28, bado COSOTA ina upungufu wa watumishi hasa kitengo cha ununuzi na vitengo vinavyohusika moja kwa moja na utekelezaji wa majukumu ya Taasisi (*technical staff*). Katika kipindi cha zaidi ya miaka miwili COSOTA haina watumishi katika kitengo cha

ununuzi na ugavi ambacho ni muhimu sana kwa Taasisi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla baada ya uchambuzi wa kina wa Kamati, imebainika kuwa katika taasisi zote zilizowasilisha taarifa zake mbele ya Kamati (Baraza la Michezo Tanzani, Baraza la Sanaa na Taasisi ya Hakimiliki Tanzania) changamoto kubwa ni upungufu wa watumishi jambo ambalo linaonekana kuzirudisha nyuma taasisi hizi katika majukumu yake kwa mujibu wa sheria zilizounda taasisi hizo pamoja na dira na dhima za taasisi hizo.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo ya kina kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Kamati pamoja uchambuzi wake naomba kuwasilisha Maoni na Mapendekezo ya Kamati ambayo Bunge lako Tukufu litayaazimia kwa ajili ya utekelezaji wa Serikali.

#### 3.1.1 Hali ya Ukatili wa Kijinsia Nchini

**KWA KUWA,** Kumekuwepo ongezeko kubwa la ukatili wa kijinsia nchini hasa kwa vitendo vya ubakaji na ulawiti,

**NA KWA KUWA,** Kuwepo kwa changamoto hii kumeongeza uwepo wa ulemavu wa kudumu, maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na wakati mwingine kusababisha vifo na hofu kubwa katika jamii,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inasisitiza ushauri wake kwamba Bunge liishauri Serikali,

(i) Kufanya utafiti wa kina kujua nini chanzo cha ongezeko la ukatili wa kijinsia nchini hususani kwa wanawake na Watoto;

(ii) Kuzifanyia marekebisho Sheria zote zinazohusu adhabu za makosa haya ili zitolewe adhabu kali kwa wale wote watakaohusika na ufanyaji wa vitendo vya ukatili hususan kwa Watoto na wanawake; na

(iii) Kuweka Mkakati wa ukusanyaji wa takwimu halisi za matukio yote ya ukatili wa kijinsia nchi nzima ili kujua ukubwa halisi wa tatizo hili.

3.1.2 **Ukatili wa Watoto Shuleni**

**KWA KUWA,** Kumekuwepo na ongezeko kubwa la matendo ya ukatili kwa watoto wawapo shuleni ama wakiwa njiani kuelekea shuleni,

**NA KWA KUWA,** Kuwepo kwa ukatili huu kwa watoto shuleni kunaweza kusababisha matokeo yasiyoridhisha, kuongezeka kwa utoro, magonjwa, ulemavu changamoto ya afya ya akili pamoja na hofu kwa wazazi,

**KWA HIYO BASI,** Bunge liishauri Serikali;

Kuweka mikakati thabiti na kuhakikisha vitendo hivi vinatokomezwa kwa kudhibiti vyanzo vyake ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kunawekwa madawati ya jinsia katika taasisi zote zinazotoa elimu nchini, kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu na katika Ofisi zote za Serikali.

3.1.3 **Upungufu wa Watumishi**

**KWA KUWA**, katika Wizara zote zinazosimamiwa na Kamati hii kumebaikina kuwa na changamoto ya upungufu mkubwa wa watumishi hasa wauguzi, madaktari, walimu, wahadhiri n.k,

**NA KWA KUWA**, Upungufu huu wa watumishi umekuwa ukileta athari katika utoaji wa huduma mbalimbali hata wakati mwingine kuchelewesha baadhi ya miradi kuanza katika muda uliopangwa,

**KWA HIYO BASI,** Bunge liishauri Serikali kutoa kipaumbele cha ajira katika Sekta hizi muhimu ili kuzinusuru.

3.2 **Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

3.2.1 **Upungufu wa Walimu Nchini**

**KWA KUWA** Sekta ya Elimu imekuwa na upungufu mkubwa sana wa watumishi, na hasa walimu,

**NA KWA KUWA** upungufu wa watumishi katika sekta ya elimu umekuwa ukileta athari katika utoaji wa huduma mbalimbali za elimu nchini ikiwemo matokeo yasiyoridhisha;

**KWA HIYO BASI,** Bunge liishauri Serikali kutoa kipaumbele cha ajira kwenye Sekta ya elimu kwa kuajiri walimu wa kutosha ili kuondoa ombwe la ukosefu wa walimu.

3.2.2 **Utengwaji na Utolewaji wa Fedha**

**KWA KUWA,** Kumekuwa na utengwaji finyu na usioridhisha wa bajeti kwa ajili ya Sekta ya elimu,

**NA KWA KUWA,** hali hii imekuwa ikiathiri utekelezaji bora wa majukumu ya Wizara, ikiwemo utoaji huduma,

**KWA HIYO BASI**, Bunge liishauri Serikali kuendelea kuongeza tengeo la bajeti kwa ajili ya Wizara ya Elimu.

### 3.2.3 Hali ya Ubora wa Elimu nchini

**KWA KUWA,** Imeonekana kuwa hali ya elimu nchini imeendelea kutoridhisha, hali inayofanya wanafunzi kushindwa kuwa na ufaulu mzuri na pia kushindwa kuajirika mara baada ya kumaliza masomo,

**NA KWA KUWA**, Serikali imeamua kupitia upya mtaala wa elimu kwa ngazi zote, ya msingi, sekondari na ualimu,

**KWA HIYO BASI,** Bunge liishauri Serikali,

(i) Kuendelea na mchakato wa kukamilisha utungwaji wa mitaala; na

(ii) Wizara ione namna ya kuharakisha jambo hili bila kuathiri ubora.

### 3.2.4 Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu

**KWA KUWA**, kiwango cha fedha kinachotolewa na Serikali kwa ajili ya kugharamia mikopo ya elimu bado hakitoshelezi mahitaji,

**NA KWA KUWA**, kukosekana kwa mikopo hiyo kunasababisha wanafunzi wengi kushindwa kuendelea na masomo yao ya juu,

**KWA HIYO BASI**, Bunge liishauri Serikali kuongeza bajeti ya Bodi ya Mikopo ili wanafunzi wengi wa elimu ya juu waweze kunufaika.

3.2.5 **Chuo cha Ualimu Mtwara**

**KWA KUWA,** Kwa muda mrefu sasa takribani miaka kumi na tisa (19), Serikali haijatimiza azma yake ya kukibadili Chuo cha Ualimu Mtwara kuwa Chuo Kikuu,

**NA KWA KUWA,** Kutokubadilishwa Chuo hiki kuwa Chuo Kikuu kumeleta athari ya kukosekana kwa wataalam, hasa walimu wa ngazi ya shahada na hivyo kuchelewesha malengo ya utekelezaji wa mipango ya Serikali kuhusu kukuza elimu nchini,

**KWA HIYO BASI,** Bunge liishauri Serikali,

(i) Kuendeleza mchakato wa kubadili Chuo cha Ualimu Mtwara kuwa Chuo Kikuu Kishiriki ili kutimiza azma yake,

(ii) Pamoja na malengo yaliyopangwa, Serikali iangalie namna ya kuweka kozi kulingana na mahitaji ya wakati huu.

3.2.6 **Vyuo vya Kati**

**KWA KUWA,** Vyuo vya Kati vimekuwa vikidahili idadi ndogo ya wanafunzi kutokana na wanafunzi wengi wengi kushindwa kugharamia ada masomo katika vyuo hivyo,

**NA KWA KUWA,** Kutokana na uzalishaji mdogo wa wanafunzi wa vyuo vya kati kumekuwa na ombwe kubwa la kuwapata wataalam ambao ndio injini ya uzalishaji wa bidhaa muhimu na mafundi *(technical skills expertise)* kwa ajili ya uzalishaji wa viwandani,

**KWA HIYO BASI,** Bunge liishauri Serikali kuanza kutoa mikopo kwa wanafunzi wa Vyuo vya kati ili kuweza kuzalisha wataalam wa kutosha wa kufanya kazi kwenye viwanda na kutoa huduma.

### 3.2.7 **Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere – Kivukoni, Dar es Salaam**

**KWA KUWA,** Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kinatoa kozi chache na ni zile zinazohusu sayansi ya jamii *(social sciences)* tu,

**NA KWA KUWA,** Uwepo wa kozi chache zitolewazo na Chuo hiki kunapunguza wigo wa utolewaji wa elimu stahiki inayohitajika kwa mazingira ya sasa,

**KWA HIYO BASI**, Bunge liishauri Serikali kukielekeza Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kuangalia uwezekano wa kuongeza kozi nyingine kama vile kozi za TEHAMA na nyinginezo ili kuongeza wigo wa utoaji elimu stahiki kwa mazingira na wakati wa sasa wenye ushindani wa kiteknolojia lakini pia kutanua wigo wa udahili.

### 3.2.8 **Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Nyerere – Butiama**

**KWA KUWA,** Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Nyerere – Butiama kimekaa takriban miaka kumi

na minne (14) bila kudahili wanafunzi licha ya kuwepo kwa wakufunzi na watumishi,

**NA KWA KUWA,** Hali hii imesababisha Chuo kutotimiza malengo yake na hivyo kutoleta thamani ya matumizi ya fedha za umma *(value for money)*,

**KWA HIYO BASI,** Bunge liishauri Serikali,

(i) Kupitia upya namna, utaratibu na sababu za kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Nyerere – Butiama;

(ii) Kuweka Mkakati wa kutekeleza haraka malengo ya kuanzishwa kwa chuo hiki;

(iii) Ichunguze kama vipo vyuo vingine vyenye changamoto kama hii ili kuepusha upotevu wa rasilimali fedha na rasilimali watu; na

(iv) Aidha, rasilimali watu iliyopo katika Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Nyerere – Butiama ipelekwe kwenye vituo vyenye uhitaji ili kuipa nafasi Serikali kukiweka chuo hicho katika mazingira stahiki ya kuanza kudahili wanafunzi na baadaye kuwarejesha mara baada ya chuo kuwa tayari.

3.2.9 **Tume ya Nguvu za Atomiki**

**KWA KUWA,** Majengo ya Ofisi ya Makao Makuu ya Tume ya Nguvu za Atomiki Jijini Dodoma yamejengwa nje ya mji na mbali na makazi ya watu,

**NA KWA KUWA,** Kutokana na ofisi za Tume hii zilizojengwa Makao Makuu Dodoma kuwa mbali na makazi ya watu kutasababisha changamoto ya usafiri kwa watumishi;

**KWA HIYO BASI,** Bunge liishauri Serikali,

(i) Serikali kuipa fedha za kutosha Tume ya Nguvu za Atomiki ili iweze kujenga nyumba za makazi kwa ajili ya watumishi, na

(ii) Serikali kuharakisha mchakato wa uhamiaji Makao Makuu Dodoma ili wananchi wa Dodoma na Taifa kwa ujumla, wapate huduma zinazotolewa na Tume hii kama ilivyopangwa.

3.2.10 **Ujenzi wa miradi ya miundombinu ya elimu nchini**

**KWA KUWA**, Miradi mingi ya elimu inachelewa kuanza kutokana na changamoto zinazotokana na kutokamilika kwa huduma ambata kama vile majengo ya nyumba za walimu na udahili wa wanafunzi,

**NA KWA KUWA**, Kuchelewa kwa miradi hii kumekuwa kikiathiri thamani halisi ya fedha *(value for money),* pamoja na kusababisha wanafunzi wanaohitaji kujiunga na shule hizi kushindwa kujiunga na hivyo baadhi yao kuishia mitaani,

**KWA HIYO BASI,** Bunge liishauri Serikali,
Mchakato wa uanzaji wa miradi hii iende sambamba na mkakati wa miradi ambata kama vile majengo ya nyumba za walimu, ajira za walimu, vyoo na udahili wa wanafunzi ili mara tu mradi unapokamilika na huduma hizi zianze. Aidha, kwa maeneo yote ambayo shule tayari zimejengwa, Serikali iharakishe ujenzi wa miradi ambata.

### 3.2.11 Ukosefu wa majengo ya mabweni kwa wanafunzi wa shule za Kata

**KWA KUWA** wanafunzi wengi wanaojiunga na shule za kata, hasa wasichana wamekuwa wakikumbana na matukio ya ukatili wa kijinsia kutokana na kutembea umbali mrefu njiani wanapokwenda ama kurudi shuleni,

**NA KWA KUWA** Kutokana na wanafunzi hao kukumbana na changamoto hizo wengi wamekuwa wakiacha shule na hasa wanafunzi wa kike kupata mimba,

**KWA HIYO BASI**, Bunge liishauri Serikali kuweka mkakati wa kujenga mabweni katika shule zote za kata ili kuwawezesha wanafunzi wa kike kusoma katika mazingira rafiki na huru hatimae kuwa na Taifa lenye ustawi.

### 3.2.12 Hali duni ya utoaji wa chakula shuleni

**KWA KUWA**, Wanafunzi wengi katika shule za Serikali hawapati chakula shuleni,

**NA KWA KUWA,** kukosekana kwa chakula shuleni ni sababu mojawapo ya utoro,

**KWA HIYO BASI,** Bunge liishauri Serikali;

Kuzingatia suala la chakula katika shule zote na kufanya mapitio na usimamizi wa mwongozo wa lishe shuleni ili kuhakikisha kunakuwapo na chakula jambo litakalofanya wanafunzi kuwa na utulivu katika mazingira ya shule.

## 3.3 Wizara ya Afya

3.3.1 **Utengwaji na Utolewaji wa Fedha**

**KWA KUWA,** Kumekuwa na utengwaji finyu na utolewaji wa fedha usio wa wakati,

**NA KWA KUWA,** Bajeti finyu na utolewaji wa fedha usio wa wakati umekuwa ukiathiri utekelezaji bora wa majukumu ya Wizara, ikiwemo utoaji huduma kwa wananchi,

**KWA HIYO BASI**, Bunge liishauri Serikali kutenga fedha za kutosha, lakini pia kuhakikisha fedha hizo zilizoidhinishwa na Bunge zinatolewa zote na kwa wakati ili kuleta ustawi bora wa huduma kwa wananchi.

3.3.2 **Uingizwaji nchini wa bidhaa bandia za chakula, dawa na Vipodozi**

**KWA KUWA**, Pamoja na Serikali kujitahidi kudhibiti bidhaa bandia za chakula na dawa bado bidhaa hizo bandia zimekuwa zikionekana kwa wingi katika maduka mbalimbali hapa nchini;

**NA KWA KUWA**, Uwepo wa bidhaa bandia umekuwa ukiathiri afya za watu na kusababisha magonjwa hivyo kupoteza nguvu kazi na kurudisha nyuma maendeleo ya nchi,

**KWA HIYO BASI,** Bunge liishauri Serikali Serikali;

(i) Kuhakikisha inadhibiti mipaka ya kuingia nchini ili kulinda usalama na afya za Watanzania,

(ii) Serikali kuwajumuisha wafamasia kwenye kanzidata, hasa wale ambao wako kwenye

taasisi binafsi ili kuweza kudhibiti kwa urahisi utoaji wao wa huduma,

(iii) Kuiwezesha TMDA kuwa na wataalam wake yenyewe wa mambo ya dawa, na

(iv) Udhibiti wa mambo ya chakula uondolewe kutoka TBS na kurejeshwa tena TMDA.

3.3.3 **Bohari Kuu ya Dawa (MSD)**

**KWA KUWA**, MSD inadai madeni makubwa ambayo bado yanaongezeka lakini ulipwaji wake ni wa kusuasua sana,

**NA KWA KUWA,** Kutolipwa kwa madeni hayo, na kuongezeka kwa madeni hayo kunasababisha MSD kutotekeleza majukumu yake ipasavyo na hivyo kusababisha kilio kwa wananchi juu ya kutopatikana kwa dawa hospitalini na katika hospitali,

**KWA HIYO BASI,** Bunge liishauri Serikali kwamba Bohari kuu ya Dawa iandae mikakati ya ziada ili kuhakikisha madeni yaliyopo na yanayoongezeka y kupatiwa ufumbuzi wa kudumu.

3.3.4 **Uwekezaji wa viwanda vya dawa na vifaa tiba kufanywa na Bohari ya Dawa**

**KWA KUWA,** Kumekuwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa dawa muhimu na za msingi za binadamu, hasa ikitokea majanga mbalimbali ya kidunia, kama vile wakati wa janga la UVIKO – 19,

**NA KWA KUWA**, Kutokana na kutopatikana huko kwa dawa kumekuwa kukisababisha kuzorota kwa huduma

katika sekta ya afya na kusababisha madhara makubwa kwa wananchi,

**KWA HIYO BASI,** Bunge liishauri Serikali,

(i) Kuweka mikakati thabiti ya kushirikisha sekta binafsi *(Public Private Partinership-PPP)* pamoja ya kuweza na kurahisisha uwekezaji wa viwanda wa vifaa tiba pamoja dawa nchini ili kukidhi soko la nje na ndani na pia kupunguza gharama uagizaji wa dawa kutoka nje ya nchi,

(ii) MSD ifanye mchakato wa haraka wa uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na pamba ili kupunguza uagizwaji wa bidhaa hizo kutoka nje ya nchi kwa kuwa malighafi ya bidhaa hizo (yaani zao la Pamba) linapatikana hapa nchini.

3.3.5 **Dawa za Asili**

**KWA KUWA** Kumekuwa na dawa za aina nyingi za asili zinazouzwa maeneo mbalimbali nchini,

**NA KWA KUWA,** Uwepo wa dawa hizi ambazo zinauzwa kiholela na wananchi kuzitumia bila kujua kama zina ubora, madhara na faida yake, kwani baadhi yake zinakuwa hazijafanyiwa utafiti,

**KWA HIYO BASI,** Bunge liishauri Serikali;

(i) Kwa kupitia Taasisi Utafiti wa Dawa nchini (NIMR) kufanya tatifi wa ubora athari na matumizi salama ya dawa hizo,

(ii) Kupitia NIMR iweke mfumo wa kuhifadhi tafiti zote zinazofanyika nchini ili kujua na kutumia tafiti zote zinazofanyika kwa maslahi ya Taifa,

(iii) Kuweka mpango mkakati wa kutenga fedha kutoka vyanzo vya ndani kwa ajili ya kufanya tafiti badala ya kutegemea fedha kutoka kwa wafadhili wa nje ili kufanya tafiti nyingi zaidi,

(iv) NIMR iwekeze tafiti zaidi katika magonjwa yasiyoambukiza kwa kuwa magonjwa hayo kwa sasa yanachangia asilimia kubwa zaidi ya vifo vya Watanzania.

3.4 **Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo**

3.4.1 **Uibuaji wa vipaji katika jamii**

**KWA KUWA,** kumekuwepo na vipaji vingi vya sanaa katika jamii ambavyo havijatambuliwa rasmi,

**NA KWA KUWA,** wasanii hawa chipukizi ikiwa wangetambuliwa rasmi na kusimamiwa vema wangeweza kuwa bora na kuongeza idadi ya wasanii hatimae kuongeza mapato yatokanayo na kazi za kisanii,

**KWA HIYO BASI**, Bunge liishauri Serikali kuendelea kuweka na kuratibu mikakati maalum ya kusimamia na kuibua na uendelezaji wa vipaji.

3.4.2 **Viwanja vya Michezo nchini**

**KWA KUWA,** Kumekuwepo na uchakavu pamoja na uhaba wa viwanja vya michezo nchini,

**NA KWA KUWA**, Uchakavu na uhaba wa viwanja katika maeneo mengi nchini huduma za sekta ya michezo,

**KWA HIYO BASI,** Bunge liishauri Serikali;

(i) Ishirikiane na wadau wengine wa michezo kuona namna ya kukarabati na kujenga viwanja vingine katika maeneo ambayo hayana viwanja vya michezo,

(ii) Kwa upande wa Sekta binafsi, Serikali iweke mfumo maalum utakaotumika kuwahimiza wamiliki wa viwanja vya michezo binafsi kufanya ukarabati na kuviboresha mara kwa mara ili vikidhi ubora unaotakiwa, na

(iii) Serikali kuweka mkakati wa kufuatilia uwepo wa viwanja vya michezo kwenye kila shule.

### 3.4.3 **Vazi la Taifa na Mdundo wa Taifa**

**KWA KUWA,** Mchakato wa kupata vazi la Taifa umekuwa wa muda mrefu;

**NA KWA KUWA,** kutokuwa na vazi la Taifa na pia kutokuwa na mdundo wa muziki wa Taifa letu kunalinyima Taifa utambulisho kwenye mambo haya muhimu ya Utamaduni;

**KWA HIYO BASI,** Bunge liishauri Serikali;

Kuhakikisha upatikanaji wa vazi la Taifa kwani mchakato umekuwa wa muda mrefu. Vilevile, kuhakikisha inaratibu upatikanaji wa mdundo wa mziki wa Taifa kwa kushirikisha tamaduni zote nchini.

### 3.4.4 **Chuo cha Michezo Malya**

**KWA KUWA,** Udahili katika chuo hiki kwa upande wa wanawake bado ni mdogo ukilinganishwa na wanaume,

**NA KWA KUWA,** kutokana na hali hiyo kumesababisha uwepo wa uwiano usio sawa wa wataalam michezo nchini,

**KWA HIYO BASI,** Bunge liishauri Serikali;

(i) Kuweka mkakati madhubuti wa kukitangaza Chuo cha Michezo Malya hasa kwa wasichana;

(ii) Kutenga fedha zaidi kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la Bweni la wanafunzi wa kike;

(iii) Kuweka mikakati ya kukitangaza chuo hiki kwa wananchi ili kiweze kupata udahili wa wanafunzi wengi zaidi.

## 3.5 **Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum**

### 3.5.1 **Watoto wa Mitaani**

**KWA KUWA,** Tatizo la Watoto wa mitaani limeendelea kuwepo,

**NA KWA KUWA,** Kuendelea kuwepo kwa Watoto mitaani kumesababisha Kuongeza kwa vitendo vya uhalifu na kufanyika kwa ukatili wa Watoto,

**KWA HIYO BASI,** Bunge liishauri Serikali;
Kuweka mikakati ya kutoa elimu kwa jamii kuhusu changamoto hii na namna jamii inavyoweza kukabiliana nalo ikiwa ni pamoja kusambaza Mwongozo wa Uwezeshwaji kwa Wanawake.

3.5.2 **Afya ya akili**

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA,** Kumekuwa na ongzeko kubwa la changamoto ya afya ya akili nchini,

**NA KWA KUWA,** Ongezeko hili la changamoto ya afya ya akili linasababisha ongezeko la matendo ya ukatili,

**KWA HIYO BASI,** Bunge liishauri Serikali,

Kuangalia changamoto hii kwa jicho la pekee na kuhakikisha madawati ya ushauri nasaha yanaboreshwa na kuwa karibu na jamii ili kutoa kutoa elimu ya masuala yote yanayohusu changamoto ya afya ya akili na namna ya kuzikabili.

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine naomba kuchukua nafasi hii tena kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, nakupongeza kwa kazi kubwa unayofanya ya kuliongoza Bunge letu vizuri. Namshukuru pia Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi nzuri wanayofanya.

**Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii kuwashukuru Mawaziri wote waliopo katika Wizara zinazosimamiwa na Kamati ambao ni Mhe. Ummy Ally Mwalimu (Mb) – Waziri wa Afya, Mhe. Prof. Adolf Mkenda (Mb) – Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima (Mb) - Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Mhe. Mohamed Omari Mchengelwa (Mb) – Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Aidha ninawashukuru Naibu Mawaziri wa Wizara zinazosimamiwa na Kamati, ambao ni; Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel (Mb) – Naibu Waziri wa Afya, Mhe.Omary Juma Kipanga (Mb) – Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Mwanaidi Ali Khamis (Mb) – Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Mhe. Paulina Philip Gekul (Mb) – Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa kwa Kamati. Aidha, nawashukuru Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu wa Wizara hizi zote tatu kwa ushirikiano mzuri wanaoutoa kwa Kamati wakati wote.

**Mheshimiwa Spika,** namshukuru sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Aloyce John Kamamba (Mb) kwa ushirikiano anaonipa mimi pamoja na Kamati kwa ujumla. Kipekee zaidi nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano walionipa katika kutekeleza shughuli za Kamati na hivyo kurahisisha kazi yangu.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Aloyce John Kamamba, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb - Mjumbe

4. Mhe. Eng. Samweli Hhayuma, Xaday Mb - Mjumbe
5. Mhe. Husna Juma Sekiboko, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Tecla Mohamedi Ungele, Mb - Mjumbe
7. Mhe.Rose Cyprian Tweve, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Kassim Hassan Haji, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Francis Leonard Mtega, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Jumanne Abdallah Sagini, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Latifa Khamis Juakali, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Kabula Enock Shitobela, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Bernadeta Kasabago Mushashu, Mb- Mjumbe
15. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Neema Kichiki Lugangira, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Mussa Ramadhani Sima, Mb - Mjumbe
18. Mhe. George Ranwell Mwenisongole, Mb – Mjumbe
19. Mhe. Dkt. Paulina Daniel Nahato, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Salome Wycliffe Makamba, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Abdallah Dadi Chikota, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Khamis Kassim Ali, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Hassan Zidadu Kungu, Mb - Mjumbe
25. Mhe. Nashon William Bidyanguze, Mb - Mjumbe
26. Mhe. Hamisi Shabani Taletale, Mb - Mjumbe
27. Mhe. Anastazia James Wambura - Mjumbe
28. Mhe. Neema Mwandabila - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru sana Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc,* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Pamoja nao namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein *ndc*, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati Ndg. Happiness Ndalu, Ndg Emmanuel Mdidi, Ndg. Hosiana John pamoja na msaidizi wa Kamati Ndg. Jane Ndulesi

kwa kuisaidia Kamati wakati wote na kwa kuratibu vyema shughuli zote za Kamati.

**4.2 Hoja**

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

Stanslaus Haroon Nyongo, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII**
2 Februari, 2023

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana.

Sasa kabla sijamuita Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, yupo mgeni ambaye ameingia baada ya tangazo la wageni na huyu ni Ndugu Muhsin Usi ambaye ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi kupitia Vijana. Huyu ni mgeni wa Mheshimiwa Juliana Masaburi na Mheshimiwa Lucy Sabu. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Abdallah Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2022 hadi Januari, 2023. Naomba Taarifa hii yote iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Majukumu; katika kipindi cha taarifa hii Kamati imeendelea kutekeleza majukumu yake kama inavyoainishwa kwenye Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, Shughuli Zilizotekelezwa na Kamati; katika kipindi cha taarifa hii kamati imetekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Taarifa zilizopokelewa na kujadiliwa kwenye ofisi hii zimeainishwa kwenye ukurasa wa nne na wa tano wa taarifa hii, ikiwepo changamoto kubwa ya migogoro ya ardhi katika Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; kwa upande wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, taarifa zilizowasilishwa na kujadiliwa mbele

ya Kamati zimeainishwa kwenye ukurasa namba tano wa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge; Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kamati imepokea na kujadili taarifa utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa kwa Serikali mwezi Februari, 2022, ambapo kwa asilimia 90 maazimio hayo yametekelezwa na yale yaliyobaki Kamati imefahamishwa kuwa michakato ya utekelezaji wake inaendelea. Taarifa ya utekelezaji wa maazimio hayo imeainishwa kwa kina katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Matokeo ya Uchambuzi wa Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati. Sehemu hii ya taarifa inaeleza kwa ufasaha majukumu yaliyotekelezwa na Kamati kwa kipindi chote cha mwaka mmoja. Uchambuzi wa kina wa matokeo ya shughuli hizo umefanyika kwa kuainisha Wizara, Taasisi na Idara inayohusika na kuonesha mafanikio na changamoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mgogoro wa ardhi katika Jiji la Dodoma; Kamati katika vipindi vitatu tofauti ilikutana na Serikali kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa kuhusu changamoto za migogoro ya ardhi katika Jiji la Dodoma na utatuzi wake. Wakati wa kujadili taarifa zilizowasilishwa, mambo kadhaa ambayo yamekuwa yakilalamikiwa na baadhi ya wananchi walioathirika katika zoezi la utwaaji wa ardhi katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma yaliibuliwa. Hata hivyo baadhi hayakupatiwa ufafanuzi wa kina kutoka kwa mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifahamishwa kwamba, katika kutatua migogoro hiyo Kamati ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Kamati ya Mkuu wa Wilaya ya Dodoma na Kamati ya Madiwani ziliundwa na watumishi wapatao 22 wa Sekta ya Ardhi waliotuhumiwa kusababisha mgogoro walihamishwa, japokuwa bado kumekuwepo na malalamiko kutoka kwa wananchi wa Jiji la Dodoma. Kamati inaona kwamba, utaratibu uliotumika kutatua migogoro hiyo haukuwa wa haki kwa kuwa wataalam waliodaiwa kusababisha migogoro ndio hao hao waliokuwepo katika timu ya utatuzi wa migogoro waliyoisababisha.

Mheshimiwa Spika, ni rai ya Kamati kuwa Serikali iendelee kutatua migogoro hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa Mradi wa Mabasi Yaendaya Haraka (*DART)*. Kamati inaipongeza Serikali kwa uwekezaji huo mkubwa. Miundombinu iliyowekeza imechangia kuongeza haiba ya mwonekano wa mandhari wa Jiji la Dar es Salaam na kuleta faida mbalimbali kama zilivyooneshwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, mradi huu una changamoto mbalimbali ikiwepo changamoto kubwa ya ukosefu wa sheria ambayo uwepo wake ungepelekea mradi kuwa na nguvu ya kisheria ya kiusimamizi na maamuzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati pamoja na kupokea na kujadili taarifa za Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini *(TARURA,)* ilikaguwa ujenzi wa barabara katika Wilaya ya Mufindi na Kilolo Mkoani Iringa zilizojengwa kwa sababu ya kusafirisha mazao ya mboga mboga na matunda

kutoka maeneo ya uzalishaji kwenda katika masoko. Kamati inaipongeza *TARURA* kwa kukamilisha ujenzi wa barabara hizo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi hiyo nzuri iliyofanywa na *TARURA,* Kamati imebaini uwepo wa changamoto kubwa ya uwepo wa magari yenye uzito wa zaidi ya tani 30 yanayopitishwa kwenye barabara hizo. Kutokana na uwepo wa zao kubwa la biashara la mbao katika maeneo zilizopo barabara hizo, hali inayosababisha uharibifu mkubwa wa barabara hizo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi, Wabunge, Halmashauri na Wadau mbalimbali nchini kuhusu ucheleweshaji wa kuanza kazi za barabara unaosababishwa na Wakandarasi kutokuwepo uwandani baada ya kuingia mikataba na kukabidhiwa mradi. Ucheleweshaji wa kuanza au kukamilika kwa miradi unatokana na taratibu za manunuzi na mabadiliko ya majira hasa nyakati za mvua pamoja na ucheleweshaji wa utekelezaji wa masharti ya mkataba kama vile utolewaji wa msamaha kwa wakandarasi kama vile *exemption*.

Mheshimiwa Spika, Kamati pamoja na mambo mengine, inasisitiza kwamba Serikali kwa upande mmoja na Mkandarasi kwa upande mwingine waheshimu na kutekeleza makubaliano waliyoingia katika mkataba ili kuharakisha utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Masoko Kariakoo linamiliki mali zenye thamani ya Shilingi bilioni 56 zikiwemo Soko Kuu la Kariakoo na maeneo mengine; Tabata Bima, *Mbezi Beach* Makonde. Pamoja na Shirika kutekeleza majukumu yake kwa mafanikio, limekuwa likikabiliana na

changamoto kadhaa zikiwepo upungufu katika Sheria ya Shirika ambayo unaathiri utekelezaji na uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa toka ilipoanzishwa mwaka 1965 hadi kufikia mwaka 2020 imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 14.66 kwa Halmashauri 57 ikiwa ni sawa na asilimia 30.9 ya Halmashauri zote nchini ambapo hadi kufikia Desemba 2022, Halmashauri 12 bado zinadaiwa madeni yenye thamani ya shilingi bilioni 4.71.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Bodi iliidhinisha mkopo wa shilingi milioni 300 kwa Halmashauri moja tu ya Kisarawe. Hata hivyo, Halmashauri hiyo haikupewa mkopo huo kwa sababu ya mabadiliko ya uongozi ambayo yamesababisha kuchelewa kusaini mkataba.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kupokea na kujadili taarifa ya utoaji na urejeshaji wa mikopo ya asilimia kumi katika makundi wa Vijana, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu katika baadhi ya Halmashauri nchini. Aidha, Kamati ilitembelea Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam kwenda kukagua utendaji wa vikundi hivyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada na mafanikio hayo yaliyopatikana na Serikali katika utekelezaji wa utoaji wa mikopo kwa makundi hayo, ipo changamoto kubwa ya uwepo wa mikopo chechefu. Kamati ilielezwa kuwa, katika kwa kipindi cha mwaka 2017/2018 hadi Desemba 2022, mikopo iliyotolewa kwa vikundi 10,334 imepita muda wa marejesho, yaani mikopo chechefu. vikundi hivyo vilikopeshwa jumla ya shilingi bilioni 42.01 ambapo hadi kufikia Desemba, 2022 jumla ya shilingi

bilioni 19.278 zimerejeshwa sawa na asilimia 46 ya mikopo iliyokopeshwa.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Shule za Sekondari za Kata kupitia mradi wa *SEQUIP*. Wakati wa kujadili taarifa ya ujenzi wa Shule za Sekondari za Kata kutoka Halmashauri 14 za Mikoa Saba nchini, Kamati imebaini kuwepo kwa tofauti kubwa kati ya gharama zilizokadiriwa na gharama halisi baada ya ujenzi kukamilika. Gharama iliyokuwa imekadiriwa ni shilingi milioni 470 kwa shule moja kwa mikoa yote. Kati ya shule ambazo taarifa zake zilijadiliwa na Kamati, zimeonesha tofauti ya gharama *(variation)* kati ya shilingi milioni 52 hadi shilingi milioni 157 zaidi ya gharama iliyokadiriwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Ujenzi wa Shule za Sekondari za Wasichana za Bweni kwa Mikoa kumi awamu ya kwanza, ambapo baadhi ya mikoa ujenzi unakaribia kukamilika. Kama ilivyo katika Shule za Kata, Kamati imebaini viashiria vya kuongezeka kwa gharama kutokana na changamoto mbalimbali katika maeneo ya ujenzi pamoja na kupanda kwa gharama za vifaa vya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imesikitishwa na Uongozi wa Mkoa wa Tanga ambapo baada ya kupelekewa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Shule za Sekondari za Wasichana, wameshindwa kuafikiana kuhusiana na sehemu gani shule ijengwe hadi ikailazimu Wizara kuchukua fedha zile na kuzipeleka katika Mkoa wa Njombe ambapo wanatekeleza mradi huo katika Halmashauri ya Wanging'ombe. Ni rai ya Kamati kuwa mivutano kama hii isiyokuwa na tija, siyo jambo linalofaa katika miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa kuhusu makusanyo ya mapato ya ndani ya halmashauri na upangaji wa fedha za matumizi mengine kwa utaratibu wa asilimia 60 kwa 40 kutegemeana na makusanyo. Kamati ilibaini kuwepo kwa tofauti kubwa katika gharama za uendeshaji wa Halmashauri zenye makusanyo madogo ukilinganisha na zile zenye makusanyo makubwa, hali iliyosababisha Halmashauri zenye makusanyo madogo kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kuhsu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Mpango wa kurasimisha rasilimali za Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA); Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya MKURABITA pamoja na kufanya ziara za ukaguzi wa masijala za ardhi katika Mkoa wa Dodoma na Morogoro. Kamati ilijulishwa kwamba jumla ya wakulima 163,568 walipimiwa mashamba yao na kupewa hati za kimila. Aidha, kwa kutumia rasilimali na biashara zilizorasimishwa, wananchi wamewezeshwa kupata mikopo katika taasisi za kifedha.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kupokea na kujadili taarifa ya taasisi ya Uongozi. Nitumie fursa hii kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutilia mkazo suala la kuwajengea uwezo viongozi ili waweze kuwatumikia wananchi kwa uadilifu na tija. Kamati ilifahamishwa kwamba jumla ya viongozi 5,428 wamepatiwa mafunzo na tumewaona wamebadilika katika uongozi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupokea na kujadili taarifa ya utendaji wa Chuo cha Utumishi wa Umma,

Kamati ilipata wasaa wa kufanya ziara ya ukaguzi wa ujenzi wa maabara ya uchapaji katika Kampansi ya Singida yenye uwezo wa kuchukua wanachuo 210 kwa wakati mmoja. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Chuo hiki, Chuo kinakabiliwa na changamoto ya kutumia majengo ya kupanga katika Kampansi ya Singida, Tanga na Mbeya jambo ambalo linakipa Chuo mzigo mkubwa wa kulipa gharama za pango kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imepokea na kujadili taarifa ya utendaji kazi wa Mfuko wa Maendeleo wa Jamii *TASAF* pamoja na kukagua miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na *TASAF* katika Mkoa wa Njombe na Singida kwa upande wa Tanzanai Bara na Mikoa ya Mjini Magharibi, Kusini Unguja, Kaskazini Pemba kwa upande wa Tanzania Zanzibar. Hadi kufikia Novemba, 2022 jumla ya miradi 550 ya Elimu, Afya, Maji, Mazingira, barabara na ujasiriamali kwa wananchi imeandaliwa. Kati ya miradi hiyo, miradi 41 yenye thamani ya Shilingi bilioni 3.34 imekamilika.

Mheshimiwa Spika, kipekee nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuongeza Bajeti ya *TASAF* ili iweze kuwafikia walengwa wengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na taarifa ya utendaji ya taasisi ya *TAKUKURU* juu ya uanzishwaji wa Mpango wa TAKUKURU rafiki. Kwa kuwa mpango huu unakwenda kuondoa hofu kwa wananchi na kuwaongezea ari ya kushirikiana na Maafisa wa TAKUKURU katika suala zima la kuzuia Rushwa nchini. Kamati inaipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuanzisha mpango huu.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Ndege za Serikali umeendelea kuwahudumia Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kutumia ndege mbili aina ya *Gulfstream G 550 na Fokker F 50* pamoja na kuratibu ununuzi wa ndege za Serikali na kuzikodisha kwa Kampuni ya Tanzania ya Ndege *ATCL.* Aidha, Serikali imeweza kujenga Karakana ya matengenezo ya ndege za Serikali awamu ya kwanza katika uwanja wa ndege wa Dar es Salaam na kuanza utaratibu wa uhamishaji wa ndege *Fokker* 28 ambayo imemaliza muda wake wa masafa ya kuruka angani kwenda Chuo cha usafirishaji cha Taifa *(NIT)* kwa ajili ya mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati kuhusiana na shughuli zilizotekelezwa katika kipindi cha kuanzia Februari, 2022 hadi Januari, 2023 ambayo yanabainisha mitazamo kwa kile kilichojiri wakati Kamati ikitimiza majukumu yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa *(TAMISEMI)*, Migogoro ya Ardhi katika Jiji la Dodoma:-

Kwa kuwa, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi kutokana na kutwaliwa ardhi yao na hivyo kusababisha migogoro ya ardhi baina ya wananchi na Jiji la Dodoma;

Na kwa kuwa, migogoro hiyo imeleta usumbufu mkubwa kwa wananchi kwa kutumia muda mwingi kufuatilia utatuzi wa migogoro na gharama badala ya kufanya kazi nyingine za kiuchumi na kijamii;

Na kwa kuwa, Jitihada za kuunda timu mbalimbali za Mkoa, Wilaya na Jiji la Dodoma kushughulikia migogoro zimeshindwa kupata ufumbuzi;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali ifanye uchunguzi wa kina ili kubaini chanzo cha migogoro na ichukue hatua stahiki kwa wahusika. Aidha, kwa wale ambao itathibitika wamedhulumiwa haki zao kwa namna moja au nyingine, Serikali ihakikishe wanapewa haki yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi kwenye Halmashauri nyingine:-

Kwa kuwa migogoro ya ardhi ni kero kubwa ambapo iko katika Halmashauri nyingi nchini;

Na kwa kuwa, migogoro hiyo imeleta usumbufu kwa wananchi na kuwafanya kutumia muda mwingi na gharama kubwa kufuatilia utatuzi na kuacha shughuli nyingine za kuwaingizia kipato;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ianzishe operesheni maalum ya kutatua migogoro ya ardhi katika Halmashauri zote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa Shirika la Masoko Tanzania:-

Kwa kuwa, Masoko mengi nchini hayawapi wananchi na wakulima unafuu wa maisha kwa sababu ya changamoto za kiuendeshaji zinazowapa fursa madalali kupanga bei za kilanguzi kwenye bidhaa za kilimo hali inayopelekea kupanda kwa bei za bidhaa;

Na kwa kuwa, uendeshaji wa masoko usioridhisha huwasababishia wakulima wengi wanaopeleka mazao yao sokoni kuuza bidhaa zao kwa bei ya hasara;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ilete Muswada wa kuanzisha Shirika la Masoko Tanzania, ambalo litasimamia uendeshaji wa masoko yote nchini.

Mheshimiwa Spika, Utungaji wa Sheria ya Usafiri wa Umma Mijini:-

Kwa kuwa mpaka sasa hakuna Sheria mahsusi ambayo inasimamia usafiri wa Umma mijini na sheria zilizopo hazisimamii moja kwa moja usafiri wa Umma mijini;

Na kwa kuwa, Mradi wa Mabasi yaendayo kwa Haraka Dar es Salaam haujawa na sheria mahususi na hivyo kupelekea mradi kuwa na mwenendo usioridhishwa, miundombinu ya mradi kuvamiwa na magari ya watu binafsi, kushindwa kupanga bei za nauli bila kutegemea mamlaka nyingine hali inayopelekea mradi kushindwa kujiendesha wenyewe kwa faida;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali iharakishe mchakato wa ukamilishaji wa Muswada wa Sheria ya Usafiri wa Umma Mijini na kuwasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini *(TARURA)*. Kuongeza Bajeti ya Dharura ya Matengenezo ya Barabara:

Kwa kuwa Miundombinu ya barabara nyingi za *TARURA* yakiwemo madaraja na vivuko vya waendao kwa miguu vimekuwa vikiharibika nyakati za mvua

Na kwa kuwa, hali hiyo huwasababishia wananchi usumbufu mkubwa wa kushindwa kutumia au kutumia kwa shida barabara nyakati za mvua na kusababisha hasara kwenye vyombo vyao vya moto au kushindwa kupata huduma mbalimbali za kiuchumi na kijamii;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali itenge bajeti ya kutosha ya dharura kwa kila Wilaya ili kukabiliana na uharibifu unaojitokeza kwenye barabara nyakati za mvua.

Mheshimiwa Spika, Kujenga Miundombinu ya barabara yenye uwezo wa kuhimili uzito zaidi ya tani 10:-

Kwa kuwa, miundombinu ya barabara za TARURA zinaharibika mara kwa mara na magari yenye uzito ama yenye kusafirisha bidhaa zenye uzito mkubwa;

Na kwa kuwa, uharibifu huo unaisababishia Serikali hasara ya fedha kwa kuelekeza fedha nyingi kwenye matengenezo ya miundombinu za barabara zinazoharibiwa pamoja na kusababisha usumbufu kwa wananchi wanaotumia miundombinu ya barabara hizo;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ifanye mabadiliko ya viwango vya ujenzi wa uzito unaohitajika kwenye miundombinu ya barabara za *TARURA* kwa kutengeneza miundombinu ya barabara unaoweza kubeba uzito wa tani 30 au zaidi.

Mheshimiwa Spika, miradi ya ujenzi wa shule za sekondari nchini:-

Kwa kuwa, Serikali imekuwa ikipanga gharama sawa za ujenzi wa Shule za Sekondari kwa nchi nzima;

Na kwa kuwa, gharama halisi baada ya kukamilika kwa mradi zimeongezeka sana ukilinganisha na gharama zilizokadiriwa, hali inayosababishwa na tofauti ya bei za vifaa vya ujenzi, upatikanaji wa madini ya ujenzi na jiografia ya maeneo husika;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali ifanye tathmini ya gharama halisi za ujenzi Kikanda.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Mamlaka ya Serikali Mtandao *(e-GA)*:-

Kwa kuwa, kumekuwa upungufu wa wataalamu wenye taaluma ya mifumo ya TEHAMA katika ngazi mbalimbali Serikalini;

Na kwa kuwa, Upungufuo huo umesababisha kuzorota au kuchelewesha utoaji wa huduma mbalimbali kwa wananchi;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali ianzishe Programu ya vituo vya kukuza vipaji vya *TEHAMA (incubation centers)* kwa vijana waliohitumu masomo ya TEHAMA ili kutoa fursa za ajira kwa vijana ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa niaba ya Kamati, napenda kutoa shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagana, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Mheshimiwa Angellah Kairuki, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Naibu Wawaziri wa Nchi, Ofisi ya Rais –

Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Deogratius John Ndenjembi, Naibu Mawaziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa *(TAMISEMI)* - Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange na Mheshimiwa David Ernest Silinde, kwa ushirikiano wao kwa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, wakiongozwa na Dkt. Laurian Ndumbaro na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na Watendaji wote, wakiongozwa na Prof. Riziki Shemdoe, kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, aidha, nitumie fursa hii kumpongeza Dkt. Moses Mpogole Kusiluka kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Vile vile Kamati inampongeza Ndugu Mululi Majula Mahendeka kwa kuteuliwa kwake kuwa Katibu Mkuu Ikulu. Kamati inaahidi kumpa ushirikiano mzuri katika utendaji wake.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana, sana, sana kwa ushirikiano walionipa katika kipindi chote cha taarifa hii. Natambua na kuthamini michango yao Waheshimiwa Wabunge ambao ni wajumbe wa Kamati hii ambayo ni adhimu na walijitoa kwao kikamilifu katika kuhakikisha Kamati yetu inatekeleza wajibu wake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe hao walitenda kazi bila kujali muda usiku na mchana. Kwa hiyo nazidi kushukuru kwa kujitoa kwao mbele ya Kamati. Kutokana na ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge yaani *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee pia ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa Wankanga Mwihambi, *ndc* kwa ushirikiano wake kwa Kamati katika kipindi chote Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake. Pia Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athumani Hussein, *ndc*, Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Magili, Makatibu wa Kamati hii Ndugu Sikudhani Mbinga na Ndugu Frank Nkya wakisaidiana na Msaidizi wetu ambaye alitusaidia sana katika Kamati Ndugu Pauline Mavunde kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kuandaa maandalizi ya Taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya kina kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo, maoni na mapendekezo ya Kamati, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, pamoja na maoni na mapendekezo yaliyotolewa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

## TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KWA KIPINDI CHA KUANZIA FEBRUARI, 2022 HADI JANUARI, 2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 naomba

kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2022 hadi Januari, 2023.

Taarifa hii inaelezea shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, katika kipindi cha mwaka mmoja wakati ikitimiza majukumu ya kikanuni ya kuisimamia na kuishauri Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu tano, ambazo ni: -

i) Utangulizi;
ii) Matokeo ya Uchambuzi wa shughuli zilizofanywa na Kamati;
iii) Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa kwenye Mkutano wa sita;
iv) Maoni na Mapendekezo ya Kamati; na
v) Hitimisho.

1.1 Majukumu

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 6(4) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, inasimamia shughuli za Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Aidha, Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 imefafanua majukumu ya Kamati hii kuwa ni: -

a) Kushughulikia Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;

b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Maazimio na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Ofisi ya Rais;
c) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na
d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Taasisi na Idara zilizo chini ya Ofisi ya Rais.

1.2 Njia zilizotumika kutekeleza Majukumu

**Mheshimiwa Spika**, Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilitumia njia mbalimbali kama ifuatavyo: -
a) Vikao na Wizara, Taasisi na Idara zilizo chini ya Ofisi ya Rais ili kufahamu Muundo na Majukumu na shughuli zinazotekelezwa;
b) Uchambuzi wa Taarifa mbalimbali za kiutendaji kutoka Ofisi ya Rais;
c) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020; na
d) Mafunzo na Semina za kuwajengea uwezo (*capacity building*) Wajumbe wa Kamati.

Lengo la kutumia mbinu hizo tofauti ni kuwawezesha Wajumbe wa Kamati kujielimisha kwa kina kuhusu nyanja ambazo wamepewa wajibu wa kuisimamia na kuishauri Serikali.

1.3 Shughuli zilizotekelezwa na Kamati

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, katika kipindi cha Februari 2022 hadi

Januari, 2023 Kamati ilipanga na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

### 1.3.1 Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo 2021/2022 na Uchambuzi wa Bajeti 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** ili kuzingatia Kanuni ya 117(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na uchambuzi wa Bajeti za Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

### 1.3.2 Kupokea na Kujadili Taarifa mbalimbali za Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kifungu cha 6(4)(a) na (b) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(d) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, katika kipindi cha taarifa hii Kamati Kwa nyakati tofauti ilipokea na kujadili taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu Wizara inayozisimamia kama ifuatavyo: -

### (i) Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Kamati ilipokea na kujadili taarifa za: -

i) Migogoro ya ardhi katika Jiji la Dodoma;
ii) Wakala wa Mabasi yaendayo kwa haraka katika jiji la Dar es salaam (DART);
iii) Wakala wa ujenzi wa barabara Vijijini na Mijini (TARURA);
iv) Shirika la masoko la Kariakoo;
v) Bodi ya mikopo ya Serikali za Mitaa;

vi) Mikopo ya asilimia 10 ya Mapato ya Ndani kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu,
vii) Ujenzi wa Shule za Sekondari za Kata;
viii) Ujenzi wa Shule za Sekondari za Bweni za Wasichana Kwenye Mikoa; na
ix) Matumizi mengineyo ya fedha za Mapato ya Ndani ya Halmashauri (60/40).

**(ii) Ofisi ya Rais ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

Kwenye Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (MUUB) Kamati ilipokea na kujadili taarifa zifuatazo: -

i) Mpango wa kurasimisha biashara za wanyonge Tanzania (MKURABITA);
ii) Taasisi ya Uongozi;
iii) Chuo cha Utumishi wa Umma;
iv) Mfuko wa maendeleo ya Jamii (TASAF);
v) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU); na
vi) Wakala wa Ndege za Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la Kamati kupokea na kujadili taarifa za Utekelezaji za Wizara inazozisimamia ilikuwa ni kutekeleza jukumu la Kibunge la kuisimamia Serikali kama inavyoainishwa katika Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ikisomwa pamoja na Kanuni ya 7(1)(c) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Baada ya kujadili Taarifa hizo, Kamati ilibaini masuala mbalimbali ambayo yanafafanuliwa katika Sehemu ya Pili ya taarifa hii.

### 1.3.3 Uchambuzi wa Miswada na Maazimio

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha taarifa hii Kamati haikushughulikia mswada wowote wa Sheria wala maazimio ya kuridhiwa na Bunge yanayotokana na Ofisi ya Rais.

**1.3.4Kushiriki katika Semina**

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa walipata fursa ya kushiriki katika semina mbalimbali zilizoandaliwa na Ofisi ya Bunge, Wizara na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, pamoja na Taasisi zisizo za Kiserikali ambazo zimekuwa zikifanya kazi na Kamati.

Semina hizo zililenga kuwaongezea ujuzi na uelewa Wajumbe wa Kamati katika nyanja mbalimbali pamoja na kuwakumbusha kuhusu wajibu na majukumu ya Kibunge ambayo wanayatekeleza katika kuisimamia na kuishauri Serikali.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE

### 2.1 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imepokea taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa kwa Serikali katika Mkutano wa Sita wa Bunge, Februari, 2022 ambapo kwa asilimia 90 maazimio hayo yametekelezwa, na yaliyobaki Kamati imefahamishwa kuwa michakato ya utekelezaji wake inaendelea. Taarifa ya utekelezaji wa maazimio hayo ni kama ifuatavyo: -

#### 2.1.1Mpango wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari za Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Katika utekelezaji wa azimio hili Serikali imeieleza Kamati kuwa imetoa maelekezo kwa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za mitaa kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 na Kanuni zake katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara haikuwasilisha kwa Kamati waraka, barua ama mwongozo wa maelekezo uliotolewa kwa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za mitaa hali iliopelekea Kamati kushindwa kupata Ushahidi wa utekelezaji wa azimio hili.

#### 2.1.2 Utaratibu wa Halmashauri Nchini kutumia asiliia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya mikopo kwa Makundi maalum.

**Mheshimiwa Spika**, Bunge lilipitisha azimio la kuitaka Serikali kufanya marekebisho ya Sheria na Kanuni juu ya

utaratibu mzima wa Halmashauri Nchini kutumia asilimia 10 ya mapato ya ndani ili mfuko huo uweze kukidhi makundi yote.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeelezwa kuwa pamoja na mambo mengine Serikali imeshaanza mchakato wa kutekeleza maagizo hayo, ambapo mpaka sasa wameshaunda timu ya kuandaa Rasimu ya marekebisho ya Sheria ili yaweze kuzingatiwa wakati wa kuandaa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2023.

### 2.1.3 Mradi wa Mabasi yaendayo kwa Haraka Dar es Salaam (DART)

**Mheshimiwa Spika**, Katika azimio hili la Bunge, Bunge iliitaka Serikali kuandaa Mswada wa Sheria utakaoweka mfumo mzuri utakaosimamia Usafiri wa Umma Mijini. Wizara imeieleza Kamati kuwa Serikali imekamilisha Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu pendekezo la kutungwa kwa Sheria ya Usafiri wa Umma Mijini. Waraka huo kwa sasa upo kwenye ngazi ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, baada ya kupita ngazi mbalimbali mswada utawasilishwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeahidi kuuleta Mswada huo Bungeni mapema iwezekanavyo.

### 2.1.4 Uendeshaji wa Masoko Nchini

**Mheshimiwa Spika**, Katika azimio hili la Bunge, Bunge iliitaka Serikali iweke utaratibu Madhubuti wa kisheria utakaobainisha ufanyaji kazi wa wahusika wote wa usimamizi wa masoko wakiwemo watu wa kati pamoja na kubainisha bei elekezi ya upangishaji wa vizimba vya sokoni.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa Serikali imefanya uchambuzi wa changamoto zilizobainishwa na Bunge na kubaini chanzo cha changamoto hii ni Sheria zinazosimamia masoko Nchini. Aidha, uchambuzi umefanyika ili kubaini mapungufu katika Sheria ndogo zinazosimamia uendeshaji wa masoko katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Uchambuzi huu utaiwezesha Ofisi ya Rais – TAMISEMI kuandaa Sheria ndogo ya Mfano itakayozingatia masuala ya bei na upangishaji wa vizimba na uwepo wa madalali katika masoko ili itumike na Halmashauri zote Tanzania Bara kuandaa Sheria zao ndogo za usimamizi na uendeshaji wa Masoko Nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imetoa ahadi (*commitment*) kuwa hadi kufikia mwezi Juni, 2023 itakuwa imekamilisha maandalizi ya Sheria Ndogo ya Mfano kwa ajili ya kutumika na Halmashauri kuandaa Sheria Ndogo za kusimamia uendeshaji wa masoko yao. Aidha, Wizara imeahidi kuuleta Mswada wa marekebisho ya Sheria Bungeni.

### 2.1.5 Shirika la Masoko ya Kariakoo

**Mheshimiwa Spika**, Katika azimio hili Serikali ilielekezwa kufanya mambo yafuatayo: -

i) Serikali iliongezee mtaji Shirika la Masoko Kariakoo ili limudu majukumu yake kikamilifu na kuchangia pato la Taifa na ustawi wa Maisha ya Wananchi; na
ii) Serikali iandae mapendekezo ya marekebisho ya Sheria iliyoanzisha Shirika la Masoko ya Kariakoo ili kusahihisha upungufu katika Sheria hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeieleza Kamati kuwa michakato mbalimbali ili kutekeleza maagizo hayo tayari imeshaanza ambapo hatua iliyofikiwa sasa ni uchambuzi

wa Sheria Sura 132 ya Shirika la Masoko ya Kariakoo na kubainisha maeneo yanayohitaji kufanyiwa marekebisho ya Sheria hiyo. Aidha, ukamilishaji wa hatua zinazofuata za kurekebisha Sheria utaenda sambamba na mwongozo wa mabadiliko utakaotolewa na Serikali.

### 2.1.6 Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA)

**Mheshimiwa Spika**, Bunge lilitoa azimio la kuitaka Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI kutafuta utaratibu endelevu utakaowezesha TARURA kupata fedha za kutosha ili iweze kutekeleza kazi zake za kukarabati na kujenga barabara mpya. Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa kuiongezea TARURA fedha kwa ajili ya matengenezo, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara kupitia vyanzo vipya vya fedha vilivyoibuliwa.

### 2.1.7 Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati Katika Halmashauri Nchini

**Mheshimiwa Spika**, Bunge liliazimia kuwa Serikali ifanye marekebisho katika Mwongozo wa Miradi ya Kimkakati utakaotoa fursa sawa kwa Halmashauri zote nchini ili kukidhi azma ya Serikali ya kuongeza mapato ya Halmashauri na kuwezesha ustawi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeelezwa kwamba Serikali kwa kushirikiana na Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo ya Mitaji (UNCDF) tayari wameshaandaa mwongozo wa Kitaifa wa Uandaaji na Ugharamiaji wa Miradi ya Kuongeza Mapato.

## 2.2 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (MUUB)

### 2.2.1 Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma

**Mheshimiwa Spika**, Bunge liliazimia kwamba Serikali ianzishe mchakato wa marekebisho ya Sheria ya maadili ya Viongozi wa umma ili kuweka Ukomo wa Viongozi wa Umma kuwasilisha Tamko la Mwisho.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza azimio hili la Bunge kikamilifu. Tarehe 14 September, 2022 Bunge ilipitisha marekebisho ya Sheria ya maadili ya Viongozi wa Umma, Na. 13 ya mwaka 1995 kwa kurekebisha kifungu cha 9(1)(c) kama ilivyokuwa imeazimiwa kwa kuweka ukomo wa muda kwa Viongozi wanaotoa tamko la mwisho wa kutumikia wadhifa.

### 2.2.2 Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa

**Mheshimiwa Spika**, Azimio la Bunge liliielekeza Serikali kufanya mambo yafuatayo: -

i) Serikali ianzishe mchakato wa marekebisho ya Sheria ya kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 kwa lengo la kuondoa upungufu katika Sheria hiyo; na
ii) TAKUKURU ijikite zaidi katika kuzuia rushwa badala ya kupambana wakati matendo ya rushwa yameshafanyika.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeieleza kamati kuwa kwenye utekelezaji wa azimio la kurekebisha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 tayari Wizara imeshakusanya maoni kutoka kwa wadau na kwamba hatua inayoendelea sasa ni kuandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri.

**Mheshimiwa Spika**, Katika utekelezaji wa azimio la Bunge kwa taasisi ya TAKUKURU kujikita zaidi katika kuzuia rushwa kuliko kupambana, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuanzisha Programu ijulikanayo kama TAKUKURU Rafiki. Programu hiyo ina lengo la kuongeza wigo wa ushiriki wa Wananchi na wadau katika kuzuia rushwa nchini.

### 2.2.3 Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)

**Mheshimiwa Spika**, Bunge liliazimia yafuatayo kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao: -

i) Serikali itoe mwongozo thabiti kwa Taasisi zote za Umma zinazoanzisha programu tumizi ikiwemo programu za ukusanyaji wa mapato, zianzie kwa Wakala wa Serikali Mtandao;
ii) Serikali Mtandao (e-GA) iimarishe na isimaie kikamilifu Mifumo mbalimbali iliyoanzishwa na iiliyopo Serikalini na kwenye Taasisi zake ili kuondoa kasoro na dosari katika utendaji wa Mifumo hiyo kwa lengo la kuleta ufanisi;
iii) Serikali izikumbushe Taasisi zote za Umma kuzingatia kikamilifu Mifumo mbalimbali iliyoanzishwa na iliyopo Serikalini na kwenye Taasisi zake ili kuondoa kasoro na dosari katika utendaji wa Mifumo hiyo kwa lengo la kuleta ufanisi; na
iv) Serikali Mtandao itengeneze Mifumo ya TEHAMA katika Taasisi zote za Umma, Vyama vya Ushirika, SACOSS na kutambua Wakulima nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweka mwongozo ambao unazitaka taasisi zote za Serikali kuwasiliana na Mamlaka ya Serikali mtandao pale wanapotaka kuanzisha programu tumizi. Aidha, Serikali imekamilisha kukusanya taarifa kuhusu mifumo yote ya

kieletronik inayotumiwa na taasisi za umma na kuziowanisha (*merge*) ili ziweze kusomana.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imetoa maelekezo kwa Taasisi zote za Umma kuzingatia kikamilifu Mifumo mbalimbali iliyoanzishwa na iliyopo Serikalini na kwenye Taasisi zake ili kuondoa kasoro na dosari katika utendaji wa Mifumo hiyo kwa lengo la kuleta ufanisi.

**2.2.4Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma**

**Mheshimiwa Spika**, Bunge liliazimia yafuatayo kwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma: -

i) Sekretarieti iongeze juhudi ya kuuelimisha Umma ili kuwanusuru watu dhidi ya utapeli na tatizo la kughushi katika mchakato wa Ajira;
ii) Mafunzo ya mara kwa mara yatolewe kwa Watumishi wa Sekretarieti ili kuweza kuendana na teknolojia ya kisasa;
iii) Serikali iiwezeshe Sekretarieti kuwa na Mfumo Madhubuti wenye uhakika wa usalama wake; na
iv) Taasisi zote za Serikali na za Umma zianze kutumia Mifumo mipya ya ufuatiliaji na utendaji kazi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa maazimio hayo yote kama yalivyoazimiwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, katika utendaji kazi wa Sekretarieti ya Ajira Kamati imebaini kuwepo na changamoto ya baadhi ya Vijana wanaoomba kazi Serikalini kukosa kigezo cha kuwa na cheti cha JKT suala ambalo kwa kiasi kikubwa halitokani na waombaji bali ni mfumo mzima wa masomo uliopo kwa sasa, ambapo vijana wengi wamekuwa hawapatiwi fursa ya kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa pindi wamalizapo masomo ya Kidato cha Sita.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuondoa changamoto hiyo kwa Vijana wetu, Kamati inaishauri Serikali ione umuhimu wa kuwawezesha vijana wote wanaomaliza elimu ya Kidato cha Sita kuhudhuria mafunzo ya JKT.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto hiyo, Kamati pia imebaini uwepo wa Changamoto inayowapata vijana waliomaliza masomo miaka ya nyuma kushindanishwa na wale ambao wamehitimu masomo yao katika miaka ya karibuni hali ambayo imekuwa ikiwakosesha nafasi ya kuwa kwenye nafasi nzuri ya kushinda katika saili wanazofanya, hasa ukizingatia kuwa aliyemaliza miaka ya karibuni anakuwa na uelewa na kumbukumbu nzuri kuliko yule aliyemaliza miaka ya nyuma.

**Mheshimiwa Spika**, Ni rai ya Kamati kuwa, Serikali ione umuhimu wa kuwatofautisha vijana hawa kwenye saili mbalimbali wanazofanya ili kuwapa nafasi kubwa ya kuweza kushinda na kupata ajira Serikalini, vinginevyo vijana hawa wataendelea kuachwa na mfumo na kukosa kabisa ajira. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendesha usaili katika Kanda hali ambayo imewapunguzia gharama wasailiwa.

### 2.2.5 Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa

**Mheshimiwa Spika,** Bunge liliazimia Serikali kuiwezesha zaidi kibajeti Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa ili ifanikishe kazi muhimu ya kuhifadhi nyaraka na kuimarisha usalama wa nyaraka zinazohifadhiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeelezwa kuwa hadi kufikia Disemba, 2022 Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za

Taifa imepokea kiasi cha Sh. 834,858,222.80 ikiwa ni asilimia 59.2 ya bajeti yote ya Maendeleo, ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022, ambapo Idara ilipokea jumla ya Sh. 340,000,000 ikiwa ni asilimia 17 tu ya bajeti yote. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza azimio hili.

### 2.2.6 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

**Mheshimiwa Spika**, Bunge liliazimia yafuatayo kwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma: -

i) Serikali ifanye jitihada za makusudi kuhakikisha kuwa Wanufaika hao wanapatiwa namba/Vitambulisho vya Taifa ili kuwawezesha kupata huduma muhimu pale inapobidi ikiwepo kupokea ruzuku kwa njia ya Kielektroniki ili waweze kujikwamua kiuchumi; na
ii) TASAF iendelee kupatiwa fedha za kutosha ili iweze kuwakomboa Wananchi wengi kiuchumi na kuboresha huduma katika Jamii ikiwa ni pamoja na kukarabati Madarasa ya zamani.

**Mheshimiwa Spika**, TASAF na NIDA wamesaini makubaliano ya kuwapatia walengwa wa Mpango Namba/Vitambulisho vya Taifa na kupokea ruzuku zao kwa njia ya kielektroniki. Hadi kufikia mwezi Disemba, 2022 zaidi ya walengwa 400,000 wa Mpango wa TASAF walipatiwa Namba/Vitambulisho vya Taifa na wanapokea ruzuku zao kwa njia ya kielektroniki ikilinganishwa na walengwa 132,569 waliokuwa wamefikiwa hadi Disemba 2021.

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia mwezi Disemba, 2022 Serikali kupitia bajeti ya Mwaka tayari imekwishatoa zaidi ya Shilingi Bilioni 17.0 kwa ajili ya utekelezaji wa Kipindi cha Pili cha Mpango huu. Aidha, Serikali imepata mkopo

wa masharti nafuu wa Dola Milioni 50 sawa na Shilingi za kitanzania bilioni 115 kutoka mfuko wa maendeleo wa nchi zinazotoa mafuta kwa wingi (OFID) na kuelekeza fedha hizo kwenye utekelezaji wa mpango wa TASAF kwenye Halmashauri 33 katika mikoa mitano ya Simiyu, Mwanza, Geita, Arusha na Njombe.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii ya taarifa inaelezea kwa ufasaha majukumu yaliyotekelezwa na Kamati kwa kipindi chote cha mwaka mmoja. Uchambuzi wa kina wa matokeo ya shughuli hizo umefanyika kwa kuainisha Wizara, Taasisi na Idara iliyohusika na kuonesha mafanikio na changamoto.

### 3.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa kutoa maelezo kuhusu matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwenye masuala yaliyobainishwa na Kamati kama ifuatavyo: -

#### 3.2.1 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)

**i. Migogoro ya Ardhi katika Jiji la Dodoma**

**Mheshimiwa Spika**, Katika vipindi vitatu tofauti, Kamati ilikutana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ili kujadili migogoro ya ardhi katika Jiji la Dodoma na utatuzi wake.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kujadili taarifa zilizowasilishwa, mambo kadhaa ambayo yamekuwa yakilalamikiwa na baadhi ya Wananchi walioathirika katika mazoezi ya utwaaji wa ardhi ndani ya Jiji la Dodoma yaliibuliwa na Wajumbe. Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na msingi na mantiki ya mwenye eneo kutoa asilimia 10 kwa ajili ya barabara, mgawanyo wa ardhi wa asilimia 30 kwa Halmashauri na asilimia 70 kwa mwenye eneo, namna kampuni binafsi za upimaji zilivyopatikana na usimamizi wake, Wananchi kuchukuliwa maeneo yao na kampuni pasipo fidia stahiki.

**Mheshimiwa Spika**, katika zoezi la kupanga, kupima na kumilikisha ardhi katika Jiji la Dodoma wananchi wamedhulumiwa au kuporwa ardhi yao kwa namna zifuatazo: -

a) Umilikishwaji kiwanja chenye hati pandikizi – yaani kiwanja kimoja kumilikishwa kwa mtu zaidi ya mmoja. Hali hiyo inaweza kuwa imechangiwa na Watumishi wa Sekta ya Ardhi kukosa uadilifu na weledi, jambo linaloweza kuwa limesababisha matumizi ya mifumo kwa maslahi yao binafsi;
b) Wananchi wenye maeneo madogo kuunganishwa pamoja katika upimaji na hivyo kuyapoteza kabisa maeneo yao bila fidia yoyote;
c) Katika upimaji shirikishi makubaliano yalikuwa baada ya kutoa asilimia 10 ya eneo kwa ajili ya miundombinu ya barabara, eneo lililobaki likifanyiwa upimaji mmiliki wa eneo anapewa asilimia 70 na Jiji linachukuwa asilimia 30. Hata hivyo, katika utekelezaji, Jiji limechukua zaidi ya asilimia 30 na mahali pengine imetwaa eneo lote bila fidia. Maswali ya kujiuliza hapa ni je asilimia 10 ya miundombinu ni kweli imetengwa kwa ajili hiyo? na kwa nini wamiliki

hawakupewa fursa ya kuchagua maeneo mbadala na badala yake Jiji lilitwaa maeneo mazuri (potential areas) na kuwaachia wamiliki wa awali maeneo yasiyo mazuri; na

d) Ofisi ya Jiji haikuandaa hadidu za rejea zinazoonesha upimaji utakavyofanyika. Hali hiyo ilisababisha kampuni za upimaji kupima viwanja kiholela na kuzalisha viwanja vidogovidogo vingi ili kujiongezea kipato. Upimaji wa namna hiyo haukuzingatia utaratibu wa kupima maeneo kwa kuzingatia mpango wa *high density, medium density* na *low density* kama ilivyo kwa mipango miji ya maeneo mengine. Sababu kubwa ni utaratibu uliotumika kuzilipa kampuni kulingana na idadi ya viwanja zilizopima.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haikuridhishwa na maelezo yaliyotolewa kwamba chanzo cha migogoro ni kukosa uadilifu, uaminifu, weledi na kutokuzingatia maadili ya taaluma inayohusika (mipango miji, upimaji na Ramani, uthamini na umilikishaji ardhi) kwa baadhi ya Watumishi wa Sekta ya ardhi waliokuwepo CDA na ambao pia walirithiwa na Jiji la Dodoma, madai ya fidia kwa mashamba/maeneo ambayo yalitwaliwa na kupimwa na CDA pamoja na uelewa mdogo wa Wananchi kuhusu masuala ya ardhi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifahamishwa kwamba katika kutatua migogoro hiyo, Kamati mbalimbali za utatuzi wa Migogoro ya Ardhi ziliundwa na Watumishi wapatao 22 wa Sekta ya ardhi waliotuhumiwa kusababisha migogoro walihamishwa. Kamati zilizoundwa ni pamoja na Kamati ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Kamati ya Mkuu wa Wilaya ya Dodoma na Kamati ya Madiwani.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na maelezo hayo na jitihada za kutatua migogoro bado kumekuwepo na malalamiko kutoka kwa Wananchi wa Jiji la Dodoma kutopewa haki yao stahiki iliyoporwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haijaridhishwa na hatua ya kuwahamisha Watumishi 22 ambao kwa maelezo ya Jiji, Watumishi hao hawana uadilifu, uaminifu na weledi katika taaluma zao na hivyo kusababisha migogoro sugu ya ardhi.  Kamati imebaini kuwa hatua iliyochukuliwa ya kuwahamisha watumishi hao haijatatua migogoro iliyopo na badala yake imehamishia tatizo kwenye Halmashauri walikohamishiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kwamba utaratibu uliotumika kutatua migogoro hii unafanana na utaratibu uliotumika Mkoani Mtwara ambapo waliotuhumiwa kutenda kosa ndiyo hao hao waliokuwa wanachunguza tuhuma.

**Mheshimiwa Spika,** haiingii akilini Wataalam wanaodaiwa kusababisha migogoro ndiyo hao hao walioko katika timu za utatuzi wa migogoro waliyoisababisha.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na maelezo ya Jiji kupeleka lawama kwa CDA, Kamati imebaini kuwa migogoro mingi ya ardhi imezalishwa na Jiji baada ya kuruhusu Kampuni binafsi kufanya upimaji. Kamati ina maoni kuwa swala la migogoro hiyo limedumu kwa muda mrefu bila ufumbuzi. Jambo hilo halina ufanisi katika kuwezesha ustawi wa watu Jijini Dodoma. Kwa sababu hiyo, kuna haja Serikali kuchunguza kwa kina tatizo hilo ili kubaini chanzo halisi cha mgogoro na hatimae kuchukua hatua stahiki dhidi ya wahusika Pamoja na kuwapatia Wananchi haki wanayo stahili.

### ii. Mradi wa Mabasi yaendayo kwa Haraka – DART

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Utendaji ya Mradi wa Mabasi yaendayo haraka katika Jiji la Dar es Salaam (DART). Aidha, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa mradi huo wa Mabasi yaendayo kwa haraka awamu ya pili na ya tatu. Kamati inaipongeza Serikali kwa uwekezaji huo mkubwa ambao miundombinu iliyowekwa imechangia kuboresha muonekano wa mandhari ya Jiji la Dar Es Salaam. Kamati imeelezwa miongoni mwa faida zilizopatikana kutokana na mradi huo ni pamoja na: -

i) Kuboresha huduma ya usafiri wa Umma katika Jiji na kupunguza muda wa safari toka saa tatu hadi dakika arobaini na tano (45) kwa safari moja, hivyo Wananchi kuwahi katika shughuli zao za kijamii na kiuchumi zinazoongeza tija kwenye pato la Taifa;
ii) Matumizi ya teknolojia katika usimamizi na uendeshaji wa usafiri wa umma umekua, mfano kwenye ukusanyaji wa nauli wa kielektroniki na mifumo ya mabasi inayotumia nishati isiyochafua mazingira;
iii) Kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Wizara ya Fedha na Mipango na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), wamesanifu na kujenga Mfumo wa kielektroniki wa kukusanya nauli uitwao (Automated Fare Collection System (AFCS), ambao unamilikiwa na Serikali, na kuwezesha ongezeko la mapato,
iv) Kununua mfumo wa kuongoza mabasi ujulikanao kama (Intelligent Transportation System (ITS), kununua vifaa vya mifumo vikiwemo kadi na mageti mapya ambayo yatasimikwa kwenye vituo vyote vya DART; pamoja na
v) Ubora wa mradi umefanya Tanzania iwe nchi ya mfano kutokana na mradi ulivyo, kwa kuwa tangu

kuanzishwa kwa mradi huu takribani nchi 12 zimekuja kujifunza zikiwemo nchi ya Zambia, Zimbabwe, Uganda, Kenya, Ethiopia, Senegal, Ghana, Rwanda, Angola, Botswana, Nigeria na Liberia.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mafanikio hayo, Mradi pia unakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo ni: -

i) Kukosa sheria mahususi ya kusimamia utekelezaji wa shughuli za mradi na kuufanya mradi huu kukosa uendelevu (sustainabililty aspect);
ii) Uvamizi wa miundombinu ya mradi;
iii) Uchache wa Mabasi;
iv) Kuongezeka kwa gharama za uendeshaji na matengenezo duni ya mabasi;
v) Bado kuna upotevu wa mapato;
vi) Ukosefu wa kadi janja;
vii) Kuchelewa kulipa fidia kwa maeneo yanayotwaliwa;
viii) Upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa mradi;
ix) Viwango vya fidia ya ardhi pale ambapo mradi unahitaji kupanuliwa na kupelekea uvunjifu wa rasilimali mbalimbali na kusababisha fidia kuwa kubwa;
x) Vibali vya ujenzi kutolewa kwenye maeneo ambayo tayari yamesanifiwa kwa ajili ya mradi;
xi) Upungufu wa Ikama ya Watumishi 48, ambapo Wakala una Watumishi 86 badala ya 134 wanaohitajika;
xii) Uwepo wa nafasi wazi 18 za uongozi; na
xiii) Ukosefu wa jengo la Ofisi.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mlolongo huo wa changamoto, changamoto kubwa ambayo inaikabili mradi huu ni kukosekana kwa Sheria inayosimamia usafiri wa umma mijini, Sheria zilizopo hazisimamii moja kwa moja usafiri wa umma mijini. Sheria hizo ni Sheria ya

Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu Na. 3 ya Mwaka 2019 inayohusika na kuanzisha mamlaka ya kutoa leseni, kupanga nauli na kupanga njia za usafiri ardhini; Sheria ya barabara Na. 13 ya 2007 inayo simamia ujenzi, udhibiti wa matumizi ya barabara na maeneo yaliyotengwa kama hifadhi za barabara; Sheria ya usalama barabarani Na. 168 ya Mwaka 1973 inayotoa mamlaka kwa jeshi la usalama barabarani kusimamia mwenendo wa vyombo vya usafiri katika miundombinu yote nchini na Tangazo la Serikali Na. 120 la 2007 lililoanzisha Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka, Dar es salaam. Sheria zote zilizoelezwa hapo juu hazijikiti moja kwa moja kusimamia na kutatua changamoto ya usafiri mijini.

**iii. Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kupokea na kujadili taarifa ya utendaji wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA). Aidha Kamati ilipata fursa ya kukagua ujenzi wa barabara katika Wilaya za Mufindi na Kilolo Mkoani Iringa. Miradi hii ya ujenzi wa barabara ilikuwa mahususi kwa ajili ya kurahisisha usafirishaji wa mazao ya mbogamboga na matunda kutoka maeneo ya uzalishaji kwenda katika masoko. Hata hivyo Kamati ilibaini barabara hizo zina uwezo wa kupitisha magari yenye uzito wa tani kumi au pungufu ya hapo. Tunaipongeza TARURA kwa kukamilisha ujenzi wa barabara hizo. Hata hivyo Kamati imebaini changamoto kubwa katika barabara hizo ni uwepo wa zao kubwa la biashara la mbao, ambalo linapitisha magari yenye uzito wa zaidi ya tani 30 na hivyo kusababisha uharibifu mkubwa wa barabara ambazo uwezo wake ni tani 10 tu. Kamati ilitaarifiwa kwamba magari makubwa yanayozidi uzito wa tani 10 hupitishwa nyakati za usiku kwa vile hayaruhusiwi

kisheria kupita kwenye barabara hizo kutokana na uzito wake.

**Mheshimiwa Spika**, hali hii inatishia uhai wa barabara hizo lakini pia ujenzi wake haukuzingatia hali halisi ya maeneo haya ya uwepo wa mazao ya misitu hususan zao la mbao ambazo zinapatikana kwa wingi na zinahitaji magari makubwa kuzisafirisha kwenda katika masoko mbalimbali ndani na nje ya nchi. Kamati inashauri Serikali katika miradi ya ujenzi wa barabara za vijijini na mijini uzingatie matumizi yote yanayopatikana katika maeneo husika na hivyo zijengwe barabara zinazoweza kuhimili uzito mkubwa.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na malalamiko mengi kutoka kwa Wananchi, Wabunge, Halmashauri na Wadau mbalimbali nchini kuhusu ucheleweshwaji wa kuanza kazi za ujenzi wa barabara unaosababishwa na mambo mbalimbali, yakiwemo matatizo sugu ambayo ni:-

i) Wakandarasi kutokuwepo uwandani baada ya kuingia mikataba na kukabidhiwa mradi;
ii) Mfumo wa utoaji kazi kwa Wakandarasi kutohusisha ngazi ya Wilaya hali inayosababisha ucheleweshwaji wa utekelezaji wa mradi;
iii) Ucheleweshwaji wa mradi unaotakana na taratibu za manunuzi kutokufanyika katika ngazi ya Wilaya; na
iv) Ucheleweshwaji wa utekelezaji wa masharti ya mkataba kama vile utoaji wa msamaha kwa Wakandarasi (exemption).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali ione umuhimu wa kuweka mifumo shirikishi hususani katika ngazi za Wilaya na itoe maelekezo kwa Wakandarasi kuwa mara baada ya kuingia mikataba kwenda

kujitambulisha kwenye Ofisi za Wakuu wa Wilaya na Halmashauri. Kwa kufanya hivyo itarahisisha jukumu la ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi kwa viongozi mbalimbali wa Wilaya. Aidha, Kamati inasisitiza kwamba Serikali kwa upande mmoja na Wakandarasi kwa upande mwingine waheshimu na kutekeleza kwa wakati makubaliano wanayoingia katika mkataba ili kuharakisha utekelezaji wa mradi.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kujadili taarifa iliyowasilishwa na TARURA Kamati imebaini kwamba, moja ya changamoto kubwa inayotajwa kucheleweshwa kuanza au kukamilika kwa mradi ni mabadiliko ya majira, hasa nyakati za mvua.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haijaridhishwa na sababu hizo zilizotolewa, kwa sababu majira na jiografia ya nchi vinafahamika, hivyo visitumike kama kisingizio cha kutokutekeleza au kukamilisha miradi kwa wakati. Kamati inashauri kuwa wakati wa kupanga utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara uzingatie mabadiliko ya Majira na Jiografia ya nchi.

**iv. Shirika la Masoko la Kariakoo (KMC)**

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Masoko Kariakoo lilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Shirika la Soko la Kariakoo Na. 36 ya Mwaka 1974 ili miongoni mwa mambo mengine, liweze kusimamia na kuendesha Soko Kuu pamoja na masoko mengine yatakayowekwa chini yake, kujenga masoko mengine katika Jiji la Dar es Salaam na kusimamia uendeshaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, Shirika hilo ambalo lipo chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI lina wanahisa wawili ambao ni

Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam (Hisa asilimia 51) na Msajili wa Hazina kwa niaba ya Serikali Kuu (Hisa asilimia 49), Shirika hilo linamiliki mali zenye thamani ya **Shilingi bilioni 56**. Aidha, mbali na Soko Kuu la Kariakoo Shirika lina maeneo mengine Tabata Bima na Mbezi Beach (Makonde).

Pamoja na shirika kutekeleza majukumu yake kwa mafanikio, limekuwa likikabiliwa na changamoto kadhaa ambazo ni pamoja; na upungufu katika Sheria ya Shirika ambao unaathiri utendaji na uendeshaji, uchakavu wa miundombinu yakiwemo majengo yaliyojengwa zaidi ya miaka 40 iliyopita, na zuio la magari yanayoleta mazao katika Soko la Kariakoo kutokana na Sheria Ndogo za Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri changamoto hizi kufanyiwa kazi ili kuwezesha shirika hili kujiendesha kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kupata sheria bora ambayo itawezesha shirika kuwekeza vitega uchumi zaidi na hivyo kuongeza wigo wa mapato na huduma kwa Wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini pia uwepo wa adha kubwa kwa Wakulima wanapokuja kuuza mazao sokoni kukumbwa na wimbi la Madalali ambao ndiyo wanaopanga bei ya kuuza mazao na kuwafanya Wakulima kukosa sauti kwenye mapatano ya kuuza bidhaa zao sokoni. Hali hiyo siyo tu inawapa Wakulima/Wafanyabiashara bei ya hasara bali pia inachangia upotevu wa mapato ya Serikali na kudhorotesha jitihada kubwa inayofanywa na Serikali katika kuinua uchumi wa Wananchi hususan Wakulima.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na changamoto ya upotevu wa mapato na huduma hafifu kwa Wananchi

zinazosababishwa na Mifumo ya uendeshaji, Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha Shirika la Masoko Nchini ambalo litasimamia uendeshaji wa masoko yote badala ya kuwa na shirika linaloendesha shughuli zake kwenye mkoa wa Dar es Salaam pekee.

**v. Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa**

**Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imeanzishiwa kwa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019. Madhumuni ya uanzishwaji wa Bodi hiyo yalilenga katika kuhakikisha kuwa mamlaka za Serikali za Mitaa zinapata chanzo mbadala cha fedha kwa njia ya mikopo yenye riba nafuu kulinganisha na taasisi zingine za fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Toka Bodi ilipoanza kutoa huduma kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa mwaka 1965 hadi kufikia mwaka 2020 Bodi imetoa mikopo kwa Halmashauri 57 sawa na asilimia 30.9 ya Halmashauri zote nchini. Mikopo iliyotolewa kwa kipindi hicho ina thamani ya **Shilingi za Kitanzania 14,661,250.563.51**. Hata hivyo hadi kufikia Disemba 2022 Halmashauri 12 zinadaiwa madeni ya mikopo yenye thamani ya **Shilingi za Kitanzania 4,710,387,143.54**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, Bodi iliidhinisha mkopo kwa Halmashauri moja tu ya Kisarawe wenye thamani ya Shilingi 300,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa maduka katika kituo cha mabasi cha Kisarawe. Hata hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe haikupewa Mkopo huo kwa kigezo cha mabadiliko ya uongozi ambayo yamepelekea kuchelewa kusaini mikataba.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Wizara kusimamia kikamilifu utendaji kazi wa Bodi hii ili kutimiza malengo au matakwa ya Kisheria ya uanzishwaji wake. Aidha, Wizara itizame upya Kanuni za uendeshaji wa Bodi hususani michango ya Halmashauri kwenye Bodi kwa kuweka ulazima wa kila Halmashauri kuchangia asilimia fulani kwenye Bodi kulingana na mapato yao. Kwa kufanya hivyo Bodi itakuwa na uwezo wa kukusanya fedha na kukopesha Halmashauri nyingi zaidi.

**vi. Utekelezaji wa utoaji na urejeshaji wa fedha za asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya mikopo ya Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika kipindi cha taarifa hii, ilipokea na kujadili taarifa ya Utoaji na Urejeshaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa makundi ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa baadhi ya Halmashauri nchini, ambapo pia Kamati ilipata fursa ya kutembelea Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam kwenda kukagua utendaji wa vikundi hivyo.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imefanikiwa kuendelea kuyawezesha Kiuchumi Makundi ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kupitia Mikopo ya Asilimia 10 inayotolewa na Halmashauri. Pamoja na jitahada na mafanikio hayo, zipo changamoto za **Mikopo Chechefu** iliyotokana na mikopo iliyotolewa kuanzia vipindi vya nyuma**.** Uwepo wa Mikopo Chechefu unarudisha nyuma utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura ya 290, kifungu 37A (4) cha kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu za mwaka 2019.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha 2017/18 hadi Disemba, 2022 mikopo iliyotolewa kwa **Vikundi 10,334** imepita muda wa marejesho (Mikopo Chechefu). Vikundi hivyo vilikopeshwa jumla ya **Shilingi 42,011,288,123.03** ambapo hadi Disemba, 2022 jumla ya **Shilingi 19,278,618,593.25** zimerejeshwa sawa na asilimia 46 ya mikopo iliyokopeshwa. Hivyo, kiasi cha **Shilingi 22,915,418,503.24** sawa na asilimia 54 hakijarejeshwa tofauti na makubaliano ya mkataba wa marejesho baina ya vikundi hivyo na Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto zingine kubwa zilizobainiwa na Kamati ni kama zifuatazo: -

i) Baadhi ya wakopeshwaji kuhamia sehemu nyingine kutokana na Halmashauri kushindwa kutambua na kuwafikia katika maeneo waliohamia wanakikundi hao hasa kwa Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam;
ii) Vikundi kusambaratika baada ya kupewa mikopo kutokana na kukosa malengo ya kufanya kazi pamoja na kutokuaminiana miongoni mwa wanachama. Aidha, Baadhi ya Mikopo iliyotolewa kupitia SACCOS, baadhi ya SACCOS hizo zilikufa Mfano SACCOS ya Uwemba katika Halmshauri ya Njombe;
iii) Mitazamo potofu wa jamii kuwa fedha hizo ni kama msaada au fadhila, hivyo, hakuna jitihada za wanufaika kurejesha mikopo hiyo; na
iv) Miradi ya wanufaika kuathiriwa na majanga mbalimbali ikiwemo moto, mafuriko, magojwa katika miradi ya ufugaji na kilimo, kufariki kwa wanachama na kuibiwa mali Pamoja na Usimamizi hafifu wa Vikundi.

**Mheshimiwa Spika**, ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali ione uwezekano wakufanya mambo yafuatayo: -

i) Kuhakikisha Mfumo wa Kielektroniki ambao umeanza kutumika mwezi Julai 2022 unasimamiwa ipasavyo na kuhakikisha changamoto ya mikopo chechefu inapungua;
ii) Serikali ikamilishe mapitio ya Sheria ili kuwezesha uchukuaji wa hatua madhubuti kwa wahusika wote wanaokiuka Sheria na Kanuni za usimamizi wa Mikopo hii wakiwemo wasimamizi na wanufaika;
iii) Kuhakikisha Kazi ya kuingiza taarifa za mikopo ya nyuma ikamilishwe kwa haraka ili kupata uhalisia wa madeni ambayo hayajarejeshwa;
iv) Serikali ijipange kuhakikisha maboresho hayo yanayofanyika hayaathiri upatikanaji wa mikopo hii kwa makundi yote wakiwemo wanufaika walioko vijijini;
v) Mikopo ambayo iko nje ya muda hatua madhubuti zichukuliwe na kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa na kutumika kama ilivyokusudiwa; na
vi) Serikali ihakikishe Mikopo inatolewa kwa watu wenye ulemavu ikiwemo mtu mmoja mwenye ulemavu kwa mujibu wa kanuni ya 6A(1) ya Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu (Marekebisho ya Mwaka 2021).

**vii. Ujenzi wa Shule za Sekondari za Kata Kupitia Mradi wa SEQUIP**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili taarifa kuhusu ujenzi wa shule za sekondari za kata. Wakati wa kujadili taarifa hizo, Kamati imebaini kuwepo kwa tofauti kubwa kati ya gharama zilizokadiriwa na gharama halisi baada ya ujenzi kukamilika. Gharama iliyokuwa imekadiriwa ni Sh. 470,000,000 kwa shule moja kwa miundombinu iliyoelekezwa kwa Mikoa yote. Kati ya shule kumi na nne katika mikoa saba ambayo taarifa zake zilijadiliwa tofauti ya gharama yaani (variation) ni

kati ya Sh. 52,000,000 hadi 157,000,000 zaidi ya gharama iliyokadiriwa.

**Mheshimia Spika,** Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya gharama halisi za ujenzi katika kanda tofauti ili wanapopanga bajeti ya miradi izingatie hali halisi ya mazingira husika ikiwa ni pamoja na umbali unaosababisha bei za vifaa vya ujenzi kutofautiana.

**viii. Ujenzi wa Shule za Sekondari za Wasichana za Bweni za Mikoa kupitia Mradi wa EP4R**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifahamishwa kuhusu mradi wa ujenzi wa Shule za Sekondari za Wasichana za Bweni kwa kila Mkoa na kwamba mikoa 10, ambayo ni Dar Es Salaam, Pwani, Njombe, Mwanza, Shinyanga, Mara, Ruvuma, Singida, Lindi na Kagera imeshapelekewa fedha za ujenzi na ujenzi unaendelea na katika baadhi ya Mikoa unakaribia kukamilika. Kamati imebaini viashiria vya kuongezeka kwa gharama kama ilivyo katika Shule za kata kutokana na changamoto zilizoelezwa ambazo ni ukosefu wa maji, umeme, barabara katika maeneo ya ujenzi pamoja na kupanda kwa gharama za vifaa vya ujenzi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza uongozi wa Mkoa wa Songwe na Halmashauri ya Mji wa Tunduma kwa ubunifu, baada ya kuomba kibali cha kujenga Shule ya sekondari ya Wasichana kwa majengo ya ghorofa badala ya majengo yaliyotawanyika kama ambavyo imeelekezwa katika ramani za ujenzi zilizotolewa na OR-TAMISEMI. Hali hii imesaidia kutumia eneo dogo na hivyo kuacha ardhi kwa ajili ya matumizi mengine.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kwamba mtindo wa ghorofa umeongeza gharama, pia umekuwa na tija

kwani umeongeza Ofisi nne, madarasa matatu na matundu ya vyoo 24 zaidi ya ile idadi iliyokadiriwa awali. Mheshimwa Spika, Kamati imeridhishwa sana na utekelezaji wa mradi huu na tunashauri OR – TAMISEMI iangalie uwezekano wa kuiga mfano huu kwa Mikoa mingine.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande mwingine, Kamati imesikitishwa na uongozi wa Mkoa wa Tanga, ambapo baada ya kupelekewa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana, wameshindwa kuafikiana kuhusu sehemu gani Shule ijengwe hadi ikailazimu Wizara kuzichukua fedha zile na kuzipeleka katika Mkoa wa Njombe ambao wanatekeleza mradi huo katika Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe.

**Mheshimiwa Spika**, mivutano kama hii isiyokuwa na tija si jambo linalofaa. Kamati inatoa rai kwa Halmashauri zote na Sekretarieti za Mikoa kukubaliana linapokuja suala la utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**ix. Matumizi mengineyo ya fedha za Mapato ya Ndani ya Halmashauri (60/40)**

**Mheshimwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili taarifa kuhusu makusanyo ya mapato ya ndani ya halmashauri na upangaji wa fedha za matumizi mengineyo kwa utaratibu wa asilimia 60 kwa 40 kutegemeana na makusanyo. Kamati imebaini kuwepo kwa tofauti kubwa katika gharama za uendeshaji wa Halmashauri zenye makusanyo madogo ikilinganishwa na zile zenye makusanyo makubwa. Mfano katika baadhi ya Halmashauri za Majiji, Manispaa na Miji matumizi mengineyo yanazidi Sh. Billion nne hadi Billion ishirini wakati katika Halmashauri zenye makusanyo madogo

matumizi mengineyo ni chini ya shs 300,000,000. Hali hii inafanya Halmashauri zenye makusanyo madogo kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuziongezea fedha za uendeshaji halmashauri zenye makusanyo madogo. Aidha, Kwa upande wa Halmashauri zenye makusanyo makubwa yanayoanzia billion 10 kuwekewa utaratibu wa asilimia 70 kwa shughuli za maendeleo na asilimia 30 kwa matumizi mengineyo.

**3.2.2 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (MUUUB)**

**i. Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kupokea na kujadili taarifa ya utendaji ya MKURABITA pamoja na kufanya ziara za ukaguzi wa ujenzi wa Masjala za Ardhi katika Mikoa ya Dodoma na Morogoro.

Kamati inaipongeza MKURABITA kwa kazi nzuri iliyowezesha Wananchi wanaomiliki rasilimali na biashara nje ya mfumo rasmi kuzirasmisha na kuzitumia kupanga mahitaji kwa ajili ya kushiriki katika uchumi wa kisasa unaoendeshwa kisheria.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kwamba jumla ya Wakulima 163,568 wamepimiwa mashamba yao na kupewa hati za Kimila. Aidha, kwa kutumia rasilimali na biashara zilizorasimishwa Wananchi wameweza kupata mikopo kutoka kwenye Taasisi za Kifedha. Kamati imetaarifiwa kwamba jumla ya mikopo yenye thamani ya TSh. Trilioni 5.604 imetolewa na Taasisi za Fedha kwa Wananchi. Kati ya fedha hizo TSh. Trilioni 1.08 zimetolewa kwa Wananchi waliorasimisha mashamba na kupata hati

za kumiliki ardhi Kimila. Shilingi Trilioni 2.703 zimetolewa kwa Wamiliki waliorasimisha viwanja mijini, na Shilingi Trilioni 1.821 zimetolewa kwa Wamiliki wa shughuli za kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** mafanikio yaliyiopatikana kutokana na urasimishaji wa rasilimali na biashara ni pamoja na mabadiliko ya kimtazamo katika uendeshaji wa biashara ambapo zaidi ya asilimia 70 ya Wafanyabiashara wanatunza kumbukumbu za biashara na hivyo kuweza kujua mwenendo wa biashara wanazoendesha. Mafanikio yaliyopatikana Kitaifa ni pamoja na kuongezeka kwa wigo wa walipa kodi, kuongezeka kwa mapato ya Serikali pamoja na kupungua kwa migogoro ya ardhi ambapo urasimishaji umefanyika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri uzoefu huu uliopatikana MKURABITA, katika kurasimisha ardhi kwa Wakulima utumike pia katika kurasimisha ardhi kwa Wafugaji ili nao wanufaike na mikopo na kuepuka kuhamahama na hivyo kupunguza migogoro baina ya Wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

**ii. Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kupokea na kujadili taarifa ya utendaji ya Taasisi ya Uongozi. Aidha, Kamati ilipewa semina kwa siku mbili kuhusu uongozi na mawasiliano kwa Umma. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutilia mkazo suala la kuwajengea uwezo viongozi ili waweze kuwatumikia Wananchi kwa uadilifu na tija.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifahamishwa kwamba jumla ya Viongozi takriban 5,428 wamepatiwa mafunzo na Taasisi ya Uongozi. Viongozi walionufaika na mafunzo hayo ni pamoja na Mawaziri, Naibu Mawaziri, baadhi ya Wabunge, Makatibu Wakuu wa pande zote za Muungano, Maafisa Waandamizi wa Mahakama, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika**, mafunzo hayo yamesaidia Viongozi kuimarisha mahusiano kati yao na Watendaji wengine, yameongeza uwezo wa timu kufanya kazi kwa pamoja na ufanisi, pia yameongeza uelewa wa kuchambua changamoto kwa kina na kuzitafutia ufumbuzi. Vile vile mafunzo hayo yamewezesha Viongozi kuweza kuboresha usimamizi wa rasilimali za Serikali na Rasilimali Watu.

**Mheshimiwa Spika**, katika mafunzo yaliyotolewa na Taasisi ya Uongozi, suala la kutumia Akili Hisia (Emotional Inteligence) limesisitizwa sana. Akili Hisia ukiitumia vizuri hukuwezesha kufahamu matarajio ya Wananchi unaowaongoza, kushirikiana nao kuzitambua changamoto walizonazo na kuzitatua kwa pamoja.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia umuhimu wa mafunzo hayo, Serikali iangalie uwezekano wa kutoa mafunzo hayo kwa Wabunge wote.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali ione umuhimu wa viongozi wote wanaoteuliwa na kuchaguliwa kupewa mafunzo ya uongozi kabla ya kuanza majukumu yao.

**iii. Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)**

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha taarifa hii, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Utendaji ya Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC). Aidha, Kamati ilipata wasaa wa kufanya ziara ya ukaguzi wa ujenzi wa Maabara ya Uchapaji (Typing Lab) katika Kampasi ya Singida yenye uwezo wa kuchukua Wanachuo 210 kwa wakati mmoja.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kazi nzuri inahofanywa na Chuo hiki, Chuo kinakabiliwa na changamoto ya kutumia majengo ya kupanga katika Kampasi za Singida, Tanga na Mbeya jambo ambalo linakipa Chuo mzigo mkubwa wa kulipa gharama za pango kila mwaka. Aidha, mwitikio mdogo wa Taasisi, Wizara na Wakala wa Serikali kukitumia Chuo cha Utumishi wa Umma kuendesha mafunzo elekezi ya awali kwa Watumishi wapya unakwamisha jitihada za Chuo kutekeleza majukumu yake.

Vile vile utaratibu wa Chuo kutumia mapato yake ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Chuo unachelewesha ukamilishaji wa miradi hiyo na hivyo kukifanya Chuo kiendelee kuwa tegemezi katika majengo ya kupanga.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa Taasisi, Wizara na Wakala za Serikali zinakitumia Chuo hiki kutoa mafunzo kwa kada mbalimbali za Watumishi wa Umma.

**iv. Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)**

**Mhesimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utendaji ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF. Aidha, Kamati ilipata fursa ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa na TASAF katika Mkoa wa Njombe na

Singida kwa upande wa Tanzania Bara na Mikoa ya Mjini Magharibi, Kusini Unguja na Kaskazini Pemba kwa upande wa Tanzania Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza TASAF kwa kazi nzuri inayofanya. Tumekagua ujenzi wa kumbi za kufanyia mtihani katika Kata za Fujoni na Kizimkazi Zanzibar, miradi ya ujenzi wa Kituo cha Afya Pemba na Jombe, tumeona pia ujenzi wa madarasa 9, Ofisi, Stoo na uzio wa Shule ya Msingi Piki iliyopo katika Shehia ya Piki, huko Pemba. Kwa ujumla Kamati imeridhishwa sana na utekelezaji wa miradi hii hasa kipengele cha nguvu na mchango wa Wananchi katika miradi hii. Wananchi wameshirikishwa na wamejitoa kwa hali na mali, hali ambayo inaonesha uendelevu na ulinzi wa miundombinu iliyojengwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kwamba kati ya Kaya 713,350 zilizohakikiwa, Kaya 158,000 zimeboreka kiuchumi na zimepewa muda wa kujiandaa ili kuondolewa kwenye Mpango na kuanza kujitegemea kiuchumi ifikapo Januari, 2023. Haya ni mafanikio yaliyofikiwa na yanaendana na dhamira na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025 iliyolenga kuwawezesha Wananchi Kiuchumi na kukuza kipato cha Kaya na mtu mmoja mmoja.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee nitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuongezea bajeti TASAF ili iweze kuwafikia Walengwa wengi Zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Nobemba, 2022 jumla ya miradi 550 imeandaliwa na kati ya miradi hiyo, miradi 41 yenye thamani ya TSh. Bilioni 3.34 imekamilika. Miradi hiyo itawezesha upatikanaji wa huduma za Elimu, Afya, Maji,

Mazingira, barabara za vijijini na miradi ya ujasiriamali kwa Wananchi wanaoishi katika maeneo husika.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi hicho hicho, jumla ya vikundi 17,519 vya kuweka na kukopa vyenye Wanachama 245,125 vimeundwa. Kati ya hivyo, vikundi 17,327 ni vya Tanzania Bara na 192 ni vya Tanzania Zanzibar. Mafunzo yametolewa kwa Wawezeshaji 884 kuhusu uhamasishaji na uundaji vikundi, uwekaji wa kumbukumbu za taarifa za fedha, usimamizi wa mikopo na utatuzi wa migogoro.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mafanikio yaliyofikiwa na TASAF, Kamati imebaini baadhi ya changamoto mbalimbali zilizoibuka wakati wa utekelezaji wa mpango huo, zikiwemo: -

i) Baadhi ya Wanufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini kugoma kutoka kwenye Mpango pamoja na kuwa hali zao kiuchumi zimeimarika hivyo kupelekea mpango kutowafikia Walengwa wengi zaidi; na
ii) Uharubifu wa miondombinu hususan barabara zinazofunguliwa na Walengwa wa Mpango, ambapo barabara hizo baada ya kufunguliwa zinakosa uangalizi kutoka kwenye mamlaka zinazohusika (TARURA) na hivyo kuishia kuharibika. Ni rai ya Kamati kuwa, TARURA ione umuhimu wa kuzisimamia na kuziangalia barabara hizo ili lengo la uwepo wake liweze kukamilika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazotoa mikopo ya asilimia 10 kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu zishirikiane na TASAF na MKURABITA kwa kubadilishana uzoefu wa namna ya kuunda, kuratibu na kusimamia Vikundi ili kuongeza tija.

v. **Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na taarifa ya utekelezaji wa maazimio iliyotolewa na TAKUKURU kwa kuwa imekidhi haja kwa kutekeleza maazimio ya Bunge yaliyotolewa kwenye Mkutano wa 6, ambapo wameanzisha mpango wa TAKUKURU RAFIKI, kwa kuwa mpango huu unakwenda kuondoa hofu kwa Wananchi na kuwaongezea ari ya kushirikiana na TAKUKURU katika suala zima la kuzuia rushwa nchini.

vi. **Wakala wa Ndege za Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Ndege za Serikali ilianzishwa mwaka 2002 kwa mujibu wa Sheria ya Wakala za Serikali, Sura 245. Awali ilikuwa chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano hadi ilipohamishiwa Ofisi ya Rais, tangu mwezi Aprili, 2018.

**Mheshimiwa Spika**, Wakala wa ndege za Serikali imeendelea kuwahudumia Viongozi wakuu wa Kitaifa kwa kutumia ndege mbili ambazo ni: -

i) Gulfstream G 550; na
ii) Fokker F 50.

Pamoja na kusimamia huduma za usafiri wa ndege kwa viongozi wakuu wa kitaifa, Wakala unaratibu ununuzi wa ndege za Serikali na kuzikodisha kwa kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa ujenzi wa karakana ya matengenezo ya ndege za Serikali awamu ya kwanza katika uwanja wa ndege wa Dar es salaam na kuanza utaratibu wa uhamishaji wa ndege Fokker 28 ambayo imemaliza masafa yake ya kuruka

angani kwenda Chuo cha Usafirishaji cha Taifa (NIT) kwa ajili ya mafunzo.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 4.1 Maoni

**Mheshimiwa Spika**, yafuatayo ni maoni ya Kamati kuhusiana na shughuli zilizotekelezwa katika kipindi chote cha mwaka mmoja, ambayo yanabainisha mtazamo wa kile kilichojiri wakati Kamati ikitimiza majukumu yake. Maoni hayo ni haya yafuatayo: -

**a) Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

i) Malalamiko ya Wananchi juu ya migogoro ya Ardhi;
ii) Masoko mengi Tanzania hayawapi Wananchi hususani Wakulima unafuu wa Maisha kwa sababu ya changamoto za kiuendeshaji;
iii) Ukosefu wa Sheria mahsusi ambayo inasimamia usafiri wa umma mijini;
iv) Uharibifu wa miundombinu ya barabara za TARURA nyakati za mvua;
v) Gharama sawa za ujenzi wa Shule za Sekondari kwa nchi nzima.

**b) Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

i) Upungufu wa wataalamu wenye taaluma ya mifumo ya TEHAMA katika ngazi mbalimbali Serikalini.

4.2 Mapendekezo

**Mheshimiwa Spika,** yafuatayo ni mapendekezo ya Kamati kuhusu shughuli zilizotekelezwa katika kipindi cha

kuanzia Februari, 2022 hadi Januari, 2023 kama ifuatavyo:-

**4.2.1Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)**

1. **Azimio kuhusu migogoro ya Ardhi kwenye Halmashauri nchini.**

**a. Migogoro ya Ardhi katika Jiji la Dodoma**

**KWA KUWA**, Kumekuwepo na malalamiko kutoka kwa Wananchi kutokana na kutwaliwa ardhi yao na hivyo kusababisha migogoro ya ardhi baina ya Wananchi na Jiji la Dodoma.

**NA KWA KUWA**, Migogoro hiyo imeleta usumbufu mkubwa kwa Wananchi kwa kutumia muda mwingi kufuatilia utatuzi wa migogoro na gharama badala ya kufanya kazi zingine za kiuchumi na kijamii.

**NA KWA KUWA**, Jitihada za kuunda timu mbalimbali za Mkoa, Wilaya na Jiji la Dodoma kushughulikia migogoro zimeshindwa kupata suluhu.

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Serikali ifanye uchunguzi wa kina ili kubaini chanzo cha migogoro na ichukue hatua stahiki kwa wahusika. Aidha kwa wale ambao itathibitika wamedhulumiwa haki yao kwa namna moja au nyingine, Serikali ihakikishe wanapewa haki yao.

**b. Migogoro ya Ardhi kwenye Halmashauri nyingine.**

**KWA KUWA,** Migogoro ya ardhi ni kero kubwa ambayo iko katika Halmashauri nyingi nchini.

**NA KWA KUWA**, Migogoro hiyo imeleta usumbufu kwa Wananchi na kuwafanya kutumia muda mwingi na gharama kufuatilia utatuzi na kuacha shughuli nyingine za kuwaingizia kipato.

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Serikali ianzishe operesheni maalum ya kutatua migogoro ya ardhi katika Halmashauri zote nchini.

**2. Uanzishwaji wa Shirika la Masoko Tanzania**

**KWA KUWA**, Masoko mengi Nchini hayawapi Wananchi na Wakulima unafuu wa Maisha kwa sababu ya changamoto za kiuendeshaji zinazowapa fursa madalali kupanga bei za kilanguzi kwenye bidhaa za kilimo hali inayopelekea kupanda kwa bei za bidhaa.

**NA KWA KUWA**, Uendeshaji wa Masoko usioridhisha huwasababishia Wakulima wengi wanaopeleka mazao yao Sokoni kuuza bidhaa zao kwa bei ya hasara.

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Serikali ilete Mswada wa kuanzisha Shirika la Masoko Tanzania, Shirika ambalo litasimamia uendeshaji wa Masoko yote Nchini.

**3. Utungaji wa Sheria ya Usafiri wa Umma Mijini**

**KWA KUWA**, Mpaka sasa hakuna Sheria mahsusi ambayo inasimamia usafiri wa Umma mijini na Sheria zilizopo hazisimamii moja kwa moja usafiri wa Umma mijini.

**NA KWA KUWA**, Mradi wa Mabasi yaendayo kwa Haraka Dar es Salaam (DART) haujawa na Sheria Mahususi na hivyo kupelekea Mradi kuwa na mwenendo usioridhishwa. Miundombinu ya mradi kuvamiwa na

magari ya watu binafsi, kushindwa kupanga bei za nauli (*autonomasly*) bila kutegemea Mamlaka zingine hali inayopelekea mradi kushindwa kujiendesha wenyewe kwa faida.

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Serikali iharakishe mchakato wa ukamilishaji wa Mswada wa Sheria ya Usafiri wa Umma Mijini na kuwasilishwa Bungeni.

**4. Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA)**

**(a) Kuongeza Bajeti ya Dharura ya Matengenezo ya Barabara**

**KWA KUWA**, Miundombinu ya barabara nyingi za TARURA ikiwemo madaraja na vivuko vya watembea kwa miguu (*calavats*) zimekuwa zikiharibika nyakati za mvua.

**NA KWA KUWA**, Hali hiyo huwasababishia Wananchi usumbufu mkubwa wa kushindwa kutumia au kutumia kwa shida barabara nyakati za mvua na kupelekea hasara kwenye vyombo vyao vya moto au kushindwa kupata huduma mbalimbali za kuichumi na kijamii.

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Serikali itenge bajeti ya kutosha ya dharura kwa kila Wilaya ili kukabiliana na uharibifu unaojitokeza kwenye barabara nyakati za mvua.

**5. Kujenga Miundombinu ya barabara yenye uwezo wa kuhimili uzito zaidi ya Tani 10**

**KWA KUWA**, Miundombinu ya barabara za TARURA zinaharibiwa mara kwa mara na magari yenye uzito ama yenye kusafirisha bidhaa zenye uzito mkubwa.

**NA KWA KUWA**, Uharibifu huo unaisababishia Serikali hasara ya fedha kwa kuelekeza fedha nyingi kwenye matengenezo ya miundombinu za barabara zinazoharibiwa pamoja na kusababisha usumbufu kwa Wananchi wanaotumia miundombinu ya barabara hizo.

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Serikali ifanye mabadiliko ya viwango vya ujenzi wa uzito unaohitajika kwenye miundombinu ya barabara za TARURA kwa kutengeneza miundombinu ya barabara unaoweza kubeba uzito wa tani 30 au zaidi.

**6. Miradi ya Ujenzi wa Shule za Sekondari nchini**

**KWA KUWA**, Serikali imekuwa ikipanga gharama sawa za ujenzi wa Shule za Sekondari kwa nchi nzima,

**NA KWA KUWA**, gharama halisi baada ya kukamilika kwa mradi zimeongezeka sana ikilinganishwa na gharama zilizokadiriwa, hali inayosababishwa na tofauti ya bei za vifaa vya ujenzi, upatikanaji wa madini ya ujenzi na jiografia ya maeneo husika,

**KWA HIYO BASI**, Basi Bunge linaazimia kwamba Serikali ifanye tathmini ya gharama halisi za ujenzi Kikanda.

**4.2.2 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

**(i) Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)**

**KWA KUWA**, Kumekuwa upungufu wa Wataalamu wenye taaluma ya mifumo ya TEHAMA katika ngazi mbalimbali Serikalini.

**NA KWA KUWA**, Upungufuo huo umesababisha kuzorota au kuchelewesha utoaji wa huduma mbalimbali kwa Wananchi.

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Serikali ianzishe Programu ya vituo vya kukuza vipaji vya TEHAMA (incubation centers) kwa vijana waliohitumu masomo ya TEHAMA ili kutoa fursa za ajira kwa vijana ndani na njee ya nchi.

## SEHEMU YA TANO

### 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mhe. Jenista Joachim Mhagana, (Mb) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Mhe. Angela Kairuki (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Naibu Wawaziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (MUUUB), Mhe. Deogratius John Ndenjembi (Mb), Naibu Mawaziri wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Mhe. Dkt. Festo John Dugange (Mb) na Mhe. David Ernest Silinde (Mb) kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

Aidha, nawashukuru watendaji wote wa ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora wakiongozwa na Dkt. Laurian Ndumbaro na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na Watendaji wote wakiongozwa na Profesa Riziki Shemdoe kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake. Aidha, nitumie nafasi hii kumpongeza Dkt. Moses Mpogole Kusiluka kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Kwa niaba ya Kamati

namshukuru sana kwa ushirikiano aliotupa katika kipindi chote alichohudumu kama Katibu Mkuu Ikulu na tunamtakia kila la kheri katika majukumu yake mapya. Vile vile Kamati inampongeza Ndg. Mululi Majula Mahendeka kwa kuteuliwa kwake kuwa Katibu Mkuu Ikulu, Kamati inahaidi kumpa ushirikiano mzuri katika utendaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee niwashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano walionipatia katika kipindi chote cha mwaka mmoja cha utekelezaji wa shughuli za Kamati. Aidha, natambua na kuthamini michango yao adhimu na kujitoa kwao kikamilifu katika kuhakikisha Kamati yetu inatekeleza wajibu wake kikamilifu.

Kwa heshima kubwa ningetamani kuwataja majina yao, hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina hayo ni haya yafuatayo: -

1. Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo, Mb, - Mwenyekiti
2. Mhe. Dennis Lazzaro Londo, Mb- M/Mwenyekiti
3. Mhe. Mwantum Mzamil Zodo, Mb- Mjumbe
4. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb - “
5. Mhe. Dkt. Thea Medard Ntara, Mb - “
6. Mhe. Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mb - “
7. Mhe. Festo Richard Sanga, Mb - “
8. Mhe. Dr. Alice Karungi Kaijage - “
9. Mhe. Amandus Julius Chinguile - “
10. Mhe. Sebastian Simon Kapufi, Mb - “
11. Mhe. Michael Constantino Mwakamo, Mb - “
12. Mhe. Lazaro Justin Nyamoga, Mb - “
13. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb - “

14. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb - “
15. Mhe. Mwantum Dau Haji, Mb - “
16. Mhe. Shanif Jamal Mansoor, Mb - “
17. Mhe. Zacharia Paul Issaay, Mb - “
18. Mhe. Seif Salum Seif, Mb - “
19. Mhe. Constantine John Kanyasu, Mb - “
20. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis, Mb - “
21. Mhe. Tunza Issa Malapo, Mb - “
22. Mhe. William V. Lukuvi, Mb - “
23. Mhe. Prof. Paramagamba Mwaluko Kabudi, Mb - “
24. Mhe. Tamima Haji Abass, Mb - “

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee pia ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Nenelwa Wankanga Mwihambi, *ndc* kwa ushirikiano wake kwa Kamati katika kipindi chote Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake. Pia, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athumani Hussein, *ndc*, Mkurugenzi Msaidizi, Ndg. Gerald Magili, Makatibu wa Kamati hii Ndg. Sikudhani Abdallah Mbinga na Ndg. Frank Rumisha Nkya na Msaidizi wa Kamati Ndg. Pauline Mavunde kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo ya kina kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo, maoni na mapendekezo ya Kamati, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kuikubali taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Abdallah Jafari Chaurembo (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA**
**NA SERIKALI ZA MITAA**
2 FEBRUARI, 2023

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI :** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana, hoja imeungwa mkono. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo orodha hapa ya Wabunge ambao wameomba kuchangia kwenye taarifa hizi mbili za Kamati zetu za kudumu za Bunge na wakati huo huo wakati nikizisikiliza hizi taarifa nikawa najiuliza sisi kama Bunge tunalo jukumu la kukuza Kiswahili.

Sasa nikawa najiuliza haya maneno sijui kama ni mapya kwenye Kiswahili yameshakubalika mimi ndio siyajui ama vipi? Na Mheshimiwa Waziri yupo hapa nadhani BAKITA watatusaidia; utengwaji ni neno la Kiswahili? Utungwaji ni neno la Kiswahili? Utolewaji ni neno la Kiswahili? Halafu kama unazungumzia kuhamia, watu kuhamia sehemu unaweza kusema mchakato wa uhamiaji wa kuelekea makao makuu?

Kwa hiyo, maneno ya Kiswahili lazima sisi tuwe mstari wa mbele. Kuna maneno mengi leo nilikuwa najifunza hapa; uanzaji wa miradi; uondolewaji; uandikishwaji; usababishaji.

Mheshimiwa Waziri nadhani akija hapa atatusaidia kama haya maneno BAKITA wameshayapitisha ama hapana, lakini ninachomaanisha ni kwamba taarifa zetu Wabunge ni lazima ziwe na Kiswahili sanifu kwa sababu hizi ni Taarifa za Kudumu na vivyo hivyo upande wa Serikali ndio maana na wao huwa wanasisitiza, lazima sisi tuwe mstari wa mbele, Kiswahili kimezaliwa hapa, kimekulia hapa na kinazeekea hapa nchini.

Waheshimiwa Wabunge, kwenye orodha yetu tutaanza na Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko ajiandae.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye mawasilisho ya Kamati hizi mbili.

Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa na niwapongeze Mawaziri wote wanao-*appear* kwenye Kamati yetu wanatoa ushirikiano mkubwa na wanapokea ushauri.

Mheshimiwa Spika, mimi nilitaka nishauri jambo la kwanza hapa kuhusiana na mikopo ya asilimia 10 inayotolewa kwenye mapato yote ya halmashauri kwa ajili ya kwenda kukopeshwa kwenye makundi ya Vijana, akina mama na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukishauri na ninaomba sasa Serikali ikubali kupokea ushauri huu, kuongeza kundi la akina baba. Inatuletea migogoro na sasa hivi imefika mahali wakina baba wanalazimika hata kama hana mpango wa kuoa inabidi aoe ili apate

mama ambaye atapata sifa ya kwenda kukopesheka maisha yaendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matatizo haya ya kijinsia tunayohangaika nayo mengine *psychologically* yanasababishwa na sisi wakina baba kukosa kitu mfukoni. Sasa unaona mama ndiye anayetoka anaenda kwenye *VICOBA*, mama ndiye anayetoka anaenda kukopeshwa, sisi wababa tunabaki ndani tusubiri mama alete. Hili jambo linatuathiri akina baba kisaikolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niiombe sana Serikali ifanye mabadiliko, sheria hii wakina baba waingizwe, makundi yote yaweze kukopeshwa na uzuri mfuko huu umeshakua sana, sasa hivi kwa mwaka zinatolewa zaidi ya shilingi bilioni 68. Kwa hiyo, naomba nianze na hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kuhusiana na soko la Kariakoo; sheria iliyoanzisha soko hili la Kariakoo ni ya mkoloni, imefanyiwa mabadiliko mwaka 2002, lakini hapa kwenye Kamati tumeshauri soko hili sasa tufanye mabadiliko ili liweze kusimamia masoko yote nchini bila kuathiri mapato ya halmashauri husika. Maana wasiende kusimamia halafu wakachukua na mapato ya halmashauri, hapana wasimamie.

Mheshimiwa Spika, sasa wakati tunapitia kwenye taarifa za utekelezaji wa soko la Kariakoo nilihangaika na wenzangu kutafuta wapi madalali wanaingia kuchangia Serikali, hatukuwaona. Kwenye *organization structure* hawamo, lakini leo ukienda pale Kariakoo umelima nyanya yako kutoka kule Ng'uni, Mkalama, ukibeba pale Kariakoo kuna watu wananitwa madalali. Hawa watu ndio wanaopanga bei, Wizara ya Kilimo hawawajui,

uongozi wa soko wenyewe hawawajui, lakini ndio wenye sauti.

Mheshimiwa Spika, leo tunazungumza Mheshimiwa Rais ametupatia bilioni 958 zimeenda kwenye Wizara ya Kilimo, lengo ni nini? Zikamguse yule mkulima wa chini. Sasa tusipomlinda huyu mkulima wa chini ambaye ndiye mzalishaji anufaike, leo analima kuna mtu anakuja kumpangia afanye nini.

Mheshimiwa Spika, kule kwangu kuna *terminology* kubwa sana za madalali na lumbesa. Mkulima akishalima, yaani kazi ya mkulima wa nchi hii yeye analima, akishavuna tu sio kazi yake. Kuna mtu pale anaitwa dalali yeye ndiye anayeamua nini kifanyike, kuna mtu anaitwa mchambuzi; kwanza bidhaa yake akishavuna kama ni kitunguu anapokea mchambuzi, anachambua ni cha aina gani? Anampa dalali na moja ya sifa/*principle* ya dalali ni marufuku mkulima kukutana na mnunuzi, yaani yeye analima anamkabidhi dalali, dalali ndiye apange. Hiki kitu naomba tukitazame vizuri, kinaua uchumi wa wakulima wetu kule chini.

Mheshimiwa Spika, kama tunawapenda hawa madalali basi kuwe na mfumo rasmi wa kuwasimamia, wachangie pato la Taifa, lakini na wao wajue kwamba Nyanya inalimwa shilingi ngapi, kuna *process* ngapi za kulima nyanya, sio kusubiri nyanya wachukue wao wapange bei.

Mheshimiwa Spika, imefika mbali sana, wakati mwingine mpaka watu wanatoka nje ya nchi wanaingia ndani mwetu, tunapenda kweli kufanya nao biashara, wanakwenda kununua kule kwa mkulima chini kupitia dalali. Jambo hili naomba sana Serikali ichukue hatua za

haraka. Jitihada hizi kubwa za Mheshimiwa Rais za kuhakikisha anamkomboa mkulima, kama hatutaangalia mwisho wa kazi anayoifanya, maana hapa tunapanga, peleka mbegu, peleka sijui umwagiliaji, peleka sijui vitu gani mwisho wa siku hatuangalii anaenda kuuzaje. Ninaomba sana Serikali ituangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili la lumbesa kule kwangu kuna majina mengi kweli kweli tumepewa, kule kuna aina nyingi; moja inaitwa neti ya kuvuta, hii inabeba ndoo kumi na mbili na anayepanga ni dalali na mchambuzi ndiye anayekwambia weka hapa, mkulima hana shida. Yule dalali anakuja tayari akiwa na risiti ya faini ya lumbesa, ameshalipa Serikali/halmashauri. Kwa hiyo, hakuna mtu wa halmashauri anayemfanya chochote kwa sababu ameshalipa faini.

Mheshimiwa Spika, kuna nyingine inaitwa shishimbi, hii inabeba ndoo kumi na nne na mimi niseme tu Mheshimiwa Mwigulu haya ndio uchumi wetu. Hizi *principle* zenu za uchumi na *theory* mnazo, maana jana nilimsikia hapa anasema Wabunge kama hujasoma uchumi sijui usichangie mambo ya uchumi. Uchumi ni haya maisha haya tunayoyazungumza na bahati nzuri Wabunge wote waliopo humu wako makini na wanajua uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kwa tafsiri nyepesi tu ukisoma wakina Smith, wakina nani, wataalamu wa uchumi duniani, wanahitimisha kwamba uchumi ni shughuli zote za binadamu zinazolenga kutekeleza mahitaji yao. Kwa hiyo, humu ndani Waheshimiwa Wabunge wote ni wachumi pamoja na wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yaani uchumi tunazungumza nyanya hapa, tunazungumza vitunguu, Mheshimiwa Mwigulu ndio uchumi huu na uchumi ukipanda au ukishuka tunauona kwenye hivi vitu. Nikiona nina kuku wangu wawili wakiongezeka wakiwa watatu ndio uchumi huo kwetu sisi. Sasa hayo ma-*principle* makubwa nendeni nayo huko duniani mtuletee fedha sisi tunataka hivi vidogo vidogo vya kwetu. Tukilima vitunguu vyetu tupate fedha ndio uchumi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, *translation* ya uchumi ishushwe ije kwa mwananchi wa kawaida ili tukizungumza uchumi tuelewane sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka nishauri hilo na kuitisha kwa kuomba sana mtusaidie hawa madalali wasiwe na sauti, ikiwezekana mkulima ndiye amwambie dalali fanya hiki na sio dalali amwambie fanya hiki na sifa ya dalali na yeye alime, akiwa analima kama ni dalali wa kitunguu tuone shamba lake, halafu ndio tumpe kazi ya kuwa dalali kwa sababu atakuwa anajua uchungu wa kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze kidogo kuhusiana na Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, hii Bodi ni ya muda mrefu na yenyewe, imeanzaishwa tangu mwaka 1953...

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kenneth Nollo.

**T A A R I F A**

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe tu taarifa mzungumzaji kuwa hoja ya dalali kwamba lazima awe na shamba, anapokuja tu *point* yake kutofika mwisho ni kwamba tuimarishe Vyama vyetu vya Ushirika viwe *strong* ili wananchi wetu wawe na uhakika wa sehemu kwenda kuuza, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, huyo ni shemeji yangu, kwa hiyo, sina namna ya kuacha kuipokea**.**

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imeanzishwa mwaka 1953.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe unapokea taarifa ya Mheshimiwa Kenneth Nollo?

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ninaipokea. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Sekunde 30 nakuongezea umalizie kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nashauri Bodi hii ya Mikopo ya Serikali za Mitaa sheria yake imekuwa ni ya muda mrefu sana, yaani ina sura bado ya kikoloni na bado ina madeni mengi sana.

Huu mfuko mpaka sasa hivi una kama bilioni 14.6 lakini una madeni ya bilioni nne na bado ni kama Waheshimiwa Wabunge hapa tukizungumza ni kama haueleweki eleweki hivi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nashauri kwa kuhitimisha mfuko ufanyiwe *reforms* ili ufanane na mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja zote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

Nilikuwa nimekwishamtaja Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, atafuatiwa na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mheshimiwa Dkt. Paulina Daniel Nahato ajiandae.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuweza kunipa nafasi ya kuchangia juu ya taarifa hizi ambazo zimewasilishwa hapa hususani katika huduma za jamii, pamoja na maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, mimi niseme tu nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais na Wizara ya Afya, lakini pamoja na Wizara ya Elimu kwa namna ambavyo wameweza kujenga miundombinu mingi sana katika nchi yetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafahamu karibu katika kila jimbo kuna majengo ya zahanati, vituo vya afya pamoja na madarasa mengi ambayo mpaka sasa hizi mengine yanakuwa yanakosa watoto. Kwa hiyo kwa hili nampongeza Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia Mheshimiwa Rais ameendelea kupambana na haya masuala ya vitendo vya ukatili kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii. Tunaona ni kwa namna gani ambavyo Mheshimiwa Waziri wetu Gwajima amekuwa akiendelea kupambana kupitia hii SMAUJATA na nini kuhakikisha zile kesi za watoto na akina mama wanaofanyiwa kule kama wale watu wa maeneo husika wanashindwa kuzingatia utaratibu wa kuzifikisha kesi mahakamni, yeye mwenyewe amekuwa akiingilia kati. Kwa hiyo, mimi niseme tu nawapongeza kwa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mjadala wangu leo mimi ninapenda nijielekeze kwenye hali ya ufaulu nchini. Tunafahamu kabisa mwaka huu hali ya ufaulu nchini imekuwa ya kusikitisha sana na kimsingi ni hali ambayo kama Taifa tunatakiwa tujitafakari na tuone ni nini kinatakiwa kufanyika kuona Watoto wetu wa Kitanzania wanapata elimu iliyo bora, elimu ambayo itakuwa na tija na kubadilisha maisha ya Watanzania wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna kauli ambayo ipo inasema *collapse of education is a collapse of the nation* (anguko la elimu ni anguko la Taifa). Natamani tulichukue hili katika hali ya uhalisia kabisa kwamba elimu hii isipopewa kipaumbele katika nchi yetu tutaendelea kuwa na taifa ambalo lina watu wasiokuwa na weledi wa kutosha kukabiliana na changamoto za maisha ambazo zinakuwa zinatukabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuaona masomo ya sayansi watoto wetu wame-*fail* sana na masomo ya sayansi ndiyo masomo mengi yanayoweza kumwezesha mtoto kuweza kujiajiri katika sekta mbalimbali. Mtu aliyesoma

maabara ni rahisi kwenda kufungua kituo chake cha maabara na kufanya ile tasnia yake pale kwa kuwasaidia Watanzania na tasnia zinginezo.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema ni nini? Ninatamani kuona Serikali yetu hii ya Chama cha Mapinduzi inachukua hatua kubwa sana kuhakikisha kuwa lililotokea mwaka huu, mwakani halitokei.

Mheshimiwa Spika, ninaumia sana kwa sababu nina uzoefu wa namna ambavyo watoto mbalimbali au wazazi mbalimbali wamekuwa wakifanya jitihada ya kuhakikisha watoto wao waweze kufanya vizuri kwenye masomo. Kuna watoto ambao wanasoma katika *private schools* (shule za binafsi), watoto hawa mimi niseme tu kwa nafsi yangu naamini ndio waliotubeba kwenye matokeo haya ya mwaka huu. Wengi ndio walikuwa na nafasi ya kuweza kufundishwa na walimu kwa kutosha, lakini pia kwa kuwa na walimu wenye uangalizi na msisitizo wa ukaribu wa kuhakikisha wafanye vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninawapongeza sekta binafsi hii ya elimu kwa namna ambavyo wametubeba angalau kwa hizi asilimia ambazo tunakuwa tunaona kwamba tuna watoto waliofaulu kama Taifa wanatusaidia.

Mheshimiwa Spika, mimi nina-*grade* kwa namna nyingine kwamba wapo watoto ambao walikuwa wanasoma kwenye shule za Serikali ambao wazazi wao walijitoa kwa kuwatafutia walimu binafsi na *tuition,* ndio ambao wameweza kutubeba na kutufikisha Taifa kama hapo. Kwa hiyo pia niwapongeze wazazi ambao wamekuwa na wito wa kusimamia elimu ya watoto wao bila kuwaachia walimu peke yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakuja kulitazama kundi la tatu la wale Watanzania ambao hawana wazazi wenye kipato kikubwa cha kwenda *private,* lakini hawana wazazi wa kuwatafutia walimu wa kuwafundisha *tuition*. Hawa ndio watoto wa Watanzania wengi, ndio wame-*fail* sana na kiukweli kwa kuliona hili ndipo ninaona *gap* la aliyenacho na asiyenacho linazidi kuongezeka katika Taifa letu. Kama Taifa nadhani kumekuwa na harakati nyingi za kupambana kupunguza *gap* la walionacho na wasiokuwa nacho. Lakini kwa kuendelea na mfumo huu wa elimu ambao watu ambao wanakuwa na fedha wanaweza kuwapeleka watoto kwenye shule nzuri na wakapata elimu nzuri na wengine wakabaki wakapata elimu yetu hii bure halafu wakakosa usimamizi mzuri, naiona hatari ya kuwa na Taifa ambalo watu wengi ni dhaifu na hawana ufikiri mzuri.

Mheshimiwa Spika, niseme tu ninaiomba Wizara hii watafute namna bora ya kuhakikisha watoto wetu wale wa Kitanzania, wale halisi wa mkulima, mfugaji, wavuvi wale watu wa chini kabisa wajasiriamali wadogo wadogo wanasaidiwa kupata elimu iliyo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaongea nikiwa na uchungu mkubwa sana, moyo wangu unaumia kwa sababu mimi ni kati ya wale watoto ambao tumesoma hizo shule lakini kwakweli bila ya yale mapambano binafsi ya mtoto kuhakikisha unajituma na nini, mazingira yalikuwa *supportive*, yanakusaidia kuweza kujituma ukawa na *access* ya hivyo vitabu, unakuta katika ripoti ya *CAG* unaona kabisa kuna vitabu havijapelekwa kwenye maeneo ya shule yetu, lakini unaona *morale* ya wazazi kuwahamasisha watoto kwenda shule imeshuka.

Mheshimiwa Spika, taarifa hizi tunaziona kwenye mabango yanayoendelea kutolewa na Mikoa mbalimbali kwamba wanafunzi idadi fulani hawajaripoti shuleni, wanafunzi kiasi fulani hawajaripoti shuleni, kwa hivyo, morali ya wazazi kusomesha watoto imeshuka, hii ni kutokana na kwamba watoto wengi ambao wamesoma wanaonekana ni mizigo wanaporudi nyumbani kwa sababu kwanza wanakuwa tayari wameshakuwa ni wavivu, hawataki kujituma na kazi zile za kawaida za kijamii zinazowazunguka hawataki kushiriki. Waliosoma wengi hata walioishia *Form Four* tu hawataki kushika majembe, hawataki kushiriki kwenye vikundi, wanajiona kama *they are extra-ordinary*, wanakuwa wako tofauti na wenzao wale ambao waliwaacha kabla hawajaenda kwenye hizo elimu zao, kwa hiyo wazazi pia morali imeshuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaona pia hata Walimu wetu, mimi naona morali ya Watumishi hususani Walimu pia imeshuka. Mwalimu badala ya kupambana kumsaidia mwanafunzi anapambana kupata *extra money* ya kujikimu yeye na familia yake, kwa sababu mwalimu mwenyewe angependa kuona mtoto wake anasoma katika shule hizo za *private* nzuri, kipato chenyewe ndiyo kama hiki ambacho tunakiona, wote tunafahamu kwamba kima cha chini cha mishahara bado siyo toshelevu kulingana na mfumko wa bei wa bidhaa mbalimbali na maisha kwa ujumla yanakuwa yamepanda gharama.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amekuwa akiendelea kuunda Tume mbalimbali, tumeona ameunda Tume ya Mambo ya Haki Jinai, lengo ni kuboresha haki ya Watanzania waweze kupata haki lakini hata elimu ni haki! Kwa hiyo, ninatamani kuona

Mheshimiwa Rais atuangalizie au atuundie Tume nyingine ya kuchunguza huu Mfumo wa Elimu utaendelea kumkandamiza au kumuumiza mtoto wa kipato cha chini mpaka lini?*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, katika suala la ufaulu nisiseme mengi niishie hapo, ufanyike utafiti wa kina wa kuhakikisha watoto wa chini wanasaidiwaje ili waweze kufanya vizuri katika masomo yao.

Mheshimiwa Spika, pia niendelee kuomba ukarabati wa shule…

**SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha kengere ya pili imeshagonga.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru naamini majengo yote ya shule za zamani yatafanyiwa ukarabati. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Paulina Daniel Nahato, Mheshimiwa Michael Constantine Makamo ajiandae.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii. Nami nianze kwa kuzipongeza Kamati zote mbili na taarifa zilizowasilishwa, lakini nimpongeze zaidi Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namuomba Mwenyezi Mungu anisaidie lakini leo nina jambo moja tu mahsusi kama

nitajaliwa kuongea na lingine basi ni kwa rehema za Mwenyezi Mungu. Jambo lenyewe ni ubora wa elimu yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2022 inaonesha tumeendelea kupata matokeo mabaya hasa kwenye mitihani ya watoto ya sayansi. Tumeendelea kuwa na matokeo mabaya hasa kwenye shule zetu za Serikali. Tumeendelea kuwa na matokeo mabaya ya sayansi lakini tumeendelea kuwa na upungufu mkubwa wa walimu wa sayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2022 tulihitaji kuwa na walimu 19,216 wa hesabu, tulifanikiwa kupata Walimu 5,537. Tunao upungufu wa Walimu 13,679 kwa asilimia, tuna upungufu wa Walimu kwa asilimia 71, huo upungufu wa walimu asilimia 71 umesababisha watoto kufeli somo la hesabu kwa asilimia 83.

Mheshimiwa Spika, suala la somo la fizikia, *(physics)* tulihitaji kuwa na Walimu Elfu Kumi na Sita na kidogo, tumekuwa na walimu elfu tatu na kidogo. Tumekuwa na upungufu wa walimu elfu kumi na mbili na kidogo, tumepata upungufu kwa asilimia 77. *Failure* ambayo imesababishwa na huo upungufu wa Walimu ni asilimia 82, tunawekeza kwenye *standard gauge*, tunawekeza kwenye ujenzi wa barabara kubwa kubwa *fly overs* tunawekeza kwenye ujenzi wa mahospitali ya rufaa chungu nzima, tumewekeza kwenye miundombinu mizuri sana *excellent* nani anakwenda kuihudumia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumewekeza vya kutosha kwenye majengo na mimi nataka nimpongeze sana mama yangu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan tumejennga sana madarasa, mama umefanya kazi kubwa mno

kwenye ujenzi wa madarasa! Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge tuishauri Serikali sasa wageukie kuajiri walimu namna pekee itakayo tutoa kwenye hii *failure* ni kusaidia kuajiri walimu walioko mtaani waende watusaidie kuwafundisha watoto.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wa 2022, walimu walioomba kuajiriwa TAMISEMI walikuwa 165,948 tumeajiri walimu takribani 16,000 kutoka kwenye 165,948. Katika hao walimu 30,000 ni Walimu wa Sayansi walioajiriwa ni takribani walimu 5000 wa sayansi kutoka kwenye walimu 30,000. Tunataka muujiza, hatutatoka kwenye hizi *failures* kama hatutawekeza vya kutosha katika kuajiri walimu kwenye nchi hii. Tutaondoa namna ya kuwa *grade* shule zilizofanya vizuri na ambazo hazijafanya vizuri, tutaondoa wala haina shida. Lakini haitakuwa suluhisho la kufuta sifuri mashuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukizungumzia walimu kuna *principle* inasema kitu chochote kisipotumika kwa muda mrefu kinakuwa butu hata kisu usipokitumia kwa muda mrefu lazima wakati wa kukitumia lazima ukinoe kwanza. Tunaajiri leo walimu waliohitimu 2015 tunawapeleka shule wanaenda kufundisha hakuna programu yoyote ya kuwanoa, kuwakumbusha kuwarudisha kwenye nafasi yao ya kwenda ku-*perform* vizuri, hatufanyi hivyo! Mbaya zaidi leo kwa taarifa nilizonazo mara ya mwisho tumewaajiri walimu wa sayansi mwisho tuliishia 2017.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2018, mwaka 2019, mwaka 2020, mwaka 2021na mwaka 2022 miaka mitano au sita hawajaariwa. Hii miaka ya karibuni wote wako mtaani hawajaajiriwa, sasa utakavyowaajiri hawa watu mtu ambaye ameshinda kwenye kijiwe cha kahawa ama

cha bodaboda kwa miaka mitano mfululizo unampeleka shuleni akafanye muujiza gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namna ya kwenda kuboresha hili nataka niishauri Serikali, walimu walioko mtaani hawa zaidi ya laki moja. Tunaupungufu mkubwa kuliko hawa walimu walioko mtaani, tukifanya hili tutasaidia Serikali katika mambo mawili. Jambo la kwanza ni kuendelea kuwafanya wawe *active*, pili tutakuwa tumepunguza pia huo upungufu wa walimu ambao umesababisha hii *failure* ambayo tunaiona sasa.

Mheshimiwa Spika, jambo lenyewe tuajiri kutumia ajira za muda mfupi. Kwa sababu nchi yetu tunaijua, bado ni nchi inaendelea bado ni nchi maskini uwezo wa kutoa ajira zote hizo kwa wakati mmoja nchi yetu haiwezi tunafanya shughuli nyingine nyingi ambazo zote tunazihitaji. Sasa kwa sababu ya upungufu wa fedha bajeti ndogo tuliyonayo tuwapeleke hawa Walimu wakafundishe kwa maana ya ajira za mkataba za muda mfupi mfupi. Tukiwatawanya kwenye mashule huko kwanza tumepunguza upungufu wa Walimu lakini *at the same time* tumewasaidia kuimarisha wasisahau, wasibweteke, wasiwe butu na mwisho wa siku kutusaidia katika kuongeza ufaulu mashuleni

Mheshimiwa Spika,sisi tulitembelea Chuo cha Mwalimu Nyerere pale Butiama. Tulikuta kwa mika kumi na tatu chuo kina watumishi zaidi ya arobaini. Kwa miaka 13 hakijafanya udahili na wale watumishi wanalipwa mishahara ya Serikali *OC* zinakwenda zinatumika lakini tukija tuna upungufu wa walimu wa hesabu tuna maprofesa tumewaweka pale *for 13 years* hawajafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, tunakwenda wapi? Hebu twende na vipaumbele kama Taifa. Kama lengo letu ni kuisaidia Nchi hii maskini ipige hatua lazima tujiulize changamoto zetu sisi ni zipi? Changamoto yetu kubwa ni elimu, elimu, elimu! Tunahitaji kuelimisha watu wetu kwanza wajitegemee. Tumezoea kuwaambia watu jamani someni mjiajiri, *well and good*! Tunaweza kujiajiri, hebu niambie mimi Mwalimu wa Historia nimefundishwa niende nikamfundishe mtoto *Zinjanthropu*s ni nini? Niende nikamfundishe mtoto *evolution of man* ni nini? Haya sijaajiriwa mimi niende nikajiajiri kwenye nini? Wapi nitapewa kazi ya kuelezea *evolution of man*… wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namna pekee ya kunitumia mimi ni kunipa nafasi ya kwenda kufundisha hiyo *evolution of man*. Mtume *Mohamed Swalala walah wasaalam* katika maisha yake alikutana na swahaba mmoja aliyekuwa na busara sana, aliona Mtume anaishi vizuri sana na watu akamfuata akamwambia, *Ya Mohammad*…' ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu nipe ushauri, nishauri mimi'. Mtume akamjibu akamwambia la tagadhabu! akarudia tena kwa sababu hakuwa anaamini kwamba huo ndiyo ushauri atakaopewa na Mtume Mohamed.

**SPIKA:** Sekunde thelethini kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, akamwambia eeh! Mtume Mwenyezi Mungu nishauri, mara tatu akamwambia la tagadhabu! anamwambia usigadhabike. Nimejitahidi sana hivi nivyozungumza nimejizuia nisigadhabike, lakini hali halisi iliyopo huko tunapotoka, mimi natoka kijiini ndugu zangu, hali halisi iliyoko huko watu wanapata shida.

Mheshimiwa Spika, mtu kasomesha mwanae bado anaenda kumhudumia 'libaba' liko pale unalipika ugali, hajaajiriwa, unaangalia aliyeko shule naye anafeli, kwa nini anafeli hamna mwalimu! mwalimu unaye nyumbani unampikia ugali! *Inna lillahi* Mwenyezi Mungu atusaidie! Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Pauline Daniel Nahato atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Constantine Mwakamo na Mheshimiwa Festo Richard Sanga, ajiandae.

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia. Awali ya yote napenda sana kumpongeza Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa sana anayoifanya, pia napenda kuipongeza Wizara ya Maendeleo, Jinsia na Watoto pamoja na Waziri wake na Naibu kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu leo utajielekeza katika suala la ukatili wa watoto. Suala la ukatili kwa watoto limekuwa ni changamoto kubwa sana katika Taifa letu na limekuwa likiongezeka mara kwa mara. Kama tunavyofahamu watoto ndiyo Taifa la kesho, watoto wanaandaliwa kuanzia wanapokuwa tumboni, tangu mama anaposhika mimba na maendeleo ya mtoto pale ndiyo yanapoanza. Mimba ikiwa haitatunzwa vizuri hata ukuaji wa huyo mtoto atakapozaliwa hautakuwa mzuri. Mimba inabebwa vizuri na mwisho mtoto anazaliwa, lakini sasa anapofika duniani na kuanza maisha anakutana na changamoto. Hili ni jambo la kusikitisha sana na katika Kamati yetu ya Huduma za Jamii tumeliangalia suala hili la vitendo vya ukatili wa watoto na jinsi ambavyo linaendelea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu za Polisi ambazo Wizara imetupatia ya mwaka 2021, inaonesha kwamba, ripoti ambazo zimeripotiwa Polisi japokuwa hizi ripoti zilizoripotiwa Polisi wote tunaamini kwamba zitakuwa siyo zote zilizoripotiwa, lakini kwa hizi chache ambazo zimeripotiwa bado zinatosha kutupatia picha halisi ya ukubwa wa hili tatizo. Kwa mfano, matukio yaliyoripotiwa jumla yake ni 11,429 ambayo hayo yametolewa taarifa katika vituo vya Polisi.

Mheshimiwa Spika, matukio yaliyotolewa taarifa ni ya ubakaji ambayo ni matukio 5,899, mimba kwa wanafunzi ni matukio 1,677 na ulawiti ni matukio 1,114 pamoja na kuzorota kwa masomo ni 790 na mashambulio ya mwili ambayo ni 350. Hizi ni zile ripoti ambazo zimeenda kuripotiwa katika vituo vya Polisi, lakini tunajua kabisa katika utamaduni wetu wa Kiafrika tofauti na tamaduni za nchi za nje ambapo mtoto hata anapopigwa kibao na mama yake anachukua simu palepale mezani na kuwapigia ustawi wa jamii na ustawi wa jamii unamchukua na kumpeleka katika vituo vya kulelea watoto na huyo mzazi hatamwona mtoto wake, hilo ni tofauti na kwetu kwa hiyo wazazi wanaogopa sana kuwafanyia ukatili watoto.

Mheshimiwa Spika, katika nchi zetu za Kiafrika na Tanzania ikiwemo, vitendo vya ukatili kwanza tafsiri yake ni ngumu, kumchapa mtoto kama Waziri Mkuu alivyosema leo na mimi pia nilikuwa nataka kusema, mimi kiboko hapana! Kiboko siyo adhabu kwangu, mtoto tiba yake ni kuongea na mtoto lakini sasa katika nchi yetu, tunaona kwamba familia hazijachukua nafasi yake. Ubakaji wa watoto takwimu zake hatuna, kwanza ubakaji umeanzia wapi kwa mtoto? Mtoto wa miaka mitatu,

mtoto wa miezi sita amebakwa imeanzia wapi? Huu ni utamaduni wa wapi? Mimba za wanafunzi! Suala kubwa ambalo mimi hapa naliona ni kwamba wazazi hatujachukua nafasi zetu kuongea na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata mtoto akizaliwa tu pale unapokuwa mama unamnyonyesha, unapoongea na mtoto anakuelewa hizo ni tafiti zinavyoonyesha. Mama unapongea na mtoto na mtoto anacheka ananyonya anakuangalia unamsemesha anaelewa! Kwa hiyo, hata baadae atakapokuwa na mwaka wa kwanza na mwaka wa pili unavyoendelea kuongea naye unasogeza ukaribu wa yule mtoto, kwa hiyo inakuwa ni mwanzo wa kuwa karibu na watoto.

Mheshimiwa Spika, suala kubwa ni kuvunja ukimya kwa watoto, tutakapovunja ukimya kwa watoto, watoto wakiwa karibu hakuna jambo watakaloficha. Kama katika nchi zilizoendelea, mtoto anaweza kupiga simu yaani mama yake amempiga tu kibao kidogo tu ananyanyua simu, anamwambia mama *I will call the social worker and she/he will call the social worker* kwa mama yake aliyemzaa, hivi kwetu Watanzania tunakwama wapi? Tukianza kuwazoeza watoto wetu kuongea mambo mazuri tu, mambo ya kawaida, mambo ya ngono, mambo ya sehemu za siri, mambo ya vitu vingine, watoto wanaelewa na watatupa taarifa na huu ukatili mwingi utapungua. Tunakuja kusubiri mtoto amelawitiwa mara thelathini, mara arobaini mpaka ameshakubuhu, siku umemkamata ndiyo mama au baba mbio unakwenda Polisi kuripoti, hasa unaenda kuripoti nini?

Baada ya muda tena, na wewe mwenyewe mzazi ni maskini unapenda pombe, unakuta tayari.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi labda napenda kusema tu, Serikali umefika muafaka wa kuchukua hatua. Tukae chini tuchukue hatua madhubuti ya kuhakikisha kwamba tunakuwa karibu na watoto na vile vile tuhakikishe tunawaweka watu ambao ni wataalamu wa kuweza kuongea na watoto pamoja na wazazi wao. Tuimarishe maongezi kati ya watoto na wazazi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili pia hizi sheria zirekebishwe. *Once* sheria imeshakuwa imewekwa mezani wazazi wasije wakasema aah! tumeshaelewana tunaomba tu hili la kijamii tukalimalizie nyumbani. Haya masuala ya kwenda kumalizia nyumbani yanawasababishia watoto ukatili; nao hao wakiwa wakubwa watafanya ukatili kwa watoto wao. Kwa hiyo, jamii itakuwa na mwendelezo wa ukatili miaka na miaka na haitaisha. Tukianza kuziba mwanya huku chini tutaweza kurekebisha hii tabia ya ukatili kwa Watoto.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho niseme kwamba, elimu itolewe hata kwa hao waathirika. Mtoto anapoathirika hili linabaki kuwa donda linabaki kwenye moyo wake na halitaisha; na ili liweze kuisha ataendelea kulipiza. Kwa hiyo, atakapokuja kuwa mtoto mvulana anaanza darasa la pili la tatu la nne atakuwa anafanya vile akifikiria kwamba anajifariji kumbe naye anaongeza tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi napenda kuishauri Serikali hili jambo tuliangalie vizuri sana. Tusilichukulie tu ukatili, ukatili, ukatili chanzo cha ukatili ni nini kwenye jamii yetu? Na katika nchi zilizoendelea wamefanya nini kupunguza ukatili? Nchi ya Norway ambako mimi nimesoma hivi vitu havipo, na watoto wakifanyiwa hivyo

hata ukimuangalia tu anakuambia *why are you looking at me*? Mtoto mdogo anakuambia *why are looking at me*? Yaani kuonesha kwamba anajielewa. Kwa hiyo, watoto wetu wa Kiafrika tuwajengee kuanzia wakiwa wadogo wajielewe, wajenge ile uwezo wa kushangaa mtu anapotaka kumwambia lolote sio hii ya kumwambia aah wewe ni mjomba, wewe ni mtoto wa kaka yangu, wewe ni mdogo wangu ngoja nikuogeshe tulale pamoja, mtotoo anaona kama ni kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tunaomba Serikali ichukue sheria kali sana na kuhakikisha kwamba elimu inatolewa ya kutosha kuweza kuhakikisha ukatili kwa watoto unaisha ili tujenge jamii inayokuja tofauti kabisa, na hii iwe ni historia ya masuala ya ukatili kwa jinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA**: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Paulina nilikuwa najiuliza hapa, kwa hivyo kumchapa mtoto kibao ni ukatili?

Mheshimiwa Paulina, kumchapa mtoto kibao ni ukatili? Inabidi aende polisi? *(Kicheko)*

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Spika, nimetolea mfano wa nchi zilizoendelea, lakini mimi sipendi kuchapa mtoto kwa ujumla, kibao, kiboko naona kwamba ni ukatili kwa sababu hata huo mkono utakao mchapa unaweza ukamsababishia kutokusikia maisha. Kwa hiyo, sijui labda umetoka kwenye *stress* zako, sio wewe Mheshimiwa, samahani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mtu ametoka kwenye pombe zake kwenye *stress* zake amegombezana na hawara zake anamchapa mtoto kibao, hajui ule mkono aliomchapa nao amemchapa kwa kiasi gani, atamsababishia kilema cha maisha, nilikuwa namaanisha hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Ahsante sana. Lazima tuwe tunaelewana maana michango hii watoto wanatazama na wazazi pia wanatazama. Sasa na sisi tuwe tumeshatengeneza mazingira pa kumpeleka huyo mtoto baada ya kuripoti kupigwa kibao na baba yake au mama yake. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Mheshimiwa Michael Constantino Mwakamo, atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Richard Sanga, kama muda wetu utaruhusu tutamalizia na Mheshimiwa Tunza Issa Malapo.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza, mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Utawala za Serikali za Mitaa, kwa hiyo, nitajielekeza kwenye taarifa ambayo Kamati yetu tumeifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijaanza kuchangia nichukue nafasi hii kuiomba Serikali hasa watumishi waliopo kwenye Wizara mbali mbali ambazo tumepata taarifa zao kwamba wachukue taarifa hizi na maazimio ambao yanapitishwa leo, yanapitishwa na vikao vya Bunge na kutoa ushauri unaofaa ili Serikali iweze kufikia malengo ya kuwahudiwa wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, mimi nitaanza na suala zima la Soko la Kariakoo. Masoko ya Kariakoo yalianzishwa kwa

historia yake mwaka 74, lakini walikuwa na soko moja tu wanaloshughulika nalo Soko la Kariakoo lililoanzishwa na sheria namba 36. Soko hili lilikuwa na wanahisa wawili kwa maana ya Jiji la Dar es Salaam lakini pia na Msajili wa Hazina kwa naiba ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa mujibu wa taarifa ambayo imewasilishwa Jiji la Dar es Salaam lilikuwa na hisa asilimia 51. Moja ya kazi kubwa ambayo walikuwa wamepewa Mashirika ya Soko la Kariakoo ni kuhakikisha wanalisimamia Soko la Kariakoo na kuyaendeleza masoko mengine ambayo watakabidhiwa nayo.

Mheshimiwa Spika, lakini sote tupo kama mashahidi, kwamba Shirika hili tangu wakati huo mpaka leo linalisimamia Soko la Kariakoo na hatujayaona masoko mengine ambayo yanaweza yakawa yalikabidhiwa kwao na yaweze kutoa tija kama ambavyo Soko la Kariakoo limetoa tija.

Mheshimiwa Spika, sasa kwenye Kamati tumeweka azimio, kwamba ni vizuri Serikali ikaangalia namna ya kubadilisha sheria hii badala ya hili shirika kuwa ni Shirika la Masoko ya Kariakoo ikiwezekana likaanzishwa Shirika la Masoko nchini. Ili tuwe na shirika moja kama ambavyo tulivyo na Shirika la Nyumba, ambalo linatoa huduma nzuri ya ujenzi na uendeshaji wa miradi hii katika nchi hii. Tutakapofanya hivi tutatumia shirika hilo kuyaendeleza masoko yote nchini ambayo yataweza kusaidia kupokea bidhaa za wakulima na kuweza kuwaongezea kipato chao.

Mheshimiwa Spika, leo hii nchi nzima tunafahamu, mkulima wa nyanya ya Iringa, mkulima wa mboga mboga kutoka maeneo yeyote, mkulima wa ndizi,

wanapakia mazao yao safari inaelekea Kariakoo. Kwa sababu wakulima wana matumaini kwamba kwa namna ya miundombinu yake ilivyo, wafanyabiashara wapo pale na wanaohitaji huduma zao watawakuta pale na wanaweza kufanya biashara za mazao yao vizuri. Kwa hiyo, endapo tutakuwa tumeanzisha kweli Shirika la Masoko nchini na likachukua jukumu la kuyaendeleza masoko nchini, tunawezekana tukawa na masoko yenye ubora na yenye kutoa tija kwenye kila kanda ikiwezekana.

Mheshimiwa Spika, na kutokana na nchi yetu ilivyokaa na Mungu alivyotujalia kila kanda ina aina yake ya mazao wanayovuna. Kwa hiyo inawezekana ikasaidia wateja wa aina fulani ya mazao wakasogea kwenye soko lililojengwa kwa ubora mzuri na linalosimamiwa kwa utaratibu mzuri, ambapo wakaenda kuchukua mazao yao na wananchi wale wakapata kipato chao kwa urahisi. Kwa kufanya hivyo, kuna hili genge ambalo ndugu yangu Saasisha amelielezea, la madalali, wanaweza wakakosa nguvu ya kumuonea mkulima kwa sababu mkulima anatumia dalali kuweza kumsafirishia mazao yake kutoka shambani mpaka sokoni, kumsimamia mauzo naye kumpatia pesa. Lakini masoko yakiwa yameenea na yana ubora maana yake wale wanunuzi ambao wanahitaji bidhaa hizo watafuata kwenye masoko ya jirani kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeshauri kwamba lile azimio la Kamati ambalo ni azimio la Bunge la kuomba Serikali kupitia na kuona namna bora ya kuanzisha Shirika la Masoko nchini lifanyiwe kazi kwa kina, kwa sababu linaweza likatuletea tija kubwa sana kwenye nchi. Kwa sababu tulipokuwa tunapitia taarifa ya masoko, Soko la Kariakoo kwa mwaka wanaingiza bilioni nne, kwa taarifa

ambayo wale waliwasilisha. Sasa tungekuwa na masoko mengi nchi ambapo kila soko limesimamiwa vizuri maana yake Pato la Taifa lingeongezeka. Kwa hiyo ni vizuri sana wataalam kwenye hizo Wizara wakatusaidia kuhakikisha wanaweza kusimamia hili azimio na likatekelezeka vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, tumeona kwa wachangiaji na kwenye taarifa; kuna suala hili linaitwa la madalali. Tumeona Serikali kupitia Wizara ya Kilimo inavyoamua kuhakikisha kwamba wakulima watengenezewe mazingira bora ya kuzalisha. Zoezi linalofanywa na Serikali leo la kuhangaika na usambazaji wa mbolea na upatikanaji wa mbegu bora. Kama tutakuwa na masoko yanayosimamiwa katika Shirika moja zuri, hizi kazi zingeweza zikaratibiwa vizuri na zikafanya vizuri kabisa na wakulima wangelima vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine, kuna chombo hapa kimetajwa hapa, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa. Chombo hiki nacho Kipo pale TAMISEMI. Ukiangalia historia inaonesha kimeanza kutoa huduma mwaka 1965, lakini imetoa mikopo kwenye halmashauri 57 tangu kianzishwe. Kati ya hizo halmashauri 57 halmashauri 12 mpaka leo zinadaiwa. Ukipitia ile taarifa, sisi tulikuwa kwenye Kamati, ukiangalia mikopo iliyokuwa inatolewa na hii bodi ya mikopo na ukiangalia jinsi pesa zile zilivyokuwa zinakopwa na halmashauri na jinsi zinavyotumika, hakuna tofauti kabisa na kilio tunacholia leo, kazi zinazofanywa na *SACCOS* mbali mbali zinazoshindwa kuendelea. Kwa sababu mtu ameanzisha halmashauri inakwenda kukopa kwenye bodi hii, anakopa pesa za kwenda kufanya ukarabati wa gari. Sasa, tija hii inapatikana wapi.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake wanashindwa kurejesha mikopo. Bodi inashindwa kujiendesha, bodi inashindwa kuwa na uwezo wa kuongeza vyanzo vingine kwa sababu wakopaji walipeleka pesa zile kwenye miradi ambayo haitoi tija. Sasa kwa sababu haitoi tij maana yake fedha zimeshindwa kurudi.

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia bodi hii chanzo chake cha mikopo eti ilikuwa ni michango ya halmashauri husika. Sasa hebu tuangalie halmashauri zimechangia nyingi lakini zilizokopeshwa mpaka leo ni halmashauri 57. Hivi yule ambaye tangu ianze hii bodi mwaka 65 hajawahi kukopeshwa anachangiaga tu, hiyo nguvu ya kuchangia anaitoa wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi ningeshauri kwamba Serikali ione namna bora ya kukisimamia hiki chombo na ikiwezekana ikiongezee vyanzo vya mapato. Pia, kuna kazi tunahangaika nayo sasa hivi ya asilimia 10 ya mikopo. Wabunge Wengi wanalia kwamba ile idara iliyopewa kukopesha inapata tabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumbe TAMISEMI tuna chombo kinaitwa Bodi ya Mikopo, kwa nini tusijifunze, tukakiongezea nguvu hiki, ikasimamia mikopo yote ikiwezekana na hiyo ili iweze kwenda kwa tija kwenye maeneo yanayostahili, ili ikakusanywa zile fedha ikaonekana tija yake?

Mheshimiwa Spika, lakini…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO**: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda umekwisha naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Richard Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja za Kamati zilizopo mezani kwetu. Ninataka kuchangia mambo mawili. Jambo la kwanza ni kuhusu Mradi wa *SEQUIP* na jambo la pili ni Wizara ya Michezo.

Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru kwa ujenzi wa shule za kata ambao umefanywa na Mheshimiwa Rais, karibu kata zote nchini. Kwa kweli sisi kama Wabunge huko majimboni tumepata kitu kikubwa cha kukisema na wananchi ambao walikuwa hawana matumaini kabisa ya kuwa na shule lakini sasa wana shule kupitia huu Mradi wa *SEQUIP,* na sehemu kubwa hii miradi ya shule Mheshimiwa Rais ametoa fedha na wananchi wametoa nguvu kazi kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, lakini, hoja yangu ni nini ambayo napenda kuishauri Serikali; kwenye hii miradi ya *SEQUIP* ambayo imelenga kwenye kila kata, ukizingumzia kila kata, si kata zote zinahitaji hiyo shule moja. Kuna kata zingine kwenye miji kwenye majiji zinahitaji zaidi ya shule mbili. Sasa tuone haja ya Serikali kuongeza kwenye kata mbali mbali kwa sababu idadi ya wanafunzi imekuwa ni wengi kwenye kata mbali mbali. Kwa hiyo tungeweza kuongeza idadi ya shule kwenye kata hizo ili iweze kuendana na wingi wa wanafunzi ulipo pale.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, kwa sisi kwenye Kamati yetu tumezungukia tumeona kwamba kumekuwa na

*variation* kubwa sana ya ujenzi wa shule hizi. Ukienda kwenye halmashauri mbali mbali kuna halmashauri ambazo zina upungufu wa zaidi ya milioni 51 ili kukaimisha ujenzi wa shule hii, lakini kuna halmashauri zingine zimefika hadi milioni 150 zinahangaika kutafuta hizo fedha ili zikamilishe ujenzi wa shule hii. Hii inatokana na umbali wa shule zilizopo pamoja na upandaji wa gharama za vifaa kwenye ujenzi wa shule hizi. Sasa Serikali ione *concern*, shule ambayo ipo Namanyere haiwezi kuwa sawa sawa na shule ambayo iliyoko Dar es Salaam kwenye gharama za ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni vyema Serikali ikaona namna gani ya kuweza kuziunga, kuzi-*support* au kuziongezea nguvu kuliko kuwaachia Wakurugenzi na halmashauri waendelee kuhangaika na ujenzi wa shule hizi ili ziweze kukamilika. Milioni 470 tu haiwezi kutosha, hata mimi kule Makete bado na changamoto ya fedha nyingi ambazo nazihitaji kwa ajili ya ujenzi wa shule hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ni kwenye suala la Wizara ya Michezo. Nimesikiliza hoja ya Kamati. Kwenye suala la Wizara ya Michezo, mimi kama Mbunge nina hoja ambazo zinazungumzia kwenye suala la ujenzi wa shule zile za michezo lakini pia kwenye suala la viwanja nchini. Kamati imeshauri kwamba Wizara ione utaratibu wa kufanya *partnership* na sekta binafsi. Mimi ninauliza, leo tunaenda karibu robo ya tatu ya utekelezaji wa bajeti, lakini hadi dakika hii ninanvyozungumza kwenye ujenzi wa viwanja nchini hakuna chochote ambacho tumeanza kukifanya. Watanzania wana swali kubwa sana huko nje, tumekuwa tukipigia kelele kuhusu ubora wa viwanja vya Taifa letu, na Serikali ilikuja hapa ikatuahidi kwamba kutokana na bajeti ya bilioni 10

kwenye viwanja saba ambavyo tumeitengea itaanza mchakato wa ujenzi wa viwanja.

Mheshimiwa Spika, mimi niiambie Serikali, suala la michezo nchini limekuwa ni suala ambalo linaleta fedha nyingi kwenye Pato letu la Taifa. Kwa mwaka 2020/2021 Serikali imeingiza zaidi ya bilioni tatu kupitia mapato ya magetini kwenye mpira wa miguu. Vilevile, Azam (Bakhresa) amewekeza zaidi ya bilioni 225 kwenye kudhamini ligi kuu, na analipa zaidi ya bilioni 34 *VAT*. Hivi ninavyozungumza, jitihada za Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara husika tunaziona, lakini je wamepata fedha zozote za kuanza mchakato huu? Tuliahidiwa kwamba watajenga shule 56 za michezo nchini lakini hadi ninavyozungumza sasa hivi hakuna hata shule moja iliyoanza kujengwa. Uzuri Waziri wa Fedha mwenyewe ni mdau wa michezo nchini. Je, ni kipi kinaichokwamisha Serikali kutoa fedha ili viwanja wa michezo vianze kuboreshwa?

Mheshimiwa Spika, ninavyozungumza sahizi, Azam ambaye anafanya *production* ya mpira kwenye Taifa letu, uwekaji wa taa kama uwanja wa Jamhuri Dodoma zile taa zimewekwa kwa *dola* laki tatu, zaidi ya milioni 700. Serikali inashindwaje kumuunga mkono kwa kuweka angalau uwanja ambao unaweza kuchezeka mpira? Anapambana kuweka mazingira mazuri ya soka kama mwekezaji lakini sisi kama Serikali bado tumekuwa tukimkwamisha kwenye suala la kuboresha miundombinu.

Mheshimiwa Spika, niiombe Wizara ya Fedha, Wizara ya Michezo inafanya kazi nzuri sana, ipatieni fedha idara hii ili iweze kuboresha viwanja nchini. Watanzania wanapenda michezo, Watanzania wanapenda soka, lakini kumekuwa na changamoto ya kuboresha

miundombinu. Leo ninavyozungumza tuna zaidi ya viwanja sita ambavyo vimefungiwa na *TFF* mpira usiendee kuchezwa kwa sababu ya ubovu wa viwanja hivyo.

Mheshimiwa Spika, na hii imekuwa ikisababisha gharama kwenye timu kuhamia kwenda eneo lingine kuwaleta wachezaji, kusafirisha timu kwa sababu ya ubovu wa viwanja vya michezo. Nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Waziri wa Fedha kama mdau wa michezo, ona umuhimu wa kuisaidia Wizara ya Michezo ili iweze kuboresha miundombinu ya viwanja vyao. Mlituahidi kwamba tutajenga uwanja Dodoma, na hapa ndiyo Makao Makuu ya nchi na Watanzania wanajua kwamba mlituahidi mtajenga uwanja lakini hadi sahizi Wizara ya Michezo haijaanza kujenga; ukifuatilia hawana fedha ambayo wamepata kutoka Serikalini *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pili, hizi shule saba ambazo mlisema angalau mtaanza nazo hakuna shule hata moja ambayo imeanzwa kujengwa. Kwa hiyo, niishauri Wizara ya Fedha, ni vyema mkatoa fedha angalau kuweza kui -*support* Wizara ya Michezo ili angalau Watanzania waone mwanga kwenye kuboresha viwanja vyetu nchini.

Mheshimiwa Spika, mimi baada ya kusema hayo, sina mambo mengine ya ziada lakini ilikuwa ni hoja yangu ya msingi, kwamba kilio cha viwanja nchini kimekua ni kukubwa na ni vyema Serikali ikachukua hatua ili kuunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais lakini pili kumuunga Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Michezo ambaye amekuwa akifanya kazi nzuri sana katika kuhamasisha michezo nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, dakika tano.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mwalimu na nimefundisha darasani kwa muda wa miaka isiyopungua tisa, kwa hiyo haya ninayotaka kuyaongea leo kwa uchache nayaongea kwa uzoefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namba moja, hakuna mtoto ambaye hafundishiki akifundishwa. Kinachotokea kwa hawa watoto wetu hawa tunaona wanafeli masomo, wanafeli kwa sababu hawafundishwi. Kwa nini hawafundishwi? Kwa sababu hakuna waalimu wa kuwafundisha. Nina maana ipi, ametoa *data* nzuri sana Mheshimiwa Husna mimi siwezi kuzirudia kwa sababu ya muda. Mtoto anaanza *form one,* mwalimu wa hesabu hayupo, mwalimu wa *physics* hayupo, mwalimu wa *chemistry* hayupo, mwalimu wa *biology* hayupo. Akifika *form two* tunamtaka mtoto huyo afanye, mtihani wa *form two* ambao unahusisha hayo masomo yote unajumlisha hayo masomo yote ambayo hajafundishwa tunamtaka afanye mtihani na afaulu. Hakuna kitu kama hicho *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa watoto tunaowaona wa shule zingine wanafaulu vizuri hakuna muujiza wowote, ni kwa sababu wanafundishwa. Hiyo ndiyo hoja yangu ya msingi leo. Sasa sisi kama Taifa tujiulize, kwamba kipaumbele chetu ni nini? Kama elimu hatuitilii mkazo kwa

namna hiyo, kila siku matamko mbalimbali ambayo hayatekelezeki tunafikiri yatatufikisha mahali? Kwangu mimi kama mwalimu nasema hayo matamko yanayotolewa na viongozi wa kisiasa kila siku bila utekelezaji hayatufikishi mahali kokote. Kwa taarifa, naongea kwa uzoefu, *issue* ya kufundisha haianzii darasani pale pale kwenda kusimama kushika chaki kufundisha. *Issue* ya kufundisha inaanzia mbali.

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kinaitwa *scheme of work,* kuna *lesson plan.* Mimi natakiwa nisome ile *content,* nisome ile mada ninayokwenda kufundisha nielewe, niingie darasani ndipo nifundishe. Sasa unapewa darasa ukafundishe lina wanafunzi 1,000. Hivi ninyi mnawajua watu 1,000? Wakikaa hapa yaani ukaambiwa watu 1,000 sisi humu ndani tuko 400 kasoro humu watu wote sisi. Sasa ndiyo umepewa darasa la watu 1,000 ukafundishe wewe mmoja na nimewaambia kufundisha hakuishii pale darasani kusimama kama kweli unataka wanafunzi wafaulu. Una watu hawa 1,000 ufundishe, ukimaliza kufundisha haki *bin* haki inapaswa uwasimamie je, wameelewa? Wameelewa, umewapa zoezi wamefanya. Ili ujue wameelewa ni lazima nisahihishe. Lazima nisahihishe na hakuna somo linalotaka kusahihisha kama somo la hesabu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kama hausahihishi unajuaje kama watoto wako wameelewa? Nitasahihishajke mimi wanafunzi 1,000 mimi siwezi wala wewe Mheshimiwa Spika huwezi wala mwingine hawezi? Huo ndiyo uhalisia. Watoto 1,000 leo niingie nisahihishe madaftari 1,000 kesho niingie nisahihishe madaftari 1,000. Mimi Tunza Issa Malapo siwezi wala mtu mwingine hawezi.

Kwa hiyo tusikae tukatafuta mchawi, kaangalieni matokeo ya *form four,* kuna shule ipo inaitwa Taifa, wanafunzi 1,032. *Form four,* yaani darasa moja, *management* inakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nachotaka kushauri, tunakaa hapa tunasema madarasa mengi yamejengwa, ndiyo yamejengwa lakini hayatoshi kwa sababu kila siku *population* inaongezeka. *Population* ya mwaka jana si ya mwaka huu. Kwa hiyo jitihada za makusudi bado zinahitajika kuwekeza katika elimu kuanzia kwenye miundombinu, waalimu na hawa waalimu hawa; unajua katika maisha hamna kitu kibaya kama kufanya kazi wakati una *stress,* asikudanganye mtu. Yaani wewe unatamani wanafunzi wako waelewe, ukiingia darasani unakutana na wanafunzi 1,000 unafundisha unajiona kabisa mimi hapa sijaeleweka, inaumiza sana kama mwalimu mwenye wito kama nilivyo mimi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine nalotaka kusema kuhusu mgogoro wa ardhi wa hapa Dodoma. Mgogoro huu ni mkubwa sana, wananchi wanalalamika, wamedhulumiwa. Sisi kama Bunge, kama Kamati tumetoa ushauri. Ukisoma kwenye maoni yetu tumeeleza. Tunaomba Serikali ifanyie kazi kwa usimamizi wetu sisi Bunge kwa sababu Bunge kazi yetu ni kuisimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Tunza hebu tusaidie, unavyosema darasa moja watu 1,000 unamaanisha, kidato kimoja wako 1,000 au wanakaa kwenye darasa watoto 1,000?

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, namaanisha kidato, siyo mkondo. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Haya. Sawa sasa hapo tumeelewana vizuri maana umesema ukienda darasani unakutana na watoto 1,000 nikawa nawaza pengine ni kama ile midahalo na mimi sitaki kuingia huko na mimi ni mwalimu lakini wa ngazi nyingine. Kwa hiyo sisi kwa kule kwetu watu 1,000 wanaweza kuwa sehemu moja na wakafundishwa lakini wale wa ngazi hizi za chini, nilitaka nielewe hilo maana tunaelekea baadae kutoa, tutakuwa na maazimio hapa sasa kama kuna darasa moja wanakaa 1,000 hilo ni suala lingine. Sasa tumeelewana.

Hoja ya Mheshimiwa Tunza ni kwamba wanakuwepo 1,000 yaani kwa maana ukisema kidato cha nne 1,000 si kwamba wote wanakaa darasa moja, wanakaa madarasa tofauti na kwa hivyo wanafundishwa kwa muda tofauti isipokuwa mwalimu anaweza akawa mmoja anayeenda kuhudumia hao watoto. Nadhani hapo tumeelewana vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo mawili hapa, tangazo la kwanza. Mnatangaziwa na Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwamba wale mabinti zetu hapa; sasa hapa wameandika vijana, pale walisema mabinti; haya, chochote. Sasa hao vijana wale tuliowatangaza hapa kwamba walishika nafasi ya pili katika yale mashindano waliyoenda kushindana katika masuala ambayo yanahusu TEHAMA, wapo na wamekuja hapa Bungeni lakini pia wanao utayari wa kuonesha ni kitu gani ambacho kiliwafanya washike hiyo nafasi ya pili. Kwa hiyo watakuwa pale nje, upande ule wa Zahanati ya Bunge

ya zamani, yaani mbele ya jengo la Msekwa kule nyuma; kwa hiyo, unaweza kwenda kutazama hawa vijana wetu kitu ambacho walikuwa wamekifanya.

Waheshimiwa Wabunge, pia kwenye tangazo ilionekana kama yale mashindano yamefanyika hapa nchini, lakini kwenye tangazo hili inaonekana walishinda nchini Uswisi. Kwa hiyo walienda huko nchini Uswisi wakatuwakilisha vizuri na wakashika nafasi ya pili, kwa sababu yalikuwa ni mashindano ya dunia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na michango na muda wetu umekwenda, baadaye pengine nitatoa ufafanuzi kidogo kuhusu hoja hii ya madalali ili tusiizungumze kwa ujumla kwa sababu madalali wanahitajika na wanafanya kazi zao kisheria katika maeneo mbalimbali. Hili eneo la kilimo kama kuna changamoto basi tushughulike nalo hilo; lakini tukisema madalali hawatakuwepo, madalali wanafanya kazi zao kisheria na katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo nitatoa ufafanuzi baadae ili tusije tukatuma ujumbe kana kwamba wale waliojiajiri kwenye hili eneo la udalali basi wanafanya jambo fulani hivi ambalo halikubaliki kwenye jamii kwa ujumla wao.

Waheshimiwa Wabunge, nilete kwenu baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambao tutaanza nao kuchangia mchana. Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mheshimiwa Constatine John Kanyasu, Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mheshimiwa Tecla Mohamed Ungele na Mheshimiwa Joseph George Kakunda, na wengine tutaendelea kuwataja huo mchana kadiri muda utakavyokuwa unakwenda.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa 11.00 jioni leo.

*(Saa 7.03 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11:00 Jioni).*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022

**na**

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022

**SPIKA:** Tunaendelea na majadiliano. Tutaanza na Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu ajiandae.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi, nashukuru pia kwa kuwa mchangiaji wa mwanzo jioni hii.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mjumbe kutoka Kamati ya USEMI, sehemu kubwa ya taarifa uliyoiona maana yake hata mimi mawazo yangu yako hapo. Nitakwenda kwenye maeneo machache kwa msisitizo.

Mheshimiwa Spika, eneo la *TARURA* kama tulivyoongea kwenye Kamati. Wenzetu wa *TARURA* kwa kweli wanafanya kazi kubwa na niseme kipindi hiki ambapo tuko kwenye majira ya mvua ukienda katika maeneo mbalimbali nchini barabara zimekatika. Kwa hiyo suala zima la Mfuko wa *TARURA* katika eneo la dharura, tukizungumzia kuongeza fedha ni kwa maana hiyo. Eneo la *TARURA* upande wa dharura.

Mheshimiwa Spika, kila sehemu, ukienda Katavi, huko kote mvua zinakonyesha hata maeneo mengine ambapo hakuna mvua. Kwa hiyo eneo la kuongeza fedha nilikuwa naomba sana.

Mheshimiwa Spika, eneo la *TARURA* pia nilikuwa naomba kuna baadhi ya maeneo kuna miradi mingine kwa kupitia *TASAF* unaweza ukakuta wananchi kwa maana ya kujipatia kipato wameelekezwa kwenye utengenezaji wa barabara. Wengine wamefikia hatua ya kuchimba mitaro. *Point* yangu ni nini? Ikiwa kazi nzuri imefanywa na wananchi kwa kupitia vyanzo vingine kama *TASAF*, au Mfuko wa Jimbo, kazi hii nzuri isipounganishwa na kazi za *TARURA* hautoiona thamani yake. Fedha nyingi inaweza ikapotea katika eneo hilo, lakini inapendeza barabara nzuri ikifunguliwa, mitaro ikichimbwa, basi na wenzetu wa *TARURA* wazipokee kazi hizo ili kuwe na uendelevu wa shughuli.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoke hapo. Eneo la pili ni kuhusu TAKUKURU rafiki. Nishukuru tumepitia kwa kupitia Kamati na tukaona mpango huu ni mwema, ni mpango mzuri, suala zima la TAKUKURU rafiki. Kwa maana siku zote tunaambiwa kama hujafanya utafiti hauna vielelezo usiongee. Wenzetu wa TAKUKURU rafiki wanatuambia 81.5% inazungumza kwamba rushwa ni tatizo nchini, lakini

92% wako tayari kwa mapambano dhidi ya rushwa na kuwapa ushirikiano Maafisa wa TAKUKURU. *Point* yangu ni nini? Mwelekeo wa dunia kwa sasa hivi au ulimwengu ni kuzuia rushwa kabla haijatokea na kwa kupitia TAKUKURU rafiki pia nao wamejikita huko kwa maana ya kuzuia zaidi.

Mheshimiwa Spika, wenzetu hawa kwa kupitia TAKUKURU rafiki na nimeeleza hivyo kwamba 92% wako tayari kutoa ushirikiano, lakini wenzetu wa TAKUKURU peke yao hawawezi, ni wachache, peke yao hawawezi, lazima wapewe ushirikiano. Niseme hivi, tutaishia kuwalaumu watu hawa, yaani mtu kama ni katika halmashauri, jiji au manispaa, usitimize wajibu wako, umemsainisha mtu ameingia kwenye kazi, mkataba haueleweki, baada ya hapo mtu huyo kapotea, amepotea kwa uzembe wa wewe kutomshirikisha kwenye mikataba, ikifika hapo unasema TAKUKURU njooni wakati wajibu wa kwanza ulikuwa ni wa kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninachotaka kusema nje ya hapo tutabebesha watu lawama, lakini naomba turudi, ndiyo maana suala zima la TAKUKURU Rafiki inatuelekeza kwenye uwajibikaji wa pamoja. Mbali na uwajibikaji wa pamoja, juzi nilikutana na familia moja nikaambiwa na mzazi wake, ananiambia mwanangu hata ukimpa fedha kiasi gani, ni mtoto mdogo, ukimpa fedha sana sana ataileta kwa mama yake. Hakuna mahali atatumia atafanyaje. Nataka kujifunza nini? Yaani mtoto mdogo akiwa na umri mdogo anaanza kujengewa maadili, hili ndilo, hili hapana, hili ndilo, hili hapana. Kwa hiyo kwake yaani fedha, yule mtoto mdogo amefika mahali ambapo hata kama atakwenda kwa makuzi hayo, anajua hiki kinanihusu, hiki hakinihusu. Nikisema hivyo nataka kumaanisha nini pia?

Mheshimiwa Spika, bado ukiacha uwepo wa vyombo hivi, na vyombo hivi kwa utamaduni vina asili ya mabavu kidogo, lakini tutoke nje ya mabavu. Kila mmoja hapa ana dini yake, wapo Wakatoliki, wapo Waislam na wengine hawana dini, lakini bado siku zote, kwa mfano mimi ni Mkatoliki, ukienda kwenye amri pale kuna sehemu unaambiwa usiibe, usiseme uongo na vitu vingine vya namna hiyo. Kwa hiyo kwenye maadili yetu ya dini yatuelekeze kwenye kusema hili hapana.

Mheshimiwa Spika, nimesikia kengele ya kwanza hiyo. Kwa hiyo ninachotaka kusema, ushirikishwaji wa pamoja wenzetu peke yao pamoja na nia yao njema bila watu kuwasaidia, hawatoweza.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya ajira. Niwashukuru sana watu wa sekretarieti ya ajira na hasa kwa sababu kulikuwa na maombi, vijana wanasafiri umbali mrefu kwenda kufanya usaili, leo sekretarieti ya ajira kwa kupitia Mheshimiwa Jenista pale wamesikiliza kilio cha Wabunge. Sasa hivi usaili umepelekwa kwenye kanda na mimi niseme hili ni jambo jema. Wakati ule ilikuwa watu wanasafiri, atoke Katavi, atoke Mwanza, atoke wapi labda kuja Dodoma au Dar es Salaam. Wazazi vipato vidogo, lakini nitoke hapo.

Mheshimiwa Spika, tumekwenda kwenye kitu kingine ambacho nacho naomba kiendelee kufanyiwa kazi. Habari ya kupata ajira kwa kigezo cha kwamba umepitia JKT niombe, Kamati imeelekeza kwa sababu nafasi za JKT hazitoki kwa kila huyo. Ukituacha sisi, mimi ni namba Z2639 *OP* Kambarage ya kutoka tarehe 15 Juni, 1990 mpaka 14 Juni, 1991. Sasa sisi wa miaka hiyo ilikuwa ukisema mtu awe na sifa ya kupita JKT ni kwa sababu ilikuwa tunapita kwa mujibu wa sheria. Sasa hivi nafasi ni chache, ukija na

kigezo kwamba mtoto lazima apite JKT wakati hakupewa nafasi ya kwenda JKT, tunawanyima nafasi. Kwa hiyo naomba kigezo cha kwamba lazima mtu apite JKT vinginevyo tutimize wajibu wetu kwa kuhakikisha wote tunawapeleka JKT halafu tuwahukumu baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuheshimu muda, naomba kuishia hapo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, atafuatiwa na Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli na Mheshimiwa Teclas Mohamedi Ungele ajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba kuwapongeza Wenyeviti wote wa Kamati zote mbili ambao wamewasilisha leo kwa taarifa zao nzuri. Pia kipekee niwapongeze Wajumbe wa Kamati hizo.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Utawala ya TAMISEMI na katika Kamati yetu tulipata bahati ya kuzikutanisha Kamati mbili. Kamati yetu ya Utawala ya TAMISEMI pamoja na Kamati ya Ardhi na tulikutanisha Kamati zote mbili baada ya karibu kila halmashauri tuliyokwenda kwenye ziara, tulikuta kuna migogoro mikubwa sana ya ardhi. Tulifanya kikao cha pamoja, lakini mwisho tulikuja na maazimio ambayo Mheshimiwa Mwenyekiti ameyazungumza kwenye hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kuzungumza kidogo kuhusu migogoro ya ardhi katika Jiji la Dodoma. Wananchi wa Jiji la Dodoma wanateseka sana na

migogoro ambayo ilitengenezwa. Tunayo maeneo ambayo yalipimwa awali kama mashamba ya mjini. Waliopimiwa wakatoweka, baada ya miaka 30 Dodoma imetangazwa kuwa jiji, wakarudi lakini maeneo hayo yaliyopimwa kama mashamba Serikali haikuyafanya kuwa mashamba yakageuka yakawa vijiji. Dodoma ilipokuwa Makao Makuu likaibuka wimbi la kupima maeneo kupata viwanja. Dodoma wakaenda kupima maeneo kwenye hivyo, kupata viwanja, matokeo yake wanasema hayo maeneo ni mali yao kwa sababu walishayapima wakati wenyeji wa maeneo hayo walikuwa bado hawajalipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, haikuwa imefanyika *land acquisition* kabla ya kutengeneza hizo *broad acres* au hizo *town farms* ni mashamba ambayo ya mjini kuwapa hawa watu na hawa watu walitoweka hawakuyaendeleza. Wenye mashamba yao wananchi wenyeji wa pale wakaendelea kuishi kwenye maeneo hayo. Wamekuja wamepima wanasema haya maeneo sasa ni ya jiji.

Mheshimiwa Spika, ninao mfano mmoja, mwananchi mmoja alikuja anaitwa Daudi Samamba kwenye stendi hii ya kuelekea Bahi. Kushoto kwake kuna *go down* ya Banj, kulia kwake kuna stendi wamepima jiji. Yeye amebaki katikati ana heka 15, wamekwenda wamepima pale wamemnyang'anya wanasema haya maeneo ni ya jiji, lakini wote wa kushoto na kulia ambao tayari wamekwishabinafsisha, wamebinafsisha kwa kuuziwa na huyo huyo kama mwenyeji. Matokeo yake huyu mtu amekwenda kwa Mkuu wa Wilaya, amekwenda kwa Mkuu wa Mkoa, amekwenda kwa Kamishna. Kamishna ameelekeza kwamba wamtafutie eneo lingine mbadala.

Mheshimiwa Spika, huyu mwananchi akapelekwa Kikombo karibu kilometa 60 kutoka hapa mjini. Kule anaenda kuambiwa alipie tena ardhi kama mnunuzi mpya. Umemnyang'anya mwananchi kutoka kwenye *prime area,* hukumpa fidia heka 15, unampeleka kumpa viwanja vitano ambavyo havifiki heka moja halafu una mwambia anunue ardhi. Huu ni udhulumaji, huu ni wizi na huu ni uonevu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Kamati yetu imekuja na mapendekezo kwamba, hauwezi ukalitengeneza tatizo halafu ukaachwa pale pale kutafuta suluhu ya tatizo hilo. Maafisa waliohusika kwenye kutengeneza tatizo la migogoro mikubwa ya ardhi katika Jiji la Dodoma, bado wapo na ndiyo bado wanawasikiliza walalamikaji. Wizara ichukue hatua, hawa watu wawekwe pembeni, watafutwe watu ambao kutoka sehemu nyingine ambao hawana *interest,* waweze kuwasaidia hawa wananchi wa Dodoma ambao wanateseka wengi kwa sababu watu wanaoshughulika ni wale wale ambao wametengeneza tatizo hilo. Wananchi wapo na nadhani jambo hili linaeleweka vizuri kwenye Kamati.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, tulikuwa na Kamati ya Mawaziri Nane. Walikuja Geita Mjini lakini mchakato unaujua vizuri. Tulianza kwa kutengeneza mchakato wa Wabunge kuleta maoni, Viongozi wa Wilaya kuleta maoni. Kwa hiyo yako maeneo ambayo sisi kama Wabunge na wawakilishi tuliamini kwamba haya yamekuwa sababu ya mgogoro wa kila siku. Wamesema baadhi ya Wabunge hapa kwamba watu wanakamatwa sana na Maaskari wa Maliasili na Maaskari wa Misitu. Nikisema maeneo haya tayari yamekwishakuwa sehemu ya makazi. Pale Geita Mjini tuna msitu wa Osindakwe.

Msitu wa Osindakwe umepoteza sifa ya msitu kwa sababu tayari kuna watu wanakaa mle ndani.

Mheshimiwa Spika, tulipendekeza msitu ule urudishwe kwa wananchi kama yalivyo maeneo mengine hasa kwenye taarifa ambayo Mheshimiwa Rais ameidhinisha, eneo lile linazuiliwa kwamba ni chanzo cha maji. Hakuna kisima, hakuna bwawa, hakuna mto, hakuna chochote. Kwa hiyo kila siku wananchi wanakamatwa pale na kutozwa faini na kunyanyaswa kwamba kuna chanzo cha maji wakati ni katikati ya mji na hakuna kitu chochote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ombi langu hapa, kuna migogoro mingine tunaitengeneza wenyewe. Tunaleta manung'uniko bila sababu za msingi kwa sababu watendaji wengi wanalazimisha kushikilia maeneo ambayo tayari walishindwa kuyazuia yakapoteza sifa.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, Kamati yetu ilizungumza na Wizara ya TAMISEMI. TAMISEMI wanaisimamia *TARURA*. Tunaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha kutoka shilingi bilioni 200 kwenda karibu shilingi bilioni 800. Bado kuna tatizo kubwa sana la barabara. Pale Geita mjini tunao mradi wa *TACTIC*. Tumeuzungumza sasa takribani mwaka wa tatu, wa nne. Kuwepo kwa mradi huu kunasababisha hata kwenye mgao wa fedha zingine za maendeleo, inapofika habari ya Geita Mjini unaambiwa kwamba ninyi mna barabara ya *TACTIC,* lakini mradi hauanzi, mradi haukamiliki. Nilianza kuuzungumza mimi wakati wa awamu ya kwanza ya ubunge wangu, sasa nakwenda awamu ya pili ya ubunge wangu, mwaka uko katikati.

Mheshimiwa Spika, ombi langu, jambo hili kama lipo, yafanyike maamuzi ya mradi huu uweze kuanza haraka ni pamoja na ujenzi wa Stendi ya Geita Mjini iko ndani ya mradi huu. Fedha tuliambiwa zipo, wamekwishakuja watu wa upembuzi yakinifu kutembea zaidi ya mara 10. Sasa mwisho unajiuliza, kama gharama hizi za kulipa posho watu njoo rudi, njoo rudi ni sehemu ya *package* hii, si mwisho itafika nusu wamelipana wao kwa ajili ya kuja kukagua eneo? Kwa sababu umeshakuja zaidi ya mara 10, kila siku unakuja unaenda, unakuja unaenda, mradi hauanzi.

Mheshimiwa Spika, ombi langu, mradi huu kama upo, uanze na kama haupo ijulikane kwamba huu mradi haupo. Hakuna kitu kinatesa wananchi kama unaambiwa mradi huu utaanza kesho halafu unachukua tena mwaka mwingine mradi haujaanza.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kusema ni jambo la ajira. Tunaishukuru sana Wizara ya Utumishi, Ofisi ya Rais, imerahisisha zoezi la *interview*. Tumepeleka kwenye kanda, lakini hoja yangu iko pale pale, kama tumeweza kupeleka kwenye kanda, zamani tulikuwa tunasafirisha watu kwenda mpaka labda Dodoma kutoka nchi nzima, tulizungumza hapa tukasema tuna watu wengi ambao wanatafuta kazi wenye sifa, shida imekuwa ni nafasi. Ile *database* ambayo imetengenezwa na Wizara ya watumishi ambao wamekwishafanya *interview* wasilazimike watu kufanya *interview* zaidi ya mara mbili au mara tatu.

Mheshimiwa Spika, tunaona, *PCCB* wanatangaza nafasi miezi mitatu, miezi mingine mitano wanatangaza tena, wanaoomba ni 8,000. Wanaochukuliwa ni 200, maana yake ni nini, wanao-*qualify* wapo zaidi ya 1,000.

Hatuna sababu ya kuendelea kila siku tunatangaza jambo lile llile kwa sababu tunaingizia watu gharama, hasara halafu unakuta mtu anafanya *interview* moja mara 20, maswali yale yale na wanakwambia ni *very simple questions.* Mtu anaulizwa maswali yale yale lakini hafaulu mtihani anafanya mara 10. Sasa tutengeneze hii kanzidata, mtu akifanya mtihani, aki-*qualify* pawe na *cut off point* ikitokea mahali kuna nafasi zimetangazwa na zipo, waitwe walio-*qualify* hata kama mwanzo walikuwa wameitwa watu 100, sasa zimepatikana 200, waulizwe je, bado una-*interest* na kazi hii? Kuliko kila tunapokuwa na ajira tunatangaza upya, tunaita watu wapya, tunaita *new brains* kutoka shuleni, watu wamekaa mtaani wana miaka minne, wamefanya mtihani mara 10, wakienda kupambana na vijana kutoka chuo kikuu juzi wanashindwa, watu wanazeeka na vyeti ndani.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, atafuatiwa na Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele, Mheshimiwa Joseph George Kakunda ajiandae.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia. Naomba nianze kuchangia kwenye Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba mwaka jana Serikali iliongeza bajeti ya *TARURA,* lakini bado kuna matatizo makubwa ya barabara. Katika Mkoa wa Dar es Salaam, kama kila siku tunavyoongea Wabunge wa Dar es Salaam, wakazi wa Dar es Salaam wanatumia sana barabara kwa sababu Mkoa wa Dar es Salaam ni mkoa wa kibiashara na watu wengi wanapofanya biashara

wanatumia barabara. Kwa hiyo kwa mpango ambao unaenda nao *TARURA*, *TARURA* ni kila mara bajeti yao haitoshi na kwa sasa hivi kwa huu mpango wa kugawana fedha kwamba mfano, Mkoa wa Dar es Salaam ugawane na mkoa mwingine tuseme kama vile labda Mkoa wa Kigoma au mikoa mingine ambayo haina watu wengi.

Mheshimiwa Spika, sisi watu wa Dar es Salaam bado tunahitaji sana barabara kwa sababu wananchi wetu kazi zao nyingi zinatumia barabara na zinatokana na barabara.

Mheshimiwa Spika, ninaongea kuhusiana na barabara za Mkoa wa Dar es Salaam *specially* Jimbo la Segerea, bado tunahitaji barabara. Nasi watu wa Dar es Salaam hatuhitaji tena barabara za changarawe. Kwa hiyo, katika Mkoa wa Dar es Salaam, barabara hizi za *TARURA* tunaomba tuongezewe bajeti ili wafanyabiashara wetu waweze kufanya kazi vizuri na mapato yaweze kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalopenda kuongelea ni kuhusiana na mradi wa *DMDP*. Mradi wa *DMDP Phase II* mpaka sasa hivi ninavyoongea haujamalizika. Bado kuna sehemu nyingi sana zina matatizo. Mfano, Stendi ya Kinyerezi. Stendi hii imejengwa, ni nzuri, lakini haina sehemu ya kupumzikia, haina sehemu ya kusimama, yaani bado haijamalizika, na hii iko kwenye *phase II.* Mpaka sasa hivi mradi wa *DMDP Phase II* haujamalizika na hii inaifanya mpaka hii *DMDP Phase III* ambayo ametoka kuiongelea hapa Mbunge aliyemaliza kwamba itaanza, tuliambiwa kwamba wanaanza mwaka 2022 mwezi wa Tatu, lakini mpaka leo

hizi barabara hazijaanza; ilikuwa pamoja na Bonde la Msimbazi, halijaanza.

Mheshimiwa Spika, kama alivyoongea hapa mwenzangu kwamba tunavyoenda kuwatangazia wananchi kwamba kuna miradi ambayo inategemea kuanza kwenye makazi yao halafu mradi hauanzi mpaka mwaka mmoja unapita, ni shida sana kwetu Wabunge kwenda kujielezea kwa nini huu mradi umesimama mpaka sasa hivi. Mpaka sasa hivi hatujui huu mradi utaanza lini? Tulikuwa tunaomba Mheshimiwa Waziri akija kujibu, basi atuambie huu mradi wa *DMDP* utaanza lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine ninachotaka kuongelea; hili ninalotaka kulisema, siyo kwamba siungi mkono wafanyabiashara kuondolewa barabarani. Ninachokipinga mimi, tumesema sawa wafanyabiashara wanaondolewa barabarani, mfano Kariakoo na sehemu nyingine ambazo kuna watu wengi. Siku hizi kumekuwa na tabia, mtu anatoka jijini ndani kabisa huko mjini, anakuja sehemu kama Bonyokwa, anamkuta mama wa watu anajiuzia nyanya; anavunja lile banda la kuuzia nyanya, anachukua na zile nyanya. Anasema ni kwa sababu yule mama amekaa barabarani. Hiki siyo kitu kizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaunga mkono kwa maeneo ya nje, hao waliokaa barabarani kuondolewa ni sawa, kwa sababu ni pamoja na usalama wao; lakini hawa ambao wapo kwenye mitaa; mtu anakuja kumvunjia au kumwondolea mtu biashara yake sehemu ambayo hata Manispaa haijajenga barabara, hakuna kitu chochote ambacho kinahusiana na Serikali imefanya hilo jambo, ametengeneza kibanda chake yuko sehemu ya vumbi,

mtu anatoka huko anakuja anamwondolea chakula chake, na biashara zake na ukiangalia ile sehemu hakuna hata gari moja linalopita. Sasa unapomwondoa pale, atapitiwa na gari gani? Kwa sababu barabara mbovu au hakuna barabara inayopita hapo, unakuja unamwondolea, huo ni unyanganyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba kabisa TAMISEMI iangalie ni jinsi gani hawa watu wake inawaelekeza. Kwa sababu hawa watu ambao wanaitwa Mgambo wanakuwa hawana busara, kwa sababu kwa akili za kawaida umemkuta mtu, unamnyang'anya vitu vyake, halafu unavichukua unaenda navyo Manispaa, siyo vizuri. Hili jambo liishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wote wa Kinyerezi ambao wako mtaani, mtu kaweka banda nje ya nyumba yake, wamebomolewa na hakuna kitu chochote ambacho kinafanyika. Hilo naomba watakapokuja waweze kutusaidia kwamba hawa Mgambo wavunje huko Kariakoo au sehemu nyingine ambazo kuna watu wengi, lakini huku wamama wanapojifanyia biashara, maisha yenyewe sasa hivi ni magumu, wamama wanajihangaikia, wanawafuata kule kule kwenye mitaa ya ndani kwenda kuwavunjia, siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kuongelea ni kuhusiana na tathmini ambayo inaendelea kwenye Jimbo langu la Segerea. Namwomba Mheshimiwa Waziri, hawa watu wamekaa tangu mwaka 1997, naishukuru Serikali sasa hivi inawafanyia tathmini na imepeleka daftari la uhakiki. Naomba watakapomaliza uhakiki hizi fedha ziwepo. Isije tena ikakaa miezi mingine sita.

Mheshimiwa Spika, ikikaa miezi sita, zoezi limefutika tunaanza upya. Kwa sababu sheria inasema kila baada ya miezi sita. Tangu tumeanza kufanya tathmini, sasa tuko mwezi wa Tano, bado tuna mwezi mmoja. Kwa hiyo, naiomba kabisa Wizara ya Fedha, tutakapomaliza, tuna siku 19 waende wakawalipe hawa wananchi ili waweze kuondoka. Tusije tena tukakaa miezi sita halafu ikaonekana kwamba hela hazijawa tayari. Kwa hiyo, wananchi wangu nitakuwa nao, nitawaambia tunaanza tathmini upya.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Nimesikia hiyo. *(Kicheko)*

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalotaka kuongelea ni kuhusiana na walimu.

**MBUNGE FULANI:** Ehe!

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Tunaishukuru sana Serikali, imeweza kuleta pesa nyingi sana ajili ya kujenga madarasa na kutengeneza miundombinu ya elimu. Tulikuwa tunaomba Serikali iajiri walimu ili hiyo kasi ya kuwa na madarasa mazuri iendane na uwepo wa walimu wa kufundisha. Kama wenzangu walivyosema kwamba darasa moja anafundisha mwalimu mmoja, tutakuwa hatupati matokeo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia madarasa yaendane na miundombinu ya walimu kwa sababu mwalimu anapokuwa anafundisha yuko kwenye darasa zuri, lakini hana ofisi nzuri ya kukaa. Naomba hizi pesa zinazoletwa ni nyingi sana, tunashukuru, lakini zinaletwa tu kwa ajili ya madarasa, hakuna ofisi za walimu. Tunaomba walimu pia wajengewe ofisi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph George Kakunda na Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, ajiandae.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii nami nichangie. Napongeza juhudi kubwa za Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwekeza miundombinu katika afya, elimu na sekta nyingine, hilo tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu unajikita kwenye Wizara ya Elimu. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. Taarifa ya Kamati imeainisha kabisa upungufu wa walimu kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nafuatilia hata taarifa ya leo, kwa mfano Wilaya ya Kilwa kule Mkoa wa Lindi, mahitaji ni walimu 1,406 wa Shule ya Msingi lakini waliopo ni 774, upungufu ni walimu 632. Hili ni tatizo kubwa. Nini maana yake? Upungufu wa walimu unaleta kuzorota kwa elimu na mwisho wa siku matokeo mabovu kwenye ufaulu wa wanafunzi. Kwa mfano, mwaka 2022 Wilaya ya Kilwa ni asilimia 75 ya wanafunzi walifaulu Darasa la Saba na ndiyo ilikuwa ya mwisho kwa Mkoa wa Lindi. Hii inasikitisha sana. Kama wengine walivyoendelea kusema kwamba ni changamoto, kukiwa na walimu wachache, kazi inakuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, kingine inasabisha utoro wa wanafunzi. Mwanafunzi anakuja, lakini hapewi kazi ya kushughulika. Kama tunavyofahamu, mwanafunzi huwa anashughulishwa. Wale walioko kwenye sekta ya elimu

wanafahamu na wale walimu kwamba mwanafunzi lazima ashughulishwe. Ila kunapokuwa na uhaba wa walimu, mwanafunzi anakuwa wakati fulani hana chochote cha kufanya, basi anaona kesho yake wala kesho kutwa, wala mwezi ujao, asiende shuleni, maana anapoteza muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nini matokeo ya upungufu wa walimu shuleni? Kunakuwa na utovu wa nidhamu kwa wanafunzi. Kama tunavyofahamu, walimu hawa ndio washauri wa watoto hawa, lakini kunapokuwa na uhaba wa walimu, inaleta utovu wa nidhamu kwa watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia upungufu wa walimu unaongeza uzito wa kazi, yaani kunakuwa na *increased workload.* Hii ndiyo inaleta msongo wa mawazo kwa walimu hawa. Hata kimwili mwalimu yule anachoka kwa kazi nyingi. Hata Wabunge wengine kwenye michango yao walisema kwamba hata maandalizi ya masomo pia, siyo tu suala la kusimama darasani ukafundisha, lakini kuna maandalizi ya masomo, pia kuna kusahihisha, kuna kumpa ushauri yule mwanafunzi baada ya kusahihisha. Hili yote tunawapa kazi walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho wa siku unaweza ukakuta hata vitendo vingine vya walimu, *behavior* nyingine wanazokuwa nazo walimu shuleni, na hata wakaleta mazingira fulani ya kuwafanyia ukatili fulani watoto hawa tunaowapeleka, ni kwa sababu ya upungufu wa walimu, pia msongo wa mawazo na ndiyo hiyo inaathiri hata afya ya akili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili tusipoliangalia huko tunakokwenda walimu watakuwa na changamoto ya

afya ya akili, watoto watakuwa na changamoto ya afya ya akili, hata wazazi na jamii pia. Kama tunavyoona viashiria vinavyoendelea sasa hivi. Sasa tusifike huko. Naamini kabisa tunaweza tukanusuru jambo hili. Ni wakati umeshafika kwa Wizara yetu ya Elimu pia na Wizara husika ya kuajiri, hebu tuangalie tuweke mkakati, kama siyo ajira zile *permanent,* basi hata za mkataba ili angalau siku hadi siku inaendelea kupunguza tatizo hili la *stress,* na kadhalika, hata matokeo ya wanafunzi kufanya vibaya katika mitihani yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni hayo tu nilikuwa nayo katika sekta hii ya elimu na ninashukuru sana. Ninaamini mamlaka husika imesikia, itafanya maboresho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph George Kakunda atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Isack Mtinga na Mheshimiwa Kwagilwa Rubein Nhamanilo ajiandae.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Nami nitumie nafasi hii kuzipongeza Kamati zote mbili, kwanza, kwa kuandaa taarifa nzuri na kuziwasilisha vizuri sana. Mmeeleweka vizuri sana Wabunge wenzetu, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi sio Mjumbe wa Kamati mojawapo, lakini ni mdau. Kwenye hizi Kamati mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti. Kwa maana hiyo, kama mdau, napenda nichangie jambo la kwanza kabisa kuunga mkono hoja zote mbili za Kamati na kuziwekea msisitizo kwamba, ninaomba Serikali izizingatie, na kwenye utekelezaji waweze kutekeleza yale yote mazuri

ambayo yameshauriwa. Maana yake huo ni ushauri wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwenye utekelezaji tunachoangalia ni utekelezaji wa sera. Sera karibu zote ni nzuri. Kwenye utekelezaji kuna kitu kinaitwa usimamizi. Naipongeza Serikali kwa kipindi cha miaka hii kumi, kumi na tano kumekuwa na uboreshaji mkubwa sana wa usimamizi. Kwenye sekta ambazo zinazozungumzwa sana kwenye zile taarifa mbili napongeza sana usimamizi ambao umekuwa mzuri sana kwenye sekta ya elimu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ujenzi wa madarasa yote ya Shule za Msingi na Sekondari umekuwa ni mzuri na unazingatia thamani ya fedha iliyotumika *(value for money)*. Ndiyo maana unaweza ukampa Afisa Elimu wa Msingi ukamwambia nakupa Shilingi milioni 20, jenga darasa na uweke humo ndani madawati, ubao, kiti cha Mwalimu na meza ya Mwalimu na Shilingi milioni 20 inatosha.

Mheshimiwa Spika, sasa tatizo liko wapi? Bado tatizo liko kwenye sekta ya afya. Hii naisema kabisa kwamba bado tatizo la usimamizi kwenye sekta ya afya ni kubwa. Mimi binafsi nimeshawasiliana na Mheshimiwa Waziri, Naibu, na ninamshukuru sana Naibu Waziri Mheshimiwa Dugange tumeshawasiliana tayari kwa yale maeneo ya kwenye jimbo langu ambayo yanahitaji kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, nisisitize kwamba ili tufanikiwe vizuri kwenye sekta ya afya, bado tunahitaji kutekeleza maamuzi ya Baraza la Mawaziri ya mwaka 2006 yaliyosema ili tutoe huduma za afya vizuri kwa watu wote, tunahitaji kila kijiji kiwe na zahanati, kila kata iwe na kituo cha afya, kila wilaya iwe na hospitali ya wilaya, kila mkoa

uwe na hospitali ya rufaa ya mkoa, kila kanda iwe na hospitali ya rufaa *specialized* ya kanda; na kwenye hospitali ya Taifa kuwe na uboreshaji wa maeneo maalum kwa ajili ya magonjwa maalum na utaalam maalum kama ambavyo wanafanya katika Hospitali ya Muhimbili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo katika utekelezaji, maeneo haya ya hospitali ya Taifa, hospitali za kanda, hospitali za mkoa na hospitali za wilaya napongeza sana sana. Bado tunadaiwa sana kwenye vituo vya afya, kata nyingi bado hazina vituo vya afya. Vile vile tunadaiwa kwenye vijiji. Kwangu nina vijiji 71. Vijiji ambavyo vina zahanati ni 27, ambavyo havina zahanati kabisa ni 44.

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu la Skonge kilometa za mraba 28,773 kutoka kijiji kimoja kwenda kingine ni zaidi ya kilometa 10. Kwa hiyo, wananchi wangu wapo ambao wanatembea kilometa 20 kwenda kuikuta tu zahanati. Sasa katika hali kama hiyo, tunakwenda kwenye Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, ninaamini katika watu ambao watapata shida na wataanza malalamiko ni watu wangu. Watachangia Bima ya Afya halafu ili apate huduma anatakiwa atembee kilometa 20 au 15 kwenda kukuta zahanati. Kwa hiyo hili jambo la ujenzi wa zahanati naomba sana litiliwe mkazo na lipewe kipaumbele na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwenye utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri, kulikuwa na mkwamo ambao ulianzishwa na wataalamu wetu wahandisi. Walipoambiwa choreni ramani sasa ambayo itatumika kujenga zahanati kila Kijiji, wakaenda kuchora ramani kubwa; vyumba zaidi 20 kwa ajili ya zahanati ya Kijiji. Matokeo yake ikashindikana kujenga zahanati kwa

wakati kwa sababu fedha iliyohitajika ni kama Shilingi milioni 250 hadi 300 kwa zahanati. Kwa hiyo, malalamiko yalikuja kwa wananchi kwa sababu wanajitolea, ikapunguza kidogo lakini bado usimamizi kwenye eneo hili la gharama.

Mheshimiwa Spika, nina wasiwasi mkubwa sana. Ni kitu gani ukiangalia kinahitajika kwenye zahanati? Kuna maeneo saba ya muhimu sana kwenye zahanati, yaani *point source of service*. Eneo la kwanza kwenye zahanati ni mapokezi; eneo la pili, kumwona mganga; eneo la tatu, maabara, eneo la nne, chumba cha dawa; eneo la tano, chumba cha sindano; eneo la sita, chumba cha kufunga vidonda na upasuaji mdogo kama upo; eneo la saba, ni chumba cha dharura au mapumziko. Hivi vyumba saba ndiyo vyumba vya *priority* kwenye zahanati. Kwa hiyo, unahitaji gharama ndogo sana kujenga vyumba saba hivyo, na hasa kwenye mapokezi wala haiwi chumba. Kwa hiyo ni vyumba sita. Kwenye mapokezi pale linaweza likawa ni eneo la wazi tu wanapokelewa pale, lakini vyumba sita ndiyo vya muhimu sana kwenye zahanati.

Mheshimiwa Spika, *we need just a point of service,* mtu anakwenda, anahudumiwa, anarudi nyumbani. Kama mtu amezidiwa, ndiyo atapelekwa kwenye kituo cha afya kwa maelekezo ya Mganga.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ni muhimu kwenye eneo la zahanati ni nyumba ya Waganga. Kwa hiyo, unaweza ukajenga nyumba aidha *two in one* au *three in one*. Kwangu kule kuna Kijiji kinaitwa Utimule, wamejenga nyumba ya *two in one* ambayo ni ya gharama nafuu kabisa. Kama Wizara ya Afya na TAMISEMI wanataka kuja Sikonge waione ile nyumba…

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya.

**T A A R I F A**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa ajili ya muda, naomba tu kumkumbusha pamoja na jitihada ya kutetea zahanati katika eneo la muhimu alilosahau ni sehemu ya kujifungulia wakati anataja zile sehemu za muhimu katika zahanati, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, naipokea, lakini mara nyingi kwa sababu ni kwenye kijiji kile chumba cha dharura ndiyo mara nyingi huwa kinatumika kama sehemu ya kujifungulia, lakini baadae kwa sababu anapokea fedha za *RBF* wanaweza wakatumia fedha za *RBF* kujenga chumba maalumu cha kujifunguliwa, lakini kwa kuanzia unaweza ukaanzia na vile vyumba sita nilivyosema.

Mheshimiwa Spika, ya pili ni nyumba ya waganga, halafu ya tatu ni kichomea taka na ya nne ni choo cha wanaume na wanawake na mwisho kabisa ni umeme na maji. Kwa hiyo, ukiwa na huduma hizi tano tayari unakuwa umeshakuwa na zahanati ambayo inaweza ikahudumia wananchi kwenye kijiji baadae uboreshaji utaendelea.

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye gharama; mimi nimepanga gharama hapa ukinipa milioni 35 naweza nikajenga jengo la zahanati kwa kushirikiana na wananchi, kwa sababu tayari wananchi wameishachangia unaweza ukajenga jengo la zahanati; ukinipa milioni 40 naweza nikajenga nyumba ya waganga, *two in one* au *three in one;* ukinipa milioni 10 naweza nikaweka vyoo vya ku-*flash* (choo cha mwanaume na choo cha wanawake); halafu ukinipa milioni 10 nyingine naweza nikajenga kichomea taka, ukinipa milioni tano naweza nikagharamia umeme na maji kwa mwaka, ina maana hiyo ni bajeti ya shilingi milioni 100 inatosha kabisa kujenga jengo la zahanati kwenye kijiji, nyumba ya mganga na hizi huduma zingine.

Mheshimiwa Spika, sasa wasiwasi wangu mkubwa uliopo ni kukosa uzalendo kwa watu wetu ambao tumewaamini kusimamia utekelezaji. Mimi namshukuru sana Dkt. Dugange nimeshampa mfano, nimempa mfano wa zahanati ya Mwamayunga.

Mheshimiwa Spika, zahanati ya Mwamayunga ilianza kujengwa mwaka 2009 kwa fedha za kutoka *ADB…*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Sekunde 30 malizia.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi ile zahanati imetumia shilingi 158,300,000 na bado haijakamilika.

Mimi naomba sana eneo la usimamizi naomba sana liboreshwe. Mtamuona baadae Mheshimiwa Waziri wa

Afya naona alikuwa anaandika andika ili nimpe *data* tuweze ku-*share*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

Mheshimiwa Francis Isack Mtinga atafuatiwa na Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo na Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala ajiandae.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Kamati ya Maendeleo na Huduma za Jamii.

Mheshimiwa Spika, mimi nitaanza kwanza kwa kushukuru Kamati zote mbili kwa kutoa maazimio mazuri kabisa ambayo yakitekelezwa yatatusaidia sana, lakini naomba nijikite sana katika suala zima la malezi ya vijana wetu, watoto wa kiume na watoto wa kike.

Mheshimiwa Spika, niishukuru jamii na Serikali kwamba tumeweka mkazo sana kwa Watoto wakike kiasi kwamba matokeo yake tumeanza kuyaona, matokeo mazuri kabisa sekta muhimu katika nchi hii zimekamatwa na wanawake hata Bunge letu, hata nchi na zinaenda vizuri kabisa. Hili ni jambo jema ambalo tumelifanya kama jamii.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi nataka tu nisikitike kidogo, tumesahau kabisa malezi ya watoto wa kiume. Watoto wa kiume wamekuwa kama kuku huria wale wa kienyeji ambao wanajichungia tu, hawana mtu wa kuangalia. Mambo mengi sasa hivi tunayoyafanya

tunamwangalia mtoto wa kike tu, tumesahau kabisa kama mtoto wa kiume ni sehemu ya familia. Hata wazazi tumeishafikia hatua ukifika nyumbani unauliza Glory yuko wapi? Hawa yuko wapi? Ukiambiwa wako ndani wanajisomea inashia hapo, huulizi Shabani yuko wapi wala Omari yuko wapi, hata wakija nyumbani saa tano usiku. Jambo hili limefanya watoto wa kiume sasa wamekuwa siyo *responsibility* kabisa kwenye familia na huko tunakoenda sasa tunaandaa bomu ambalo tutakuja kushindwa kabisa jinsi ya kulidhibiti.

Mheshimiwa Spika, mimi ningeomba Wabunge, hasa wanawake wajiweke zaidi kwenye uzazi, wasiweke kwenye ule kutetea haki za wanawake, jiweke kama mzazi una watoto wa kike na wa kiume, halafu uangalie huyu mtoto wa kiume jinsi ambavyo sasa ameachwa na baadae tutakuwa na Taifa ambalo sijui litakuwa na muunganiko wa namna gani? Kwa sababu tu ukisema unajenga mabweni utasikia watoto wa kike, ukisema sijui unataka kufanya nini watoto wa kike. Sasa watoto wa kiume inatokea hata mchango wao sijui tunaandaa nini?

Mheshimiwa Spika, kwa mila na desturi za kwetu na kwa dini zetu zote haitaondoa hata siku moja kwamba mtoto wa kiume ni kichwa cha familia. Sasa sijui tunandaa hiki kichwa cha familia baadae kitakuwa kichwa cha namna gani? Kwa sababu tutafika mahala tutakuwa na watoto wa kiume ambao ni *useless* kwenye jamii. Angalia matokeo kama ya *panya road* sasa hivi, matokeo mengine yote yanaonesha kabisa watoto wa kiume, hakuna watu *panya road* watoto wa kike hawapo, ni watoto wa kiume kwa sababu wamesahaulika na jamii na mtazamo kiasi kwamba sasa tunatengeneza bomu kubwa sana.

Mheshimkiwa Spika, mimi nataka niitake Serikali ije sasa na mkakati maalum wa kumrudia mtoto wa kiume iliko muacha, kwa sababu tunakoenda tunakwenda mahali pa hatari sana, tumemuacha mtoto wa kiume na dunia hii haiwezi kukamilika bila wanaume, haiwezi hata siku moja, yaani itafika mahala tutaanza kuwatafuta wanaume mahala waliko, hawana uwezo wa kuzalisha kwa sababu wameishashughulikiwa vya kutosha, kwa sababu wameachwa na tutafika mahala tutakuwa sijui tuna Taifa la aina gani.

Mheshimiwa Spika, niitake Serikali sasa ikumbuke kwamba hili ni bomu tunalitengeneza na si la utani na matokeo yake tumeishaanza kuyaona, wala hayana muda mrefu yata-*backfire* kabisa. Kwa hiyo mimi nafikiri sasa tukae kama wazazi…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtinga kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko.

**T A A R I F A**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa mchangiaji kwamba inawezekana ana hoja anaijenga, lakini kiuhalisia mtoto wa kike alikuwa ameachwa mbali sana, alikuwa katika *marginal group* hata ukiangalia makazini *ratio* ya wanaume kwa wanawake bado ni ndogo sana. Hata ukiangalia *composition* ya Mawaziri huku ndani wanaume kwa wanawake, Mawazari wako wengi sana, popote pale utakapoenda.

Kwa hiyo, nilikuwa tu nataka nimpe taarifa kwamba bado watoto wakiume hawajafikia kiwango cha kuwa kama ni *vulnerable* kama unavyosema. Bado mtoto wa kike anatakiwa apewe kipaumbele ndiyo maana Serikali inawekeza hata kwenye mashule na kwingineko kuweza kumnyanyua huyu mtoto wa kike sasa ambaye pia ni *victim* katika mambo mengi mengi hata ukatili ambao tunazungumzia humu ndani. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis unaipokea taarifa hiyo? Mheshimiwa Francis Mtinga.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, huyu ni *mate* wangu tumesoma naye. Taarifa yake naipokea lakini mimi sijasema watoto wa kike hawana umuhimu; wana umuhimu mkubwa na ndiyo maana wanaongoza nchi leo na inaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachosema tumewasahau watoto wa kiume, tunatengeneza bomu la hatari, tutakapokuja kuwarudia hatutaweza, leo tumeweza kumchukua mtoto wa kike kwa sababu aliachwa, tumemfikisha hapa tulipofika, lakini jinsi tunavyomuacha mtoto wa kiume nyuma tutakapo mrudia hatutaweza ni bomu ambalo ni baya.

Mheshimiwa Spika, kwa mtoto wa kiume madhara ni makubwa, ameongelea ubakaji sasa watoto wa kiume wanalatiwa, sasa tunafika mahala…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtinga, hebu tuelewane kidogo hapo; ukiwa na watoto wawili mmoja wa kike, mmoja wa kiume kwa hali ilivyo sasa hivi utamlipia ada yupi kati ya hao wawili? *(Makofi)*

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, mimi kama baba nitalipia watoto wangu wote ada.

**SPIKA:** Haya huyo ni wewe; mzazi wako wa kizazi chake ulipokuwepo wewe mtoto wa kiume na mtoto wakike alikuwa anamlipia ada yupi? *(Makofi)*

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, historia inaonesha kwamba mtoto wa kike aliachwa nyuma, mimi sijakataa, na tumefanya juhudi kubwa kama Taifa kumkomboa mtoto wa kike na tumefanikiwa kiasi kikubwa. Nachofanya naikumbusha jamii...

**SPIKA:** Sawa sasa, ngoja tunaenda taratibu, ngoja kwanza.

Hoja yako ni nzuri na ni nzito, nataka ufike mahali unaposema kwa kumtazama mtoto wa kike mtoto, huyu mtoto wa kiume anaachwa nyuma wakati huyu wa kike mpaka sasa hivi kitakwimu yupo nyuma, anajaribu kusogezwa alipo huyu wa kiume na siyo kwamba wa kiume kaachwa, huyu msichana ameshampita huyo wa kiume halafu bado wa kiume kaachwa. Ni kwamba wa kike anasogezwa pale alipo wa kiume sasa, kama unazo takwimu tutaenda kwa takwimu, lakini aliyekupa taarifa hapa naye kaja na takwimu angalia hata humu ndani Wabunge wanawake wako wangapi humu ndani asilimia yao? *(Makofi)*

Wabunge wanaume humu ndani mko asilimia ngapi? Kwa hiyo, hoja yako ni nzito, lakini ujumbe unaoutuma ni kana kwamba mtoto wa kike ameshamkuta huyu mtoto wa kiume, ameshampita mtoto wa kiume, ameachwa wa kiume nyuma, hapana.

Mtoto wa kiume bado yuko mbele anavutwa wakike amkute wakiume ili waende wote pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mtinga dakika moja malizia mchango wako. *(Makofi)*

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, mimi nafurahi jinsi ulivyomalizia umenielewa kwamba mtoto wa kike tumemfikisha mahala pazuri na tutaendelea, lakini watoto wa kiume tusiwaache nyuma kwa sababu tunatengeneza bomu ambalo litakuja kutushinda. Kwa hiyo nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa.

Mheshimiwa Mtinga nilikupa dakika moja na haya makofi lazima ujue yanaonesha wingi wa wanaume humu ndani, ndiyo yanaonesha wingi wa wanaume humu ndani kwa sababu hakuna namna wanawake watapiga makofi yafikie ya wanaume. *(Makofi)*

Haya sekunde thelathini malizia mchango wako *(Makofi)*

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba nimalize hoja yangu kwa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote hasa wanawake, wabebe nafasi ya uzazi zaidi tusiwe *feminist,* tukumbuke katika uzazi tunawatoto wa kike na wa kiume wote wanahitaji huduma ya jamii na huduma ya familia, ahsante. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na michango, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Kwagilwa

Reuben Nhamanilo, atafuatiwa na Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni ajiandae.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia ripoti zetu za Kamati zetu hizi mbili na *specifically* nataka nichangie ripoti ya Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa kumi na moja wa taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wetu wa Kamati hii unaongelea habari ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati katika halmashauri nchini. Wanasema Bunge limeazimia kupitia upya miongozo ya namna ya kutekeleza miradi hii, na kwamba Kamati imejulishwa na Serikali kwamba tayari imeshafanya mpango wa kushirikiana na *UNCDF* kwa ajili ya kuandaa mipango hiyo mipya ili miradi hii iweze kutekelezeka *fairly*.

Mheshimiwa Spika, miradi hii ya kimkakati ni kielelezo kinachoishi, kinachoonesha namna gani kama Taifa hatuko sawa katika ugawaji wa rasilimali za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, miradi hii ya kimkakati ni kielelezo kinachoishi, kinachoonesha kwamba kama Taifa hatuko sawa katika ugawaji wa rasilimali zetu, nitaelezea.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia miradi hii ya kimkakati sharti lake kubwa la kwanza lilikuwa ni halmashauri itenge fedha, halafu ipeleke andiko. Kwa jinsi halmashauri zetu zinavyotofautiana kimapato mathalani unapozungumzia Halmashauri ya Handeni Mjini *own source* yetu hata milioni 700 haifiki, tutaigawaje gawaje hiyo fedha mpaka tupate fedha ya kuwekesha ili Serikali ije kutuunga mkono

kupata mradi wa kimkakati. Hiyo ndiyo kusema wale *giants* wote wataendelea kupata miradi hii, halafu sisi ambao siyo *giants* tutaendelea kukosa miradi hii. Tunatengeneza Taifa ambalo linawapendelea wengine na kuwatweza wengine. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa naomba na naiomba sana Serikali huu mwongozo wanaouandaa kwanza pana kitu cha ajabu sana, mimi nilifikiri kwamba mwongozo wanamna ya kugawanya miradi hii Wizara tu ingeweza kufanya kwa maana Serikali tu inaweza kufanya. Yaani sisi kuandaa muongozo wawape Mradi uende mpaka tulete *UNCDF*? Yaani ndiyo Serikali mmefikia hapo? Yaani kwamba ninyi hamuwezi kufikilia kabisa namna gani tugawanye *fairly* mpaka tulete hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu jinsi ilivyo unavyogawanya kwa kupeleka kwenye miji mikubwa peke yake unasababisha vijana wetu kutoka Handeni na maeneo mengine ya Tanzania wahame kwenda kwenye hii miji mikubwa, unaenda kusababisha mrundikano pale, watoto wetu wanatafuta ajira pale, vijana wetu wamejaa Dar es Salaam, wamejaa Arusha, wamejaa Mwanza wametoka kwenye vijiji huko kwa sababu hatupeleki miradi hii.

Mheshimiwa Spika, nitaongelea kwa pamoja na mradi huu wa *TACTIC* maana ni yote hii ni miradi inayokwenda sambamba. Mradi huu wa *TACTIC* unatupa *master plan* kwenye mradi, unatupa barabara, unatupa soko na unatupa stendi, cha kushangaza hii miji inayosema ni *giants* na inayopewa hii miradi ya kimkakati ndiyo hii hii tena ambayo ipo kwenye *TACTIC* na imepewa kipaumbele ya kwanza, yaani kule kwenye mradi wa kimkakati mliwajengea soko, halafu

mmewaweka tena kwenye *TACTIC* na ambako nako watapata soko, halafu unaacha miji kama Bunda inashangaa shangaa, Handeni Mjini tunashangaa shangaa, Ifakara tupo tupo tu, Kondoa, Mafinga, Makambako tunatengeneza Tanzania gani hiyo ya kujenga Dar es Salaam kila siku?

Mheshimiwa Spika, lazima tufike mahala rasilimali za nchi yetu tuzigawe kwa usawia na hili niwaombe wenzetu wa TAMISEMI wakae na watu wa Wizara ya Fedha, kaeni na watu wa Wizara ya Fedha kama fedha hizi tulizonazo zetu za mapato ya ndani na hizi tulizokopa *World Bank* hazitoshi kuendeleza miji yetu, kaeni na Wizara ya Fedha ili twende tukatatue tatizo hili kwa kutumia Sera za Kikodi. Hivi nani hapa anaweza akasimama aniambie eti Mbuga ya Katavi siyo bora kuliko Serengeti? Katavi iko vile leo ni kwa sababu miundombinu iko mibovu tu pale. Kwa nini hatugawanyi rasilimali hizi kwa kufuata huo uhalisia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali na hususani TAMISEMI waachane na hii habari ya kuzunguka nchi nzima eti wanatambua vyanzo vya mapato. Sasa ukienda Handeni unatambua vyanzo vya mapato? Utakuta sisi ni mnada tu pale kila siku sisi ni mnada tu. Kutengenezwe *district economic profiles* kwa nchi nzima ambazo zitaonesha…

**MHE. ENG. ISACK A. KAMWELWE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nhamanilo kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Isack Kamwelwe.

**T A A R I F A**

**MHE. ENG. ISACK A. KAMWELWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kumpa taarifa mzungumzaji anaeendelea kwamba mwongozo wa bajeti ya mwaka ujao wa fedha TAMISEMI wameelekeza halmashauri zinazokusanya mapato chini ya bilioni moja kwenye mapato yake zitenge asilimia 20 tu ya maendeleo, lakini zile ambazo zinapata zaidi ya bilioni tano zinatenga asilimia zaidi 50 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Kwa hiyo, unachozungumza kama Handeni milioni 700 asilimia ishirini tu zitaingia kwenye maendeleo, lakini zingine zote ziingie kwenye *OC*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nhamanilo unaipokea hiyo taarifa hiyo?

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, namuheshimu sana mzee wangu, kama amenisadia nashukuru sana unajua nina moto hapa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nimepokea taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Reuben, unaipokea taarifa ya Mheshimiwa Isack Kamwelwe?

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, ninaipokea taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachokisema tusiwe waumini wa vyanzo vya mapato, tunachotakiwa ni kutengeneza *district economic profiles* na siyo hizi ambazo mmeweka kwenye *website* eti *district economic profile* inaongelea tu watu, eti kuna watu idadi kadhaa, idadi kadhaa tengenezeni *district profile* ambazo zinaangalia *potentials*

za eneo husika ili mjue ni mradi gani mkiwapelekea unawa-*boost*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunacho Chuo cha Mipango, Mheshimiwa Waziri wa Fedha upo, chuo hicho mnacho wenyewe kwa nini makitumii kupanga? Kwa nini hamkitumii kutengeneza hizi *Districts profile* kwa ajili ya kuangalia *potentials* za uchumi wa kila eneo ili tupeleke fedha maeneo hayo kwenye miradi hii ya kimkakati tuka-*boost* eneo lile? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatamani sana na ninashauri kwenye maazimio yetu tuongezee azimio, ikiwa tu hii miradi ya kimkakati ambayo Serikali imekuwa ikiiendesha miaka yote hawakuwa hata na mWongozo mpaka leo, na yenyewe ni ya bilioni kama 200 na kitu, je, itakuwaje kwenye huu mtadi mkubwa wa *TACTIC* ambao ni wa karibu bilioni 600? Wanauendeshaje? Ile tu ya kujenga soko, stendi, hapa na pale hawakuwa hata na mwongozo, huu mkubwa! Ni nani aliyewaambia kwamba, hii *first tire* inatakiwa iwe hii Miji, kwa nini isiwe Handeni na sehemu nyingine? Tuweke azimio la kwamba mradi huu wa *TACTIC* ukapitiwe upya na upangwe kulingana na namna ambavyo Halmashauri zinazohitaji kusaidiwa kwa uharaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo ningependa nimalizie…

**SPIKA:** Sekunde 30, malizia.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo ningependa nimalizie ni hapohapo kwenye kuangalia sera za kikodi kulingana na eneo husika. Kwa mfano, Tanga tunalima mkonge, kwa

nini isiwekwe sera ya kikodi kuliendeleza eneo la Tanga kwenye uzalishaji wa mkonge? Mathalani, Mwekezaji yeyote atakayewekeza Tanga ndani ya miaka hii 20 hatatozwa *corporate tax*. Eeh! ni mfano tu, si watu wote wataenda ku-*flock* huko? Kwa mfano, Katavi unasema Mwekezaji yeyote atakayejenga hoteli *corporate tax* yake tutamtoza tano siyo kwamba watu watapeleka hoteli huko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama watu wa Serikali wamechoka kufikiria wapishe hizo siti wakalie watu wengine wafikirie. Baada ya kuyasema haya nakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Yussuf Majala, atafuatiwa na Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma ajiandae.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia wasaa na mimi wa kuweza kutoa mchango wangu kwenye hizi Kamati zetu mbili, USEMI, lakini na Huduma. Ninawashukuru na niwapongeze Kamati kwa kazi kubwa waliyoifanya, hususan Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuwasemea wana-Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Spika, wakati tunapata uhuru ardhi ya Manispaa ya Dodoma au ya Halmashauri wakati huo ya Dodoma ilikuwa chini ya wana-Dodoma, lakini mnamo mwaka 1973 Serikali ikaamua kuiweka ardhi yetu chini ya Ustawishaji wa Makao Makuu *(CDA),* ili Dodoma kama Makao Makuu ya nchi iweze kupangwa na kupangika ili ifafane na miji mingine duniani.

Mheshimiwa Spika, *CDA* ikaishi takribani miaka 43 kuanzia mwaka 1973 mpaka 2016 ambapo Hayati Rais John Pombe Magufuli aliamua kuivunja *CDA*. Ilivunjwa kwa sababu *CDA* hawakuweza kufanya kazi ya kupanga Mji badala yake walikuwa ni chanzo cha migogoro kwa wana-Dodoma. Tukaivunja, ikavunjwa *CDA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matarajio ya wananchi wa Dodoma yalikuwa baada ya kuondolewa *CDA* ardhi yao imerudi Halmashauri kwamba, wana-Dodoma sasa watakwenda kumiliki ardhi yao na migogoro itakwenda kuisha. Kwa bahati mbaya sana hivi tunavyozungumza wananchi leo wa Dodoma wanasema ni afadhali ya *CDA* kuliko ardhi ilivyorudi kwenye Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Spika, hawa Watumishi baadhi baada ya *CDA* kuvunjwa, baadhi walipelekwa kwenye Halmashauri zingine, baadhi wamebaki ndani ya Jiji la Dodoma kwenye kitengo cha ardhi. Mkurugenzi leo wa Dodoma ndiye aliyekuwa Afisa Mipango ndani ya *CDA*. Leo ni Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, anafahamu vizuri suala la mgogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tuna hati wananchi kiwanja kimoja kina hati zaidi ya tatu. Wale wenye fedha wenye mabavu ndiyo wanaoweza kumiliki ardhi leo kwenye Jiji la Dodoma, wale wanyonge hawawezi kumiliki ardhi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, kwenye ushirikishwaji wa upangaji ama wa upimaji wa ardhi, makubaliano yalikuwa ardhi yako ukionesha unatoa asimilia 10 kwa ajili ya barabara, asilimia 30 wanachukua Jiji, asilimia 70 unapewa mwananchi, haifanyiki hivyo. Wale wengine ambao wana viwanja vidogovidogo wanaunganishwa

hapo baadae wakija kuhoji viwanja vyao viko wapi wanaambiwa kimeliwa na barabara, kwa hiyo huna kiwanja. Hayo ni mateso wanayopitia watu wa Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Spika, hiki kitu iinaumiza sana. Tuna wajane, tuna wagane, tuna watoto yatima wako hapa ambao leo wananyimwa ardhi yao kwa sababu ya Watanzania wenzetu ambao tumewapa nafasi, waweze kuwasaidia na wao watoke kwenye wimbi la umaskini walilonalo, wao wako wanaatamia ile ardhi, wanaitumia wanavyotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imesema kwamba, watu wachukuliwe hatua kuhusiana na suala zima la migogoro ya ardhi ya Dodoma. Naomba niongezee, hawa watu ambao walikuwepo tangu *CDA* na mpaka leo bado wako pale ofisini wapaki magari yao pembeni, uchunguzi upite, wakiwa wao wako pembeni, ili tujue shida iko wapi Dodoma, kwa nini Dodoma na siyo sehemu nyingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nihame kwenye suala zima la Dodoma, naomba niende kwenye suala zima la elimu. Tunashukuru Serikali kwa kutuongezea madarasa kwenye shule zetu mbalimbali, lakini wakati tunaomba haya madarasa wakati mwingine na sisi huku vijijini ama kwenye maeneo yetu tunakuwa tunaendelea kuwaza tufanye nini ili watoto wetu waweze kupata elimu yenye mazingira rafiki.

Mheshimiwa Spika, tunayo changamoto moja Halmashauri ya Wilaya ya Chemba. Tulipewa Shilingi Milioni 140 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa Saba shule ya Sekondari Mrijo. Kata ya Mrijo ina Vijiji Saba, Vijiji Vitatu

mwanafunzi anatakiwa kutembea zaidi ya kilometa 60 kwenda na kurudi. Wananchi wakaamua kujihamasisha waweze kutoa Kijiji ambacho kipo katikati wajenge, waanzishe pale shule ili waweze kujenga shule nyingine ya sekondari, waache shule mama ya Mrijo waje wajenge shule nyingine pacha ya Mrijo ambayo itakuwa inaitwa Mrijo Juu.

Mheshimiwa Spika, sasa tukawaomba na wananchi wakajitolea, wamefyatua tofali, wamesomba mchanga, wamesomba…

**SPIKA:** Sekunde 30, malizia.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, tukawaomba Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa haya madarasa saba badala ya kupelekwa pale Mrijo Chini ambako tuna madarasa 24 tunaomba tuyalete huku Mrijo Juu ili wanafunzi wetu ambao wanatembea zaidi ya kilometa 60 kwenda na kurudi tuwapunguzie huo umbali ili waweze kusoma katika mazingira rafiki, lakini Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hawajaweza kutuelewa hilo. Kwa hiyo, niombe sana hebu watuone kwenye jicho hilo, kutembea kilometa 60 ni mtoto wa Mbunge gani anayeweza kutembea kilometa 60 kwenda na kurudi halafu sisi tunawanyima wananchi wetu kwa kodi zao wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe sana Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwenye suala hili waweze kuliangalia vizuri. Nakushukuru kwa wakati. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, atafuatiwa na Mheshimiwa Samweli Xaday

Hhayuma. Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile ajiandae.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii, lakini kabla sijachangia ninazipongeza Kamati zote mbili kwa uwasilishaji mzuri na ushauri mzuri kwa Bunge, nadhani imekuwa ni mwanga mzuri wa kutusaidia kulijadili jambo hili kwa upana wake.

Mheshimiwa Spika, nadhani sote ni mashahidi katika wakati huu wa Serikali ya Awamu ya Sita ni wakati pekee kwa uzoefu wangu mimi wa kuishi Tanzania ambapo nimeona pesa nyingi sana za miradi ya maendeleo zinapelekwa kwenye Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya. Pesa zinazohusu madarasa, pesa zinazohusu vituo vya afya, zahanati, zinapelekwa kwa wingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sote hapa ni mashahidi na ni Madiwani huko kwenye Halmashauri zetu, hata Watumishi wetu wameingiwa na ugumu kwenye kusimamia pesa hizo nyingi zinazokuja. Sasa mimi nimesimama kuchangia kwenye Kamati hii ya Utawala na Serikali za Mitaa pamoja na Huduma za Jamii, nataka kujikita kwenye kutoa ushauri wangu wa namna bora ya kusimamia pesa za maendeleo ambazo zinapelekwa kwenye Halmashauri zetu. Pesa nyingi ambazo zikisimamiwa vizuri zitaacha historia isiyosahaulika kwenye nchi yetu na zitampa heshima kubwa sana Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu binadamu yeyote anapopewa pesa hapendi sana kusimamiwa, anapenda aachwe afanye vile anavyoona yeye. Na pesa daima ni sabuni ya roho, kila mmoja akiona pesa

anatamani kuitumia yeye ndio maana zikawekwa taratibu za usimamizi. Ndiyo maana kwenye *level* ya Serikali Kuu lipo Bunge tunaisimamia Serikali, lakini kwenye *level* ya Halmashauri yapo Mabaraza ya Madiwani yanasimamia zile Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema Mabaraza ya Madiwani hapa leo?

Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya Madiwani kusimamia kwake Halmashauri wanasimamia kupitia ziara mbalimbali, kupitia vikao, miradi inapopelekwa kule inaenda kukaguliwa na Madiwani kwenye ziara. Hivi ninavyoongea kuna nafasi ambayo imetolewa na Wizara yetu pendwa ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia maelekezo mbalimbali na nyaraka mbalimbali, Halmashauri za Wilaya badala ya kusimamiwa kwa nguvu zote na Madiwani utendaji wa Madiwani, Halmashauri za Wilaya sasa zinaendeshwa kwa hisani za Wakurugenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Waheshimiwa Madiwani kwenye baadhi ya Halmashauri za Wilaya, ikiwepo ya Kwimba, Kamati ile ya Huduma ya Jamii ambayo ilikuwa Elimu, Afya na Maji na Kamati ya Uchumi hazifanyi kabisa ziara kwa sababu, Halmashauri zinasema kuna nafasi inatoka kwenye kanuni ya kuwafanya wao waamue kama Madiwani waende ziara au wasiende. Kwa hiyo, hela zote tunazopeleka zile Kamati za Madiwani hazikagui hizo pesa, sasa hii ni hatari kubwa kuacha pesa zetu zisisimamiwe huko vizuri! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na hayo Halmashauri zetu ili zisimamiwe vizuri, hapa nilishawahi kusema na leo ninarudia, ukiwa na mali yako unaweka mlinzi aliyeshiba.

Ukiweka mlinzi mwenye njaa una hatari ya kuibiwa kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na nafasi hii kwa ruhusa yako naomba nisome waraka ambao ulitoka Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwenda kwenye Halmashauri ambao unatoa *loop*. Unasema hivi, katika kipengele cha nne; "*Posho za kujikimu za Waheshimiwa Madiwani zinapaswa kulipwa kwa kuzingatia mahali, sehemu na umbali Diwani anakotoka. Msingi mkubwa wa kuzingatiwa ni kuwa Diwani husika sharti awe amesafiri na kulala nje ya makazi yake ili aweze kuhudhuria kikao kinachofuata.*" *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sharti hili limekuwa likitumika vibaya, yaani Mkurugenzi ndio anaamua Diwani amelala au hajalala. Mwisho wa siku sasa Mabaraza ya Madiwani, Madiwani wanapoenda kwenye vikao vyao wanalipwa kwa hisani, yaani kitu kinaitwa mahusiano. Wasipokuwa na mahusiano mazuri na Mkurugenzi hawalipwi vile inavyotakiwa. Zile *per diem* za Madiwani zinaamuliwa kwa mahusiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba Bunge lako Tukufu kupitia Kamati hii tumuelekeze Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa atoe maelekezo mahsusi kuliko maelekezo kama haya yanayotoa *loop hole* ya watu kucheza na Mabaraza ya Madiwani yashindwe kusimamia Halmashauri zetu. Atoe maelekezo mahsusi yanayozielekeza Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Majiji kulipa pesa kwa Madiwani kwa kuzingatia uhalisia kwamba, Madiwani wengi wanapokuja, hasa kwenye Halmashauri za Wilaya, wengi wanalala.

Mheshimiwa Spika, huwezi kusema Diwani wa Sumve um-*judge* kwa umbali wakati miundombinu yake haimruhusu, hakuna daladala, akishatoka kule akamaliza kikao saa 12 lazima alale Ngudu. Sasa unapomwambia kwamba, umbali wake na Halmashauri zetu hizi tunaanza kuweka, yaani imekuwa ni kwamba, ni hisani za watu wanafikiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako lielekeze Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itoe waraka mahsusi ambao unaondoa mkanganyiko wa ulipaji wa posho za kulala za Madiwani kwenye Halmashauri za Wilaya na Miji ambazo kwa asilimia kubwa Madiwani wanapoenda kwenye vikao wanaenda wanalala ili waweze kukaa kwenye vikao wakiwa na amani, wasimamie pesa zetu vizuri ili sisi tunapopeleka pesa kule ziwe salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani jambo hili tumekuwa tukilisema mara kwa mara kuhusu usimamizi wa Halmashauri kwa kuboresha maslahi ya Madiwani…

**SPIKA:** Sekunde 30, malizia.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, naomba sasa Bunge lako Tukufu litoe maelekezo mahsusi na tumuombe Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa atoe maelekezo mahsui kwenye Halmashauri ambayo yataondoa mkanganyiko wa ulipaji wa wasimamizi wetu wa Halmashauri. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma atafuatiwa na Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile. Mheshimiwa Bernadetha Kasabago Mushashu ajiandae.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia naunga mkono hoja za Kamati zetu zote mbili za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wenzangu wameongea sana suala la upungufu hasa wa walimu na jinsi unavyoathiri ufaulu wa watoto wetu, lakini changamoto hiyo pia ipo kwenye sekta ya afya. Kwamba, tunao upungufu mkubwa kiasi kwamba, huduma zinazotolewa zinaathirika kwa sababu ya upungufu wa watumishi, lakini haya mimi nilitaka tu ni *high light*.

Mheshimiwa Spika, nitaongea zaidi suala la usimamizi wa rasilimali chache tulizonazo. Una Mwalimu anakaa karibu kilometa 40 kutoka Halmashauri, hapo nimechukua wastani wa kawaida. Anazo stahiki zake ambazo hazina uhakika kila siku anarudi Halmashauri, hivyo hafanyi kazi iliyokusudiwa ya kufundisha wanafunzi. Watumishi wa afya vivyo hivyo, ana stahiki zake Halmashauri atarudi kila siku.

Mheshimiwa Spika, natoa mfano, kwenye suala la kuwapandisha watumishi vyeo. Unaweza ukakuta kwamba, aidha Halmashauri ina watumishi 700 nafasi zinatolewa 400, unampa mtihani Afisa Utumishi je, atachaguaje hao 300 kati ya 700 ambao wote wanastahili? Sasa unakuta kila mtu anafanya *lobbying* badala ya watu kufanya kazi muda wote wanashinda Halmashauri ili angalao waweze kuangaliwa. Maeneo hayo yapangwe vizuri kwenye suala la kuwasimamia watumishi. Kama Halmashauri ina watumishi 700 ikiwezekana twende kwa *phases,* Halmashauri ngapi zinapandisha watumishi ili wawe *comfortable* wafanye kazi.

Mheshimiwa Spika, Serikalini kumekuwa na kuongea suala la kuweza kusawazisha watumishi, kuweka usawa. Kwamba, kuna maeneo mengine watumishi wamekuwa wengi kuliko maeneo mengine, lakini tumeongea sana suala la kuboresha mazingira au wale wanaofanya kazi kwenye mazingira magumu wapewe posho maalum, badala ya kuhangaika kuangalia sehemu gani kuna watumishi wengi, sehemu gani hakuna watumishi wengi, maeneo ambayo yana hali ngumu wapewe posho maalum ya mazingira magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, wanaokaa mijini wanayo maji, wanao umeme, usafiri siyo mgumu sana. Wanaokaa vijijini wanakaa maeneo ambako hakuna umeme, hakuna maji, akitaka kusafiri ni changamoto kubwa, hao wapewe vivutio mahsusi ili waweze kufanya kazi kwa utulivu kwenye maeneo hayo. Ukifanya hivyo wale wa mijini wakiona kuna usawa wa huduma kati ya mijini na wa vijijini hawataona taabu kwa sababu wanapata zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri iliyofanyika kwenye ujenzi wa miundombinu ya elimu, ujenzi wa miundombinu ya afya, lakini ninaomba kwenye kupanga miundombinu hii si lazima kila sehemu tupeleke kituo cha afya kilichokamilika, tunaweza tukaangalia yale mahitaji ya msingi. Mheshimiwa Kakunda ameongea kidogo vitu ambavyo vinahitajika, zipo Kata nchi hii ambazo zimepata zahanati zile za mwanzo, tunaweza tukachagua tukajenga *OPD* nzuri ikawa na vyumba vile vyote vinavyohitajika, tukaweka huduma ya mama na mtoto wakati huo tukiendelea kutanua kila Kata ipate kituo cha afya. Tunaweza tukajenga kwa awamu wakati

huo tukijielekeza kwamba, maeneo mengi yapate hizo huduma kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ule mtazamo wa Serikali wa kwamba, Makao Makuu ya Tarafa lazima kuwe na kituo cha afya cha kisasa, safi kabisa, ili angalao yale ambayo tunayatengeneza kwenye Kata yaweze kupata rufaa na huduma zilizokamilika kwenye ngazi ya Tarafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasema hivi, unaweza kukuta kata ambayo kituo cha afya au zahanati imejengwa sasa hivi na ile ambayo ilikuwa nayo kabla tofauti ni kubwa sana. Suala la ramani ameshaliongea Mheshimiwa Kakunda, kwamba ramani tulizokuwa nazo mwanzo na zilizopo sasa ni tofauti kabisa. Zile za zamani hazikidhi, hivyo maeneo yale yakaangaliwe.

Mheshimiwa Spika, tumeongea sana masuala ya udhibiti wa vifaa tiba, dawa chakula na vipodozi. Kwenye chakula kuna vitu vinaitwa, bidhaa ambayo ni dawa au chakula, kwenye vipodozi kuna vipodozi vidogo dawa au Kipodozi tunaita *bodyline products* zinakosa udhibiti makini kwa sababu zinadhibitiwa na taasisi mbili tofauti. Naomba bidhaa hizi, bidhaa za chakula vipodozi ambavyo vilikuwa vinadhibitiwa na *TFDA* ambayo kwa sasa tunasema Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba; bidhaa hizi zote zidhibitiwe na taasisi moja ili kuhakikisha zile *border line products* zinasimamiwa vizuri ili kulinda Afya ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana kwa sababu kwa sasa bidhaa zinazodhibitiwa na *TBS*, kuna changamoto ya utaalam, lakini wanasimamia bidhaa nyingi hivyo hawatoi umuhimu mkubwa kwenye upande wa chakula na vipodozi.

Mheshimiwa Spika, niseme kidogo kuhusu suala la vipaumbele vya namna ya kuamua mradi gani utekelezwe sehemu gani. Sasa hivi kumekuwa na utamaduni kwamba Wizarani wanasema kuna fedha *either* ya kujenga shule, ya kujenga Zahanati au ya kujenga jengo la utawala ilhali kwenye maeneo halisia unakuta mahitaji ya Wananchi ni Shule, Mahitaji ya wananchi ni ukarabati wa shule. Ninachoomba ile mipango inavyopangwa ianzie kule chini kwenye ngazi ya vijiji ili kujua mahitaji halisi ya chini. Badala ya tunasema tuna fedha kwa ajili ya kujenga majengo ya utawala, tunafedha kwa ajili ya kujenga zahanati. Tuangalie mahitaji halisi ya maeneo yetu. Kuna shule imechakaa tujielekeze kwenye kukarabati shule, nyumba za walimu hazipo tujielekeze kujenga nyumba za walimu.

Mheshimiwa Spika, lakini tunachangamoto kubwa sana; tumejenga shule za kata nyingi lakini umbali ni mkubwa kutoka wanako kaa watu. Ili kufika shuleni kwenda na kurudi unatembea zaidi ya Kilometa 40. Sasa tuone namna ya kujielekeza kujenga mabweni kwa ajili ya watoto wetu ili wawe salama na waweze kusoma vizuri. Unakuta wanachoka kabla ya kufika shuleni hawana namna ya kujifunza kwa utulivu, tuwekeze kwenye eneo hilo. Inawezekana fedha ni nyingi lakini tuwashirikishe wadau wa elimu ili kuhakikisha tunatatua changamoto hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile atafuatiwa na Mheshimiwa Benadeta Mshashu, Mheshimiwa Magreth Sita ajiandae.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi. Mimi ni mjumbe wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa. Awali niunge mkono maoni ya Kamati zote mbili kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo anafanya bidii ya kuhakikisha maisha bora ya Watanzania yanendelea kupatikana.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na timu yake kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wameendelea kuifanya. Wakati wamekuja mbele ya Kamati tuliendelea kuridhishwa sana na utekelezaji wa maazimio ya Bunge lako. Pia nimpongeze Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI na timu yake kwa kazi kubwa na nzuri, kwakweli kazi zinaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ninanyongeza ya ushauri kwenye maeneo kadhaa kwa sababu maazimio haya na maoni ya Kamati na mimi ni sehemu yake.

Mheshimiwa Spika,najielekeza kwenye *TARURA*, tuendelee kuwapongeza, wenzetu *TARURA* wanafanya kazo kubwa na nzuri kwelikweli katika maeneo ya nchi yetu. Hata hivyo bado niendelee kuomba kwa Serikali waendelee kuwezeshwa kifedha, bajeti yao iongezwe na hasa kwenye eneo la dharula. Inapotokea Msimu wa mvua hali inakuwa ni ngumu na wanakuwa na kazi kubwa kwelikweli. Wakiwezeshwa wataendelea kuimarisha utoaji wa huduma, na kwa kweli miundo mbinu kwenye maeneo yetu itaendelea kuimarika.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hilo hilo la *TARURA* tuliendelea kushauri na bado naendelea kusisitiza

kuishauri Serikali; bado eneo la manunuzi liendelee kusogezwa namna ambavyo itawezekana kufika kwenye eneo la Wilaya. Kwa namna ilivyo sasa hivi manunuzi na *tendering* hufanyiwa kwenye ngazi ya mkoa. Wale mameneja wa *TARURA* walioko kule wilayani kwenye halmashauri wanabaki kama *PS,* hawana mamlaka kwa hawa wakandarasi kwa kuwa tayari wamepewa *tender* kutoka huko mkoani. Sasa matokeo yake wanakosa namna ya kusimamiwa vizuri kule kwenye halmashauri; na hata sisi tulioko kule tunashindwa namna ya kuwasimamia vizuri. Lakini kazi inayofanyika na *TARURA* ni nzuri na wanaendelea kufanya kazi kwenye mazingira hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoke hapo nijielekeze kwenye mradi wa ujenzi wa Shule za Sekondari. Niipongeze sana Serikali kwa uamuzi huu; na kweli hizi shule ni nzuri na zinapendeza. Hata ukifika kule kwenye jimbo langu la pembezoni la Nachingwea unakuta shule iliyojengwa kwa mradi huu wa *SEQUIP* inapendeza kweli kweli, tunaishukuru Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini bado na mimi niendelee kusisitiza kwenye eneo lile la gharama halisi ya hizi shule. Milioni 470 yako maeneo mengine huwezi kumaliza uhitaji wa hiyo shule. Bado tuendelee kuangalia kulingana na eneo. Huwezi kufananisha eneo la Dar Es Salaam na eneo la Nachingwea au kule Tunduru. Niiombe sana Serikali ipitie upya jambo hilo, na kama ni suala ambalo linaweza likarekebishika basi tuweze kupata ufumbuzi wa haraka.

Mheshimiwa Spika, nijielekeze kwenye mchango tena kwenye Kamati ya Huduma. Nimepitia vizuri hapa, lakini yapo mapendekezo kadhaa na maoni ambayo Kamati wametoa. Ni ukweli usiopingika kwamba kwenye

ukatili wa kijinsia wako baadhi ya wanaume na wenyewe wanapata kadhia hiyo. Kwa sababu ya kitamaduni ya Kiafrika na Kitanzania hatuna mahala pa kulalamika, yawezekana wengine tuko ndani humu lakikini hakuna anayeweza kutuzungumzia.

Mheshimiwa Spika, kwenye mapendekezo ya Kamati na mimi naomba nipendekeze nyongeza kwenye ukurasa wa 41(i) kuishauri Serikali, kufanya utafiti wa kina kujua nini chanzo cha ongezeko la ukatili wa kijinsia nchini hususani kwa wanawake na watoto. Hapa iongezwe na wanaume, kwa sababu tunachoshauri hapa ni kufanya utafiti. Kama bado wako wanaume ambao nao wanakumbwa na mazira haya tujue.

Mheshimiwa Spika, hii inaweza ikawa ni kichekesho lakini yapo. Wapo wanaopigwa, wapo wanaofungiwa na manyanyaso mengine kadha wa kadha. Lakini ugumu wa kujitokeza na kusema mimi nimefanyiwa haya mazira kwa sababu ya tamaduni zile zile za Kitanzania na Kiafrika tunashindwa kufanya hivyo. Lakini huo ndio uhalisia; na kwa sababu hapa tunachoshauri ni kwenda kufanya utafiti basi na hilo ipendeze liingie kwenye utafiti ili watuletee sasa tafiti zinasema nini. Hilo jambo lipo sawa basi kama halipo tutamshukuru Mungu, tutaendelea na lile lile kwamba wanawake na Watoto.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naendelea kurudia tena yale maoni ya Kamati na mimi ni sehemu yake. Kwa hiyo naunga mkono kwa asilimia mia moja. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Benardeta Kasabago Mushashu, atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima ajiandae.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niendelee kuchangia kwenye hoja ya Kamati hizi mbili, Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii pamoja na Kamati ya *USEMI*. Mimi ni mjumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya jamii, kwa hiyo mimi ni sehemu ya mapendekezo yaliyowekwa kule.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nipende kushukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hasan kwa ujenzi mkubwa sana wa miundo mbinu katika elimu na afya. Wote tumeshuhudia ujenzi mkubwa wa madarasa, zahanati, vituo vya afya hata hospitali. Tunasema Mama ahsante sana kwa sababu wewe unawajali Watanzania. Tatizo lililobaki ambalo ni kubwa sana ni tatizo la uhaba wa watumishi ambalo sasa linaanza kufunika na kufifisha kazi nzuri iliyofanywa na Serikali. Serikali imejenga majengo yake pale lakini kama hakuna watumishi inaonekana kwamba hatujapata thamani ya pesa iliyotumika.

Mheshimiwa Spika, daktari leo akifanya makosa wakati anatekeleza kazi zake athari utaziona pale pale Mgongwa ataugua zaidi au atafariki; lakini kwenye mfumo wa elimu kosa likitokea leo athari utakuja kuziona miaka kadhaa baadaye. Kwa hiyo ndugu zangu tunachokiona leo cha kushuka kwa ufaulu wa wanafunzi katika mitihani ya kidato cha nne ni kwa sababu, haya matokeo yanatokana na uchache wa walimu uliokuwepo kwa miaka mingi kadhaa. Pale ambapo kuna walimu wa kutosha ufaulu uko juu na pale ambapo kuna walimu wachache ufaulu uko chini. Kwa mfano, ukiangalia taarifa za ufaulu katika kidato cha nne mwaka 2022 kwenye masomo ya Historia, Geografia, Kiswahili ambapo unakuta upungufu wa walimu ni asilimia 5, 8, 24

hata ufaulu uko juu, kwa sababu unakuta kwenye Kiswahili wameshindwa asilimia nne kwenye historia wameshindwa kama asilimia 46. Hata hivyo, lakini ukienda kwenye masomo ya sayansi na hisabati huko ndio kuna kasheshe wanafunzi wengi wanashindwa.

Mheshimiwa Spika,*Physics* tuna upungufu wa walimu asilimia 77 na wanafunzi wameshindwa kwa 82, *mathematics* wameshindwa kwa asilimia 83 kwa sababu tuna upungufu wa walimu zaidi ya asilimia 71. Lakini ndugu zangu, hebu angalia sasa hivi kwenye shule zetu za kata tumeanza kupata *division one*, tunapata *division two*, tunapata *division three*. Ukiona shule ambazo zimeanza kutoa matokeo mazuri kama hayo ujue kwamba kuna walimu wazuri kwenye shule hizo lakini kule ambapo hakuna walimu hali ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa najiuliza hali hii ikiendelea kwa miaka kumi na tano ijayo watoto wakaendelea ku *fail mathematics*, waka *fail physics*, waka *fail biology*, waka *fail chemistry* itakuaje? Tutawakosa wana sayansi, tunawakosa wanateknolojia ambao tunawahitaji kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika,Je, hawa wanafunzi ambao wamesoma kwenye hizi shule ambazo zina walimu watatu mpaka watano badala ya kuwa na walimu kumi na tano mpaka ishirini, kwa hiyo wamesomeshwa nusu nusu maisha yao yatakuaje? Huyu mtoto anapomaliza kidato cha nne utakuta wamemuandika kwamba aliyeshinda ameandika *pass* na aliyeshindwa ameandika *fail.* Huyu ambaye hakuwa na walimu ni kweli ame-*fail*?

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali na wale wa Baraza la Mitihani waongeze *category* ya tatu, kuwe

kuna *pass, fail* na huyu hakufundishwa; maana huyu unam-*labe*l kwamba ameshindwa miaka yake yote lakini kumbe wewe hukuweza kumpatia walimu wa kumfundisha. Kwa hiyo pamoja na kazi nzuri ambayo inafanywa ya ujenzi wa miundombinu katika afya na elimu nilikuwa na pendekeza yafuatayo;

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tungesimamisha kidogo mambo ya ujenzi. Najua kwamba bado tunacho kibarua cha kujenga majengo mengine kwenye afya na elimu kwa kuwa hayajatosha, lakini ili kusudi tusi-*compromise* ubora, tusimamishe kidogo ujenzi; tutumie hizo fedha ili Serikali itoe vibali, tuajiri watumishi kwenye afya na elimu.

Mheshimiwa Spika, najua Serikali haiwezi kuajiri walimu wote na watumishi wote wanaokosekana kwa kuwa tunao wengi waliosoma wako mitaani. Wengine tunawakuta mpaka kwenye maduka ya wahindi wanafanya kazi ili mradi wanapata kitu chochote cha kujikimu. Tuwaajiri hawa wote kwenye *basis* ya kujitolea. Wakiambiwa waende kujitolea wakakubali Serikali iwalipe posho kidogo kidogo; na pale itakapo tokea ajira basi hao wapate kipaumbele cha kwanza kuweza kupata hizo ajira; na tutakuwa tumeziba lile ombwe la kukosa watumishi na kukosa kutoa elimu bora au afya iliyo bora.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Sekunde thelathini malizia.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, vituo vyetu vya afya havina maji. Tumetembelea miradi mingine tumekuta kwamba wanavuna maji ya mvua. Unakuta kwenye maeneo yetu tunayo mvua lakini

tunashindwa kuvuna maji lakini tunashindwa kuya-*treat*. Maeneo ya hospitali unakuta kuna *nurse* anaamka asubuhi anakwenda kwanza kuchota maji akafanye usafi halafu ndipo arudi kuja kuwahudumia watu. Maji yenyewe yanatoka kwenye visima vifupi, kwa hiyo sio safi na salama.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napendekeza kwa Serikali, sasa hivi kila mradi wa zahanati na vituo vya afya vitakavyojengwa *component* mojawapo ni lazima iwe na mfumo wa maji safi na salama. Tuvune maji tutengeneze ma *tank* tutumie *ultraviolet water disinfection* tuweze ku *disinfect* hayo maji.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja za Kamati zote mbili. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa ajiandae.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja zilizoko mezani. Nawapongeza Wenyeviti wote, nawapongeza pia Waheshimiwa Mawaziri wanao husika na Kamati zote kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, mimi nitajikita kwenye upande wa walimu. Wenzangu wameongea umuhimu wa kuangalia walimu kwa sababu tumeangalia wanafunzi wanavyo-*fail* na wanavyofaulu. Pia tuangalie na walimu wanaotoa huduma, jinsi gani tunaweza kuboresha

huduma kwa walimu ili wafanye kazi vizuri. Kwa takwimu nilizonazo sasa hivi walimu wote wa sekondari na msingi wapo 258,291 lakini sisi wote bado tunaomba Serikali iongeze. Sasa ndio unaangalia jinsi gani ambavyo walimu wengi kama walivyo wanaweza kupata huduma bora.

Mheshimiwa Spika, na hili Serikali ililiona ndio maana ikaanzisha *TAC* sasa mimi leo naomba nijikite kwenye *TAC* kwa dakika zilizobaki. Je, Serikali ilipounda *TAC* ilihakikisha kwamba sheria iliyounda *TAC* inatekelezwa kama ilivyoundwa? Kwa mfano, ningekuwa na muda ningesoma *functions,* yaani kazi za tume ambazo ziko 12; lakini nitasoma mbili tu kwa sababu ya muda. Mojawapo inasema hivi *to appoint, promote and discipline teachers, maintain and administer the teachers' service*. Wamewapa majukumu; hii *TAC* kumuangalia mwalimu la kwanza wamesema kum *appoint*, ku *promote* hii kazi inafanywa?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nataka kusema hivi, sisi kama Kamati tulishaiomba *TAMISEMI* iangalie suala hili.

Mheshimiwa Spika,na mimi leo kwa kuwa ninaunga mkono taarifa nzima ya *TAMISEMI* naomba na mimi nitoe mapendekezo yafuatayo kuhusu hasa *TAC*. Kwanza kabisa ni kusema hivi Serikali iipe nafasi Sheria ya *TAC* ifanye kazi iliyokusudiwa. Mpaka sasa hivi kazi zilizokusudiwa hazifanyiki.

Pili, *TAC* ijengewe uwezo wa kifedha na rasilimali watu ili itekeleze majukumu yake ipasavyo. Tatu, Taasisi ambazo hazihusiki ziache kufanya kazi ya *TAC* kwa mfano *Teachers Profession Board* haina haja ya kuwepo, hiyo kazi yote ingefanywa na *TAC*. Serikali ilete muswada wa

kufuta *Teachers Profession Board* ili majukumu yake yafanywe na *TAC*. Halafu pia *TAC* iwe na *register* ya walimu wote nchini ili mwalimu yeyote anayeingia darasani katika shule zote nchini awe na *license* ya kufundishia kutoka *TAC*.

Mheshimiwa Spika, pendekezo lingine, watumishi wote wanaohudumia Walimu wapelekwe *TAC*. Ukiangalia shughuli nyingi zinazofanywa za Walimu, wale watendaji au watumishi wako nje ya *TAC*. Hata hivyo ukiangalia sheria ilivyo, wako wengine ambao wanapaswa kurudi wafanyie kazi ndani ya *TAC* kwa sababu *TAC* ndio chombo ambacho kilipewa wajibu wa kuhudimia Walimu ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda niulizie swali moja tu, hivi kazi zinazofanywa na *TAC, TAC* inapaswa iwe chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia au iendelee kukaa chini ya TAMISEMI? Kwa sababu ukiangalia kwa mfano kazi yake namba (g) inasema, *supervise teachers in service training programs*. Halafu (h) inasema, *conduct research and evaluation on matters relating to teachers service and advice the Minister accordingly*. Kwa hiyo nafikiria pengine hii pia waiangalie, kule iliko *TAC* ibaki kule kule.

Mheshimiwa Spika, jambo la muhimu ningependa kumalizia, kuna haja tuiombe Serikali ya kuiangalia Sheria iliyoiunda *TAC* na kuhakikisha kwamba inafanya kazi ipasavyo ili iwahudumie hawa Walimu wengi ambao tunaomba waongezwe, wapate nafasi ya kufanya kazi bila kufikiria kwamba sijapanda daraja, sijarekebishiwa mishahara yangu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, kama ingekuwa *TAC* ni binadamu sasa hivi angekwenda mahakamani kuishitaki Serikali kwamba sijatendewa haki kama nilivyopaswa kuwa. Mwisho naiomba *TARURA* iongezewe hela tunahitaji sana fedha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Doroth Gwajima, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohammed Mchengerwa na Mheshimiwa Angela Jasmine Kairuki ajiandae.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia machache kuhusu taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo na Huduma za Jamii.

Awali ya yote natoa shukrani sana za pekee kwa Mheshimiwa Dkt. Stanslaus Nyongo pamoja na Wajumbe wa Kamati hii ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa kazi nzuri waliyoifanya. Amewasilisha taarifa hapa na kwa uongozi wake makini mpaka hapa tulipo, Wizara hii imetimiza sasa takribani mwaka mmoja ikiwa na utekelezaji kama uliowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya na uongozi wake kwa kuiunda hii Wizara na kuweza kuipatia fedha katika mtiririko mzuri hadi katika miezi sita ya kwanza karibu asilimia 50 ya fedha zilishapatikana na kazi ikafanyika kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maeneo yote ya utekelezaji naipongeza Kamati kwa kuibua changamoto

ambazo baadhi wameziripoti hapa na nitazazisemea baadhi ambazo ni za msingi sana katika kuendelea kuifanya Wizara hii kuwa na utekelezaji mzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu wa watumishi, tutaendelea kuomba nafasi za ajira kwa kadri ya uwezo wa Serikali. Hata hivyo, tutakuja na ushawishi ili sekta zote sasa za binafsi pamoja na za umma zione umuhimu wa kuajiri hizi kada za maendeleo ya jamii. Kwa sababu katika zama za sasa na changamoto tunazokwenda nazo kiuchumi, Maafisa Maendeleo wanahitajika katika kila taasisi, lakini maafisa Ustawi wa Jamii nao wanahitajika kila taasisi. Yaani ukiwa na kundi la watu bila ustawi wa jamii matatizo yake ndiyo kama haya tunayoyaona, kwa sababu wale watu wanakuwa bado hawajaandaliwa kubadilika fikra waende na nyakati za sasa.

Mheshimiwa Spika, tunaandaa pia sheria ya taaluma hizi za maendeleo na ustawi wa jamii ili waweze kusajiliwa kama wanataaluma, waweze pia kupata fursa ya kufungua huduma binafsi kama ilivyo huduma za elimu na afya hivyo kuongeza wigo wa wataalam hawa na upatikanaji wa huduma, wananchi waendelee kunufaika sambamba na ajira za Serikali ili walioko kule sokoni waweze kupata hizi ajira.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukatili wa kijinsia na kwa watoto. Imeibuka hapa hoja nzuri sana ya masuala ya ukatili hasa kwa Watoto na pia kwa jinsia, imeonekana na wanaume pia ni wahanga.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kwanza kwa Watoto; kwa upande wa watoto na wanawake tunao mpango wa Serikali tangu mwaka 2017, tulikuwa

tunatekeleza, unaitwa Mpango Kazi wa Kutokomeza Ukatili kwa Wanawake na Watoto. Mpango huu umejielekeza kuangalia mambo mtambuka yakiwemo masuala ya kuinua uchumi wa kaya, jambo ambalo Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hasan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imelitilia mkazo sana, kwa sababu wanawake walikuwa wameachwa nyuma sana kama ilivyoelezwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hapa.

Mheshimiwa Spika, hatuna maana ya kuwaacha wanaume nyuma, tuna maana ya kupiga mbio ili tuvute kundi la akinamama lisogee na wenyewe juu ili huu ukatili unaopatikana kutokana na uchumi, wenyewe urudi chini. Hata hivyo, tunazo programu zingine mbili ambazo zinawalenga jinsia zote wa kiume na wa kike. Moja inamlea mtoto kuanzia miaka 0-8 na nyingine inachukua kuanzia miaka 10-19, kuwaandaa hawa vijana kuanzia umri wa awali mpaka wawe vijana balehe wavuke salama. Huku tukiangazia kuwafundisha elimu, kuepuka magonjwa, lishe nzuri pamoja na fursa za uchumi. Kwa hiyo akinababa tunaomba mtupe nafasi kwanza tuwasogeze sogeze akinamama, mliwaacha nyuma sana, hatuna maana tutawarudisha nyuma, tutakwenda pamoja kupitia hizi programu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango huu wa kutokomeza sasa ukatili mpaka kule vijijini, kuna Kamati za Kutokomeza Ukatili kwa Wanawake na Watoto. Hata hivyo, hawa watoto ni wa kiume pia mle ndani. Sasa suala la akinababa kwamba wanakatiliwa, tunawakaribisha kwenye madawati ya jinsia. Yapo kwenye vituo vyote vya polisi. Ukiona umepigwa na umeonewa karibuni. Sasa hivi tuna mitandao ya akinababa wanaonyanyaswa na wake zao. Tukajiunge

huko tupaze sauti, tufanye utafiti vizuri tuje na program baadaye ambayo inasheheni *data* za kitaalam. Maana hamjitokezi, tunashindwa kujua ukubwa wa tatizo. Kwa hiyo tunawakaribisha kwenye madawati ya kijinsia.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba vita ya kupinga ukatili haitatokea tu kwa mikakati, sera na sheria nzuri, bali kwa mabadiliko ya kifikra, tunaposema tuwe karibu na watoto, tuwe karibu na watoto, tunapoimbaimba *don't touch here and there,* sio kwamba tunachekesha chekesha. Tuimbe wote ili watoto waimbe na sisi, waelewe ishara kama unavyomwambia pale pana nyoka haendi, aelewe kwamba hata maeneo haya na haya mtu akikugusa ukatae. Hatuchekeshi tuko *serious,* kuwa karibu na watoto tuunge mkono. Nawapongeza wotu wanaoimba *don't touch,* moto uendelee mpaka watoto tucheze nao, turuke nao sarakasi, ukutiukuti ili akiguswa kama ambavyo akiona nyoka au simba anakueleza. basi pia iwe ni ishara ya yeye kwenye fahamu zake kuona kwamba hili ni hapana nimwambie baba na mama.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, nashukuru sana kwa Kamati, mapambano yanaendelea, ukatili Tanzania haukubaliki, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mohammed Mchengelwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Angela Jasmine Kairuki na Mheshimiwa Ummy Mwalimu ajiandae.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikupongeze wewe kwa kuiunda Kamati hii ambayo tunafanya kazi nao kwa karibu sana chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Stanslaus Nyongo. Tunawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa

sababu wakati wote ambao tumekuwa tukipokea maoni ya Kamati hii tumekuwa tukifanyia kazi ipasavyo. Unaweza ukaona hakuna hoja nyingi kuhusu Wizara yetu. Zipo hoja tano ambazo Kamati imeibua na moja ambayo Mheshimiwa Festo Sanga ameizungumza mdau wa karibu sana katika sekta hii ya michezo na sisi tunamshukuru sana kwa ukaribu wake.

Mheshimiwa Spika, lazima tukiri kwamba wakati Mheshimiwa Rais anaianzisha Wizara hii alizingatia yale maelezo ambayo Rais wa Awamu ya Kwanza aliyatoa wakati anaanzisha Wizara ya Vijana na Utamaduni. Tutahakikisha kwamba yale maono na fikra za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan tunaziendeleza na tunatambua kwamba anguko la sekta zetu ambazo tunazisimamia hasa Sekta ya Utamaduni ni anguko la Taifa letu. Kwa hiyo tutapambana kuhakikisha kwamba yale maono ya wazee wetu, viongozi wetu waasisi wa Taifa hili tunayalinda na kuyasimamia ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuwashukuru sana wadau katika sekta zetu hasa sekta za michezo, kwa kuona namna ambavyo Serikali inafanya kazi kubwa katika kuboresha sekta hii. Nawashukuru wadau kwa kukubali mapinduzi makubwa ambayo tunakwenda nayo katika Sekta ya Michezo, Sanaa na Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, nilipe taarifa Bunge lako Tukufu kwamba, leo tumepokea taarifa kwamba nchi yetu ni miongoni mwa nchi ambazo zinafanya vizuri sana hasa katika ligi bora Afrika na Tanzania. Kwa takwimu ambazo zimetolewa leo ni ligi namba tano katika ligi bora kabisa Afrika, kidunia Tanzania ni ligi namba 39 kwa ligi ambazo zinafanya vizuri kabisa Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutahakikisha tunaendeleza yale ambayo viongozi wetu Mheshimiwa Rais anatamani yatokee katika sekta hii. Nikiri kwamba tuko katika mapinduzi makubwa kwenye sekta hii na tunatambua kwamba hii ndio sekta ambayo Serikali tunatumia kama nguvu shawishi yaani *soft power* ya nchi. Hivyo, tutahakikisha maelekezo ya viongozi, maelekezo ya Kamati na maelekezo yako tunayafanyia kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, tunayo mambo matano ambayo yameibuliwa, lakini nianze na hili suala la kuhusu Kiswahili (BAKITA) kama ambavyo wewe mwenyewe ulivyosema. Niseme tu kwamba maneno yote ambayo uliyazungumza yaliyowasilishwa ni maneno fasaha na sanifu kama ambavyo yamewasilishwa kwa mujibu wa sarufi ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, katika Kiswahili kuna kauli tano za msingi zinazoathiri maumbo ya vitenzi, kauli hizi ni kama ifuatavyo:-

(a) Kauli ya kutenda;

(b) Kutendwa;

(c) Kutendewa;

(d) Kutendana; na

(e) Kutendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sarufi za Kiswahili zina kanuni ya kubadilisha vitenzi kuwa nomino na katika kukamilisha mchakato huo, kiambishi "u" huwekwa mwanzoni na kiambishi "g" huwekwa mwishoni. Kwa hiyo yale ambayo

yamezungumzwa ni Kiswahili fasaha na sanifu kama ambavyo naomba nielekeze hapa. *(makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya Kamati iliibua mambo kadhaa, jambo la kwanza, ilikuwa ni msingi wa uibuaji wa vipaji; jambo la pili, ni ujenzi wa viwanja kwa ushirikishwaji wa wadau; jambo la tatu, ni kuhusu vazi la Taifa; jambo la nne ni kuhusu mdumdo wa Taifa *(beats);* na jambo la tano, ni kuhusu Chuo chetu cha Malya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Festo Sanga aliuliza kuhusu hatua ambayo Serikali imefikia katika ujenzi wa viwanja. Sisi kama Serikali tumefanya kazi kubwa sana ya kuwashirikisha wadau katika kuibua vipaji. Hata hivyo, nichukue fursa hii katika kushukuru Maafisa Utamaduni kote nchi nzima ambao wamekuwa wakifanya kazi kubwa na kazi nzuri sana ya kutambua vipaji katika maeneo yetu. Tunatambua katika vijiji, vitongoji, kata na wilaya kuna vijana wengi sana wenye uwezo na wenye vipaji vikubwa, lakini hawatufikii kwa ukaribu kwa sababu ya maeneo waliyopo. Tumekwishawaagiza na tumefanya vikao kadhaa na Maafisa Utamaduni ambao tumewekeana mikakati ya namna gani tunaweza kwenda kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaibua vipaji.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nitumie fursa hii kuwapongeza sana Watanzania ambao wanatumia vipaji vyao kama mtaji wao hasa wale Ramadhan *Brothers* ambao wamefanya kazi kubwa kutangaza nchi yetu, kutangaza utalii wa Tanzania, vile vile na wadau wengine wadau wengine ambao wamekuwa wakiibuka, akiwemo bwana Mandoga amekuwa akifanya kazi nzuri, nje ya mipaka ya Tanzania, anaitangaza vizuri Tanzania. Hata hivyo sisi kama wizara tunawapongeza sana kwa

kazi kubwa na kazi nzuri ya kuendelea kuitangaza nchi yetu kupitia vipaji walivyo navyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekwishaanzisha mchakato wa mtaa kwa mtaa. Tunatambua kwamba katika nyakati ambazo tulikuwa tunaanza mchakato huu hatukuwa na bajeti ya kutosha. Tunaishukuru Kamati kwa kuendelea kutupigania, lakini tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuridhia. Basi tunaamini kabisa katika bajeti ijayo tutakuwa tumeweka kifungu maalum kuhakikisha kwamba tunakwenda kwa kasi sana kuhakikisha kwamba tunafika kila mtaa. Dhamira yetu na dhamira ya Mheshimiwa Rais ni kwenda mtaa kwa mtaa kusaka vipaji, vipaji vya mpira lakini na vipaji vingine.

Mheshimiwa Spika, eneo hili la ujenzi wa viwanja, nichukue fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa ushirikiano wa karibu ambao tumekuwa nao. Pia nichukue fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu, tunatambua kwamba inawezekana huko nyuma hatukuwa na mipango mizuri, inawezekana ndio sababu ya kwa nini tumechelewa kuhakikisha mchakato wa ujenzi wa viwanja unaanza. Hata hivyo, nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba mipango imekamilika, michoro imekamilika na tunaishukuru Wizara ya Fedha kwa kuridhia sisi kuendelea kwa hatua ya kutafuta mkandarasi na hatua nyingine.

Mheshimiwa Spika, nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba zabuni ya ujenzi wa uwanja wa Dodoma tayari imekwishatangazwa. Vile vile dhamira yetu sisi kama Serikali, kama Wizara ni kwenda kujenga uwanja wa kisasa ambao Afrika hakuna. Kwa hiyo tutajenga uwanja wa kisasa kweli kweli hapa Dodoma na Zabuni

tumekwishaitangaza. Kwa hiyo mategemeo yetu mwezi wa tatu tutamkabidhi Mkandarasi *site* kwa ajili ya kuanza ujenzi wa uwanja wa mpira wa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa viwanja vya sanaa, tayari zabuni tumeitangaza na hata Waheshimiwa Wabunge wanaweza kuingia kwenye tovuti ya Serikali wakaweza kuona zabuni ya uwanja wa sanaa tayari imekwishatangazwa. Hata hivyo, Mkandarasi wa ujenzi wa viwanja changamani; vya Dodoma pamoja na Dar es Salaam tayari amekwishapatikana. Kwa hiyo, tunategemea wakati wowote mchakato wa ujenzi utaanza. Kwa hiyo, naomba niendelee kuwatia matumaini Watanzania. Sisi katika Wizara hii tumekwishakubaliana kufanya kazi kwa bidi, tumekubaliana mimi na wasaidizi wangu kufanya kazi usiku na mchana.

Mheshimiwa Spika, tutawathibitishia Watanzania kwamba yale mapinduzi ambayo wanatamani kuyaona yatatokea katika nyakati ambazo Rais wetu wa Awamu ya Sita, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amedhamiria kuleta mabadiliko hayo.

**SPIKA:** Sekunde thelathini, kengele imeshagonga.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nitoe taarifa tu kwamba ule mchakato wa ujenzi wa shule 56 tayari umekwishaanza. Tumekwishaanza kule Tabora na tutakuwa na shule saba za mfano za kuanzia na naamini kufikia mwezi wa Machi au Aprili, Mkandarasi atakuwa amekwishapatikana kwa kuwa tayari wizara ya Fedha imekwishatupatia fedha za kuanzia. Tunamshukuru sana Waziri wa Fedha na Mipango kwa kazi kubwa na nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema tu kwamba, Watanzania wana matumaini makubwa sana na Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan na sisi katika wizara tutahakikisha tunafanya kazi usiku na mchana katika kuleta mabadiliko makubwa katika Sekta hii ya Michezo, Sanaa na Utamaduni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja ya Kamati iliyotolewa mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Angela Jasmine Kairuki, atafuatiwa na Mheshimiwa Ummy Mwalimu na Mheshimiwa Profesa Mkenda Adolf ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami niungane na Wabunge wengine wote ambao wamepongeza Kamati hizi mbili na kipekee nipongeze Kamati yangu ya Utawala na Serikali za Mitaa kupitia kwa Mwenyekiti Mheshimiwa Chaurembo na Wabunge wote kwa taarifa hii nzuri, ya kina, ambayo kwa kweli maudhui yake yatatusaidia sana pamoja na ushauri na maoni mbalimbali ambayo wameweza kuyatoa.

Mheshimiwa Spika, nikienda katika mapendekezo yaliyosomwa na Mwenyekiti, lile la kufanya uchunguzi wa kina kuhusiana na suala zima la migogoro ya ardhi lile lililoko katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma. Nipende kusema kwamba tunapokea mapendekezo haya, tutayatekeleza na vile vile tutazingatia wakati wa kufanya uchunguzi huu wa kina, kuhakikisha kwamba watumishi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma hawahusiki katika timu itakayofanya uchunguzi. Hata hivyo tumewasikia hapa

Wabunge lakini pia Kamati ikieleza kwa kirefu kuhusiana na suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *TARURA,* tunashukuru kwa namna ambavyo maoni na mapendekezo yaliyojitokeza na hasa kutokana na suala zima la ufinyu wa bajeti. Nipende kusema kwamba suala hili tumelipokea, tumekuwa tukiendelea kuwasiliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha, tunalifanyia kazi ili kuendelea kuona ni kwa namna gani *TARURA* itaweza kuongezewa fedha nyingi zaidi ili kuhakikisha kwamba wanaweza kuwa na bajeti inayowatosheleza. Kwani kwa sasa tuna bajeti ya shilingi bilioni 838 na mahitaji bado ni makubwa. Ukiangalia bado tuna vikwazo vingi katika wilaya zetu na bado tunahitaji fedha nyingi kwa ajili ya kufungua na kuondoa vikwazo hivyo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati. Kwanza ningependa kusema, hakuna upendeleo katika utekelezaji wa miradi hii na pili, nadhani kuna mkanganyiko kidogo, wako ambao walikuwa wanasema kwamba miradi hii haiangalii halmashauri ambazo ni ndogo ndogo. Nipende tu kusema kwamba miradi hii ya kimkakati inatekelezwa kwa vigezo mbalimbali. Tumekuwa tukishirikiana na Wizara ya Fedha katika kuhakikisha kwamba miradi inayoibuliwa na halmashauri ile ambayo inakidhi vigezo basi ndiyo miradi ile ambayo inaweza kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo changamoto kubwa ambayo tuliiona, unajikuta katika baadhi ya halmashauri walikuwa Maafisa Mipango wengine hawana uwezo mkubwa sana wa kuandaa maandiko ya miradi hii mikubwa ya kimkakati na ndio maana pale nilisikia hoja

ya nadhani Mheshimiwa Kwagilwa, akisema kwamba nyie hamna uwezo wa kuandaa sijui moja, mbili, tatu, sijui mpaka muandaliwe mwongozo.

Mheshimiwa Spika, siyo kwamba tumeandaliwa mwongozo, ni pamoja na kutoa mafunzo kwa Maafisa Mipango wetu wa Halmashauri ili waweze kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kuandaa maandiko zana, kufanya upembuzi yakinifu pamoja na usanifu wenyewe pamoja na masuala mengine kadha wa kadha. Hii ni kuhakikisha kwamba miradi itakayopelekwa Wizara ya Fedha ili iweze kuzingatiwa, basi kweli iwe ni miradi ambayo itakuja kuleta thamani halisi ya fedha badala ya kuwa tu na miradi yoyote kama ambayo walikuwa wanakopiana zaidi kama miradi ya stendi na miradi ya masoko.

Mhesimiwa Spika, unakuta Halmashauri kama ya Ukerewe kumbe huenda wangeweza kuja na mradi mkakati wa kuweza kutengeneza chakula cha Samaki, mradi wa kutotolesha vifaranga vya Samaki, nyavu za kuvulia samaki na vitu vingine kadha wa kadha. Kwa hiyo, siyo kwamba tumekuwa tukipendelea au kutafuta watu ambao hawahitajiki.

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, huu mwongozo tunaandaa pia na suala zima la *special purpose vehicle*. Nitoe tu mfano wa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, pale wana Kiwanda cha Chaki pamoja na Halmashauri nyingine. Sasa je, wanapokuwa wamefungua kampuni, au wanapotekeleza mradi wa aina hiyo, wautekeleze kwa mfumo gani?

Mheshimiwa Spika, na lenyewe hilo ukiangalia dhana nzima ya suala la *special purpose vehicle* suala jipya

kidogo kwetu. Kwa hiyo, ni vema pia na lenyewe tupate maelekezo ya kina kupitia mwongozo ambao Halmashauri zetu zitaweza kuuelewa na kuweza kujua ni kwa namna gani wanaweza kutekeleza. Kwa hiyo, kwenye hili tutaendelea nalo na siyo kwamba watu hawana uwezo wa kuweza kufanya hilo, lakini tunataka tujenge uwezo mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba Mungu niweze kupata muda wa kutosha kwa suala la upungufu wa Walimu. Wabunge wamelieleza kwa uzito mkubwa. Ukiangalia tuna upungufu wa walimu zaidi ya 238,000. Tunashukuru kwamba kupitia jitihada za Mheshimiwa Rais, ndani ya muda mfupi sana tangu ameingia, utaona alipoingia tu tuliweza kupata kibali cha kuajiri walimu 9,800. Siyo hilo tu, tunaendelea na jitihada hizo na kuhakikisha kwamba tunaendelea kujairi kwa mujibu wa mahitaji na kwa kuzingatia uwezo wa kifedha wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mkenda ataongea kwa kina kuhusiana na Mwongozo wa Walimu wanaojitolea. Tumefurahi kuona kwamba Wabunge pia wameona hili litakuwa na mvuto na litaweza kusaidia sana katika kupunguza changamoto ya Walimu wetu. Pia wamejitokeza wadau wengi ambao wako tayari kushirikiana na Serikali katika kuona ni kwa namna gani tutakapoanza sasa kuendelea kuweka mfumo sahihi namna gani Walimu wanaojitolea waweze kujitolea, wako tayari kuweza kutuunga mkono. Kwenye hili, tayari tumeshaanza mashauriano na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete pamoja na *UNICEF* na wengine pia ambao wamekuwa tayari kuunga mkono jitihada hizi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja ya *DMDP II* na kwamba mradi umechelewa. Napenda tu kumweleza

Mheshimiwa Bonnah, Wabunge wa Dar es Salaam na wengine ambao wanaufuatilia mradi huu, tayari *concept note* tulishaiandika, tumeshaiwasilisha Benki ya Dunia, na kwa sasa tunaendelea na majadiliano na na Benki ya Dunia kupitia Wizara yetu ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mradi wa *TACTIC,* na yenyewe pia ilijitokeza kwamba ni miji ile ile inayopewa miradi ya mikakati, na wenyewe tena wanapewa mradi huo wa uboreshaji wa miundombinu ya miji ya kimkakati ile 45. Napenda kusema kwamba miradi hii iliibuliwa kwa kufuata vigezo na hasa vigezo vya kupata wanufaika hivi vilitokana na taarifa ya idadi ya watu, na pia ongezeko la ukuaji wa idadi ya watu kwa mujibu wa taarifa ya Tume yetu ya Takwimu ya *NBS* na tumeweza kuzingatia hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwa nini mradi umechelewa? Kulikuwa kuna majadiliano mbalimbali na Benki ya Dunia. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, na leo hii Mheshimiwa Naibu Waziri Silinde ameweza kujibu maswali hapa kwamba kuanzia mwaka huu wa fedha tutaanza na wale waliopangiwa katika awamu ya kwanza miji 12, awamu ya pili tuna miji 15 na awamu ya tatu tutakuwa na miji 18. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote, ifikapo 2025 mradi huu wa *TACTIC* kwa miji hiyo 45 yote itakuwa imeshatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwatoe hofu kwa wale ambao wako katika makundi ya mwisho. Anayecheka mwisho ndiye anayecheka sana. Kwa hiyo, kama kuna hofu nyinginezo huko, wale ambao mko mwishoni mwishoni pia naamini mtaweza kucheka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa kulikuwa kuna ile hoja ya madarasa 8,000 kuhamishwa, nadhani ilikuwa hoja ya Mheshimiwa Kunti. Napenda kutoa ufafanuzi kidogo kwenye hili. Katika yale madarasa 8,000 tulikuwa tunahangaika na changamoto ya wanafunzi 1,076,037 ambao wameanza Kidato cha Kwanza tarehe 9 mwezi Januari. Tulikuwa tuna siku 75 tu za kuweza kutekeleza mradi. Sasa kweli watu walituletea shule nyingine mpya, kwa nini badala ya madarasa haya manne, na haya manne kwa shule hii tunisiyaunganishe nipate madarasa nane nikajenge shule mpya moja? Kwa nini limeshindikana?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Dakika moja malizia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, tulipata mapendekezo ya shule 465, na ili shule iwe kamili inatakiwa iwe na walimu siyo chini ya 11. Kwa hiyo, tulitakiwa tuwe na Walimu wapya zaidi ya 5,115 ndani ya miezi miwili. Wote tunajua taratibu za ajira na masuala mengine, kwa muda huo isingeweza kupatikana, lakini vilevile miundombinu mingine siyo madarasa tu, kuna maktaba, maabara, pamoja na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, niwatoe hofu kwamba kupitia mradi wetu wa *SEQUIP* Februari hii mpaka June tutajenga shule 184 na tutaendelea kujenga shule nyingine zote za kata mpaka tufikishe idadi ya shule 1,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii ya Kamati na mapendekezo yote yaliyopendekezwa tutayatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda na Mheshimiwa Jenista Mhagama ajiandae.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma ya Maendeleo ya Jamii inayoongozwa na Mheshimiwa Mbunge Stanslaus Haroon Nyongo kwa maoni na ushauri wao katika kuboresha utoaji wa Huduma za Afya kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nami nasema kwamba naishukuru sana Kamati, hawakueleza mambo mengi, sana sana mambo ambayo yameibuka katika maazimio ya Kamati au maoni na ushauri wa Kamati ni mambo matano na nitayatolea ufafanuzi kama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu utengwaji wa bajeti kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Wizara na kutekeleza miradi ya maendeleo, tumelipokea, na niseme kwamba Serikali naendelea kutoa fedha nyingi kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za sekta ya afya na pia kwa miradi ya maendeleo. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ambaye kwa kweli huduma za afya ni moja ya vipaumbele vyake. Kwa hiyo, hili suala tunahakikisha kwamba fedha zitakuja.

Mheshimiwa Spika, pia tuliahidi Bunge lako Tukufu tunapata pia fedha za maendeleo kutoka kwa wadau wa maendeleo, nazo tutazisimamia kikamimilifu kuhakikisha kwamba sambamba na fedha zinazopitishwa na Bunge, lakini pia fedha hizi za wadau wa maendeleo nazo zinatumika kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ya Kamati ilikuwa ni kuhakikisha kwamba tunaimarisha utendaji wa Taasisi ya Dawa na Vifaa Tiba ili kuzuia uingizwaji wa bidhaa bandia za chakula dawa na vipodozi. Hili nalo tunalipongeza na tumetunga kanuni ambayo inasimamia uingizaji wa dawa katika mipaka 15.

Mheshimiwa Spika, naomba nikiri. Kweli tunayo changamoto kwa sababu ya mipaka yetu isiyo rasmi. Kwa hiyo, tupo katika mipaka rasmi, hivyo ni kweli mipaka ambayo siyo rasmi dawa zinaingizwa na vifaa tiba ambavyo havina ubora. Tumeamua kung'atua madaraka ya *TMDA* kwa watu ambao ni wataalamu wa dawa katika ngazi za Halmashauri, na wenyewe tumewapa vitambulisho, wanaweza wakafanya pia ukaguzi wa dawa na vifaa tiba katika maduka ambayo yako mitaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo tumeliona ni kuimarisha utendaji wa Baraza la Wafamasia. Sasa hivi Baraza la Wafamasia wanafanya ukaguzi wa maduka ya dawa na sehemu za kuhifadhi dawa, *TMDA* naye anafanya. Kwa hiyo, tunataka Baraza la Wafamasia wao wasimamie fani; wataalamu wa famasia, kama Baraza la Madaktari na Baraza la Wauguzi yanavyofanya, halafu tumwachie *TMDA* mamlaka ya dawa na vifaa tiba kazi ya kukagua *premises* (maduka ya dawa). Kwa hiyo, Baraza la Famasia akienda kwenye famasi au sehemu

yoyote anamwangalia mwanataaluma, siyo suala la dawa, vifaa na vifaa tiba. Tunaamini kwa hatua hii pia itaimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa dawa na vifaa tiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo pia limeelezwa na Kamati, na Mheshimiwa Hhayuma ambaye pia ni mtaalamu wa eneo hili, ni kuhakikisha kwamba tunaratibu udhibiti wa chakula na vipodozi ndani ya Serikali. Suala hili lilifika kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, tayari linafanyiwa kazi ndani ya Serikali kati ya *TBS* na *TMDA*. Naamini Serikali itafanya maamuzi kuhusu udhibiti na usimamizi wa chakula na vipodozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli anachokisema Mheshimiwa Hhayuma na Kamati, dawa na vipodozi vinauzwa katika sehehmu moja. Pia sasa hivi tumeona kuibuka kwa *supplements, vitamins;* sasa *regulator* siyo tena mtu ambaye anasimamia *public health*. Kwa hiyo, ni jambo ambalo tumeliona ndani ya Serikali tunaamini kwamba suluhisho litapatikana.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni la *MSD* (bohari ya dawa). Tunaishukuru sana Kamati, na kipekee kwa kweli tunapongeza maboresho ambayo yameanza kuonekana ndani ya *MSD,* na Kamati sasa inatushauri tuweke mikakati thabiti ya kushirikisha sekta binafsi katika uwekezaji wa Viwanda vya Dawa na Vifaa tiba vinavyozalishwa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, jambo hili tunalikubali. Nami nilishawaelekeza *MSD, as long as* dawa au kifaa tiba kinazalishwa na kiwanda cha ndani chenye ubora na bei; na bei tumesema kama dawa hiyo au kifaa tiba hicho kinazalishwa na kiwanda cha ndani cha Tanzania, bei

yake imezidi kwa asilimia 15 wanunue bidhaa hiyo ambayo inazalishwa ndani ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kutoa mfano. Tumeanza kununua *IV fluids* kutoka *Kairuki Pharmaceticals* badala ya kununua kutoka Uganda. Nitoe rai kwa wazalishaji wa ndani wa dawa na vifaa tiba. Naogopa isije kutokea tukapiga marufuku tusinunue kutoka nje ya nchi, lakini labda hawana uwezo au *capacity* ya kukidhi mahitaji ya dawa na vifaa tiba ya ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nilikutana nao mwezi Januari, tumekubaliana. Kwa hiyo, tutafanya tathmini; huyu uwezo wake ni kuzalisha dawa zipi na kiasi gani? Tukishajua tumeshamwelekeza *MSD,* marufuku kuleta dawa kutoka nje ya nchi kama dawa hiyo inapatikana ndani ya nchi na ina ubora na pamoja na suala la gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wazalishaji wa ndani wa viwanda vya dawa pia wametuambia, tukinunua nje ya nchi, tunawapa *Letter of Credit,* ndani ya nchi hatuwapi chochote. Kwa hiyo, suala hili tayari nimemwomba Waziri wa Fedha, tutakutana nao. Hata kama hatutawapa *Letter of Credit,* lakini tuangalie kama tunaweza tukawapa *advance amount* ili waweze sasa kujipanga vizuri kununua *raw material* ili waweze kuzalisha dawa na vifaa tiba ambavyo vinahitajika ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limeelezwa na Kamati ni kuimarisha tafiti za ubora athari na matumizi salama ya tiba asili chini ya *NIMR, Medical Research Institute*, Taasisi ya Magonjwa ya Binadamu. Tunapokea ushauri wa Kamati, tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunaona ni kweli, kuna ujanja ujanja. Utaambiwa dawa hii inatibu saratani, dawa hii inatibu kisukari, dawa hii inatibu magonjwa ya moyo, lakini ukiangalia ufanisi *(efficacy)* wake, tumeona Watanzania pia wanaibiwa. Ila kwa kweli tunakubali kwamba wapo Watanzania ambao wanatengeneza tiba asili ambazo zingeweza kusaidia na kuokoa maisha ya wengi. Kwa hiyo, tutaongeza fedha za ndani kwa *NIMR* kama kamati ilivyo tushauri ili weweze kufanya utafiti.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limeelezwa na kaka yangu Mheshimiwa Kakunda, nimelipokea kuhusu michoro ya vituo vya kutoa huduma za afya, tutaliangalia. Naomba nitahadharishe, tujengeni miundombinu ya kutoa huduma za afya kwa kuangalia mahitaji ya sasa na mahitaji ya miaka 20, 30 inayokuja. Maana sasa hivi jinsi unavyoboresha huduma, ndivyo wananchi wanavyodai huduma bora zaidi, ndivyo wananchi wanavyodai huduma za ngazi ya juu zaidi kuliko zahanati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakubaliana na kaka yangu Mheshimiwa Kakunda katika suala la gharama, lakini gharama hii itakidhi mahitaji ya sasa ya kutoa huduma za afya kwa kizazi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** dakika moja Mheshimiwa Waziri umalizie.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Kakunda tumepokea ushauri wako, tutaufanyia kazi, tutatoa michoro kwa kushirikiana na TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalize kwa kukushukuru sana lakini kuishukuru Kamati yetu ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, wanafanya kazi kubwa na nzuri sana ya kutushauri, nasi tunawaahidi kwamba tutaboresha utoaji wa huduma za afya *especially* tunapoelekea kwenye Bima ya Afya kwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, atafuatiwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama na watoa hoja wajiandae.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii. Nami naungana na wenzangu wote kupongeza Kamati zote mbili kwa kazi nzuri na ushauri mzuri sana na pongezi kubwa kwa Kamati inayotusimamia, Kamati ya Huduma za Jamii chini ya uongozi wa Mheshimiwa Nyongo, tunafanya nao kazi vizuri sana. Wanatuelekeza na kutushauri na kwa kweli hapa tulipofika kwa sehemu kubwa ni kufanya kazi pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nampongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wizara ya Elimu tunajivunia kuona kipaumbele cha elimu katika Serikali. Nitoe mifano miwili tu. Mfano, sasa hivi tunazungumzia kujenga *VETA* katika wilaya zote Tanzania, shughuli ambayo inaanza kabla ya mwisho wa mwaka huu, nadhani mwezi huu wa Pili tutakuwa tumeanza kazi hiyo. Hazina tayari wametuambia tunachukua fedha zote, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ametuambia na kazi itaanza.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunasambaza Kampasi za Vyuo Vikuu katika mikoa 14 ambayo ilikuwa haijawahi kupata Kampasi ya Chuo Kikuu. Haya yote ni maelekezo ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nawapongeza sana na ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao, kwa kweli tutazingatia. Tumekuwa tukichukua kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi sana ya kusema kwa sababu mengi ya ushauri tutayabeba kama ambavyo tumeyapokea. Ila kuna jambo moja kubwa ambalo limezungumzwa napenda nilisisitize, hili ambalo tumelisikia wote hapa Bungeni kuhusu umuhimu wa walimu. Imeelezwa umuhimu wa kuwa na walimu wa kutosha na umuhimu wa walimu katika elimu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alilianzisha asubuhi kwa kueleza umuhimu wa kuwaenzi walimu wetu, nasi hilo tunalizingatia. Kama mnavyojua, Rais wetu tangu aingie madarakani, wakati tulikuwa tume-*freeze employment* kwa ujumla alipoingia madarakani tu tumeanza kuona, kama alivyosema Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ajira za Walimu zimeanza na zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, tumekamilisha mwongozo sasa hivi wa kuhakikisha kwamba Walimu wanaojitolea tunaweza tukawa-*engage* vizuri kwa ajili ya kuchangia idadi ya walimu ambao watatosha kutoa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaangalia vilevile suala la ufundishaji wa walimu. Katika mageuzi ya elimu ambayo yanakuja, jambo ambalo ni wazi kwamba tutakuwa

tunazingatia sana suala la ufundi stadi; hawa wenzetu wa Zanzibar wanasema mafunzo ya amali. Kwa hiyo, tutangalia vilevile tunavyo-*train* walimu kuelekea huko. Nilikuwa Mtwara juzi, kuna hili moja limesemwa, nimeangalia Vyuo viwili vya Ualimu vya Mtwara. Kimoja kinaitwa Mtwara Kawaida na kingine kinaitwa Mtwara Ufundi, vimekaa vimeshikana vimepakana, lakini vyote ni Mtwara kawaida, kwa sababu ufundi haufundishwi.

Mheshimiwa Spika, tutarudi huko kwenye ufundi na kuangalia namna ya kufanya vyuo vyote viwili iwe Kampasi moja ambayo inafanya kazi na Vyuo Vikuu lakini kwa ajili ya kufundisha masomo ya kuandaa walimu kwa ajili ya Mafunzo ya Elimu ya Amali kwa sababu na fursa ile ni kubwa, karakana zipo lakini hazijatumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wake, suala la kuwaenzi walimu ni zuri sana. Napenda niseme hivi kwa sababu najua walimu wengine watakuwa wanasikiliza. Wamesikiwa Waheshimiwa wabunge wanavyowasemea vizuri, wamemsikia Mheshimiwa Waziri Mkuu anavyowasemea vizuri, tunajua kabisa kwamba hapa karibuni kumekuwa na *clip* zinatoka ambazo zinasababisha mpaka watu waanze kuwa na jicho tofauti kuhusu walimu. Walimu wetu popote mlipo sikilizeni Waheshimiwa Wabunge wanavyowasemea na kuwatetea na hasa tukizingatia alichosema Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kazi inayofanywa na Walimu wetu ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kuna mwalimu mmoja mfano *clip* yake inazunguka na napenda nimtaje hapa, anaitwa Mwalimu Yusuph Mohamed Yusuph. Huyu ni Mwalimu wa Shule inaitwa Ikorongo, iko Wilaya ya Serengeti Mkoa wa Mara. Huyu Mwalimu anaitwa Yusuph Mohamed Yusuph,

maarufu kama Yusuph Pangoma. Ana ubunifu mkubwa sana wa kufundisha, na ninatarajia wakati wa kusoma bajeti tutamwalika hapa kwa ajili ya kupewa pongezi na walimu. Wako walimu wengi sana wanafanya kazi kubwa, wanajitolea na ubunifu kwa kutegemea mazingira yale yale ambayo wanafanyia kazi. Tutaendelea kuwaenzi sana walimu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi *clips* ambazo zimekuwa zikizunguka kama Kamati yetu ilivyosema na Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyosema hapa, kuna suala kubwa la malezi shuleni na suala la maadili ambalo ni jukumu letu vilevile. Tunashirikiana na Wizara mbalimbali; tunashirikiana na Mheshimiwa Dkt. Gwajima, TAMISEMI, tunashirikiana na Wizara mbali mbali chini ya uongozi wa Waziri Mkuu, lakini ndani ya Wizara yetu ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tuna jukumu la kufanya vilevile.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kusema, pamoja na kwamba tumeona hizo *clip,* walimu wetu wengi karibia wote ni wazuri sana na wanalea Watoto wetu vizuri sana kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu, tuendelee kuwaenzi walimu hao.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa wale wachache ambao wanakiuka maadili, unyanyasaji wa watoto kwa namna yoyote ile, kesho Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Francis Michael atatangaza sasa namba ambazo zitatumika kama *call center* ili kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa kwamba hivi sisi tutaripoti wapi kama tukiona matukio kama haya.

Mheshimiwa Spika, mtu yeyote hasa walimu wengine ambao mkiona kuna unyanyasaji wa aina yoyote, vitendo vya uvunjaji wa maadali katika shule yoyote

hapa nchini, unapiga ile namba *whether* unataka jina lako litajwe au lisitajwe, Serikali ipo kila mahali mpaka vijijini na kwenye vitongoji. Tukipata hiyo namba sisi tutafuatilia na kuhakikisha kwamba tunadhibiti hali kama hiyo na kuhakikisha kwamba hivi vitendo vichache sana ambavyo vinaondoa taswira kwa sababu sisi wenyewe tunafundisha kwamba samaki mmoja akioza kwenye tenga wote ameoza. Kwa maana hiyo hawa wachache wanaoharibu taswira ya walimu tutahakikisha kwamba tunawadhibiti na kwa ajili ya kulinda watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limezungumzwa sana hapa ni umuhimu wa hasa masomo ya hisabati na sayansi, kwa hakika. Kwa kuangalia matokeo, tukiangalia *trend* kwa mfano *form four* sio kwamba imeenda chini ukilinganisha na miaka mingine lakini bado hairidhishi. Tungependa ufaulu uongezeke hasa katika masomo ya sayansi na hisabati na nitawakumbusha tu Waheshimiwa Wabunge, ninyi mliridhia hapa Bungeni kuanzisha *scholarship* maalum kwa wanafunzi wanaofanya vizuri sana kwenye masomo ya sayansi. Wakimaliza *form six* wanasomeshwa na Serikali *full time,* baadaye ile *scholarship* tumeiita *Samia Scholarship*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ilikuwa ni njia mojawapo ya kuhakikisha kwamba tunahimiza watu wasome na tumesikia na tunapata mrejesho mashuleni kwamba sasa watoto wanasema ili kumwondelea mzazi wangu shida ngoja nisome sayansi na nitajitahidi ni faulu vizuri sana ili nihakikishe kwamba kweli nipata *scholarship* ya kwenda kusoma.

Mheshimiwa Spika, tayari wameshapata *scholarship*, wapo vyuoni, tutakuwa na siku moja ya kutangaza na kuonesha majina, kuonesha jinsi tulivyowachagua kwa sababu tulisema tutawachagua kwa njia ya haki kabisa kuhakikisha kwamba kila moja ambaye anaweza kupata nafasi hiyo atapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile tutazingatia katika hii walimu wa kujitolea, mwongozo na vilevile ajira zinazokuja kuhakikisha kwamba tunatoa kipaumbele kwa ajili ya walimu wa sayansi na hisabati kwa sababu kwa kweli maeneo hayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya elimu ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa fursa hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri, swali moja tu. Hizi taarifa za huyu Mwalimu Yusuph kutoka Serengeti umezipataje?

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Mheshimiwa Spika, huyu mwalimu nimezungumza naye vilevile na nawasiliana naye.

**SPIKA:** Aah, yaani yeye alikupigia akakuambia kuhusu ubunifu wake ama alijirekodi ukaona kitu? Ama ni kata iliripoti? Shule iliripoti? Kata? Yaani taarifa zake ulizipataje? Ni hicho tu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Mheshimiwa Spika, aliwasiliana na mimi mapema sana na baadaye niliziona hizo ambazo zimekuwa *recorded* anavyofundisha, nikawasiliana na wenzetu wa TAMISEMI

tukam–*track down,* tukahakiki kweli ni mwalimu na mimi nipo *constant in touch with him. (Makofi)*

**SPIKA:** Yaani swali langu…, nafikiri nimekuelewa, kwamba ulianza kwa kuona ndio mkawasiliana. Ulianza kwa kuona. Ahsante sana.

Kwa hiyo, nadhani mawasiliano ni muhimu sana, lakini pia naamini hiyo inafungua wigo mpana kuonesha namna ambavyo Wizara inayo utayari wa kuwatambua wale ambao ni wabunifu katika ufundishaji wao ikiwa ni pamoja na huyu ambaye tayari ameshaonesha hiyo njia ili na wengine wajifunze huko haya aliyoyafanya yeye. Basi nadhani mtafute namna ili awafikie na walimu wengine na wenyewe waanze kutafuta ubunifu wao pengine wataonwa na Mheshimiwa Waziri. Jambo zuri sana, mimi nawapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, ajiandae Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**WAZIRI WA NCHI, OFIS YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, na mimi nianze kwa kuungana na Waheshimiwa Wabunge, lakini Waheshimiwa Mawaziri wenzangu kuzipongeza sana Kamati na kipekee nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati wa USEMI, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakika naomba nikiri Kamati hiyo imetusaidia sana Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kutekeleza majukumu yetu

sawa sawa. Kwa kweli tunawashukuru na tunawapongeza na ninaahidi kuendelea kuwapa ushirikiano wa karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiujumla nilipongeze sasa Bunge na Waheshimiwa Wabunge na niendelee kutuma ujumbe kwa wananchi wa Tanzania kwamba Bunge letu hili na Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakishauri mambo ya muhimu na mambo ya msingi na pale yanapofanyiwa kazi yameweza kuzaa matunda mazuri na yatatoa *relief* kubwa sana kwa maisha ya kila siku ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, leo Wajumbe wa Kamati na Taarifa ya Kamati ya USEMI ilizungumzia kuhusu mfumo wa *recruitment* kwenye ajira hapa nchini. Hata wakati wa bajeti, Bunge lako tukufu lilitupa maelekezo Serikali kuangalia ni kwa kiasi gani tunaweza tukawarahisishia watoto wa Kitanzania kufikiwa na huduma hii ya usaili katika maeneo waliopo, kuliko kuwakusanya hapa Dodoma kila siku na kusababisha hasara kwa wazazi. Wakati mwingine watoto wamekuwa wakija hapa mara nyingi, anafanya *interview* sita, hajafanikiwa, anapoteza fedha na anaendelea kuitia umaskini familia yake.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan na ndani ya Wizara yetu tumesikiliza kwa makini hoja hiyo na tumekwisha kuiripoti ndani ya Kamati na tumefanya maamuzi yafuatayo; jambo la kwanza, ile *database* ya kutunza matokeo ya watoto waliofaulu tumei-*upgrade* kutoka miezi sita mpaka mwaka mmoja. Kwa hiyo, sasa ina uwezo wa kutunza majina ya watoto waliofaulu kwa mwaka mmoja. Lengo lake ni nini? Mtoto leo anaweza kuja kufanya *interview* labda ya nafasi ya *procurement*, anashindwa kupata hiyo nafasi kwa ushindani kwamba labda nafasi zilikuwa tatu, yeye

amekuwa wa nne ama amekuwa wa tano, anaingizwa kwenye *database*. Kwa hiyo, kukitokea nafasi nyingine ya *procurement* yule aliyeshinda achukuliwe badala ya kumrudisha tena kuja kufanya *interview* na kumsababishia usumbufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa kuifanya *database* ikae mwaka mmoja itasaidia kuwakusanya wale waliofaulu na kama kuna nafasi zinatokea na zinawahitaji wale waliofanya usahili kwenye nafasi hizo hizo itoshe tu waliokwisha kufaulu wachukuliwe kuliko kurudishwa kurudishwa kurudishwa.

Kwa hiyo, sasa tulichokifanya pamoja na kuipeleka *database* kutoka miezi sita mpaka mwaka mmoja, tumefuata taratibu zote na tumeshatangaza kwenye Gazeti la Serikali, Mwanasheria Mkuu alishapitia kwa hiyo kila kitu kipo tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwezi wa kwanza mwaka huu na mwezi wa pili, usaili wowote utakaofanyika jumlisha wale ambao walionekana walifaulu nyuma na wakawekwa kwenye *database* tunataraji sasa watoto wa Kitanzania 1,769 watachukuliwa kutoka kwenye *database* na hawatasumbuliwa tena kurudi kuja kufanya usahili. Kwa hiyo, sasa *database* yetu itaanza kutumika. Kwa hiyo, tumetekeleza agizo hilo na tutaendelea kulisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye ajira; tumshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, alipoingia tu kwenye Serikali yake ya Awamu ya Sita, Waheshimiwa Wabunge nadhani tumpongeze. Kwa mwaka 2021 mpaka Januari, 2023 tumekwishakutoa ajira 56,059 kwa fani mbalimbali. Hizo ni ajira mpya, lakini naomba niseme kwa mwaka

2022/2023 ajira zilizotolewa asilimia 53 zimeenda kwenda sekta ya elimu na sekta ya afya na zote hizo zimeenda kwenye *primary health* na kwenye *primary education,* kwa hiyo asilimia 53 zimeenda huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ninyi Waheshimiwa Wabunge mlitupitishia bajeti, mwaka 2022/2023 tumebajeti ajira nyingine 30,000 na ajira hizo 30,000 Mheshimiwa Rais amesema kipaumbele kiwe ni elimu, kipaumbele kiwe ni sekta ya afya.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais na Serikali wanajua kabisa kwamba jambo hili ni la msingi na hivyo tutaendelea kulisimamia kuona maelekezo ya Bunge lakini na matamanio ya Mheshimiwa Rais ya kupunguza tatizo la ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tumeendelea kuwa-*challenge* wenzetu kwenye *Regional Secretariat* mwaka 2022 tumebadilisha muundo wa *Regional Secretariat*. Tumempa kazi Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulika na Utawala na Rasilimali Watu kuangalia suala zima la ajira pale kwenye eneo lake. Suala hili la ajira, sasa hivi ndani ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, tumeanzisha mfumo wa *HR Assessment (Human Resource Assessment)*. Tunataka kuangalia hivi haya malalamiko ya ukosefu wa watumishi yanafananaje tumeanza kupata hiyo picha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiangalia *job weight* ya mfanyakazi mmoja ya mfanyakazi mmoja mwingine zinatofautiana. Kuna baadhi ya wafanya kazi unaweza ukaangalia majukumu yao ukilinganisha na wengine, majukumu yao hayalingani kama vile inavyotakikana.

Kwa hiyo, tumefikiri kwamba tufanye *assessment* ya kutosha, je, wataalam tunaowahitaji ni wa namna gani? Na hawa wataalam tunaowahitaji kwa zama hizi za Serikali tulionayo, mapinduzi ya nne ya viwanda yanayoendana na TEHAMA, tufanye nini? Kwa hiyo, tumeamua sasa tuboreshe muongoz wa *HR Planning*, watu wa *plan* matumizi ya rasilimali watu kwa kadiri ya mahitaji halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumeamua tena kutengeneza mwongozo wa *HR Succession Plan*, masuala ya urithishaji, mtu mmoja kwenda kwenye nafasi nyingine yaweje. Tukiweza kuitumia rasilimali watu tuliyonayo na *Regional Secretariat* wakatusaidia kuwaangalia waliopo kwenye mikoa yao tuna uwezo wa rasilimali ndogo hii hii tulionayo ikaanza kutusaidia kupunguza uhaba wa watumishi wakati tukiendelea kubajeti na ku-*control wage bill* ambayo tunayo ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spia, lakini kwenye eneo la *TASAF;* tumeona *TASAF* inakwenda vizuri ingawa kuna *challenge* ndogo ndogo na Kamati imetushauri hapa. Eneo linalotupa changamoto hasa ni namna gani wale ambao wamekwisha kuwa na maisha bora wanaweza kuondoka na wakaingia wengine. Hapa tunapata shida, lakini tunashukuru, wanufaika wa *TASAF* 1,992 wako tayari kuondoka kwenye mpango wa *TASAF*, wanasema tayari maisha yao yako bora, wanufaika 200,000 tunawafanyia *assessment*.

Mheshimiwa Spika, na hapa nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge na halmashauri zetu zote tunaomba sana huko kwenye halmashauri, Wakurugenzi wasiwaondoe wanufaika wa *TASAF* bila kuwasiliana na sisi. Wasubiri, tuna miongozo, hatujamaliza kufanya

tathmini. Tuna mikataba ya kufanya tathmini mpaka tujiridhishe, tusije tukamuondoa mnufaika leo, kesho anaingia kwenye wimbi la umaskini, anadai tena kurudi kwenye mpango wa *TASAF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaomba…

**SPIKA:** Dakika moja Mheshimiwa Waziri, malizia.

**WAZIRI WA NCHI, OFIS YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwa tunaomba mtusaidie sana.

Mheshimiwa Spika, lakini tumepokea ushauri kuhusu TAKUKURU Rafiki na namna gani tuataendelea kuzuia rushwa kuliko kupambana nayo. Hiyo tunaifanyia kazi, tume-*present* kwenye Kamati mpango mpya wa TAKUKURU Rafiki, tuna uhakika utatusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, kwenye *eGA* tumechukua ushauri wa Kamati kwamba ni lazima tuanzishe *incubations center*. Naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge tayari tumekwisha kuianzisha na tayari vijana 222 wameshapita kwenye *incubation center*, vijana 59 wanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tu nikupe taarifa hata mfumo wa TEHAMA unaotumika Bungeni vijana hao 59 wameshiriki kuuandaa na kuweza kufanya utumike pamoja na mifumo mingine mingi.

Ninaomba tu niseme kwamba tutaendelea kusimamia haki na stahiki za watumishi, walimu wamezungumzwa sana hap. Ninaomba nikuhakikishie Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan,

imekwishakupandisha madaraja watumishi 264,491 wengi wao wakiwa ni walimu na hiyo ni kuonesha *appreciation* ya Serikali kwa walimu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tumeendelea kulipa malimbikizo ya mishahara, tumeendelea kufanya *re-categorization*.

Mheshimiwa Spika, lakini unakumbuka pia tumeshughulikia umri wa bima ya afya kwa watoto na wategemezi wa watumishi wa Serikali, lakini vilevile tumeshughulikia masuala ya kuondoa *retention fee…*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaendelea watumishi wa umma iliwaweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kushukuru kwa nafasi hii, Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea kuwajali watumishi na kuangalia kero za kiutumishi ili utendaji kazi uweze kuwa na tija kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii aje ahitimishe hoja yake.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana,

mimi tu niendelee kuchukua au kuomba fursa hii kwa maana ya kwamba nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia siku ya leo na hasa katika kuchangia hoja ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, tumepata wachangiaji wengi, Wabunge takribani 15 wamechangia na Mawaziri ambao wamechangia moja kwa moja kuhusiana na Kamati yetu ni Mawaziri wanne.

Mheshimiwa Spika, nishukuru tu kwamba wachangiaji wote wameungana na Kamati, wameungana na hoja zote za Kamati na mapendekezo ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niendelee tu kumpongeza, nimpongeze Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya na hasa ya kutoa fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali ya Wizara hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kuwapongeza Mawaziri ambao wanasimamiwa na Kamati yetu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, kwa kweli wamekuwa wanafanya kazi na kazi hiyo wanayoifanya ni ya ushirikiano wa hali ya juu na Kamati yetu. Hapa leo wamekuja kujibu hoja mbali mbali kwa kweli Mawaziri hawa wameonesha *commitement* ya hali ya juu kwa maana kwamba wanakwenda kutekeleza yale majukumu au yale maoni ambayo Kamati yetu imeyatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee tu kusema kwamba maazimio ya Kamati ambayo tunakwenda kuyapitisha leo hapa katika Bunge lako tukufu basi waende wakayasimamie, wayafanyie kazi kadri jinsi walivyotoa

maelezo yao na jinsi tulivyoweza kutoa maelekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati baada ya kutoa maoni, wachangiaji wengi wameweza kuchangia na kabla sijaenda kwenye Wizara moja moja kuna hoja za jumla ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, katika michango yote ya Wabunge, jambo lililojitokeza kubwa zaidi ni suala zima la upungufu wa watumishi hasa katika sekta ya afya na sekta ya elimu kwa maana ya walimu.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa yetu ya Kamati iliyopita ya mwaka jana, tulisema na tulisisitiza kwamba Serikali ichukue jukumu maalum au jukumu mahsusi kuhakikisha kwamba inaajiri walimu, madaktari na manesi ili kusudi waende wakatoe huduma kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaendelea kusema kwamba ninaishukuru Serikali imechukua hatua za dhati, lakini bado jukumu ni kubwa, wanatakiwa waajiriwe walimu wa kutosha pamoja na watumishi wa sekta ya afya.

Mheshimiwa Spika, leo umesikia hapa masomo ya sayansi ni kilio kikubwa, upungufu wa walimu wa sayansi umeonesha unaendana kabisana *failure* ya wanafunzi katika masomo ya sayansi. Kwa maana hiyo, kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya ufaulu mdogo wa wanafunzi katika masomo ya sayansi na upungufu wa walimu wa masomo hayo. Hivyo basi jukumu hili Serikali tunaomba ilichukuwe, ilibebe kwa hali ya upekee ili kusudi tuondokane na changamoto hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limezungumzwa zaidi ni ukatili wa kijinsia kwa kina mama na watoto. Nimshukuru sana na Mheshimiwa Waziri Mkuu leo ndiyo ilikuwa mada yake kuu. Ukatili wa kijinsia umezidi kukithiri na hata leo hapa Waheshimiwa Wabunge wamesema hata kwa watoto wa kiume napo tutupie jicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili halipingiki ni lazima tuchuke hatua za kipekee. Sasa hivi ukiwa na mtoto wa kike unatakiwa umlinde, lakini ukiwa na mtoto wa kiume naye unatakiwa umlinde tena zaidi, haya yote nadhani ni vizuri tuamue kwa pamoja, tupambane na ukatilii huu wa kijinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine katika masuala ya kijumla ni afya ya akili; suala la afya ya akili limekuwa ni changamoto kubwa, tuchukue sasa juhudi za kipekee kuhakikisha kwamba tunapambana na matatizo ya akili ambayo wanachi wetu yanawakabili.

Mheshimiwa Spika, kwa Wizara ya Afya ni kwamba namshukuru sana Mheshimiwa Waziri ametoa *commitement* kubwa na kwa suala la *MSD,* tunaomba sana wawekezaji wa ndani wapewe nafasi na fursa kwa ajili ya kuzalisha dawa kwa ajili ya kuondoa changamoto ya upungufu wa dawa, lakini vilevile kwa ajili ya kufanya biashara katika nchi ambazo tuna mahusiano nazo kwa maana ya nchi za *SADC* na nchi za Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, vilevile suala la *TMDA* pamoja na *TBS;* yale majukumu ya *TBS* aliyozungumza Mheshimiwa Waziri na yeye ametoa *support* hiyo ni kwamba kweli majukumu ya chakula basi yarudishwe kwa *TMDA* aweze kuyashughulikia kwa sababu ana utaalamu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, kwa Bodi ya Mikopo kwenye suala la Wizara ya Elimu, wewe katika Bunge lako hili hapa majuzi, Bunge lililopita uliweza kutoa, ulituongoza na Bunge likatoa ushauri kwa Serikali kwa wanafunzi ambao walikuwa hawajapata mkopo wapatiwe mikopo mara moja na waweze kuingia madarasani waendelee na masomo.

Mheshimiwa Spika, uamuzi huu ulikuwa ni uamuzi wa busara na wa kipekee na umakini wa hali ya juu uliotoka katika Bunge lako la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jana nashukuru Kaka yangu, Ndugu yangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba hapa alisema kwamba Bunge hili, Wabunge wangekuwa kidogo makini wangetoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais. Naomba niseme umakini wa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wa kusahauri Serikali iongeze fedha kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi ulikuwa ni umakini wa hali ya juu kupita kiasi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikupongeze sana wewe, ninakupongeza sana na Bunge lako kwa maamuzi haya, tunaomba na tumesema katika taarifa ya Kamati, Bodi ya Mikopo iongezewe fedha. Udahili wa wanafunzi siyo suala la dharura. Udahili wa wanafunzi ni suala linaloweza kufanyiwa *forecasting* ya kutosha, fedha iliyotoka, Shilingi Bilioni 570 ilijulikana, na udahili wa wanafunzi kwa mwaka huu uliongezeka na Bodi ya Mikopo ilitoa taarifa kwa Wizara ya Fedha ili iongeze fedha kwa ajili ya mikopo, tunaomba siku nyingine Wizara itambue kwa wepesi na kwa haraka kwamba kuna ongezeko la udahili ili iweze kuongeza fedha kwa ajili ya kuwapa wanafunzi mikopo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile suala la maendeleo katika Sekta ya Maendeleo ya Jamii, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuanzisha sekta hii au Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii. Ukatili unaoendelea, msimamizi mkuu wa masuala haya ni Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Makundi Maalum. Waziri huyu ana *instrument* yake. Yanapotokea matukio kama haya wakati mwingine yeye ndiyo anatakiwa akemee. Hivyo basi, tuangalie Serikali iangalie kwa umakini, Wizara hii ikiwezekana iwe chini ya ofisi kubwa za Serikali, aidha iwe chini ya Waziri Mkuu au iwe chini ya Makamu wa Rais, au iwe chini ya Ofisi ya Rais ili Waziri huyu anapoona kuna suala lolote la kukemea au suala lolote ambalo linaonekana kuna uvunjifu wa amani au ukatili wa kijinsia awe na *power* ya kumwambia Waziri wa Mambo ya Ndani, Waziri wa Sheria, Waziri wa Elimu au Waziri yeyote ambaye anashughulika na watoto na akina mama awe na *power* hiyo, nadhani hili tutakwenda vizuri zaidi tukilirekebisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Dakika moja malizia Mheshimiwa.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO-MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mwisho kwa Wizara ya Utamaduni na Michezo, tunawashukuru sana na tunampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya. Wizara hii ilikuwa haionekani sasa hivi imekuwa ni Wizara ya mfano, wanafanya kazi vizuri sana, hivyo waendelee kujenga viwanja, waendelee kuhakikisha kwamba vijana wa Kitanzania wenye *talent* za kufanya michezo au kucheza michezo mbalimbali waweze kuonesha *talent* zao, na iwe chanzo cha vijana hawa kupata fedha.

Mheshimiwa Spika, matajiri vijana na watoto wanatokana na *talents.* Matajiri wanaotengenezwa katika umri mdogo ni wale wenye vipaji maalum. Wizara hii tukiiwezesha, tutapata matajiri vijana kutokana na vipaji walivyonavyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niseme sasa naomba kutoa hoja. Ahsante.

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana. Sasa Waheshimiwa Wabunge, baada ya hoja kuungwa mkono nitawahoji na niwakumbushe tena ninavyokuwa ninawahoji, pamoja na kwamba watu wamechangia, wengine wakasema naongeza Azimio. Ili uongeze Azimio humu lazima Mwenyekiti akija hapa mbele aseme mabadiliko hayo. Kwa hiyo kinachohojiwa ni hiki kilichoko kwenye taarifa na maazimio ambayo Kamati iliyaleta. Sasa hata yale ambayo Mwenyekiti ameyasema hapa mbele kayasema kama ushauri kwa maana ya kwamba Serikali iyachukue na yeye ndiyo fursa yake ya kuchangia hapa mbele lakini yanayohojiwa ni yale yako humu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kuhusu hoja ya huduma na maendeleo ya Jamii kuhusu taarifa ya utekelezaji wa majukumu na shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia Januari 2022 hadi Januari 2023.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge Lilipitisha Maazimio ya Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Abdallah Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuhitimisha hoja hii.

Mheshimiwa Spika, pili, nitoe shukurani za dhati kwa Wabunge wote ambao wamechangia katika taarifa yetu hii ya Kamati, tumepata michango ya zaidi ya Wabunge 13 na Mawaziri Watatu ambao kiukweli katika michango yote wameelezea na wameunga mkono mapendekezo yaliyotolewa na Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika michango iliyotolewa na Wabunge hawa, ambao walimekuwa makini katika michango yao, hoja nyingi zinaenda kumgusa mwananchi wa kawaida ambaye yeye ndiye mwananchi namba moja katika nchi hii. Hoja nyingi zimezungumzwa hapa lakini zipo hoja mahsusi tatu ambazo zimezungumzwa na Wabunge walio wengi.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ilitokana na *TARURA* kuhusiana na fedha za dharura na ujenzi wa barabara. Tunapozungumza fedha za dharura maana yake tunajiandaa endapo tatizo litatokea tuweze kutatua tatizo hilo. Tumefuatilia fedha hizi zinazoombwa za

dharura zinaenda kutengeneza barabara ambazo zimekuwa zikitengewa fedha kila mwaka na *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, sasa tunatakiwa tujiulize hapa, *TARURA* kila mwaka tunatenga fedha lakini barabara hizo zikijengwa baada ya muda fulani zinaharibika. Yawezekana katika ujenzi wa barabara hizo vipo vitu vya kitaalam vinakuwa havikidhi vigezo. Moja ya jambo ambalo limeonekana sana, huwezi kujenga barabara usipoweka mifereji. Kwa sababu barabara nyingi zinajengwa bila ya mifereji matokeo yake inapofika wakati wa mvua barabara zile zinaharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napitisha dodoso kwa baadhi ya Wabunge kuwaambia wanitajie barabara moja ambayo ndani ya miaka mitano imetengewa fedha kiasi gani za *spot improvement, periodic maintenance* na matengenezo mengine. Nilivyojumlisha katika zile barabara nimeona kama fedha zile zote zingejumlishwa kwa pamoja basi barabara ile kwa mwaka mmoja ingejengwa kwa kiwango kikubwa na hatimae tungeondokana na hii kadhia ya kuomba fedha za dharura kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

Mheshimiwa Spika, suala la barabara limechukua mjadala mpana sana katika Bunge letu leo kwa maana kila Mbunge aliyezungumza na wengine waliochangia kwa maandishi wamekuwa na kero kubwa ya barabara. Kutokana na hayo, nimepokea nyongeza ya maazimio katika suala hili la *TARURA,* kwa sababu ulitoa maelekezo toka jana, naomba kwa idhini yako sasa nilisome. Azimio hilo linasema kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, Serikali imetoa mwongozo kwa Halmashauri zote nchini kutenga asilimia 10 za fedha za

mapato ya ndani katika ujenzi wa miundombinu ya barabara;

Na kwa kuwa, Halmashauri nyingi hazitekelezi mwongozo huo,

Hivyo basi, Bunge linaitaka Serikali kuandaa sheria ya utengaji wa asilimia 10 ya mapato ya ndani katika ujenzi wa miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Spika, tunakumbuka huko nyuma Serikali ilitoa mwongozo wa utengaji wa asilimia 10 lakini kwa sababu ulikuwa siyo wa kisheria basi watu walikuwa wanafanya kadiri watakavyo na baada ya kuufanya wa kisheria, Halmashauri nyingi zimekuwa zikitekeleza. Kwa hiyo naomba na hili nalo liwe katika sehemu ya azimio.

Mheshimiwa Spika, nasema hili sababu ukichukua baadhi ya Halmashauri hasa za Dar es Salaam, kwa mfano Halmashauri ya Ilala kwa mwaka inatenga Shilingi Bilioni 6.2 kwa ajili ya matengenezo ya barabara kwa ajili ya zile asilimia 10. Sasa fedha hizi zikitumika vizuri kila mwaka tunazungumzia kilometa takribani 10 za lami nyepesi. Kwa maana hiyo, ndani ya miaka mitano tutakuwa tumetengeneza takriban kilometa 50 za lami nyepesi.

Mheshimiwa Spika, suala jingine ambalo limechukua nafasi kubwa katika mjadala wetu ni mgogoro wa ardhi katika Jiji la Dodoma. Ni wakati sasa Serikali ilichukulie jambo hili *very serious*. Wananchi wengi katika Jiji la Dodoma na Halmashauri nyingine nchini wamekuwa wakilalamikia masuala haya ardhi. Ukienda pale Kawe, kule Nyakasangwe, sijui wapi, kuna migogoro mikubwa ya ardhi. Kwa hiyo, Serikali sasa tutayarishe mpango

maalum wa kwenda kutatua hii migogoro ya ardhi. Migogoro hii mara nyingi inawahusu wananchi wanyonge. Kwa hiyo tunapowaonea wananchi wanyonge tafsiri yake wananchi walio wengi wanaenda kupata uonevu mkubwa katika maeneo yetu. Kwa hiyo ninaomba na kusisitiza sana, migogoro ya ardhi ichukuliwe hatua stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala jingine ambalo limechukua nafasi kubwa ni miradi ya *TACTIC,* kuna mradi mwingine wa *RISE* na mradi wa uboreshaji wa Jiji la Dar es Salaam yaani *DMDP.* Ninaiomba sana Serikali miradi hii Wabunge wengi wanaitegemea, tuangalie uwezekano mkubwa wa kila maeneo yenye mahitaji basi miradi hii ifanyike na hatimae sasa tuweze kuondoa tatizo kubwa la miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, suala zima la TAKUKURU rafiki. Tunazungumzia habari za fedha nyingi za maendeleo katika maeneo yetu lakini Wabunge tusipopata uelewa mzuri wa TAKUKURU rafiki, fedha hizi zinaenda kupotea. TAKUKURU rafiki inamuhusisha moja kwa moja mwananchi wa kawaida wa pale kijijini kwenda kujua fedha zilizoletwa na namna gani atakayezisimamia zile fedha ili ziweze kutekeleza ule mradi kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni rai yangu, Serikali sasa ione namna bora ya Wabunge hawa kuwapa uelewa mkubwa wa dhana nzima ya TAKUKURU rafiki ili na wao waende kutoa maelezo hayo kwa wananchi hawa. Ukisoma ile sheria ya 288 ya uanzishwaji wa Serikali za Mitaa utaona kazi ya Mtendaji wa Kata ni kumsaidia Mkurugenzi katika utekelezaji wa majukumu yake. TAKUKURU rafiki wakielekezwa hawa Watendaji wa Kata

na Mitaa wataenda kuisaidia halmashauri, wataenda kuisaidia mapato ya Serikali kuhakikisha miradi ya maendeleo inatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kutoa hoja kwamba mapendekezo yote ya Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa yakubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. SEBASTIAN H. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Mwenyekiti naomba umpe hilo Azimio ambalo umelirekebisha, hebu mpe huyu Msaidizi ili nilione hapa mbele. Hoja imeungwa mkono na hivyo natakiwa niwahoji lakini wacha nipate hicho alichokisoma hapo Mwenyekiti ili kama kinaweza kuingia hapa niweze kuwahoji na hiki kikiwa sehemu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwenye taarifa ile ya Kamati, Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwenye Sehemu ya Nne halafu kipengele cha Nne, taarifa inasema kuhusu Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (*TARURA)* imeanza hapo na (a) Kuongeza bajeti ya dharura ya matengenezo ya barabara. Sasa Mwenyekiti hapa ameongeza jambo ambalo nilisome tena kwenu, anasema, hapa yaongezeke maneno haya:-

Kwa kuwa, Serikali imetoa mwongozo kwa Halmashauri zote nchini kutenga asilimia 10 za fedha za mapato ya ndani katika ujenzi wa miundombinu ya barabara,

Na kwa kuwa, Halmashauri nyingi hazitekelezi mwongozo huo,

Hivyo basi, Bunge linaitaka Serikali kuandaa sheria ya utengaji wa asilimia10 ya mapato ya ndani katika ujenzi wa miundombinu ya barabara.

Waheshimiwa Wabunge, sasa hapa mwishoni kidogo panahitaji, kwa sababu hili agizo la asilimia10 tukiitaka kwamba Serikali iandae sheria kwa ajili ya hii asilimia 10 hiyo sheria sijui itakuwa ina fananaje. Kwa hiyo, nafikiri kuna marekebisho kidogo kwenye hili azimio ili likae vizuri. Nafikiri kwa ngazi hii kwa sababu limekuja hapa na Mwenyekiti amelipata kutokana na mawazo ya Waheshimiwa Wabunge, nadhani hoja ya msingi ni Bunge kuazimia kwenye zile Halmashauri kuhakikisha zile asilimia10 ambayo ina maelekezo kwamba ielekee kwenye miundombinu ya barabara ni kuhakikisha inakwenda.

TAMISEMI isimamie zile Halmashauri na kuhakikisha ile asilimia 10 iliyotengwa inatengeneza barabara, halafu huko baadae sasa kamati itatazama namna kama utekelezaji wa hili azimio unaendaje watapata sasa fursa ya kukutana na upande wa Wizara ili waone namna ya kuliweka vizuri, lakini kwa ngazi hii kusema tuiagize Serikali itunge sheria kidogo tunakuwa hatujapata muda sana wa kulitafakari kama tunahitaji sheria nzima kwa ajili tu ya hii asilimia 10. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nami ninakushukuru hapo hapo kwa sababu unajua kuna baadhi ya vitu vingine unakuta labda unafanya *affirmative action,* kama wakati ule ilikuwa mikopo ya asilimia 10 kwa wanawake na makundi maalum lakini hapo unaangalia suala la miundombinu. Pia Halmashauri zenyewe hazilingani uwezo, kwa hiyo ni lazima tu-*craft* kwa namna ambayo isije baadae ikatuletea shida labda liwekwe kwa namna ambayo baadae tufanye mashauriano.*(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa hivyo itakuwa sahihi, nataka kuondoa hii hoja ya sheria, yale ya kwa kuwa naona yamekaa sawasawa. Hapa kwenye Bunge linaazimia nini? Bunge linaitaka TAMISEMI izisimamie Halmashauri kuhakikisha ile asilimia 10 inaenda kwenye miundombinu. Hilo si litakuwa liko vizuri zaidi Waheshimiwa Wabunge? Halafu hapo baadae Kamati sasa italitazama na Wizara kuona kama kutakuwa na sababu ya kuitengenezea sheria au hapana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaafikiana na haya marekebisho madogo?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kuhusu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa ya mwaka kuhusu shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2022 hadi Januari, 2023.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge Lilipitisha Maazimio ya Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, haya ahsanteni sana. Nitumie fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa namna mlivyoshiriki mjadala wa taarifa hizi mbili za Kamati; na namna ambavyo mmewasikia hapa wenyeviti wakihitimisha kuashiria kwamba michango mliyoitoa hata wale ambao si wajumbe wa hizi Kamati, mmewasaidia kupata hata mawazo mapya ambayo baadhi yao wamekuja nayo hapa mbele.

Waheshimiwa Wabunge, pia upande wa Serikali nao wamepata fursa ya kuchangia na wameonesha kwa kweli namna ambavyo mnashirikiana kwa pamoja na kwa sababu taarifa zote mbili zimeonesha namna ambavyo Serikali imeyafanyia kazi maazimio yale yaliyopita. Na kwa kufanya hivyo yale ambayo Serikali imesema wakati ikichangia hapa kwa maana ya mawaziri ni dhahiri kwamba wamesema wameyachukua wanaenda kuyafanyia kazi yale ambayo yako kwenye maazimio.

Waheshimiwa Wabunge, pia michango yenu mbalimbali ambayo mmeitoa humu ndani wameisikia na hata kama haikuwa sehemu ya maazimio nayo wanaichukua wanaenda kuifanyia kazi. Kwa hiyo na wao niwashukuru sana kwa huo utayari na kwa huo ushirikiano uliopo ambao unaonesha kwamba kila mtu ana nia njema na kila upande una nia njema ya kuhakikisha wananchi wetu wanaendelea kustawi.

Waheshimiwa Wabunge, kipekee kabisa niwashukuru wenyeviti na makamu wenyeviti wa kamati zetu hizi mbili kwa kuzisimamia kamati zetu vizuri na kuhakikisha tunaweza kupata mawazo kama haya mazuri na hata sasa yameshakuwa maazimio ya Bunge. Kwa hiyo ni jambo la kupongeza na ninawashukuru sana kwa kazi hiyo.

Mambo machache Waheshimiwa Wabunge, la kwanza pamoja na kuishukuru Serikali kwa utayari wa kuyafanyia kazi yale yote ambayo tumeyasema Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI hii hoja ya migogoro ya ardhi hapa Dodoma imeshasemwa muda mrefu; na wewe umeeleza hapa utayari wako wa kuifanyia kazi. Mimi sasa badala ya kuliacha wazi kwa sababu limeachwa wazi kwa muda mrefu kwa hivyo hatujui litaenda mpaka lini kwa sababu taarifa tena ya kamati kama hii tutaipata mwaka ujao, *Inshallah* Mwenyezi Mungu atuweke, tutaipata mwakani mwezi kama huu ama mwezi Januari.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hivyo nafikiri ukipewa kipindi hiki taarifa ijayo ya Kamati siyo ije na mapendekezo na mawazo, ije na maamuzi ambayo Serikali imefikia kuhusu migogoro hii. Wale wanaopaswa kulipwa tuje tusikie hapa Halmashauri ya Jiji la Dodoma limewalipa hao watu. Wale ambao malipo yao hayana shida na wameonewa ni wazi na dhahiri walipwe fedha zao. Muda unavyoendelea kuwa mrefu mgogoro unazidi kuwa mkubwa sana halafu baadaye Serikali itakuja kupata hasara kubwa zaidi kuliko hata hivyo viwanja vyenyewe vilivyopimwa. Kwa hiyo nafikiri kwa mwaka huu mkipewa TAMISEMI nafikiri mnaweza kufanyia kazi hayo.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ambalo limesisitizwa ni kuhusu hao watumishi. Kama hawachukuliwi hatua ndiyo maana migogoro inaendelea kuzalishwa sio tu Dodoma na maeneo mengine. Sasa tunafahamu changamoto ipo kwa sababu watumishi hawa wengine wapo TAMISEMI wengine wako ardhi, lakini Serikali ni moja na mnafanya kazi pamoja. Watumishi waliozalisha hiyo migogoro wachukuliwe hatua; na mtakapokuwa mnaleta taarifa hapa Bungeni mtatueleza pia watumishi wangapi walibainika kushiriki kwenye kuwadhulumu hao wananchi na hatua mlizochukua kwao kwa utaratibu wenu wa kawaida kabisa Serikalini wa kuwachukulia hatua. Kwa sababu pia kumhamisha mfanyakazi ile sio adhabu na ukimhamisha kule anakoenda anaenda kutumia utaratibu alioutumia hapa na kule anaenda kuzalisha migogoro. Kwa hiyo upande wa TAMISEMI mkishirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi jambo hili lifike mahali kila mtu ajue haki za mtu, haki za ardhi; ni haki zake asidhulumiwe kwa mtu kuwa na cheo ofisini.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo nafikiri mwaka ujao tutakapokuwa tunakutana kwa ajili ya mambo kama haya tutakuwa sasa na taarifa kutoka upande wa Serikali; na ninaamini taarifa itatokea huko kwenye Kamati. Sasa Wabunge wasije wakafikiri Waziri atasimama hapa kuleta taarifa, tutataka kusikia kutoka kwenye kamati ikileta hapa kwamba Serikali imetueleza mambo haya yamekamilika kama ambavyo leo hapa kamati zetu zimetueleza namna ambavyo Serikali imefanyia kazi maazimio. Kwa hiyo maazimio ya kamati kwenye hoja hii naamini tutayafanyia kazi na mambo yataenda vizuri, hilo lilikuwa la kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, jambo la pili ambalo halina uhusiano na maazimio. Nafikiri mmemsikia hapa Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mimi niwapongeze sana kwa hatua ambayo mmeichukua ya kutambua ubunifu wa huyu mwalimu Yusuph. Nawapongeza kwa sababu hakuwa ametumwa, chochote alichokifanya mimi sijakiona lakini nawapongeza kwamba mmechukua hatua ya kumtambua na pia ulimuahidi kwamba utamwalika kuja Dodoma; ni jambo zito kutambuliwa na Waziri. Na naamini Bunge letu linafatiliwa atatambuliwa hata na Mheshimiwa Rais kwa sababu atamwona yuko humu ndani. Kwa hiyo ni jambo kubwa mimi nawatia moyo. Sasa nawatia moyo kwa maana ya kwamba muendelee kufanya hivyo pia kwa wabunifu wengine ambao wanajitahidi kuendelea kuhakikisha elimu yetu inakuwa bora zaidi. Kwa hiyo nawapongeza sana lakini tupanue wigo kwa wale wabunifu wengine, na naamini hilo liko ndani ya uwezo wenu.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine dogo lililozungumzwa hapa, nadhani kuna Mbunge alikuwa anachangia kuhusu mgambo, nadhani ni Mheshimiwa Bonnah Mbunge wa Segerea. Sasa hawa mgambo, kuna kitambo kimepita kidogo, nadhani tuipongeze Serikali kwa hatua mbalimbali inazozichukua. Yako maeneo mbalimbali ambako watu walipata changamoto hapa na pale lakini tukawaona hawa watu ambao wamefanyiwa hiyo sijui tuite dhuluma ama vipi, wakaitwa na viongozi kwa hiyo hatua zikachukuliwa. Mimi nafikiri huo ndio ubinadamu, kwa sababu hata wale mgambo wanaendelea nao kujifunza wanapoona hivi wanajua jambo hili nililolifanya si zuri. Kwa sababu kumfukuza mtu, kumwaga vitu vyake, kukanyaga vitu vyake; wewe mwambie abebe vitu vyake aende. Kwa sababu hicho

chenyewe alichonacho hapo inawezekana amekopa mkopo wa halmashauri; na ndiyo tunaambiwa huku mikopo hailipiki kwa sababu huyu alivunjiwa vitu vyake na mambo kama hayo.

Kwa hiyo mgambo anaendelea kujifunza na sisi tuendelee kuwafundisha lazima wawe na sura ya ubinadamu. Mama kabeba machungwa anakimbizwa, machungwa yanamwagika, wanayakanyaga haileti picha nzuri, lakini Serikali inajitahidi kuchukua hatua inapoona mambo kama hayo, nimeona niliseme hilo.

Dogo lingine la pili kutoka mwisho ni lile alilolichangia Mheshimiwa Mbunge kuhusu nyumbani na watoto wetu pengine kwamba wanachapwa vibao na mambo kama hayo. Sasa isije ikatuma ujumbe kana kwamba Bunge linakataza wazazi kuchukua hatua mbaliambali. Sheria tulizotunga wenyewe zinaruhusu marekebisho ya mtoto, lakini haijasema kama unamrekebisha kwa kibao ama vipi lakini imeweka mipaka ya yale marekebisho. Kwa hiyo ni vizuri wazazi tukajielimisha ile mipaka ya kisheria ambayo ipo, lakini sheria zinaruhusu kumrudi mtoto, kumrekebisha mtoto; ila usimsababishie yale maumivu ambayo yanaweza yakamletea kuumia mwili wake. Si kwa maana ya maumivu yale ya; sijui nielezeje; usimsababishie kama msongo wa mawazo na vitu kama hivyo. Lakini adhabu sheria zetu zinaruhusu kumpa adhabu mtoto.

Waheshimiwa Wabunge, unampa adhabu gani, mipaka imewekwa pale, kwa hiyo isije ikatuma ujumbe wa namna hiyo; na ndiyo maana hata ule mwongozo unazungumza kuhusu viboko lakini umetaja idadi ya viboko. Kwa hiyo hata viboko vinaleta maumivu lakini lengo lake si kumuumiza mtoto lengo lake ni

kumrekebisha yule mtoto. Kwa hivyo hata mzazi anatarajiwa atumie mipaka hiyo sio kwa maana ya viboko vinne lakini atumie utaratibu ule ambao sheria imeweka. Hizi ni sheria za jinai zinasema hivyo na pia sheria ile ya mtoto inasema hivyo; kwamba marekebisho yanatakiwa lakini usilete marekebisho yale ambayo yatamfanya sasa mtoto aone kama ametwezwa utu wake. Kwa hiyo ni muhimu hilo nikaona niliseme.

Mwisho ni lile ambalo nilisema ningelizungumza lakini nilikuwa nimeshaligusia kwa hiyo sitazungumza kwa kirefu, la kuhusu madalali. Madalali waliozungumziwa hapa asubuhi ni wale wanaowanyonya wakulima, hata kama mtu anafanya kazi yake ya udalali afanye kazi yake kisheria lakini pia asimnyonye yule wa upande mwingine. Kwa sababu tukisema tu hawa wataondoka hapa katikati si rahisi kila mkulima akalifikia soko liliko anamuhitaji huyu mtu wa katikati. Kwa hiyo huyu mtu wa katikati ndiye tunataka na yeye awe na hiyo sura ya kibinadamu lakini pia afuate utaratibu, afuate sheria, asimkandamize mkulima. Mkulima apate haki yake, huyu dalali apate haki yake na yule mnunuzi apate mazao anayoyataka. Nimeona niliweke hivyo ili madalali nisije nikasikia kesho wananitafuta ofisini kwa sababu wameambiwa pengine kwa namna fulani.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo niwashukuru sana kila mmoja wenu kwa namna alivyoshiriki Bunge siku ya leo ahsanteni sana na sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 2.08 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 3 Februari, 2023, Saa Tatu Asubuhi)*